Hakikat Kitabevi Toleo Namba 4

# NJIA YA PEPONI

**Muhammad Kutbudyn Izniky**

Toleo la Kituruki lilitolewa na
**Hüseyn Hilmi Işık**

**TOLEO LA KWANZA**

Darüşşefeka Cad. 53/A P.K.: 35
**34083** Fatih-ISTANBUL/TURKEY
Tel: 90.212.523 4556–532 5843 Fax: 90.212.523 3693
http://www.hakikatkitabevi.com
e-mail: info@hakikatkitabevi.com
MWEZI WA SABA, 2022

# NJIA YA PEPONI

## UTANGULIZI

Allahu taala amewapelekea watu mitume “sallallahu alayhi wasallam” ili waweze kuishi kwa raha, furaha, utulivu na waweze kuunganisha mioyo yao waishi kama ndugu na wawafundishe na maana ya kutekeleza majukumu yao wakiwa ni watumwa wake. Kwa kupitia waja hawa ambao ni bora kwa kila hali kupita viumbe wengine, binaadamu hujifunza njia iliyo bora kabisa ya maisha. Muhammad „alaihis-salaam” ndie bora na wa mwisho wa mitume “sallallahu alayhi wasallam” yote, nae ni mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa watu wote hadi itakapofika siku ya kiama. Mtume “sallallahu alayhi wasallam” huyu anayependwa sana na Allah, kwa muda wa miaka ishirini na tatu aliteremshiwa **(Quran)** yenye kujuvya maamrisho yake Allah na makatazo yake. Kwa vile Quran ni ya kiarabu na ina ndani yake mambo ambayo akili ya kawaida haiwezi kuyapambanua, Mtume “sallallahu alayhi wasallam” aliisomesha na kuipambanua yote kwa masahaba zake ridhwanullahi alayhim. Mtume “sallallahu alayhi wasallam” amesema **(Mwenye kuielezea Quran visivyo nilivyoeleza mimi basi huyo ni kafiri)** Wanazuoni wa kiislam Allah awarehemu, waliyapokea maelezo ya Quran aliyoyatoa Mtume “sallallahu alayhi wasallam”, kutoka kwa masahaba ridhwanullah alayhim na wakayapanua kwa mtindo ambao kila mtu ataweza kufahamu na hivyo waliandika vitabu vya tafsiri ya Quran. Hawa huitwa wanazuoni wa Ahli sunna. Wanazuoni hawa kwa kuzingatia maelezo ya Quran na maelekezo mengine aliyoyatoa mjumbe wa Allah waliandika vitabu vya elimu za kiislam. Wale wanaotaka kujifunza dini aliyoishusha Allah kwenye Quran kwa usahihi bila makosa basi na wasome hivi vitabu **(vya elimu za kiislam -Ilm-i-hal)** vya wanazuoni hao.

Kitabu hichi cha **(njia ya peponi)** tunachokileta kwenu jina lake la asili ni **(Miftahul Jannah) yaani ufunguo wa mlango wa peponi.** Kiliandikwa na Muhammad Kutbudyn “rahmatullahi alaih” Izniky aliyekufa Edirne mwaka 885 hijria (1480 miladia).

Mwanazuoni gwiji wa kiislam Sayyid Abdulhakim Efendi amesema (Mwandishi wa **(Miftahul Jannah)** ni mtu salih. Wasomaji wake watafaidika.) Kutokana na hayo ndio tunakieneza kitabu hiki. Baadhi ya sehemu chache ambazo zimewekwa maelezo basi maelezo hayo yemeingizwa kwenye mabano[ ]Maelezo hayo yameteuliwa kutoka katika vitabu vyengine na kuingizwa humu. Hakuna mawazo ya mtu binafsi katika haya. Allah atulinde sote na mitego na mgawanyiko

wanaosababisha maadui wa waislam, watu walio waovu wenye kubeba majina ya kiislam au hata kujiita ni maalim, wasio na madhehebu na waletao mabadiliko katika dini. Allah atuweke kwenye njia ya Mtume “sallallahu alayhi wasallam” wetu kupitia uongozi wa wanazuoni wa madhehebu ya **(Ahlu sunna)**. Allah atuwezeshe kupendana na kusaidiana.

[Binaadamu anapofanya jambo kwanza hujiwa na fikira katika moyo. Jambo hili ndilo analotaka kufanya. Hii huitwa **(Nia)**. Ili kulitekeleza hilo, huvipa amri viungo vyake. Kuvipa amri viungo huitwa Kusudio. Viungo kufanya hilo jambo huitwa amali **(Chumo)**. Mambo yafanywayo na moyo ndio hutengeneza maadili. Moyo unapokea manenezo kutoka vyanzo sita. Manenezo yatokayo kwa Allah huitwa **(Wahyi)** na haya hupewa mitume “sallallahu alayhi wasallam” tu. Manenezo yatokayo kwa malaika huitwa **(Ilham)**. Haya huwajia mitume “sallallahu alayhi wasallam” na wale walio wema miongoni mwa waja. Manenezo yatokayo kwa waja wema huitwa **(Nasaha)**. Wahyi, ilham na nasaha mara zote zinakuwa ni njema na zenye faida. Manenezo yatokanayo na shetani huitwa **(Wasiwasi)**. Yale yanayotokana na nafsi yake mwenyewe mtu huitwa **(Hawaya)**. Na yale manenezo yatokanayo na rafiki mbaya huitwa **(Mghafala)**. Nasaha hupewa kila mtu. Wasiwasi na hawaya huingia kwenye mioyo ya makafiri na waislam walio mafasik. Hivi viwili ni viovu tena vyenye madhara. Jambo ambalo Allah analipenda na kuliridhia hilo huitwa jambo jema. Yale asiyoyapenda huitwa mambo maovu. Kutokana na wingi wa rehema zake, Allah ameyabainisha mema na maovu ndani ya **(Quran karim)**. Akaamrisha kuyatenda yaliyo mema na kukataza yaliyo maovu. Haya maamrisho na makatazo huitwa **(Ah-kamil islamiyya)** (hukmu za uislam). Ikiwa moyo utapokea nasaha za marafiki wema na akili ikatumika kwa kufata hukumu za kiislamu basi moyo hupata nuru na kuwa msafi. Hupata furaha na utulivu duniani na akhera. Iwapo nafsi itafuata maneno na maandishi mapotofu yenye kughafilisha ya watu waovu na wazandik na nafsi ikamtii shetani na kuacha kufuata hukumu za kiislam basi moyo huingia kiza na kuharibika. Moyo msafi wenye nuru, hupenda kufuata maamrisho ya kiislam. Moyo ulioingia kiza hupenda kufuata marafiki waovu, shetani na nafsi. Kutokana na rehema zake Allah Watoto wanaozaliwa kila sehemu huwaumba wakiwa na mioyo misafi. Kisha baba na mama zao na marafiki zao ndio huitia kiza na kuwafanya wawe kama wao.]

**NJIA YA PEPONI ........ - 6 -**
UISLAMU ........ - 6 -
ALLAHU TAALA YUPO NA NI MMOJA........ - 6 -
SIFA ZA IMANI........ - 15 -
SIFAT-I-DHATIYYA ........ - 16 -
SIFAAT-U-THUBUUTIYYA ........ - 17 -
WAKE NA VITA ALIVYOPIGANA MTUME........ - 37 -
KUHUSU VIPAMBANUZI VYA IMANI ........ - 39 -
MAMBO YENYE KUSABABISHA UKAFIRI ........ - 42 -
HUKUMU ZA UISLAM........ - 50 -
JENGO LA UISLAM ........ - 54 -
MLANGO WA SALA ........ - 56 -
MLANGO WA KUKOGA ........ - 59 -
DUA YA TAWHIDI........ - 67 -
YANAYOHUSU HEDHI NA NIFASI........ - 67 -
YANAYOHUSU UDHU ........ - 81 -
YANAYOHUSU MAJI ........ - 81 -
YANAYOHUSU KUTUMIA MSWAKI ........ - 83 -
DUA ZA UDHU........ - 86 -
MLANGO WA KUTAYAMMAM........ - 88 -
ISTINJAA, ISTIBRAA NA ISTINQAA ........ - 92 -
NAMNA YA KUTEKELEZA SALA........ - 94 -
ADHANA YA MUHAMMAD ........ - 97 -
FADHILA ZA SALA YA JAMAA ........ - 112 -
UIMAM NDANI YA SALA ........ - 112 -
KUTULIA KATIKA NGUZO ........ - 113 -
SALA YA SAFARINI........ - 114 -
FADHILA ZA TAKBIRA YA UFUNGUZI........ - 116 -
YANAYOHUSU PEPO TUKUFU........ - 118 -
SALA ZA KADHA ........ - 120 -

KUANGUKA KWA SALA KWA MAITI ..................................................... - 126 -
YANAYOHUSU SALA YA IJUMAA ..................................................... - 129 -
KUSALI ..................................................... - 134 -
KUWA NA UDHURU ..................................................... - 135 -
SALA WAKATI WA UGONJWA ..................................................... - 137 -
UMUHIMU WA SALA ..................................................... - 140 -
KUTOA ZAKA ..................................................... - 148 -
MLANGO WA FUNGA ..................................................... - 158 -
SHARTI ZA KUCHINJA NI TATU: ..................................................... - 164 -
NGUZO ZA HIJA NI TATU: ..................................................... - 165 -
FARDHI HAMSINI NA NNE ..................................................... - 166 -
KUHUSU MADHAMBI MAKUBWA ..................................................... - 170 -
SEHEMU ZA UTUPU NA STARA YA MWANAMKE ..................................................... - 173 -
SIFA ZA MUUMINI ..................................................... - 180 -
KUZITAMBULISHA TABIA NJEMA ..................................................... - 182 -
FADHILA ZA MASAHABA ..................................................... - 183 -
MAELEZO JUU YA VYAKULA ..................................................... - 186 -
YANAYOHUSU NDOA ..................................................... - 189 -
KUMTAYARISHA MAITI, KUMKAFINI NA KUMZIKA ..................................................... - 196 -
HALI ZA KIFO ..................................................... - 198 -
KIFO CHA WALIO MAASUM (WATOTO) ..................................................... - 203 -
KIFO CHA MWANAMKE MUISLAM ..................................................... - 204 -
KIFO CHA WATU WALIODHULUMIWA, WANYONGE WENYE SUBIRA - 207 -
KIFO CHA MAKAFIRI ..................................................... - 208 -
KUZURU MAKABURI NA KUSOMA QURAN ..................................................... - 212 -
JUZUU YA TATU, BARUA YA 9 ..................................................... - 215 -
JUZUU YA TATU BARUA YA 84 ..................................................... - 217 -
BARUA YA 114 ..................................................... - 218 -
NENO LA MWISHO LA KITABU CHA NJIA YA PEPONI ..................................................... - 221 -

# NJIA YA PEPONI

**Al-hamd-u-lillâh-illedhî je’alenâ min-et-tâlibîna wa lil’ilmi min-er-râghibîna wa-s-salât-u-wa-s-salâm-u-’alâ Muhammadin-il-ledhî erselehu rahmatan lil’âlamîna wa ’alâ Âlihi wa Ashâbihi ajma’în.** (Sifa njema ni za Allahu taala aliyetuweka miongoni mwa wanaotafuta mema na wenye kupenda elimu. Sala na salamu zimshukie mtume “sallallahu alayhi wasallam” Muhammad, ambaye alitumwa hali ya kuwa rehma kwa walimwengu na masahaba zake wote.)

## UISLAMU

## ALLAHU TAALA YUPO NA NI MMOJA

[Allahu taala aliumba viumbe vyote. Mwanzoni hapakuwepo na kitu chochote. Allahu taala pekee ndiye aliyekuwepo. Yeye yupo daima. Yeye si kiumbe aliyezuka baadae. Kama asingekuwepo kabla, basi pangelazimika kuwepo nguvu zilizomuumba yeye. Kwani kukosekana kwa nguvu za kukiumba kitu ambacho hakipo, hukifanya kitu hicho kisiweze kuumbwa hivyo kuendelea kuwa hakipo. Ikiwa mwenye uwezo wa kukiumba alikuwepo, basi Allahu taala ni wa azali na milele na ndiye ambaye humiliki nguvu hizo za kuumba. Kinyume na hayo, inawezekana kuhoji kwamba hizo nguvu za kuumba zilikuja baadae, hiyo ina maana kabla yake zilipaswa kuwepo nguvu nyingine zenye uwezo wa kuumba, jambo ambalo litakubalisha kuwepo kwa waumbaji kadhaa ambao idadi yao haina kikomo. Hata hivyo, hii ina maana kwamba hakuna mwanzo kwa waumbaji. Kutokuwepo kwa muumbaji wa mwanzoni husababisha kukosekana kwa uumbaji ambao ungetekelezwa. Ikiwa muumbaji atakosekana, basi viumbe wote hawa wa kimwili na kiroho ambao tunawaona au kuwasikia katika mazingira yetu wasingekuwepo. Lakini, kwa vile viumbe wa kimwili na kiroho wapo, basi lazima wawe na muumbaji mmoja wa azali na anayeishi milele.

Allahu taala aliumba kwanza madutu sahali, ambavyo ndio viundio vya viumbe vyote vya kimwili, kiroho na malaika. Madutu sahali leo hutambulika kama elementi/vipashio. Kuna vipashio vipatavyo mia moja na tano ambavyo leo hii vinajulikana. Allahu taala ameumba, na kila uchao anaendelea kuumba kila dutu na kila kitu kutokana na vipashio hivi mia moja na tano. (Wakati kitabu hichi kinachapishwa kulikuwa na vipashio mia moja na tano ambavyo vikitambulika .Leo idadi yake inatambulika kuwa ni mia moja na kumi na nane.) Chuma, salfa, kaboni, gesi ya oksijeni, gesi ya klorini, kila kimoja wapo ni

kipashio. Allahu taala hakusema ni miaka milioni ngapi iliyopita ndipo alipoviumba vipashio hivi wala hakutufahamisha ni lini alianza kuumba ardhi, mbingu na viumbe hai, ambavyo ni natija ya vipashio hivi. Kila kitu, kiwe kiumbe chenje uhai au kisicho na uhai, kina umri fulani ambao kitaishi. Allah hukiumba muda ukiwadia na hukiangamiza umri wake ukifikia mwisho. Yeye haumbi kitu kutokana na kutokuwepo tu kwa kitu hicho, lakini pia hukiumba kitu kingine kutokana na kingine, pole pole au ghafla, na kile cha mwisho kuumbwa kikija maishani, cha mwanzo husita kuishi.

Allahu taala alimuumba mwanaadamu kutokana na madutu sahali na roho. Mwanaadamu hakuwepo kabla. Wanyama, mimea, majini na malaika walikuwa wameumbwa kabla ya mwanaadamu huyo wa kwanza kabisa. Huyo mwanaadamu wa kwanza aliitwa Adam “alahis-salaam”, amani ya Allah iwe juu yake. Kutokana naye, Allahu taala alimuumba mwanamke aitwae Hawa. Kutokana na hawa wawili, watu walizaana. Tunaona kwamba vitu vyote vilivyo na uhai na visivyokuwa na uhai sawia, vinabadilika. Kile ambacho ni cha milele hakipaswi kubadilika. Kuna mabadiliko miongoni mwa maumbile, hali na madutu. Tena mifanyiko ya kikemikali hubadilisha dhati na hali yake. Madutu yanasita kuishi huku mengine yakija kwenye uhai. Kwa upande mwingine, katika matukio ya kinyuklia, hata elementi/ vipashio vya kinyuklia hubadilika na kuwa nishati. Mchakato huu wa vitu kujitokeza vikitokana na vingine hauwezi kuwa wa azali usiokuwa na mwanzo. Lazima vilitokana na madutu ya mwanzo kabisa yaliyoumbwa na hayakuweko kabla. Kwani azali ina maana ya kutokuwa na mwanzo.

Maadui wa Uislamu wanajifanya wanasayansi na wanasema kwamba wanaadamu waliumbwa kutokana na kima. Wanasema kwamba daktari wa Muingereza anayeitwa Darwin alisema hivyo. (Ni waongo). Darwin Charles [1809-82] hakusema hivyo. Alianzisha harakati za jinsi ya kuendelea kuishi miongoni mwa viumbe hai. Katika kitabu chake kiitwacho **(The Origin of Species)** aliandika kwamba viumbe hai viliendeleza tabia zilizoendana sana na mazingira yao na kwa kufanya hivyo vikapitia mabadiliko muhimu. Hakusema kwamba atomi moja hubadilika na kuwa nyingine. Katika kikao ambacho Jumuia ya Uingereza ya kuendeleza Sayansi iliandaa huko Salford mwaka wa 1980, Prof. John Durant wa Chuo cha Swansea alisema kwamba mtazamo wa Darwin wa kimageuzi kuhusu asili ya mwanaadamu umegeuzwa katika kisasili/uongo/ubunifu wa kisasa, jambo ambalo lina madhara kwa sayansi na maendeleo ya kijamii, kiasi kwamba uongo wa kisekula (elimu ya sekula) kuhusu mageuzi ulikuwa na

taathira kubwa kwa utafiti wa kisayansi, ambazo zilisababisha upotoshaji, mgogoro usiohitajika na matumizi mabaya sana ya sayansi. Alihitimisha kwamba nadharia ya Darwin sasa imeenda mbali sana na hali ya kuwa imeacha nyuma marundo ya mawazo haribifu na danganyifu. Matamko haya aliyoyatoa Prof. Durant kumuhusu mwenzake ni miongoni mwa majibu yenye kuvutia sana yaliyotolewa kwa wana Darwin kwa jina la sayansi. Sababu kuu iliyojificha nyuma ya jitihada zilizopo za kujaza watu shauku na nadharia hii ya kimageuzi katika ngazi fulani ya kitamaduni ni itikadi kengeushi. Hazihimili matilaba ya kisayansi. Ile iitwayo nadharia inatumika kama chombo cha kuingizia falsafa ya kiyakinifu. Hoja kwamba mwanaadamu alitokana na kima haina msingi katika elimu na ni mbali sana na sayansi. Wala si hoja ya Darwin. Inajikita katika uongo wa maadui wajinga wa Uislamu ambao hawana habari juu ya elimu na sayansi. Mtu mwenye elimu au mwanasayansi hawezi kutoa matamko ya kijinga na dhihaka kama hayo. Kama mtu aliyehitimu chuoni ataishi maisha ya upotovu na kusahau yale aliyosoma shuleni badala ya kujiendeleza na masomo yake katika taaluma aliyozamia, kamwe hawezi kuwa mtu mwenye elimu au mwanasayansi. Baya zaidi ni kuchukuwa kwake kinga ya Uislamu na kujaribu kusambaza maneno yake na maandishi ya uongo kwa jina la elimu na sayansi na hivyo yakaishia kuwa kama msingi danganyifu yenye madhara kwa jamii. Katika hali hiyo diploma yake, cheo na wadhifa wake vitakuwa mitego ya hadaa ya kuwawinda vijana. Wanasayansi walaghai wanaosambaza uongo wao wenyewe na kashfa kwa jina la elimu na sayansi wanajulikana kama **(Walaghai wa sayansi)**.

Allahu taala anachotaka ni watu kuishi kwa raha na amani duniani na wapate kujivunia huko akhera. Kwa sababu hii, anawaamrisha kufanya mambo yenye faida yatakayowapelekea kupata raha na anawakataza yale yenye madhara yatakayosababisha maangamizi. Endapo mtu atatenda, bila kujali ni mshikadini au si mshikadini, muumini au sio muumini, aliyeshikamana na sheria za kiislamu, yaani maamrisho na makatazo ya Allahu taala, hali ya kuwa anafanya hivyo kwa kujua au kutojua, kiwango cha raha na amani watakachopata katika maisha ya dunia hii yatakuwa sambamba na kiwango cha utiifu wao kwa mfumo huo wa sheria. Ni sawa na kaida isemayo kwamba (yeyote anayetumia matibabu muafaka atapona maradhi). Mafanikio ya hivi sasa wanayojivunia wasoshika dini ya Allah mengi ni kwa sababu ya kutenda matendo yao kwa namna ambayo imetokea kuafikiana na Quran tukufu. Hata hivyo, kujivunia kwa milele kwa kutii Quran tukufu, huwezekana tu iwapo utiifu huo utatekelezwa na muumini kwa kujua.

Sheria ya kwanza ya Allahu taala ni kuwa na **(Imani)**. **Ukafiri** ni jambo aliloliharamisha kabla ya uovu wowote mwingine. Imani maana yake ni (kuamini ukweli kwamba Allahu taala ni mmoja asie na mshirika wala mfano na Muhammad rehma na amani ziwe juu yake ni mtume "sallallahu alayhi wasallam" wa Allahu taala wa mwisho). Allahu taala alimpa yeye maamrisho yake kupitia ufunuo. Yaani aliteremsha kwake sheria zake za kiislamu kupitia malaika, naye akazifafanua zote kwa watu. Neno lililoteremshwa kupitia kwa malaika linajulikana kama **(Quran)** tukufu. Kitabu ambacho kina matini yote ya Quran iliyoandikwa inajulikana kama **(mas-hafu)** (nakala ya Quran tukufu). Quran tukufu si matamko ya mtu binafsi aliyoyatoa Mtume "sallallahu alayhi wasallam" Muhammad "sallallahu alayhi wasallam", bali ni neno la Allahu taala. Hakuna mwanaadamu anayeweza kutoa tamko hata moja ambalo linafanana na aya zake katika ukamilifu. Sheria zilizofundishwa katika Quran tukufu, kwa pamoja zinajulikana kama **(Uislamu)**. Mtu mwenye kuziamini kwa moyo wake anajulikana kama **(Muumini)** na **(Muislamu)**. Kuchukia hata sheria moja tu ni **(Ukafiri)**. Kuamini kufufuliwa baada ya kifo, uwepo wa majini na malaika, ukweli kwamba Adam "alaihis-salaam" ni baba wa binaadamu wote na ni mtume "sallallahu alayhi wasallam" wa kwanza kabisa, ni kazi ya moyo tu. Mambo haya ya ukweli yanaitwa mafundisho ya **(Imani)** au **(Akida)**. Ama kuhusu maamrisho ambayo yanapaswa kutekelezwa na makatazo ambayo yanapaswa kuepukana nayo kwa matendo na kwa moyo, ambayo ni lazima kuyaamini na kuyatenda au kuyaacha hayo huitwa mafundisho ya sheria za Uislamu. Kuyaamini ni miongoni mwa vitendo vya imani pia. Kuyaweka vitendoni au kuyaacha ni **(Ibada)**. Ni kitendo cha ibada kutekeleza sheria za kiislamu kwa kuleta nia kwanza. Maamrisho na makatazo ya Allahu taala yanaitwa sheria za Kiislamu ama sheria za kiibada/kiungu. Maamrisho yanaitwa **(Fardh)** na makatazo yanaitwa **(Haram)**. Ni dhahiri kwamba mtu anayekana na kuchukia hata kitendo kimoja kati ya vitendo hivyo huwa **(Kafiri)** [adui wa Allahu taala]. Mtu anayeamini sheria hizo lakini akawa na udhaifu katika kuzitilia maanani hawi kafiri bali ni muislamu ambaye ni **(Fasik)** (mtenda madhambi). Muumini ambaye huyaamini mafundisho ya Uislamu na akayatekeleza kwa uwezo wake wote huitwa muislamu mwema (**Muslimun salih**). Muislamu anayetii Uislamu akampenda murshid (muongozaji) kwa ajili ya kupata huruma na mapenzi ya Allahu taala huitwa mtu mwema. Muislamu ambaye ameshapata huruma ya Allah na mapenzi yake huitwa **(Arif)** au **(Walii)**. Walii ambaye hutoa huduma kama njia mojawapo ya wengine kupata mapenzi ya Allah anaitwa **(Murshid)** (muongozaji). Watu hawa wote

wateule kwa pamoja huitwa watu wa kweli. Wote ni watu wema. Muumini mwema kamwe hataingia motoni. Kafiri (adui wa Allahu taala) bila shaka ataingia motoni. Hatatoka motoni kamwe na atapewa adhabu zisizo na kikomo. Endapo kafiri ataamini (atakuwa muumini), madhambi yake yataghufiriwa mara moja. Endapo muasi atatubia kisha aanze kutenda vitendo vya ibada, ima hataingia motoni kamwe, na ataenda peponi moja kwa moja kwa kupata maombezi au pasi na njia yoyote katikati, au atachomwa motoni kadri anavyostahiki kutokana na madhambi yake na aingie peponi baadae.

Quran tukufu ilipoteremshwa, sarufi yake inalingana na lugha ya Kiarabu iliyokuwa ikizungumzwa na watu wa zama hizo, na katika umbo la kishairi. Yaani ina mizani kama ushairi. Imesheheni Kiarabu ambacho ni kigumu kutambulika. Imeboreka katika sayansi za lugha ya Kiarabu na balagha kama vile elimu ya al-badi'i (taaluma inayochunguza ujumi wa lugha), elimu ya albayani na elimu ya al ma'ani. Kwa hiyo, ni ngumu kuielewa, mtu asiyekuwa na asili ya Kiarabu hawezi kuelewa vyema Quran tukufu, hata kama ni mjuzi wa Kiarabu. Hata wale waliokuwa na uasili huo hawakuweza kuifahamu, kwa hiyo bwana wetu Mtume "sallallahu alayhi wasallam" alieneemeshwa, alieleza sehemu kubwa (ya Quran). Ufafanuzi wa mtume "sallallahu alayhi wasallam" wa Quran tukufu unaitwa **(Hadithi sharif)**. Masahaba wa Mtume "sallallahu alayhi wasallam" radhi za Allahu taala ziwe juu yao wote, walifikisha mafundisho waliyoyasikia kutoka kwa Mtume "sallallahu alayhi wasallam" [(rehma na amani ziwe juu yake)] kwa vizazi ambavyo vilikuwa vidogo kabisa. Katika kipindi fulani nyoyo za watu ziliingiwa kiza kiasi kwamba baadhi ya waislamu wapya walijaribu kuitafsiri Quran tukufu kwa maoni na mawazo yao finyu, na kwa kufanya hivyo wakatoa maana zisizokubaliana na ufafanuzi wa bwana Mtume "sallallahu alayhi wasallam". Kutokana na uchochezi wa nyufa uliofanywa na maadui wa Uislamu, palizuka madhehebu sabini na mbili ya uongo. Waislamu wanaofuata madhehebu hayo wanaitwa **(Wanabid'a)** au **(Waliopotea)**. Kwa yakini makundi hayo yote sabini na mbili ya bid'a yataenda motoni lakini kwa vile ni waislamu, hawataishi motoni milele, hatimae wataingia peponi. Kama imani anayoishikilia mtu itatofautiana na ile iliyoko kwenye mafundisho ya Quran tukufu na hadithi tukufu, mtu huyo huwa hana imani na huitwa **(Mulhid)** (anae pinga kuwepo kwa mungu). Mulhid anajidhani kwamba ni muislamu.

Wanazuoni wa Kiislamu Allah awarehemu waliojifunza mafundisho ya akida, yaani mihimili ya imani kwa usahihi kutoka kwa sahaba

watukufu "radhi za Allahu taala" ziwe juu yao wote na wakayaandika mafundisho hayo yaliyo sahihi katika vitabu wanajulikana kama **(Ahlu sunna)**. Wao ni wanazuoni waliofikia kiwango cha ijtihad katika mojawapo ya madhehebu manne. Wanazuoni hawa walishikilia imani kama walivyojifunza kutoka kwa masahaba watukufu wala hawakujaribu kuelewa maana ya Quran tukufu kulingana na maoni na mitazamo yao binafsi. Walisambaza mafundisho ya ukweli waliyojifunza kutoka kwa Mtume "sallallahu alayhi wasallam" wetu, badala ya kufuata uelewa wao binafsi. Dola la Uthman lilikuwa dola la kiislamu na lilishikilia imani ya kisunni.

Kama inavyoeleweka kutokana na yaliyoandikwa mpaka sasa, na yaliyoandikwa kwenye vitabu vingi vyenye thamani, ili kusalimika kutokana na maafa ya dunia hii na akhera, na kuishi maisha yenye raha na furaha, ni muhimu kushikilia imani iliyofundishwa na wanazuoni wa ahlu sunna na watu walioongoka, yaani kujifunza mihimili yake na kuiamini yote. Mtu asiyeshikamana na imani ya kisunni na ya walioongoka huitwa **(Mwanabid'a)**, yaani muislamu muasi au kafiri. Wajibu wa pili wa muislamu mwenye imani ya kweli na akida sahihi ni kuwa salih, yaani kufikia huruma na mapenzi ya Allahu taala. Kwa kuzingatia lengo hilo, lazima mtu apate mafundisho ya Uislamu yanayohusu ni nini ambacho kinapaswa kufanyika na yale yanayopaswa kuachwa, kimwili na kiroho na aishi kulingana na muongozo huo. Kwa maneno mengine mtu anapaswa kutekeleza vitendo vya ibada. Wanazuoni wa ahlu sunna na watu walioongoka walielezea vitendo vya ibada kwa namna nne tofauti. Hali hiyo basi ilipelekea kujitokeza kwa **madhehebu** manne yanayotambulika katika Uislamu. Kwa vile masuala ambayo wao wanahitilafiana ni madogo na si muhimu sana, wanahurumiana na kuheshimiana madamu mihimili inayowaunganisha ni sawa. Kila muislamu anapaswa kutekeleza vitendo vyake vya ibada kwa kutii moja wapo ya madhehebu haya manne na ya watu walioongoka. Kusema kwamba mtu asiyeshikamana na madhehebu yoyote kati ya madhehebu hayo manne na ya watu walioongoka atakuwa ameacha njia pekee iliyosahihi ya ahlu sunna na ya watu walioongoka ni ukweli usiopingika ambao umeandikwa pia katika sura iitwayo Dhabaih, sherehe ya Ahmad bin Muhammad bin Ismail Tahtawi [aliyefariki dunia mwaka wa 1231 (1815 A. D.) Allahu taala amrehemu] ya kitabu cha Alauddin Haskafi (1021-1088 [1677 A. D.]) kiitwacho **(Durr-Ul-Mukhtar)**.

Kafiri akisema "Nimesilimu", ni lazima kumuamini hata kama ni mateka wa vita au amesema hivyo wakati wa amani. Lakini anapaswa

kujifunza nguzo **za sita imani** na kuziamini haraka iwezekanavyo. Baadaye atajifunza na kutekeleza maamrisho ya Uislamu yaitwayo fardh na kuepukana na makatazo yake yajulikanayo kama haram kila inapomuajibikia na endapo atapata fursa ya kufanya hivyo. Wasipojifunza mambo hayo, au wakidharau na kupuuza hata jambo moja kati ya mambo hayo baada ya kuwa wamejifunza, watakuwa wamepuuza dini ya Allahu taala na watapoteza imani yao. Watu wanaopoteza imani yao kwa namna hii wanaitwa **(Murtad)** (waasi). Murtadi ambao wanajigamba kuwa washikadini lakini wakawa wanawapotosha waislamu wanajulikana kama **(Zindik)**. Hatupaswi kuwaamini mazindik wala uongo wao. Kama ilivyoandikwa katika ukurasa wa mia moja na kumi na sita wa kitabu kiitwacho **(Siyar-i-kabir)** cha Kituruki, na pia katika sehemu ya mwisho ya kitabu kiitwacho **(Dur-ul-mukhtar)** sura inayohusu ndoa ya kafiri, mtu akibaleghe pasi na kusilimu au kutambua katika moyo wake kwamba ni muislamu, ikiwa kwa sababu ni mbumbumbu haujui Uislamu na sio kutokana na kuzama kwake katika matamanio ya dunia, basi atahukumiwa kuwa murtad (mkanaji dini/muasi). Imeandikwa katika sehemu ya mwisho ya (Durr-ul-Mukhtar) sura inayohusu ndoa ya kafiri kwamba msichana muislamu aliyeolewa katika ndoa ya kiislamu akibaleghe bila kuujua Uislamu, ndoa yake huwa batili. [Kwa maneno mengine yeye huwa murtadi]. Itabidi afunzwe sifa za Allahu taala. Itabidi arudie/akaririr yale anayosikia na aseme, (Naziamini). Ibn Abidin "rahmatullahi alaih" anafafanua suala hili kama ifuatavyo, "Msichana akiwa mdogo (yaani akiwa haja baleghe), anakuwa muislamu, kwa vile dini yake hutambulika kutokana na ile ya wazazi wake. Akibaleghe hatategemea tena dini ya wazazi wake. Akibaleghe akatoka kwenye Uislam hali ya kuwa mbumbumbu katika Uislamu, atakuwa murtadi. Mtu asiyeamini nguzo za Uislamu pamoja na kwamba amezisikia, akitamka tu neno la tawhidi, yaani iwapo atasema, **(La ilaha illallah Muhammadun Rasulullah)**, kitendo hicho hakitamfanya kuwa muislamu. Mtu anayeamini nguzo sita zilizoelezewa katika tamko, (Aamantu billahi…) na anayesema, (Nimekubali kufuata maamrisho na kuacha makatazo ya Allahu taala,) huwa muislamu. Kwa hiyo, Waislamu wote wanapaswa kuhakikisha kwamba watoto wao wanahifadhi nguzo sita za imani zilizotajwa katika tamko, (Aamantu billahi wa malaaikatihi (na malaika wake) wa kutubihi (na vitabu vyake) wa rusulihi (na mitume "sallallahu alayhi wasallam" wake) wal- yaumil akhiri (na siku ya mwisho) wa bil- qadari khairihi wa sharrihi minallahi taala (kheri na shari zinatokana na Allahu taala) wal-baathu baadal mauti haqqun (na kufufuliwa baada ya kufa ni haki) (Ash-hadu an La ilaaha illallah wa ash-

hadu-anna Muhammadan ‘abduhu wa rasuuluh‘.) (Na nashahadia kwamba hakuna mola anayepaswa kuabudiwa kwa haki isipokuwa yeye Allah taala na Mtume “sallallahu alayhi wasallam” Muhammad rehma na salamu zimshukie juu yake ni mja wake na mtume “sallallahu alayhi wasallam” wake) na ajifundishe maana yake sawa sawa. Mtoto asipoamini nguzo hizi au mojawapo ya maamrisho na makatazo ya Allahu taala na asiposema anaziamini, atakuwa murtadi, na siyo muislamu, akibaleghe.) Maelezo kamili kuhusu nguzo hizi sita hupatikana katika kitabu kiitwacho **(Imani na Uislam** (mojawapo ya machapisho ya Hakikat Kitabevi katika maktaba ya Istanbul). Kila muislamu anahimizwa kukisoma kitabu hicho, yeye na watoto wake, ili kuimarisha imani, na pia wajitahidi kadri ya uwezo wao kuwahimiza marafiki zao kukisoma. Ni muhimu kuchukua tahadhari ili watoto wetu wasikuzwe wakiwa murtadi (wasikulie katika hali ya uasi/kumkana Allah). Katika hatua za kwanza za utoto, tunapaswa kuwafunza imani, Uislamu, kutawadha, kuoga na sala. Kazi muhimu ya wazazi ni kuwalea/kuwakuza watoto wetu kama Waislamu (juu ya msingi wa Uislamu).

Imetajwa katika kitabu kiitwacho **(Durar wa Ghurar)** kwamba (Mwanaume anayeritadi anapaswa kuambiwa asilimu). Lazima aachane na shaka zake. Akiomba apewe muda wa kufikiria, atawekwa jela kwa siku tatu. Akitubia (yaani akitubu juu ya dhambi zake kubwa akamuomba Allah msamaha), huku akimuahidi kuwa kamwe hatatenda tena dhambi hiyo kubwa, toba yake itakubaliwa. Asipotubia, basi atauliwa na hakimu wa kiislamu. Mwanamke anayeritadi hatauwawa. Atatiwa mbaroni na kuwekwa gerezani mpaka atakaposilimu. Akitorokea katika nchi ya vita (iliyotangaza vita dhidi ya nchi ya kiislamu), madhali yumo katika nchi hiyo, hatakuwa jariya (mtumwa). Akichukuliwa mateka atakuwa jariya (mtumwa). Akisharitadi ndoa yake itabatilika. Mali yake yote itatoka kwenye milki yake (yaani haitakuwa tena milki yake). Akisilimu tena itakuwa milki yake. (Mwanamke) akifariki dunia au akitorokea katika darul harb nchi ya vita [au akiritadi akiwa katika nchi ya vita], mali yake itakuwa turathi ya warithi wake. [Kama hana warithi, mali hiyo itarithiwa na watu wanaostahiki kupewa kitu kutoka kwenye mfuko wa baitul maal]. Murtadi hairithi mali ya murtadi mwingine. Mali inayomilikiwa na murtadi (mwanamume au mwanamke) haitakuwa milki yake. Itakuwa milki (fey) ya Waislamu. (Neno fey limetafsiriwa katika sura ambayo kichwa chake ni Ndoa ya makafiri na imeambatanishwa kwenye sura ya kumi na tano ya kitabu kijulikanacho kama **(Endless Bliss)**. Vitendo

vyake vyote vya kijamii kama vile kununua na kuuza, mikataba ya kupangisha, na sadaka, vitakuwa batili. (Tafadhali tazama sura ya thelathini na moja ya Endless Bliss kwa maelezo ya (batil)). Itarejea katika hali yake ya kwanza na kuwa sahihi ikiwa atakuwa Muislamu tena. Hatatakiwa kufanya kadhaa kwa vitendo vyake vya ibada vilivyotangulia, isipokuwa kitendo cha hija, ambayo atapaswa kuitekeleza upya. Vitendo vitatu vya kwanza vya ibada ambavyo muumini mpya anapaswa kujifunza ni namna ya kutawadha, kuoga na kusali.

Nguzo sita za imani ni, kuamini kwamba Allahu taala yupo na ni mmoja na kuamini sifa zake, kuamini malaika, mitume "sallallahu alayhi wasallam", vitabu vilivyoteremshwa kutoka mbinguni, matukio yatakayo tokea Akhera, qadhaa na qadar. Baadaye, tutafafanua kila mojawapo ya nguzo hizo.

Kwa ufupi, lazima tutekeleze maamrisho ya Allahu taala na tuepukane na makatazo yake kiroho na kimwili na nyoyo zetu lazima ziwe katika tahadhari ili zisije zikazama katika mghafala (usahaulifu, ujinga, uvivu). Moyo wa mtu usipokuwa chonjo (yaani asipotambua uwepo na ukubwa wa Allahu taala na ladha ya fikra za baraka katika mbingu na hisia kali za adhabu ya moto wa jahannam), itauwia vigumu mwili wa mtu huyo kushikamana na Uislamu. Wanafiq´hi hutoa fat´wa kadhaa wa kadhaa (yaani majibu ya wanazuoni wa Kiislamu ambao ndio wenye mamlaka juu ya kujibu maswali yanayohusu namna ya kutekeleza vitendo vya ibada). Hunakiliwa kwa waja wa Allahu taala ili ziwe rahisi kutekelezeka. Ili watu washikamane na Uislamu kwa hima, wepesi na kuridhika, kuna haja ya kuwa na nyoyo safi. Hata hivyo, ikiwa mtu atazingatia tu usafi wa moyo na uzuri wa tabia ilhali anapiga kikumbo utiifu wa sheria za kiislamu, basi mtu huyo ni **(Mulhid)**. Mafanikio ya kimaajabu ya watu kama hao [kama vile kutoa utabiri wa yale yasiyojulikana na kuwaponya wagonjwa kwa kuwapulizia] yanachukuliwa kama **(Istidraj)** (kupewa muda mtu aendelee kufanya madhambi yake ili kuzama katika dimbwi la maasi) na yatawakokota wenyewe pamoja na wale wanaopendezwa nayo hadi motoni. Dalili ya moyo ulio msafi na nafsi tulivu (tiifu) ni kushikamana na maamrisho na kuachana na makatazo ya Allah na kuwa mtu wa Uislamu kwa hiyari. Kujigamba kwa watu wasioelekeza hisia na miili yao kwa Uislamu ni maneno matupu (yasiyokua na mashiko). Kwa kusema hivyo, wanajidanganya na kuwadanganya watu waliowazunguka.]

# SIFA ZA IMANI

Wanazuoni wanasema kwamba imani ina sifa sita.

**AAMANTU BILLAHI**: Naamini kwamba Allahu taala yupo na ni mmoja.

Hana mshirika wala nadhwir. (Hana mshirika wala anayemfanana).

Yeye ni munazzah (yuko huru, ametakasika) kutokana na makan (mahali). Hayuko katika mahali mahsusi.

Yeye ni muttasif (anasifika) na sifa zake za ukamilifu (kamal), yuko mbali na sifa za upungufu.

Yeye hana sifa hizo.

Sifa za ukamilifu zipo kwenye dhati yake na sifa za upungufu zipo kwetu sisi wanaadamu.

Sifa za upungufu tulizo nazo ni mapungufu kama vile kuwa na mikono au miguu au macho, ugonjwa na siha, kula na kunywa, na mengine mengi kama hayo.

Sifa alizonazo Allahu taala ni za ukamilifu kama vile kuumba kwa ardhi na mbingu na viumbe wote wapigao mbizi, waishio angani, majini, ardhini na chini ya ardhi, kuwahifadhi wakati wote viumbe wengi tunao watambua baadhi yao na wengine wengi tusiowatambua kutokana na uwezo wa mwanaadamu uliowekewa mipaka, riziki yake kwa viumbe hawa wote (chakula, kujikimu), na sifa zake nyingine za ukamilifu. Yeye ni qadir-il-mutaq (Mwenye nguvu). Kila kiumbe ni zao linalotokana na sifa za ukamilifu wa Allahu taala.

Kuna sifa ishirini na mbili zinazomhusu Allahu taala na ni wajibu kwetu kuzijua. Aidha, kuna sifa nyingine ishirini na mbili ambazo ni muhali (haifikiriki, haiyumkiniki kwake yeye kusifika nazo).

Wajibu maana yake ni lazima. Sifa za aina hii anazo Allahu taala. Allahu taala hana sifa zilizo muhali. Muhali ni kinyume cha wajibu. Maana yake ni (Haiwezekani kuwepo).

Kuna sifa moja inayomhusu Allahu taala ijulikanayo kama sifat-i-nafsiyya na ambayo ni wajibu juu yetu kuijua, **(Wujuud)** ambayo ina maana ya (kuwepo).

Ushahidi wa kuthibitisha kwamba Allahu taala yupo ni kauli tukufu isemayo **(Innani ana Allahu)**. Ushahidi wa kuthibitisha kiakili ni kwamba bila shaka muumbaji yupo aliyeumba viumbe hawa wote. Ni muhali kwake yeye kutokuwepo.

Sifat-i-nafsiyya ina maana kwamba kwa dhati pasi na yeye ni jambo ambalo haliwezi kutambulika wala kufikirika.

# SIFAT-I-DHATIYYA

Kuna sifa tano zinazohusika na Allahu taala zinazorejelewa kama sifat-i-dhatiyya na ambazo ni wajibu juu yetu kuzijua, zinajulikana pia kama **(Sifa za Uluhiyya)** (sifa za Uungu).

1- **Qidam,** ambayo inamaanisha kuwa uwepo wa Allahu taala hauna mwanzo.

2- **Baqaa**, humaanisha kuwa uwepo wa Allahu taala hauna mwisho. Hurejewa pia kama wajibul wujuud. Ushahidi wake kutokana na Quran tukufu ni aya ya tatu ya Suratul hadyd. Ushahidi wake wa kiakili ni kuwa uwepo wake ungalikuwa na mwanzo au mwisho angalikuwa asie na uwezo na angekuwa mwenye upungufu. Na asie na uwezo na mwenye upungufu asingeliweza kuwaumba viumbe wengine. Hivyo basi, ni muhali (haiwezekani uwepo wake kuwa na mwanzo au/na mwisho).

3- **Qiyam binafsihi,** ambayo humaanisha kuwa Allahu taala hana haja na yeyote katika dhati yake, sifa zake wala vitendo vyake. Ushahidi wake kutokana na Surat Muhammad, aya ya mwisho. Ushahidi wa kiakili ni kwamba asingelikuwa na sifa hizi asingelikuwa mwenye uwezo na angekuwa mwenye upungufu. Kutokuwa na uwezo au kuwa mwenye upungufu ni muhali kwake yeye Allahu taala.

4- **Mukhaalafat-un-lilhawaadith,** humaanisha kwamba Allahu taala hafanani na mtu yeyote katika dhati yake na pia katika sifa zake. Ushahidi wake kutokana na andiko takatifu ni tangazo lake Allahu taala katika aya ya kumi na moja ya Surat Ashuaraa. Ushahidi wake kiakili ni kwamba asingelikuwa na sifa hizi asingelikuwa na uwezo na angalikuwa na upungufu. Kutokuwa na uwezo na kuwa na upungufu ni muhali kwa Allahu taala.

**5- Wahdaaniyyat,** humaanisha kwamba Allahu taala hana mshirika wala amfananaye, sio katika dhati yake tu bali pia katika sifa na vitendo vyake. Ushahidi kutokana na Quran tukufu aya ya kwanza ya Suratul Ikhlas. Ushahidi wa kiakili ni ukweli kwamba angalikuwa na mshirika viumbe wote wasingalikuwepo. Kwani mmoja wao angalipenda kuumba kitu na wakati huo huo mwengine angelizuia kisiumbwe.

[Kwa mujibu wa wanazuoni wengi wa Kiislamu, **(Wujuud)**, yaani uwepo, ni sifa bainifu. Hivyo basi, kuna sifa sita chini ya dhana ya **(Sifaat-i-Dhaatiyya)**].

## SIFAAT-U-THUBUUTIYYA

Kuna sifa nane zinazomuhusu Allahu taala ambazo ni wajibu kwetu kuzijua na ambazo huangukia katika sifati dhati zijulikanazo kama Sifaat-u-thubuutiyya nazo ni Hayat (uhai), Ilmu (elimu (yaani ujuzi au maarifa ya uwelewa)), Sam'u (kusikia), Baswar(kuona), Iraad(kutaka), Qudrat (kukadiria au kupanga), Kalam (kuzungumza au kuongea), Takwin ( kuumba).

Maana ya sifa hizi ni kama ifuatavyo:

1- **Hayat,** humaanisha kwamba Allahu taala yupo hai. Ushahidi wake ni sehemu ya kwanza ya aya ya mia mbili hamsini na tano ya Suratul Baqarah. Ushahidi wa kiakili ni ukweli kwamba Allahu taala asingelikuwa hai, viumbe hawa wasingelikuwepo.

2- **Ilmu,** humaanisha kwamba Allahu taala ana ujuzi. Ushahidi wake ni aya ya ishirini na mbili ya Suratul Hashr. Ushahidi wa kiakili juu yake ni ukweli kwamba Allahu taala asingelikuwa na uwezo na ukamilifu kama hakuwa na ujuzi. Kutokuwa na uwezo na ukamilifu ni muhali kwa Allahu taala.

3- **Sam'u,** humaanisha kwamba Allahu taala anasikia. Ushahidi juu yake ni aya ya kwanza katika Suratul Israa.

4- **Baswar,** humaanisha kwamba Allahu taala anaona. Ushahidi wake pia ni aya ya kwanza ya Suratul Israa. Ushahidi wa kiakili ni kwamba kama Allahu taala angekuwa hana uwezo au ukamilifu asingekuwa na sifa ya kuona. Kutokuwa na uwezo na ukamilifu ni muhali kwa Allahu taala.

5- **Iraada,** humaanisha kwamba Allahu ni mwenye kutaka. Alitakalo huwa. Hakuna litokealo pasi na yeye kutaka liwe. Alitaka viumbe wawepo akawaumba. Ushahidi wake ni aya ya ishirini na saba ya Surat Ibrahim. Ushahidi wa kiakili ni kwamba asingekuwa na uwezo na ukamilifu kama hakuwa na sifa ya kutaka liwe liwalo. Kutokuwa na uwezo na ukamilifu ni muhali kwa Allahu taala.

6- **Qudrat,** humaanisha kwamba Allahu taala ni Mwenye nguvu. Ushahidi ni aya ya sitini na tano ya Surat Aali-Imran. Ushahidi wa kiakili ni kwamba asingekuwa mwenye nguvu basi asingekuwa mwenye uwezo na ukamilifu. Ni muhali kwa Allahu taala kutokuwa mwenye nguvu na ukamilifu.

7- **Kalam,** humaanisha kuwa Allahu taala ana uneni yaani kuongea. Ushahidi wake ni aya ya mia moja sitini na nne ya Suratun Nisaa. Ushahidi wa kiakili ni kwamba asingelikuwa na uneni yaani kuongea

asingelikuwa na uwezo na ukamilifu. Kutokuwa na uwezo na ukamilifu ni muhali kwa Allahu taala.

8- **Takwiin,** humaanisha kwamba Allahu taala ni Muumbaji, (yaani ana nguvu za kuumba, kwa hiyo anaumba). Yeye pekee ndiye anayeumba kutokana na hali ya kutokuwepo. Ushahidi ni aya ya sitini na mbili ya Surat Az-Zumar. Ushahidi wa kiakili ni kwamba yeye ameumba viumbe anuwai aina tofauti tofauti vyenye kustaajabisha ardhini na mbinguni, na ni muumbaji pekee wa viumbe wote. Ni kitendo cha ukafiri kusema (uumbaji) ukimrejelea yeyote ambaye si Allahu taala. Mwanaadamu hawezi kuumba kitu chochote.

Allahu taala ana sifaati maanawiyya (sifa zisizokuwa za mguso) ambazo ni wajibu juu yetu kuzijua nazo ni Hayyun, Aliimun, Samiiun, Baswiirun, Muriidun, Qaadirun, Mutakallimun, Mukawwinun.

Maana za sifa hizi ni:

1- **Hayyun,** Allahu taala yu hai.

2- **Samiiun,** Allahu taala anasikia na kusikia kwake ni kwa milele (sam'il qadiim).

3- **Baswiirun,** Allahu taala anaona.

4- **Muriidun,** Allahu taala anataka na kutaka kwake ni kwa milele (Iraadatil

qadiima).

5- **'Aliim,** Ana ujuzi wa milele unaorejelewa kama 'ilmil qadiim.

6- **Qadiirun,** Allahu taala ni mwenye nguvu na nguvu zake ni za milele (Qudratil qadiima).

7- **Mutakallimun,** Allahu taala ni mwenye kuzungumza na kuzungumza kwake ni kwa milele (Kalaamil qadiim).

8- **Mukawwinun,** Allahu taala ni Muumbaji na anaumba kila kitu.

Sifa ambazo ni muhali kwa Allahu taala ni kinyume cha zile zilizotajwa hapo awali.

**WA MALAAIKATIHI**: Na kuamini pia malaika wa Allahu taala. Allahu taala ana malaika kadha wa kadha. Aliwaumba kutokana na nuru. Ni wenye miili (ajsaam). Mwili (jism) uliotajwa katika muktadha huu si ule uliotajwa kwenye vitabu vya fizikia. Hawali wala hawanywi. Hawana jinsia. Huteremka na kupanda mbinguni. Hujitokeza katika sura mbalimbali. Hawamuasi Allahu taala hata kiasi cha kufumba na kufumbua jicho wala kutenda madhambi kama sisi. Miongoni mwakuna muqarrab na mitume "sallallahu alayhi wasallam".

**WAKUTUBIHI**: Na kuamini pia vitabu vya Allahu taala.

Allahu taala ana vitabu. Kuna vitabu mia moja na nne vilivyotajwa katika Quran tukufu. Mia moja kati yao ni vitabu vidogo vidogo. Vinajulikana kama (Suhuf). Vinne kati yao ni vitabu vikubwa. **Taurat** iliteremshwa kwa Nabii Musa "alaihis-salaam", **Zabuur** ikateremshwa kwa Nabii Daaud "alaihis-salaam", **Injiil** ikateremshwa kwa Nabii Issa "alaihis-salaam", na **Quran karim** kwa bwana wetu Mtume "sallallahu alayhi wasallam" Muhammad "sallallahu alayhi wasallam". Chapisho letu moja hutoa taarifa kamili kuhusu vitabu vinavyojulikana kama **(Taurati)** na **(Injiil)** ambavyo husomwa na mayahudi na wakristo wa siku hizi.

Kati ya suhufi mia moja, kumi ziliteremshwa kwa Adam "alaihis-salaam", hamsini kwa Seth "alaihis-salaam", thelathini kwa Idris "alaihis-salaam", na kumi kwa Ibrahim "alaihis-salaam". Suhufi zote ziliteremshwa na Jibriil "alaihis-salaam". Qur´an tukufu ni kitabu cha mwisho kati ya vitabu vilivyoteremshwa kutoka mbinguni. Kuteremshwa kwa Quran, kwa muda tofauti tofauti kulingana na matokeo na mahitaji kwa sura nzima na aya, kulichukuwa miaka ishirini na mitatu na sheria zake zitadumu hadi mwisho wa dunia. Imehifadhiwa kutokana na hali ya kutiwa mkono, kubadilishwa na kufanyiwa mageuzi na binadamu [kutokana na kubadilishwa na kunajisiwa na mwanaadamu].

**WA RUSULIHI**: Na kuamini pia mitume "sallallahu alayhi wasallam" wa Allahu taala.

Allahu taala ana mitume "sallallahu alayhi wasallam" (Amani iwe juu yao). Mitume "sallallahu alayhi wasallam" wote ni wanaadamu. Adam "alaihis-salaam" amani iwe juu yake ni mtume "sallallahu alayhi wasallam" wa kwanza na Muhammad rehma na amani iwe juu yake ni mtume "sallallahu alayhi wasallam" wa mwisho. Kati ya mitume "sallallahu alayhi wasallam" hawa wawili kuna mitume "sallallahu alayhi wasallam" wengine wengi waliokuja. Allahu taala ndie anayejua idadi yao.

Kuna sifa tano ambazo tunapaswa kuzijua kuhusu mitume "sallallahu alayhi wasallam" amani iwe juu yao. Nazo ni Swidiq (ukweli), Amana (uaminifu), Tabligh (ufikishaji), I'iswimat (kuhifadhiwa na kulindwa na kutofanya maasi) na Fatwana (uhodari wa akili ya vipawa vya juu).

1- **Swidiq,** Mitume "sallallahu alayhi wasallam" wote amani iwe juu yao ni waaminifu katika yale wayasemayo, Yote wanayosema ni ya ukweli.

2- **Amanat,** Ni waaminifu kwani hawavunji ahadi.

3- **Tabligh,** Wanayapokea na kuyafahamu maamrisho na makatazo ya Allahu taala yote na huyafikisha kwa wafuasi wao.

4- **I'iswimat,** Inamaanisha kwamba wameepukana na madhambi makubwa na madogo sawia. Hawafanyi madhambi. Mitume "sallallahu alayhi wasallam" amani iwe juu yao ni kundi pekee la watu ambao hawana madhambi. [Mashia wanadai kuwa kuna kundi jingine la watu ambao hawafanyi madhambi].

5- **Fatwaanat,** Inamaanisha kwamba mitume "sallallahu alayhi wasallam" wote amani iwe juu yao ni werevu kuliko watu wengine.

Kuna sifa tano ambazo zinafaa kwa mitume "sallallahu alayhi wasallam" kuwa nazo. Wanakula na kunywa, wanaugua maradhi na wanakufa, wanahama kutoka dunia hii na kuelekea katika dunia nyingine ambayo ni akhera, hawapendi sana dunia hii.

Kuna mitume "sallallahu alayhi wasallam" wapatao ishirini na nane ambao wametajwa katika Quran tukufu. Kuna kauli ya wanazuoni isemayo kwamba kuyajua majina yao ni jambo la lazima kwa kila mtu.

**Majina ya mitume** "sallallahu alayhi wasallam" Amani iwe juu yao.

Adam, Idris, Nuh, Shis (Seth), Hud, Swaleh, Lut, Ibrahim, Ismail, Is´haq, Yaqub, Yusuf, Shua'ib, Musa, Harun, Daud, Suleiman, Yunus, Ilyas, Alyasa, Dhul-kifl, Ayyub, Zakariya, Yahya, Issa Muhammad "sallallahu alayhi wasallam". Kuna kutofautiana kuhusu Uzair, Luqman na Dhulqarnain. Baadhi ya wanazuoni walisema kwamba watu hawa pamoja na Khidir pia walikuwa mitume, huku wengine wakisema kwamba walikuwa mawalii. Imeandikwa katika barua ya thelathini na sita toleo la pili la Maktuubaat-i-Ma'thuumiyya kwamba kuna kauli ya kisomi yenye kuridhisha isemayo kwamba Khidir amani iwe juu yake alikuwa mtume "sallallahu alayhi wasallam". Kama ilivyotajwa katika barua ya mia moja themanini na mbili, kujitokeza kwa Khidir kwa sura ya mwanaadamu, na kutenda matendo fulani fulani hakuoneshi kwamba yuko hai. Allahu taala aliruhusu roho yake pamoja na roho za mitume "sallallahu alayhi wasallam" wengi na mawalii kuonekana katika sura za wanaadamu. Kuwaona haina maana kwamba wako hai.

Kwa hiyo, unapaswa kusema Alhamdulillahi mimi ni kizazi cha Adam "alaihis-salaam" na ni miongoni mwa umma wa mtume "sallallahu alayhi wasallam" wa mwisho, Muhammad swala na salamu ziwe juu yake. Mawahabi wanakana kwamba Adam "alaihis-salaam" amani iwe juu yake alikuwa mtume "sallallahu alayhi wasallam". Kwa hiyo na kwa vile wanawaita waislamu washirikina, wao ni makafiri.

**WALYAUMUL AKHERA**: Aidha, naamini siku ya mwisho kwa vile Allahu taala katupa taarifa juu yake. Siku ya Qiyama inaanza wakati watu wanapofufuka kutoka makaburini mwao. Kuendelea hadi wanapoenda kwenye mahali pao ima peponi au motoni. Sote tutakufa halafu baadae tutafufuliwa. Pepo, moto na mizani na daraja la Siraat na hashr [mkusanyiko] na nashr [mtawanyiko kutoka kwenye mkusanyiko kuelekea peponi au motoni] na adhabu za kaburini na kuulizwa maswali na malaika wawili Munkar na Nakiir yote hayo ni ya ukweli. Bila shaka yatapitiwa.

**WABIL QADARI KHAIRIHI WA SHARRIHI MINALLAHI TAALA:** Nakuamini pia kwamba matukio yote yaliopita na yatakayo kuja mbeleni, mazuri na mabaya ni sawa, yaliyotokea na yatakayotokea kutokana na kudra ya Allahu taala, yaani yanalingana na ujuzi wake na maamuzi yake yaliyokwisha fanywa, na kutokana na kuyaumba kwake na kuyaamulia yatokee katika nyakati maalumu na kuyaandika kwake kwenye Lauhin-mahfudh. Hakuna hata chembe ya shaka moyoni mwangu.

**Ash-hadu an laa ilaaha illallah wa ash hadu anna Muhammadan abduhu wa rasuluhu.**

Nguzo za imani zinazoshikiliwa na makundi mengine sabini na mbili ni ya uongo na ni ya uzushi na wataenda motoni. Waislamu wanao wapenda masahaba watukufu [radhi za Allahu taala ziwe juu yao] wanajulikana kama **(Ahlu sunna)**.

Masahaba wote watukufu walikuwa wasomi na waislamu waadilifu. Walikuwa na usuhuba na mtume “sallallahu alayhi wasallam” (yaani swala na salamu ziwe juu yake) na walimsaidia. Hata sahaba aliyepata usuhuba ule (wenye thamani) ulio mdogo zaidi humshinda walii ambae ni wa kiwango cha juu zaidi miongoni mwa mawalii ambao si sahaba. Hali aliyekuwamo sahaba mmoja na tawajjuh za kipenzi cha Allahu taala rehma na amani ziwe juu yake na ukamilifu ulofikiwa chini ya athari za mitazamo yake na pumzi zake zenye baraka havikumuangukia mtu yeyote asiyepata ukuruba na baraka zake. Masahaba wote watukufu walinusuriwa kutokana na matamanio ya nafsi zao punde tu baada ya kupata usuhuba wa mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allahu taala. Tumeamrishwa kuwapenda wote. Imeandikwa katika kurasa za mwanzo za maelezo juu ya kitabu kijulikanacho kama **(Shir’atul islam)** kwamba unapozungumza kuhusu masahaba watukufu [Radhi za Allahu taala ziwe juu yao] unapaswa kufanya hivyo kwa uangalifu kadri inavyowezekana. Usimkashifu yeyote kati yao. Kuhusu makundi sabini na mbili yaliyopotea huku baadhi yao yakienda

mbali sana katika upotofu, baadhi yalizingatia uaminifu wao, ilhali mengine yakiangukia upande wa falsafa na wanafalsafa wa Kigiriki. Hivyo, walifanya mambo yasiyokuwa ya kiislamu na yanayopingana na Uislamu. Walikumbatia bid'a (yaani imani na matendo yasiyohusiana kwa vyovyote vile na Uislamu na ambayo yamezuliwa kwa jina la imani za kiislamu na matendo yake). Waliipa kisogo Sunna. Watu waliochukia vigogo wa kiislamu kama vile Abu Bakr as-Siddiq na Umar bin khattab "radiyallahu anhüma" ambao ni wa daraja la juu zaidi miongoni mwa maswahaba watukufu kwa mujibu wa ijmaa (makubaliano ya wanazuoni wa Kiislamu), walijitokeza. Kusema kweli, hisia za chuki walizoonyesha baadhi yao kuhusu maswahaba zilimuhusu pia Mtume "sallallahu alayhi wasallam" rehma na salamu za Allahu taala ziwe juu yake. Palijitokeza watu waliokana ukweli kwamba bwana wetu, Mtume "sallallahu alayhi wasallam", alikuwa amechukuliwa mbinguni kimwili na kiroho katika usiku unaojulikana kama Mi'raj [ambao umeelezewa kwa tafsiri (upana) katika sura ya sitini ya sehemu ya tatu ya Endless Bliss].

Inasikitisha kuwaona baadhi ya Wanazuoni wa Kiislamu wa kisasa wakihudumu kama wazungumzaji wa kundi linalojulikana kama **(Ismaa'iliyya)**, kundi ambalo ni hatari zaidi kati ya makundi sabini na mbili (ya uzushi). Wanakazana kuyapotosha na kuyapa sumu marika ya vijana kwa kuandika na kueneza uongo kama kusema kwamba wahenga wa bwana wetu Mtume "sallallahu alayhi wasallam" wa kiume na wa kike waliobarikiwa hawakuwa waumini na kwamba bwana wetu Mtume "sallallahu alayhi wasallam" ziwe juu yake alikuwa akitoa wanyama kama sadaka kwa masanamu kabla hajateuliwa kama mtume "sallallahu alayhi wasallam" na wananukuu baadhi ya vitabu vya Kishi'a kuthibitishia upotovu wao. Inaonekana wazi kwamba lengo la watu waoga kama hawa ni kujaribu kuionea dini ya kiislamu, kuwapokonya vijana imani na kuwaingiza kwenye ukafiri. Hadithi sharifu inasema kwamba **(yeyote anayetafsiri Quran kulingana na fikra zake atakuwa kafiri.)** Wanazuoni wa kiislamu walikuwa na adabu (walipambwa na tabia njema kama ilivyopendekezwa na Uislamu). Walikuwa wakiongea na kuandika kwa uangalifu. Huwa makini sana ili wasije wakasema maneno ya uongo. Kuongea pasi na kuchuja, kwa mfano kujaribu kuwasilisha maoni ya mtu binafsi ambayo ni ya uongo na upotovu kwa jina la Uislamu badala ya kutoa taarifa sahihi kutoka kwenye misingi ya sheria, yaani misingi mikuu minne ya elimu ya kiislamu, si jambo linalofaa kufanywa na muislam wa kawaida, ukiachilia mbali mwanazuoni wa kiislamu. Tunapaswa kuchukulia maneno na maandishi haribifu na yenye uchafu ya watu wajinga kama

hao ambao hawajatambua umuhimu wa mtume “sallallahu alayhi wasallam” wetu rehma na salamu ziwe juu yake, kama sumu (inayoweza kumuua mtu papo hapo).

Mshairi wa kiajemi ansema:

***Natetemeka kama jani la mti ulioota karibu na maji wanaposhambulia imani yangu.***

Allahu taala aongeze katika nyoyo zetu upendo wa wapendwa wake. Atunusuru kutokana na kuanguka katika fitna ya kuwapenda maadui zake. Dalili ya uwepo wa imani katika moyo ni kuwapenda wale awapendao Allahu taala na kuwachukia maadui zake. Katika utekelezaji wa amali yoyote ya ibada kwa upande wa kisuni kuna madhehebu manne.

Nayo ni madhehebu ya Imam mkuu Abuu Hanifa, Imam Shafi’i, Imam Malik, na Imam Ahmad bin Hanbal “rahmatullahi alaih” ziwe juu yao.

Inafaa kushikamana na moja wapo ya madhehebu haya manne ili uwe sunni. Madhehebu ya maimamu hawa wanne yote ni ya ukweli na sahihi. Yote ni miongoni mwa madhehebu ya ahlu sunna.

Waislamu wanaomfuata Abuu **Hanifa** madhehebu yao wanajulikana kama wahanafi. Tunasema Madhehebu ya Imam Adham ni swawab na sahihi. Kuna uwezekano pia kwamba yanaweza kutokuwa sahihi. Madhehebu mengine matatu si sahihi. Kuna uwezekano pia kwamba yanaweza kuwa sahihi.

Ili imani ya mtu kudumu, inategemea masharti sita:

1- Tunapaswa kuamini yaliyo ya ghaib. Tunaamini mambo ya ghaib (yasiyojulikana ama yasiyo onekana), ambayo si dhahiri. Kwani hatujawahi kumuona Allahu taala kwa macho yetu. Hata hivyo, tumeamini kama kwamba tumemuona. Hatujawahi kutilia shaka jambo hilo.

2- Hakuna kiumbe hata kimoja ardhini na mbinguni miongoni mwa wanaadamu, majini, malaika na mitume “sallallahu alayhi wasallam” (amani iwe juu yao) ambaye ana elimu ya ghaib. Allahu taala peke yake ndiye aliye na ujuzi wa yale yaliyojificha na hutoa elimu aitakayo ya ghaib kwa viumbe wateule. [Ghaib humaanisha kile (kitu) ambacho hakiwezi kutambulikana kwa kutumia ala za hisi ama kueleweka kwa kupiga mahesabu au kufanya majaribio].

3- Kujua mambo ya haramu kama ni haramu na kuamini hivyo.

4- Kujua mambo yaliyo halali kama ni halali na kuamini hivyo.

5- Kutokuwa na hisia kwamba umesalimika kutokana na adhabu za Allahu taala na kumcha Mungu daima.

6- Kutokata tamaa kutokana na rehma za Allahu taala pasi na kujali kiasi cha madhambi uliyotenda.

Iwapo mtu atashindwa kutimiza masharti haya sita, hata kama ametimiza matano au ikiwa atatimiza sharti moja tu na asitimize matano yaliyobaki, imani na Uislamu wa mtu huyo hautakuwa sahihi.

Kuna mambo arubaini [40] yanayoweza kumpelekea mtu aliye na imani kuipoteza baadae.

1- Kufanya mambo ya bid'a (uzushi), yaani kuwa na dosari katika imani ya mtu. [Ukiukaji mdogo wa nguzo za imani zilizofundishwa na wanazuoni humfanya mtu mwanabid'a au kafiri]. Ikiwa mtu atakana kitu ambacho ni lazima kukiamini, mtu huyo hua amekufuru hapo hapo. Ni **(Bid'a)** au upotofu **(Dhalala)** kukana kitu ambacho ni lazima kukiamini. Bid'a au dhalala humpelekea mtu kufa imani au kudhoofika.

2- Imani dhaifu, yaani imani isiyoambatanishwa na amali (vitendo vya ibada).

3- Kuvifanya viungo sita vya mwanaadamu viepukane na njia iliyo sahihi.

4- Kuendelea kufanya madhambi makubwa. [Kwa hiyo, muislamu hapaswi kunywa pombe, na wanawake na wasichana waislamu hawapaswi kuonesha vichwa vyao, nywele zao na vifundo vya mikono yao kwa wanaume wasio maharim wao.]

5- Kutokuwa na shukrani kwa neema ya Uislamu.

6- Kutohofia uwezekano wa kwenda akhera bila imani.

7- Kueneza ukatili.

8- Kutosikiliza adhana inayofanyika kwa mujibu wa sunna. [Mtu anayepuuza adhana huwa fasiki]. (Adhana na jinsi inavyoadhiniwa kulingana na sunna, yaani Uislamu, imeelezewa kwa tafsiri katika sura ya kumi na moja ya juzuu ya nne ya Endless Bliss).

9- Kutowatii wazazi. Kukataa kijeuri amri zao zinazowiana na Uislamu na ambazo ni mubah.

10- Kuapa mara kwa mara hata kama viapo vyenyewe ni vya ukweli.

11- Kupuuza tumaanina (kutulia) katika nguzo za sala (yaani katika rukuu, i'itidaal, baina ya sijda mbili, na juluus (kukaa baina ya sijda mbili). Taa'dil il arkaan maana yake ni kuwa katika hali ya utulivu (tuma'nina) kwa kipindi kinacho mtoshelezea kusema "Sub´hanallah".

12- Kufikiria kwamba sala si muhimu. Kutojali kujifunza na kuwafundisha sala watu wa familia na watoto, na kuwazuia watu wengine kuswali.

13- Kunywa pombe au kinywaji kingine kinacholewesha kikitumika katika kiasi kikubwa. Sheria hiyo hiyo inatumika hata kama pombe ni kidogo.

14- Kuwatia waumini mashakani.

15- Kujifanya walii au msomi katika mambo ya Uislamu. Kujifanya mshikadini, muhubiri, bila kupata mafundisho ya Uislam. [Vitabu vya uongo vilivyoandikwa na waongo kama hao havistahili kusomwa. Hutuba na mahubiri yao hayafai kuhudhuriwa].

16- Kuyasahau madhambi yake mtu, kuyachukulia kama jambo dogo.

17- Kiburi (yaani kuwa na kiburi kingi).

18- Kujikweza au kujiona (kujifakharisha), yaani kujifakharisha kwa usomi na uchamungu.

19- Kuwa mnafiki, yaani unafiki, kuwa na nyuso mbili.

20- Hasad (kumhusudu ndugu yako Muislamu).

21- Kutotii amri za serikali au bwana wako ikiwa amri zao hazipingani na Uislamu. [Haifai kutii amri zinazopingana na Uislamu].

22- Kusema kwamba fulani na fulani ni mtu mwema kabla hujampa mtihani.

23- Kuwa muongo.

24- Kuwakwepa wasomi. [Kutosoma vitabu vilivyoandikwa na wanazuoni wa kiislamu wa ahlu haki].

25- Kufuga masharubu na kuyarefusha kupindukia kiasi kilichopendekezwa na sunna.

26- Wanaume hairuhusiwi kuvaa hariri. Ni ruhusa kwao kuvaa hariri bandia (ya kutengeneza) au hariri kidogo ikichanganywa kwenye pamba nyingi.

27- Kuwa mwenye tabia ya kusengenya.

28- Kuwasababishia majirani zako matatizo hata kama si waumini.

29- Kudhihirisha hasira nyingi juu ya mambo ya dunia.

30- Kupokea na kutoa riba.

31- Kuvaa mavazi yalio marefu sana kwa lengo la kujishaua.

32- Kufanya mambo ya uchawi.

33- Kutomtembelea jamaa ambaye ni Muislamu (mwema) mchamungu.

34- Kutompenda mtu ambaye hupendwa na Allahu taala na kumpenda mtu ambae unajua kwamba anauchafulia jina Uislamu.

35- Kumkasirikia ndugu yako muislamu kwa zaidi ya siku tatu.

36- Kuwa na tabia ya kuzini.

37- Kufanya liwati pasi na kutubia juu ya dhambi hilo baadaye. Liwati ni kuingiza dhakari kwenye sehemu ya kukidhia haja kubwa ya mtu mwingine.

38- Kuadhini katika nyakati zisizopendekezwa kwenye vitabu vya fiq´hi au kwa njia isiyoamrishwa na Sunna, au kutoipa adhana heshima inayostahiki wakati unapoisikia na inapowasilishwa kwa namna inayokubalika na Sunna.

39- Kutomkanya mtu umuonapo akitenda munkari [yaani kutomzuia mtu huyo asifanye hivyo] kwa kutumia lugha ya mvuto hali ya kuwa una uwezo wa kufanya hivyo.

40- Wanawake ambao una haki ya kuwapa nasaha kama vile mke wako na binti yako, kuwaachia kutoka nje na hali hawajifuniki vichwa vyao, mikono yao na miguu yao, au kujipamba au kujitia marashi na manukato.

**Imani** humaanisha kutangaza kwa ulimi na kuthibitisha ukweli ambao mitume “sallallahu alayhi wasallam” waliwasilisha kutoka kwa Allahu taala. Na **Uislamu** humaanisha kumuamini Muhammad rehma na salamu za Allahu taala ziwe juu yake na kutekeleza (amali) mafundisho yake.

Aidha, **Dini** au **Millat** ni itikadi yaani ni nguzo za kiimani ambazo mitume “sallallahu alayhi wasallam” walileta kutoka kwa Allahu taala.

**Uislamu** ama sheria za Uislamu humaanisha amali, yaani nguzo za kimatendo alizozileta mtume “sallallahu alayhi wasallam” wetu Muhammad kutoka kwa Allahu taala.

Aidha, iman-i-ijmaali (imani kwa muhtasari), humaanisha imani kwa ujumla wake, nayo humtoshelezea mtu (haja ya kuwa muumini, muislamu). Si lazima kwenda katika tafsiri au ufafanuzi au kuijua imani kwa upana. Imani ya muqallid, yaani mtu anayeamini na hali haelewi, itasihi (Hata hivyo, maelezo kamili huhitajika katika baadhi ya mambo).

Kuna viwango vitatu vya imani. Iman-i-taqliidii, Iman istidlaalii na Iman-i-haqiiqii.

**Iman-i-taqliidii** (imani ya kuigiza). Mtu mwenye kiwango hiki cha imani hajui faradh, wajib, sunna wala mustahab. Wanawaigizia tu wazazi wao katika imani na vitendo vyao vya ibada. Imani ya watu kama hao inaweza kusababisha matatizo.

**Iman-istidilaalii** (imani dokezi). Watu wenye kiwango hiki cha imani wanajua faradh, wajib, mustahab na haram, na hutii sheria za kiislamu. Wana ujuzi na uwezo mkubwa wa kuwasilisha mihimili ya imani. Wamejifunza mihimili hiyo kutoka kwa walimu wa kidini na kwenye vitabu. Imani ya watu kama hawa ni thabiti.

**Iman-i-haqiiqii** (imani ya kweli ama halisi). Kama viumbe wote wangeungana na kukubaliana kumkana Mola wao (Allahu taala), mtu aliyoko katika kiwango hiki cha imani asingemkana Allahu taala. Watu wa namna hii hawana hata chembe ya shaka katika nyoyo zao. Imani yao hufanana na ile ya manabii (mitume "sallallahu alayhi wasallam"). Kiwango hiki cha imani ni cha juu zaidi kuliko vile vingine viwili.

Aidha, sheria za kiislamu zinahusiana na amali (matendo ya ibada) na sio imani. Imani, peke yake, haimtoshelezi mtu kuingia peponi. Na vile vile, haiwezekani kuingia peponi kwa kutegemea amali (yaani kwa kutekeleza matendo ya ibada). Imani bila amali inakubalika. Kwa upande mwingine amali bila imani haina faida yoyote. Matendo ya ibada yanayofanywa, matendo ya uchamungu yanayotendwa na zaka inayotolewa na watu wasiokuwa na imani, vitu hivyo vyote havitowafaa lolote akhera. Imani haiwezi kutolewa kama zawadi kwa mtu mwingine, ijapokuwa thawabu zinazochumwa kutokana na amali zinaweza kuzawadiwa. Mtu hawezi kutoa wala kuandika agizo kuhusu imani kwenye wasia wake wa mwisho. Ingawa mtu anaweza kuwaagiza warithi wake kutenda amali kwa niaba ya mtu mwingine (baada ya mtu huyo kuaga dunia). Mtu anayepuuza kutenda amali hatakuwa kafiri. Lakini yule anaetupilia mbali imani au kuichukulia amali kama jambo lisilokuwa na maana atakuwa kafiri. Mtu mwenye udhuru au yule asiekuwa na uwezo wa kutenda amali atasamehewa. Lakini hakuna namna ambayo mtu atasamehewa katika suala la imani.

Kuna aina moja tu ya imani ambayo mitume "sallallahu alayhi wasallam" wote waliwasilisha kwa wafuasi wao. Pamoja na hayo wanatofautiana katika sheria, utekelezaji na matendo ya kidini.

Halikadhalika kuna aina mbili za imani. Moja ya aina hizo ni iman-i-khalqii na nyingine ni iman-i-kasbii.

**Iman-i-khalqii** ni ile ya kiuzawa yaani kukubali kwa mja ahadi ya kukiri kuwa Allahu taala ndiye Mola wake.

**Iman-i-kasbii** ni imani anayoipata mtu baada ya kubaleghe. Imani ya waumini wote ni sawa. Ingawa wanatofautiana katika amali.

Imani ni faradh-i-daaim (ni faradhi ya kudumu), huku amali ikiwa faradh (faradhi) muda wake ukiwadia.

Imani ni jambo la faradhi kwa kafiri na muislamu ni sawa. Amali ni faradhi kwa muislamu pekee.

Na vile vile kuna vigawanyo nane vya imani:

**Iman-i-matbuu’** ni imani ya malaika.

**Iman-i-ma’suum** ni imani ya mitume “sallallahu alayhi wasallam”.

**Iman-i-maqbul** ni imani ya waumini.

**Iman-i-mauquuf** ni imani batilifu ya watu wa bid’a.

**Iman-i-marduud** ni imani ya uongo ambayo wanafiki hujigamba kuwa nayo.

**Iman-i-taqliidii** ni imani ambayo watu waliipata kutoka kwa wazazi wao na ambayo hawakufundishwa na walimu wa kidini. Imani ya watu hao inaweza kumsababishia mtu matatizo.

**Iman-isdilaalii** ni imani ya mtu anayemjua Mola Mtukufu kwa kurejelea ushahidi unaothibitisha uwepo wake. Imani ya mtu huyo ni imara.

**Iman-i-haqiiqii**. Mtu mwenye aina hii ya imani hawezi kumkana Mola wake (Allahu taala) hata kama viumbe wengine wangekubaliana kumkana Mola wao na hakutakuwa na chembe ya shaka ama kusitasita katika moyo wa mtu huyo. Kama tulivyotaja hapo awali katika matini hii, aina hii ya imani ndiyo bora kuliko nyingine zote.

Umuhimu wa imani umejikita katika mambo matatu.

Kwanza, huiokoa shingo ya mtu kutokana na upanga.

Pili, huiokoa mali ya mtu kutokana na kodi zijulikanazo kama jizya na kharaj (malipo wanayo lipia makafiri wakiwa katika ulinzi na usimamizi wa kiislam).

Tatu, huokoa mwili wa mtu kutokana na moto wa milele wa jahannam.

**(Amantu billaahi…),** hujulikana pia kama Sifaat-i-imaan au mu’minuuna bih-dhaat-i-imaan au asl-i-imaan, kutokana na heshima yake na taadhima. (Ni tamko la nguzo za imani ambalo ni kama ifuatavyo)… **wa malaaikatihi, wa kutubihi, wa rusulihi, walyawmil-aakhiri, wa bil- Qadari khayrihi wa sharrihi min Allaahi Ta’ala, wal-ba’athu ba’adal-mawt haqqun, ash-hadu anlaa ilaaha illallah wa ash-hadu anna Muhammadan ‘abduhu wa rasuuluhu).**

Aidha, kuna madaraja mawili ya imani, yaani nyakati ambazo kwanza inamwajibikia mtu kuwa na iman.

Pili umri wa kutoa maamuzi na umri wa kubaleghe.

Pia, kuna sababu mbili za kuamini. kuumbwa kwa viumbe wote pili na kuteremshwa kwa Quran tukufu. Halikadhalika, kuna aina mbili za

ushahidi. Daliil-i-aqlii (ushahidi wa kiakili) na daliil-i-naqlii (ushahidi unaotokana na maandiko).

Imani pia ina rukn mbili (mihimili), asl (asili), Ikraar bil-lisaan (kukiri kwa ulimi) na tasdiiqun bil jinaan (kuthibitisha kwa moyo). Na kuna masharti mawili yaliyowekewa rukn hizo.

Sharti iliyofunganishwa moyo ni kwamba usiwe na shaka yoyote wala wasiwasi na sharti inayohusu ulimi ni kutambua yale ambayo mtu huyatamka.

Aidha, tunaweza kujiuliza je, imani ni kiumbe? Jibu ni kwamba imani si kiumbe kwa vile ni hidayat (uongofu) kutoka kwa Allahu taala. Kwa upande mwingine, ni kiumbe kutokana na mtazamo kwamba ni uthibitisho na azimio la mja kimaumbile.

**Yaqiin** humaanisha kuijua dhati ya Allahu taala na ukamilifu wake.

**Khawf** humaanisha kumcha Allahu taala.

**Rajaa** humaanisha kutokata tamaa na rehma ya Allahu taala.

**Mahabbatullah** humaanisha kumpenda Allahu taala na mtume "sallallahu alayhi wasallam" wake rehma na salamu za Allahu taala zimshukie juu yake na kuipenda dini ya Uislamu na waumini.

**Hayaa** humaanisha kuona haya mbele ya Allahu taala na mtume "sallallahu alayhi wasallam" wake rehma na salamu zimshukie juu yake.

**Tawakkul** humaanisha kutegemea mambo yote kwa Allahu taala. Kuweka imani yako kwa Allahu taala wakati unapoanza kufanya jambo lolote.

Ni nini maana ya Uislamu, imani na ihsani?

**Imani** maana yake ni kuamini ukweli ulioelezewa na mtume "sallallahu alayhi wasallam" Muhammad rehma na salamu zimshukie juu yake.

**Uislamu** ni kutekeleza maamrisho ya Allahu taala na kuepukana na makatazo yake.

**Ihsani** ni kutenda matendo ya ibada kana kwamba Allahu taala unamuona. Na kama wewe humuoni basi yeye anakuona.

**Maana ya imani** kila siku ni uthibitisho. Katika Uislamu (kitaaluma) neno hilo humaanisha kuamini nguzo sita za Imani.

**Ma'rifat** ni kutambua kuwa Allahu taala ana sifa za ukamilifu na kwamba yupo mbali na sifa za upungufu.

**Tawhiid** maana yake ni kuamini kuwa Allahu taala ni mmoja na hana mshirika.

**Uislamu (Sheria za Kiislamu)** ni maamrisho na makatazo ya Allahu taala.

**Dini na millat** ni azimio linalohusiana na nguzo za imani analolifanya mtu muda wa uhai wake.

Imani vile vile inalindwa katika ngome tano.

1- Yaqiin

2- Ikhlaas

3- Kutenda matendo ya faradh na kuepukana na haramu.

4- Kushikamana na Sunna.

5- Kuimarisha adabu na kuwa muangalifu nayo.

Yeyote anayekuwa imara katika ngome hizi atakuwa imara pia katika imani. Kupuuza ngome yoyote kutampelekea adui kupata ushindi. Mwanaadamu ana maadui wanne. rafiki mbaya kuliani, matamanio ya nafsi yake kushotoni, upendeleo wa dunia mbele yake na shetani nyuma yake. Maadui hawa hupania kuichukua imani. Marafiki wabaya si wale wanaomdhulumu mtu mali yake, pesa zake na mambo mengine ya dunia. Marafiki wabaya na walio hatari zaidi ni wale wanaokazana kuondoa dini ya mtu, imani, adabu, haya na uungwana na kwa kufanya hivyo, wamevamia furaha ya mtu duniani na kujivunia kwa milele huko akhera. Tunamuomba Allahu taala ailinde imani yetu kutokana na uovu wa maadui kama hao na upotofu unaopangwa na maadui wa Uislamu.

Maana ya **(Kalima-i-tawhid)**, yaani tamko **La ilaaha illallah**, ni Hakuna anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allahu taala. Hana mshirika wala anayelingana naye. Hafungamani na wakati wala mahali maalum.

**Muhammadun Rasulullah** maana yake ni bwana wetu. Muhammad Mustafa “sallallahu alayhi wasallam” sala na salamu zimshukie juu yake, ni mja na mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allahu taala wa haki. Alhamdulillahi sisi ni umma wake.

Tamko la Tawhidi lina majina nane.

1- Kalimat us-shahada.

2- Kalimat ut-tawhiid.

3- Kalimat ul-ikhlaas.

4- Kalimat ut-taqwaa.

5- Kalimat ut-twayyiba.

6- Da’wat ul-haqq.

7- Urwat ul-wuthqaa.

8- Thamarat ul-janna.

Masharti ya Suratul Ikhlas ni nia, kujua maana yake na kuisoma au kuikariri kwa heshima.

Mtu anayefanya dhikri anahitaji mambo manne (Tasdiiq, ta'adhwiim, halaawat na hurmat).

Mtu anayeacha tasdiq anakuwa mnafiki, anaeacha ta'adhwiim hua mwanabid'a, anayeacha halaawat hua mnafiki na anaeacha hurmat hua fasik. Na ikiwa atakanusha basi atakuwa kafiri.

Kuna aina tatu za dhikr:

1- Dhikrul-awaam.

2- Dhikrul-khawaas.

3- Dhikrul-akhas.

Dhikrul-awaam ni ile ya wasiosoma. Dhikrul-khawaas ni ya wanazuoni wa Kiislamu na dhikrul-akhas ni ya mitume "sallallahu alayhi wasallam".

Viungo vya binadamu vinavyohusika katika dhikr ni vitatu:

1- Ulimi hufanya dhikr kwa kutoa tamko la shahada.

2- Kumpwekesha Allahu taala, kumhimidi na kusoma Quran tukufu.

3- Dhikr inayofanywa na moyo.

Moyo hufanya dhikri ya aina tatu:

1- Kuzingatia juu ya ushahidi na ishara zinazomuongoza mtu katika utambuzi wa sifa za Allahu taala.

2- Kuzingatia kuhusiana na ushahidi juu ya sheria za Allahu taala.

3- Kuzingatia kuhusiana na miujiza ya Allahu taala.

Wanazuoni wa tafsiri wanaielezea aya ya mia moja na hamsini na mbili (152) ya Suratul-Baqarah kama ifuatavyo. Quran tukufu hutangaza kwamba **(Enyi waja wangu! Mkinidhukuru kwa kunitii (kwa kutenda matendo ya kumtii Allahu taala), na mimi nitakudhukuruni kwa neema zangu** [janna]**. Mkinidhukuru katika hali ya upweke, basi nitakudhukuruni katika mkusanyiko mkubwa (yaani mahali pa mah´shari). Mkinidhukuru nyakati za ukiwa/ufukara, nitakudukuruni kwa msaada wangu. Mkinidhukuru kwa kuitikia wito wangu, (yaani kwa kutekeleza maamrisho yangu), basi nitakudhukuruni kwa kuwapeni hidaya (uongofu). Mkinidhukuru kwa ukweli na ikhlas, basi nitakudhukuruni kwa nia ya nusura na uokovu. Mkinidhukuru kwa Al-Fatiha tukufu na kwa rububiyya ilioko kwenye Al-Fatiha tukufu, basi nitakudhukuruni kwa rehma zangu).**

Hivyo, wanazuoni wametaja mamia ya faida za kufanya dhikri. Tutataja tu baadhi yake:

Muislamu anapofanya dhikri, Allahu taala humfurahikia. Malaika watamfurahikia. Shetani atahuzunika. (Moyo wa mtu huyu utalainika).

Atafanya ibada kwa kupenda na hamasa. Dhikri itaondoa huzuni katika nyoyo wake, itaweka uchangamfu katika nyoyo yake, na itang'arisha uso wake kwa nuru. Mtu huyo atakuwa shujaa na atajinyakulia upendo wa Allahu taala. Mlango wa maarifa utafunguliwa kwa ajili yake ili wapokee faydh kutoka kwa mawalii. Watapambwa na sifa thamanini za tabia njema.

**(Ash-hadu anna Muhammadan abduhu wa Rasuuluh)**. Maana ya tamko hili ni mtume "sallallahu alayhi wasallam" wetu Muhammad Mustafa rehma na salamu zimshukie juu yake, ni mja wake na mtume "sallallahu alayhi wasallam" wake alikula, akanywa na alioa wanawake.

Alikuwa na watoto wa kiume na wa kike. Wote walikuwa watoto wake Khadija "radiyallahu anha" za Allah zimshukie juu yake, isipokuwa Ibrahim ambaye mamake ni Maariya Aliefariki akiwa mdogo. Watoto wake wote walifariki kabla yake isipokuwa Fatuma "radiyallahu anha" (radhi za Allahu taala zimshukie) ambae alimuozesha Ali "karramallahu wajhahu". Hasan na Husein "radiyallahu anhüma" ni watoto wa Ali "radiyallahu anh" na Fatuma "radiyallahu anha". Fatuma "radiyallahu anha" alikuwa na hadhi ya juu miongoni mwa watoto wake wote. Alikuwa akipendwa sana na Mtume "sallallahu alayhi wasallam" rehma na salamu zimshukie juu yake.

Mtume "sallallahu alayhi wasallam" rehma na salamu zimshukie alikuwa na wake kumi na mmoja ambao ni Khadija, Sauda, Aisha, Hafsa, Ummu Salama, Ummu Habiba, Zainab bint Jahsh, Zainab bint Khuzaima, Maimuuna, Juwairiyya na Safiyya radhi za Allahu taala ziwashukie.

**(Dalili za kisheria)** zimeundwa na Kitabu (Quran), Sunna, Ijmaa na Qiyas. Kutokana na vyanzo hivyo vinne wanazuoni wa Kiislamu walipanua elimu yao ya kidini. Neno la Allahu taala linajulikana kama Kitab (kitabu). Sunna ni kauli za mtume "sallallahu alayhi wasallam" (matamko ya mtume "sallallahu alayhi wasallam" wa Allahu taala), af'al-ur Rasuul (matendo na tabia za mtume "sallallahu alayhi wasallam" wa Allahu taala) na taqriir-u-Rasuul (idhini ya mtume "sallallahu alayhi wasallam"). Ijmaa ni makubaliano yaliyofikiwa na mujtahidin ambao waliishi katika karne moja, kwa mfano masahaba watukufu radhi za Allahu taala ziwe juu yao, au maimamu wa madhehebu manne. Qiyas ni malinganisho yaliyofanywa na mujtahidin kati ya mambo mawili yanayotofautiana.

Maana za kilaksia zilizoelezewa na madhehebu mbalimbali ni za namna mbili tofauti. Ya kwanza ni mkondo wetu wa kiitikadi na nyingine ni ule wa kimatendo.

Imamu wetu, yaani kiongozi, katika itikadi ni Abu Mansur Maturidii "rahmatullahi alaih" Allah amrehemu. Mkondo wake unajulikana kama **(Ahlu sunna)**. Kiongozi wetu katika mkondo wa matendo ni Imam Abu Hanifa Allah amrehemu. Mkondo wake unajulikana kama **(Madhehebu ya Hanafii)**.

Abu Mansur Maturidii "rahmatullahi alaih", jina lake ni Muhammad, jina la babake ni Muhammad na jina la babu yake ni Muhammad. Mwalimu wake ni Abu Nasr al-iyaad "rahmatullahi alaih" Allah amrehemu.

Jina la mwalimu wa Abu Nasr al-iyaad ni Abu Bakr-aljurjaani ambaye alisomeshwa na Abu Sulaiman aljurjaani, aliyesomeshwa na Abu Yusuf na Imam Muhammad Shaybaani. Na mwalimu wa hawa magwiji wawili ni Imam Abuu Hanifa "rahmatullahi alaih" Allah amrehemu. Kwa hiyo, Imam mkuu ndie kiongozi mkuu wa madhehebu yetu kiitikadi na kimatendo.

Waislamu wote wana maimamu watatu (viongozi), kuwajua ni jambo la lazima. Imamu wetu anayetuhimiza kutekeleza maamrisho na kuepukana na makatazo ni Quran tukufu. Imamu wetu anayetuambia mambo hayo, yaani Uislamu ni Bwana Mtume "sallallahu alayhi wasallam" rehma na salamu zimshukie. Imamu wetu anayesimamia utekelezaji wa mafundisho hayo kwa niaba ya Mtume "sallallahu alayhi wasallam", yaani anayehakikisha kuwa yanafuatwa, ni kiongozi wa taifa la kiislamu.

Mwalimu wa Imamu mkuu anaitwa Hammad ambae alisomeshwa na Ibrahim an-Nahaaii aliefundishwa na 'Alqama bin Qays ambae mjomba wake Imam An-nahaaii. Mwalimu wa 'Alqama ni 'Abdullahi bin Masoud "rahmatullahi alaih" Allah amrehemu aliyepata elimu yake kutoka kwa mtume "sallallahu alayhi wasallam" wa Allahu taala rehma na salamu za Allahu taala zimshukie.

Ama mtume "sallallahu alayhi wasallam" wa Allahu taala rehma na salamu zimshukie, alipokea elimu yake kutoka kwa Jibriil "alaihis-salaam" rehma na salam ziwe juu yake ambae aliamrishwa na Allahu taala.

Allahu taala amemjaalia mwanaadamu majohari manne. ´Akili (moyo, busara, hoja), imani, haya na utendaji wa matendo mema´.

Sala na matendo mema hukubalika iwapo masharti matano yatatimizwa. Masharti hayo ni imani, ‘ilm, niyya, ikhlas na kuwapa watu haki zao. Kwanza kabisa, lazima mtu ajue masharti ya kusihi katika kutekeleza matendo ya ibada yanayopaswa kufanywa. [Usahihi wa tendo fulani hutofautiana na ukubalifu wake. Matendo ya ibada yenyewe yana masharti yake na fardhi zake zinazopaswa kutimizwa ili yachukuliwe kuwa sahihi. Sharti hata moja ikikosekana, tendo la ibada linalofanywa halitosihi. Itakuwa sawa na kutotendwa kwa tendo hilo la ibada na mtu hatanusurika na adhabu na mateso (kwa vile huhesabiwa kaliacha). Hakuna adhabu itakayomkumba mtu kutokana na tendo la ibada ambalo ni sahihi hata kama si kubalifu. Pamoja na hayo, muislamu hatopata thawabu (ujira maalum) kwa ajili ya ibada yake isiyotakabaliwa. Ili itakabaliwe lazima kwanza isihi, yaani masharti matano yaliotajwa hapo awali yawe yametimizwa. Haki zilizoelezewa, ni miongoni mwa masharti haya. Imam Rabbanii Allah amrehemu alitaja katika barua ya thamanini na nane, mjeledi wa pili wa maandishi yake yanayojulikana kama Maktubaat. (Endapo mtu atatenda tendo linalofanana na la mtume “sallallahu alayhi wasallam” halafu akazuia haki ya mtu (hata kama ni chembe ndogo sana), hataingia peponi mpaka ailipe). [sala zake hazito kubaliwa].

Ibn Hajar al-Haythami al-Makki “rahmatullahi alaih”, akielezea tendo la maasia la mia moja thamanini na saba, katika kitabu chake **(Zawajir)**, alisema kwamba Aya ya mia moja themanini na nane ya suratul-Baqarah inasema **(wala msichukuliane mali zenu kwa batili…)**. Maana ya tamko ‘kwa batili’, ni udanganyifu unaofanyika kupitia riba, kamari, wizi, ulaghai, uhaini, kutoa ushahidi wa uongo, na uhalisia kuna hadithi tukufu isemayo **(Muislamu asiyekula halali ya watu, akatenda matendo ya faradh, akaepukana na haramu na kuwadhuru watu, ataingia peponi)** na **(Mwili unaolishwa haramu utachomwa moto)** na **(ikiwa watu hawatasalimika kutokana na kuonewa na kuudhika, mtu huyo hatapata manufaa yoyote katika imani yake au rehma au zaka)** na **(Ikiwa kanzu iliyovaliwa na mtu ilipatikana kwa njia ya haramu, basi sala anayosali haitotakabaliwa).** [Jilbaab ni vazi refu livaliwalo na wanawake. Jilbaab pia ni kanzu inayovaliwa na wanaume]. Hadithi ambayo ameinukuu kuelezea dhambi la mia mbili inasema **(Mtu anayeuza bidhaa iliyochafuliwa si miongoni mwa umma wetu. Marejeo yake ni motoni).** Imetajwa katika hadithi inayozungumzia dhambi la mia mbili kumi na saba kwamba **(Motoni ni marejeo kwa mtu amdhuruye (anaemfanyia ubaya) jirani yake kwa ulimi wake hata kama anaswali na kufunga na kutoa zaka sana).** Hata kama

majirani wa mtu sio waumini, haifai kuwadhuru (kuwatendea ubaya). Bali kinachofaa ni kuwatendea wema na kuwaonea huruma. Imetajwa katika hadithi tukufu katika kuelezea tendo la dhambi la mia tatu na thelathini kwamba **(Mtu anayemuua kafiri kwa dhuluma wakati wa amani, hatoingia peponi).** Hadithi nyingine inasema **(Waislamu wawili wakipigana kwa ajili ya matamanio ya kidunia, basi aliyeua na aliyeuliwa wataingia motoni).** Imetajwa katika hadithi inayozungumzia dhambi la mia tatu kumi na saba kwamba **(Mtu anayechochea uadui kati ya watu ataadhibiwa hadi siku ya kiyama).** Hivyo hivyo, ataadhibiwa endapo atachochea uadui (uhasama) kati ya makafiri. Katika hadithi inayozungumzia dhambi la mia tatu hamsini. **(Watu aina tatu, dua zao bila shaka zinakubaliwa. Mwenye kudhulumiwa, msafiri na wazazi).** Na katika hadithi nyingine **(Mtu aliedhulumiwa, dua yake haitokataliwa hata kama ni kafiri). (Katika hadithi inayoelezea dhambi la uhaini dhidi ya serikali, imetajwa kuwa adhabu yake haitocheleweshwa).** Mwisho wa tafsiri kutoka kitabu cha **Zawaajir**. Ewe muislamu! Ikiwa unapenda kupata rehma za Allahu taala na matendo yako kutakabaliwa, hifadhi hadithi zilizonukuliwa hapo juu moyoni mwako. Usihujumu mali, maishani mwako na usivunje heshima ya mtu yeyote, muislamu na asiyekuwa muislamu. Usimdharau mtu yeyote. Wape watu haki zao. Ni mojawapo ya haki za binaadamu mwanamme kumlipa mahari mwanamke ambae amemuacha. Asipolipa mahari hiyo, atastahili adhabu kote kote duniani na akhera. Haki ya binaadamu iliyomuhimu zaidi na ambayo adhabu yake ni kali sana ikivunjwa, ni kuwacha kuwafundisha jamaa wa karibu Uislamu, hasa wakiwa chini ya usimamizi wa mtu na ulinzi wake. Mtu akizuia jamaa zake na watu wengine kujifunza Uislamu na kufanya ibada, kwa kuwaadhibu na kuwadanganya, atachukuliwa kuwa kama kafiri au adui wa Uislamu. Mfano wa muelekeo huo usio wa kidini ni kujaribu kuyachafua mafundisho ya Uislamu, mkakati unaofuatwa na wanabid'a wanaofanya uzushi katika dini na watu wasiofuata madhehebu maalum kwa kutoa matamko yanayolenga kuukashifu Uislamu na kuandika makala ya uchochezi. Usiipige vita serikali wala sheria zake. Lipa kodi. Ni hatia kuiasi serikali, hata kama ina udhia au matatizo kama alivyosema Muhammad Mustafa Haadimi Allah amrehemu, aliyefariki mwaka wa 1176 [1762 A. D. ] huko Haadim, Konya, Uturuki, katika kitabu kijulikanacho kama **(Beriqa)**. Hata kama uko katika Dar ul-harb, yaani moja wapo ya nchi za makafiri, usivunje sheria wala haki zao. Usizushe fitna. Usifanye urafiki na watu wanaouhujumu Uislamu, na wanabid'a wazushi katika dini au wasiofuata moja wapo ya madhehebu yoyote yale katika madhehebu

ya haki. Usisome vitabu vyao wala magazeti yao. Usiruhusu vipindi vya redio zao na televisheni kuingia nyumbani kwako. Amrisha mema (yaani mafundisho ya Uislamu), kwa wale wanaotaka kukusikiliza. Kwa maneno mengine, wape nasaha, kwa uso wenye tabasamu na maneno matamu na laini. Kwa kutumia tabia yako nzuri, onesha utukufu na heshima ya dini ya kiislamu kwa watu wote wanaokuzunguka.

Ibn Abidin Allah "rahmatullahi alaih" amrehemu, anaeleza katika juzuu ya kwanza kama ifuatavyo. (Saw'atayn, yaani sehemu ya siri ya mbele na ya nyuma, ni aura ghaliidh (uchi mzito) kwa mujibu wa madhehebu yote. Ni faradhi kusitiri sehemu hizi kwa mujibu wa madhehebu hayo yote. Mtu asiyetilia maanani suala la kusitiri sehemu hizo, atakuwa muasi mwenye dhambi kubwa na laana. Mwanamme asiyesitiri magoti yake anapaswa kushauriwa ili ayasitiri. Pamoja na hayo, kuamrisha mema kunapaswa kufanyika kwa maneno laini. Na mtu akiitikia kwa ujeuri anapaswa kujibiwa kwa ukimya. Kwa upande mwingine, ujeuri wa mwanamume aliyeonesha mapaja yake unapaswa kukabiliwa na kuadhibiwa/kuadhiriwa. Endapo mwanamme atadhihirisha uchi wake kwa ujeuri (pamoja na kwamba ameonywa), basi anapaswa kushitakiwa kwenye mahakama ya kisheria ili alazimishwe kuusitiri. Hukumu iko kwa mtiririko huu huu katika hali ya ukiukaji wa sheria kwa anayeangalia sehemu za siri za mwanamme.) Katika madhehebu yote manne, ni lazima kwa wanawake kuisitiri miili yao yote, isipokuwa viganja vyao na nyuso zao, kwa wanaume ambao si maharimu wao na wanawake wasiokuwa waislamu, hii ina maana kwamba wanapaswa kusitiri miguu yao, mikono yao na nywele zao wakiwepo watu kama hao (yaani wanaume wasio maharimu wao na wanawake ambao si Waislamu.) (Watu ambao si maharimu kwa jinsia zote mbili wameelezewa katika sura ya tano ya kitabu kiitwacho Endless Bliss.) Kwa mujibu wa madhehebu ya kishafi, ni lazima pia kwa wanawake kutoonyesha nyuso zao kwa watu hao waliotajwa hapo awali. Ikiwa wanawake wenyewe au wazazi wao au ndugu zao au waume zao hawataitilia maanani sheria hii, basi watakufuru. Ni dhambi kubwa kwa wavulana kucheza densi ngoma au michezo huku mapaja yao yakionekana. Na ni dhambi kwa wasichana kufanya hivyo bila kusitiri vichwa vyao na mikono yao, na kuwatazama wakifanya hivyo. Muislamu hapaswi kupoteza muda wake wa faragha kwa kucheza michezo au kufanya mambo yasiyokuwa ya manufaa ya aina yoyote, badala ya kujinufaisha na kujielimisha na kusali. Kwa mujibu wa **(Kimyaa-i-sa'aadat)**. (Kama ilivyo haramu kwa wanawake na wasichana kutoka nje hali ya kuwa vichwa vyao, mikono yao na miguu

yao iko wazi, ni haramu pia kwao kutoka nje wakiwa wamevaa nguo nyembama zinazowabana na zilizopambwa na kufukizwa kwa uturi au mafuta mazuri. Na ikiwa Wazazi wao, waume zao na ndugu zao wanaridhika na kupenda vitendo hivyo watachukuliwa kama washirika wao katika dhambi hilo na kwa hivyo watapata sehemu ya adhabu ya dhambi.) Kwa maneno mengine, watachomwa pamoja motoni. Lakini wakifanya toba wataghufiriwa madhambi yao na hawatachomwa. Kwani Allahu taala huwapenda watu wanaotubia.

## WAKE NA VITA ALIVYOPIGANA MTUME

Mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allah alikuwa na umri wa miaka arobaini wakati alipojiwa na Jibril na kumpa utume. Baada ya miaka mitatu akautangaza utume wake Makka. Mwaka huo unaitwa mwaka wa **(Bi’that)**. Alishiriki vita vya jihadi mara ishirini na saba. Kati ya hizo mara kumi na nane alikuwa ndie jemedari mkuu na mara tisa alishiriki kama askari wa kawaida. Mtume “sallallahu alayhi wasallam” alikuwa na watoto wa kike wanne, watoto wa kiume wanne, wake kumi na moja, shangazi sita na ami kumi na mbili. Alimuoa Khadijatul kubra wakati akiwa na umri wa miaka ishirini na tano. Mwaka mmoja baada ya kufa Khadija, wakati mtume “sallallahu alayhi wasallam” akiwa na umri wa miaka hamsini, alimuoa Aisha binti wa Abubakar siddik “radiyallahu anhu” baada ya kuamrishwa na Allah kufanya hivyo. Alikuwa na umri wa miaka sitini na tatu wakati alipokufa ndani ya chumba cha mama Aisha kilichokuwa pembeni ya msikiti mtukufu wa Madina. Alizikwa katika chumba hicho ambapo pia baadae ndipo walipozikwa Abubakar na Umar “radiyallahu anhuma”. Wakati wa kutanuliwa msikiti, chumba hicho nacho kilimalizikia kuwa sehemu ya msikiti. Katika mwaka wa saba alimuoa Ummu Habiba mtoto wa Abu Sufyan bin Harb ambae alikuwa ni mmoja wa wakuu wa makuraishi wa Makka. Abu Sufyan ni baba wa Muawiya “radiyallahu anhu”. Yeye alisilimu baada ya kufunguliwa mji wa Makka. Mtume “sallallahu alayhi wasallam” pia alimuoa Hafsa mtoto wa Umar. Katika mwaka wa tano wa hijra mtume “sallallahu alayhi wasallam” alimuoa bibi Juwayria. Bibi huyu kutoka kabila la Bani Mustalaq alikuwa ni mtoto wa chifu na alitekwa katika vita vya Mureys. Mtume “sallallahu alayhi wasallam” alimnunua, akamuachia huru, kisha akamuoa. Pia kwa sababu mbali mbali za kidini aliwaoa Ummu salama, Sauda, Zaynab binti Huzayma, Maymuna na Safiyya “radiyallahu anhuma” Allah awawie radhi wote. Ndoa yake na Zaynab alifungishwa na Allahu taala.

Jibril “alaihis-salaam” alimjia Mtume “sallallahu alayhi wasallam” mara ishirini na nne elfu kwa ujumla wake. Alipelekwa safari ya Miraji akiwa na umri wa miaka hamsini na mbili. Katika umri wa miaka hamsini na tatu alihama Makka kwenda Madina. Yeye na Abubakar walihama pamoja na walikaa katika pango kwenye Mlima Thawr kwa muda wa siku tatu na wakaonda hapo pangoni usiku wa siku ya Jumatatu. Baada ya safari ya wiki moja waliwasili Quba, Kijiji kilicho ndani ya mji wa Madina. Ilikuwa ni siku ya Jumatatu tarehe 20 Septemba. Ijumaa iliofuata waliwasili Madina mjini.

Vita vya Badr vilipiganiwa mwaka wa pili hijria, siku ya Jumatatu ndani ya mwezi mtukufu wa Ramadhani. Jeshi la kiislam la watu 313 lilikabiliana na jeshi la makafiri wa kikureshi 1000. Masahaba 13 waliruzukiwa shahada. Abu Jahal na makafiri wengine 70 waliuliwa katika vita hivi.

Vita vya Uhud vilipiganwa katika mwezi wa Shawwal katika mwaka wa 3 Hijria. Jeshi la waislam lenye askari 700 lilikabiliana na jeshi la makafiri 3000. Masahaba 70 waliruzukwa shahada. Baada ya miezi minne, masahaba sabini walitumwa kwenda Najd kwa ajili ya kuwalingania wakazi wa huko. Walipofika katika sehemu inayoitwa **(Bi’ri Mauna)** walivamiwa na wote wakafa shahidi isipokuwa wawili tu.

Mwaka wa tano ulishuhudia vita vya Handak. Waislam 3000 walikabiliana na makafiri 10000. Makafiri waliuzingira mji wa Madina ambao tayari waislam walikwishauzungushia handaki. Mwaka mmoja kabla ya vita vya Khaybar ambavyo vilifanjika mwaka wa saba makubaliano yaitwayo **(Bi’atu Ridhwan)** yalifanyika hapo katika mji wa Hudaybiya. Vita vya **(Muta vilipiganiwa)** dhidi ya Mfalme wa Byzantine, Heraclius. Waislam 3000 chini ya kamanda Khalid bin Walid walipata Nusra dhidi ya Wabyzantin 100, 000. Jaffar Tayyar “radiyallahu anhu” aliruzukiwa shahada katika vita hivi. Makka ilifunguliwa katika mwaka wa nane. Vita vya **(Hunain)** ni vita vikubwa maarufu ambavyo pia vilimalizika kwa ushindi wa waislam. **(Haybar)** ilikuwa ni ngome maarufu ya Wayahudi. Mtume “sallallahu alayhi wasallam” alimpeleka Sayyid´na Ali na ngome hiyo ikafunguliwa. Sehemu hii ndipo mtume “sallallahu alayhi wasallam” alipopewa chakula chenye sumu na akakataa kukila. Wakati wa kurudi safari hii ndipo mama Aisha alipokumbwa na balaa la uzushi ambao ulimpa huzuni sana mtume wa Allah “sallallahu alayhi wasallam”. Uzushi huu baadae ulielezewa na kukanushwa kwa kushushwa aya tukufu. Ushindi wa Taif nao ni mashuhuri.

**Ikiwa unataka furaha ewe kiumbe,**
**Shikamana na uislam, ewe mwana kila wakati.**

**Fardhi, wajib, sunna na mandub,**
**Kuamrisha mema kwa ujumla wake.**

**Tekeleza kila wakati, usiachem,**
**Usiseme hili kubwa hili dogo.**

**Acha kila la haramu na makruh,**
**Hasa haki ya mja, chukua tahadhari.**

**Jifunze kutoka kwa ahli sunna,**
**Tekeleza kwa elimu usipitwe na muda**.

## KUHUSU VIPAMBANUZI VYA IMANI

Imani ina vipambanuzi kumi na mbili. Mola wangu mlezi ni Allah. Dalili yangu ya uthibitisho ni aya ya 163 ya Suratul Baqara. Mtume "sallallahu alayhi wasallam" wangu ni Muhammad "sallallahu alayhi wasallam". Dalili yangu ya uthibitisho ni aya za 28 na 29 za Suratul Fat´h. Dini yangu ni Uislam. Dalili yangu ya uthibitisho ni aya ya 19 ya Surat Ali Imran. Kitabu changu ni Quran tukufu. Dalili yangu ya uthibitisho ni aya ya 2 ya suratul Baqara. Kibla changu ni Kaaba sharif. Dalili yangu ya uthibitisho ni aya ya 144 ya suratul Baqara.

Madhehebu yangu ya kiitikadi ni yale ya **(Ahli sunnat wal jamaat)**. Dalili yangu ya uthibitisho ni aya ya 153 ya Suratul An'am.

Asili yangu ni Adam. Dalili yangu ya uthibitisho ni aya ya 172 ya Suratul A'araf

Mila yangu ni Uislam. Dalili yangu ya uthibitisho ni aya ya 78 ya Suratul Haj.

Umati wangu ni umati wa Muhammad alayhi salaam. Dalili yangu ya uthibitisho ni aya ya 110 ya Suratul Ali Imran.

Mimi ni muumini wa kweli. Dalili yangu ya uthibitisho ni aya ya 4 ya Suratul Anfal. Alhamdulillah ala tawfiq wa astaghfirullah minkulli taq´syr.

Elimu ni bora kuliko amal kwa sababu tano. Amali hutegemea elimu. Elimu ni muhimu na amali haiwezi kuiepuka elimu. Elimu inaweza ikawa na manufaa hata ikiwa pekee ila amali bila ya elimu haiwezi kuwa na manufaa.

Elimu ni bora kuliko akili kwa sababu elimu ni ya azali wakati akili imekuja baadae.

Pambo la mja ni ikhlas. Pambo la ikhlas ni iman. Pambo la iman ni Jannah. Pambo la Jannah ni mahuri, ghilman na kuuona uzuri wa Allahu taala.

Lau kama ingekuwa amal ni sehemu ya iman, basi kinamama wasingetengwa na swala wakati wa hedhi, kwa sababu imani si kitu chenye kuweza kutengwa.

Ni fardhi kusema neno la shahada kwa uchache mara moja katika uhai wake mtu. Dalili yake ya uthibitisho ni aya ya 19 ya Surat Muhammad.

Kuna masharti manne ambayo lazima yakamilishwe wakati wa kutamka shahada. Kuuhudhurisha moyo wakati ulimi unapotamka. Kujua maana ya unayoyatamka. Kuyasema kwa moyo yenye ukweli. Na kulisema hilo tamko kwa kulitukuza.

Kuna faida mia na thelathini za kutamka neno la shahada ila kama yatapatikana mambo manne basi faida hizo zote hutoweka. Mambo manne yenyewe ni shirki, shaka, tash´bih na ta’til.

Shirk ni kumfanyia Allah ushirika. Shaka maana yake ni kukosa uhakika. Tash´bih maana yake ni kumfananisha Allah na kiumbe fulani. Ta’til (likizo) ni kuamini na kusema (Allah hajishughulishi tena na mambo ya viumbe. Palipobakia ni kwamba viumbe vinakuja tu ufikapo wakati wao.)

Pia tunataja katika kitabu hiki thelathini kati ya hizo faida mia na thelathini. Miongoni mwa hizi thelathini tunazozitaja tano ni za duniani, tano ni za wakati wa kukata roho, tano ni za kaburini, tano ni za sehemu inayoitwa Arasaat, tano ni za motoni na tano ni za peponi. Faida tano azipatazo mtu duniani ni hizi zifuatazo:

1- Jina lake huitwa vizuri.

2- Hukmu za kiislam kwake huwa ni fardhi.

3- Shingo yake inasalimika na upanga.

4- Allah anamridhia.

5- Waumini wote wanampenda

Faida tano azipatazo mtu wakati wa kufa ni hizi zifuatazo:

1- Izra´il alaihis-salaam atamjia kwa sura iliyo nzuri.

2- Malaika wataitoa roho yake kwa upole na wepesi.

3-Harufu ya peponi ataanza kuisikia wakati huo.

4- Roho yake itapanda kwenda sehemu iitwayo Iliyun (mabustani matukufu) na malaika watahudhuria hapo.

5- Atakaribishwa kwa sauti itakayombashiria pepo.

Faida tano azipatazo mtu kaburini ni hizi zifuatazo:

1- Kaburi lake litakuwa pana lenye nafasi.

2- Malaika wenye kuwasaili watu kaburini watakuja kwa sura nzuri.

3- Malaika atamfunza yale asiyoyajua.

4- Allah atamuingizia ndani ya fahamu zake yale asiyoyajua.

5- Ataoneshwa malazi yake ya peponi.

Faida tano azipatazo mtu Arasaat ni hizi zifuatazo:

1- Atafanyiwa wepesi katika kusailiwa kwake.

2- Atapewa kitabu chake kwa mkono wa kulia.

3- Matendo yake mema yatakuwa mazito kwenye mizani.

4- Atakaa chini ya kivuli cha Arshi ya Rahman.

5- Atapita kwenye daraja la Sirat kwa haraka kama umesa.

Faida tano azipatazo mtu motoni ni hizi zifuatazo:

1- Lau kama ataingia motoni basi macho yake hayatakuwa rangi ya kiviju kama ya watu wengine wa motoni.

2- Hatogombana na shetani wake.

3- Hatofungwa pingu za moto wala hatavishwa vikuku vya moto shingoni.

4- Hatonyeshwa maji yaitwayo Hamim.

5- Hatoishi milele ndani ya moto.

Faida tano azipatazo mtu peponi ni hizi zifuatazo:

1- Malaika wote watamsalimia.

2- Atakuwa ni rafiki wa wale waitwao Siddiq

3- Atadumu milele peponi.

4- Allah atamridhia.

5- Atapata neema ya kuuona uzuri wa Allahu taala.

Kadhi Ahmed Efendi (1133-1197 Hijria [1783 miladi]) alisema maneno yafuatayo katika kuisherehesha **(Amantu)** katika kitabu kiitwacho **(Faraidhul fawaid).** Jahannam imeumbwa kwa tabaka saba. Kila tabaka, moto wake ni mkali zaidi kuliko tabaka la juu yake. Waislamu ambao wana dhambi ambazo hazikusamehewa wataingizwa katika moto wa tabaka ya mwanzo na kukaa humo kwa kadiri ya hesabu yao, kisha wataingizwa peponi. Tabaka sita zilizobaki ni za makafiri na watapangiwa tabaka kwa kadiri ya ukafiri wao. Wanafiki watakuwa katika tabaka ya chini kabisa. Hawa ni wale ambao

walikuwa wakijidhihirisha kama waumini lakini kiuhakika walikua ni makafiri. Wakati makafiri watakapochomwa na kuwa jivu, wataumbwa tena ili warudie kuchomwa, na hili litakuwa ni zoezi endelevu. Hivi sasa Jannat na Jahannam zipo tayari. Kufuatana na baadhi ya wanazuoni, Jahannam haijulikani ilipo. Wengine wanasema kwamba iko chini ya tabaka la saba la ardhi. Maneno haya yanaonesha kuwa haipo katika dunia kwa sababu dunia, jua na nyota zote ziko katika uwingu wa kwanza. Kwa popote tulipo katika dunia tunajua kwamba kuna mbingu saba hivyo Jahannam iko katika moja ya mbingu hizo.

## MAMBO YENYE KUSABABISHA UKAFIRI

Kuna aina tatu za ukafiri. Ukafiri wa inadi; ukafiri wa ujinga na ukafiri wa hukmu.

Ukafiri wa inadi ni ule ukafiri wa makusudi unaofanywa na watu wenye kuijua haki. Mfano wa hawa ni Abu Jahal, Namrudh, Shadad bin Ad na Firauni. Ni sahihi kusema kuwa hawa ni watu wa motoni.

Ukafiri wa ujinga; Hawa ni makafiri miongoni mwa watu wa kawaida ambao wanafahamu kwamba hii ni dini ya haki na wanasikia adhana ya Muhammad. Ila unapowaambia njooni kwenye Uislam hukujibu kwamba sisi tunaishi kwa mfumo ule tulioukuta kwa mababu zetu. Hii ndio njia yetu na tunaendelea nayo.

Kufuru ya hukumu maana yake ni kudhalilisha pale inapolazimu kutukuza na kutukuza pale inapolazimu kudhalilisha.

Vile vile ni kufuru kuwadhalilisha mawalii, mitume “sallallahu alayhi wasallam”, wanazuoni na matamshi yao, vitabu vyao na fatwa zao. Vile vile ni ukafiri kupenda tunu za makafiri na kuvaa bila ya dharura yale mavazi hasa kwa ajili ya dini yao kama ukanda wa padre au kuvaa msalaba.

Ukafiri unasababisha madhara saba. Unaondosha imani na kubatilisha ndoa. Kuwa kidufu anachokichinja na kuharamika kuliwa. Lile analolifanya na yule aliye wa halali kwake huwa zin´a. Kuwajibika kuuwawa. Janna huwa mbali nae. Jahannam huwa karibu nae. Akifa katika hali hiyo hasaliwi.

Mtu yeyote ambae ataapa kwa hiari yake na kusema kwa mfano (Mtu fulani hana kitu fulani. Kama si kweli niwe kafiri mimi au myahudi.) Ikiwa jambo hilo aliloliapia ni la kweli au sio la kweli, mtu huyu anakuwa tayari amejipelekea kwenye ukafiri yeye mwenyewe na ana wajibu wa kuitengeneza tena upya imani yake.

Jambo jengine linalotia katika ukafiri ni kutamani yawe halali yale mambo yaliyoharamishwa, mfano zin´a , riba na kusema uongo.

Ikiwa mtu atasema kwamba anamuamini Muhammad “sallallahu alayhi wasallam” lakini hajui juu ya utume wa Adam basi huwa kafiri. Vile vile ni ukafiri kutokutambua kuwa Hadhrat Muhammad ndie mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa mwisho.

Inaelezewa na wanazuoni kwamba kama mtu atasema (Ikiwa haya anayotuambia mtume “sallallahu alayhi wasallam” ni kweli basi tutaokoka.) Basi atakuwa kafiri. Birgivi “rahmatullahi alaih” ameongeza kwa kusema (Ikiwa mtu atasema hivyo kudhihirisha wasi wasi alionao basi huyo atakuwa kafiri. Lakini kama atasema hayo ikiwa ni sehemu ya hoja katika mjadala basi hatokuwa kafiri.)

Imeelezwa na wanazuoni wa kiislam kwamba, iwapo mtu atawaidhiwa ili asali nae akajibu hatosali basi huyo nae amekuwa kafiri.

Ila ikiwa kusudio lake kusema hivyo ni kwamba hatosali kutokana na maneno ya mzungumzaji lakini atasali kwa kutaka radhi za Allah, basi hatokuwa kafiri.

Ikiwa mtu ataambiwa asikate ndevu zake zikapungua urefu wa mkamato wa kiganja au asizirefushe kuzidi hapo, au akaambiwa akate kucha kwa sababu hiyo ndio sunna ya mtume “sallallahu alayhi wasallam” nae akasema hafanyi, basi huwa kafiri. Hiyo ndio hukumu ya sunna zote nyengine ambazo ni maarufu na zimepokelewa kwa njia ya tawatur na hakuna khitilafu katika usunna wake. Mfano wake ni kupiga mswaki wakati wa udhu. Hadhrat Birgivi ameongeza maelezo katika nukta hii kwa kusema (Itakuwa ni kufuru kama atasema kwa nia ya kukanusha hilo tendo la sunna. Lakini ikiwa anakusudia kusema kuwa hatotekeleza kwa kufuata maneno ya msemaji lakini atatekeleza kwa kuwa ni sunna basi hatokuwa kafiri.)

Katika kitabu kiitwacho **(Alhalal wal haram fil islam)** katika juzuu ya nne, ukurasa wa themanini na moja, mwandishi Yusuf Kardhawy anasema. Hadithi iliyonukuliwa katika kitabu kiitwacho **(Bukhari)** sharif (au Jamii sahih) inasema **(Ziachieni ndevu zenu na punguzeni sharubu zenu. Jitofautisheni na washirikina.)** Hadithi hii inakataza kunyoa ndevu zikawa fupi chini ya mkamato wa kiganja. Wanaoabudia moto hukata ndevu zao, na wengine hunyoa kabisa. Hadithi hii inatutaka tutofautiane na hao. Baadhi ya wanazuoni wa fik´h wanasema hadithi hii inaonesha ni wajibu kuweka ndevu na ni haramu kunyoa. Mmoja kati ya wanazuoni hao ni Ibn Taymiya. Yeye ameandika kwa jazba sana dhidi ya kukata ndevu. Kuna baadhi ya wanazuoni

wengine wanaoliona jambo la kuweka ndevu kuwa ni la kimila na wala sio la kiibada. Katika kitabu kiitwacho Fath kimemnukuu Iyad akisema kuwa ni makruh kukata ndevu bila udhuru. Huo ndio ukweli wa jambo hili. Hadithi hii haioneshi kuwa ni wajibu kuweka ndevu. Kuna hadithi inayosema **(Mayahudi na wakristo hawatii rangi nywele na ndevu. Fanyeni kinyume nao.)** Hadithi hii haioneshi kwamba ni wajib kupaka rangi nywele au ndevu. Inaonesha kuwa ni mustahab kufanya hivyo. Baadhi ya masahaba walipaka rangi nywele zao na ndevu zao, ila wengi wao hawakufanya hivyo. Lau kama lingelikuwa ni jambo la wajibu basi wote wangelilifanya. Na hukumu ndiyo hiyo hiyo kwa hadithi izungumziao kuweka ndevu. Inaonesha kwamba ni mustahab kuweka ndevu na wala sio wajib. Hakuna mwanazuoni aliyetajwa kunyoa ndevu zake kwa sababu ndio iliyokuwa mila ya wakati wao (kutokufata mila inaonesha uovu, bali inaweza kuwa haramu kama italeta fitna). Maelezo kutoka kitabu cha Yusuf Kardhawi yanamalizika hapa. Mwanzoni mwa kitabu chake, Qardhawi ameandika kwamba yeye anachanganya fikh za maimamu wote wanne na wala hahisi ulazima wa mtu kujinasibisha na dhehebu fulani. Kwa mtizamo huo amekengeuka mafunzo ya wanazuoni wa ahli sunna. Wanazuoni wa ahli sunna wanaeleza kwamba muislam anatakiwa kumfuata mmoja wa wanazuoni wanne na yule mwenye kuchanganya madhehebu zote basi atakuwa hana madhehebu, mzandik. Lakini kwa vile maandishi ya Qardhawi kuhusu hukumu ya ndevu yamewiana na mafunzo ya madhehebu ya Hanafi, hivyo imeonekana kuwa hakuna tatizo kuyatumia maneno yake kama dalili. Hadhrat Abdulhaqi Dahlawi "rahmatullahi alaih" (958 -1050 hijria, 1551-1642 miladia) amesema katika juzuu ya tatu ya kitabu kiitwacho (**Ashiatul lamaat)** (Wanavyuoni wa kiislam hufuata mila za sehemu wanazoishi katika jambo la kupaka rangi ndevu na nywele, kwa vile huonekana ni ukorofi kutokufuata mila ya mji wako (katika mambo yaliyo halali) jambo ambalo kiuhakika ni makruh. Muhamad bin Mustafa Hadimy "rahmatullahi alaih" (alikufa 1176 hijria, 1762 miladia, Hadim , Konya , Uturuki) amesema katika kitabu chake kinachoitwa **(Berika)**, imetajwa katika hadithi kwamba **(Zifanyeni fupi sharubu zenu na zifanyeni ndefu ndevu zenu).** Hivyo imekatazwa kunjoa au kukata ndevu zikawa ndogo kuliko mkamato wa kiganja. Ni sunna kuachia ndevu hadi zikafikia urefu wa mkamato wa kiganja. Vile vile ni sunna kuzipunguza zitakapozidi urefu huo. Mkamato wa kiganya ni sawa na upana wa vidole vinne kuanzia chini ya mdomo wa chini. Wakati sultan anapoamrisha jambo la sunna, hata kama litakuwa ni jambo la mubaha, basi inakuwa ni wajibu kulitekeleza. Wakati linapotekelezwa na Sultan

na watu wengine, basi katika sehemu kama hiyo itakuwa ni wajibu kuziachia ndevu kwa urefu wa mkamato wa kiganja. Kuzikata zikawa fupi kuliko mkamato wa kiganja au kuzinyoa kabisa itakuwa ni kuliwacha jambo la wajibu. Hiyo itakuwa ni Makruh tahrimy. Haifai kwa mtu kama huyo kuwa imam wa sala msikitini. Katika nchi za kikafiri inaruhusika kukata au kunyoa ndevu bali pia inaweza kuwa ni wajibu katika baadhi ya hali kama vile kuadhibiwa, kupoteza ajira au ikiwa itashindikana kutoa huduma kwa waislam au itaathiri imani yako na heshima yako. Ni makruh kukata ndevu zikawa fupi kuliko mkamato wa kiganja na itakuwa ni bid'a kama mtu atakuwa akiendeleza tabia ya kukata hivyo hali ya kuamini kwamba anafanya sunna. Hio ina maana ya kuibadilisha sunna. Kufanya bid'a ni dhambi kubwa kuliko kujiua.

Ikiwa mtoto wa kike na wa kiume wamefikia ukubwa na wakaozeshwa ndoa ya kiislam lakini walipoulizwa juu ya imani wakashindwa kujibu, hii ina maana hawakuwa waislam. Ndoa yao itasihi baada ya wao kufunzwa nguzo za iman na kisha kufungishwa tena ndoa. Angalia mlango unaohusu fardhi hamsini na nne.

Ikiwa mtu atapunguza sharubu zake na mwenzie alie pamoja nae akamwambia (sio vizuri), basi huyu mtu wa pili anakhofiwa kupoteza imani yake. Hii ni kwa sababu kupunguza sharubu ni sunna na huyu ameonesha kutokuijali sunna hiyo.

Ikiwa mwanamme atavaa hariri ikamfunika kiwiliwili kizima halafu akaambiwa na mwenzie (ubarikiwe kwayo) pia inakhofiwa kuwa huyu msemaji anaweza akapoteza imani yake.

Ikiwa mtu atafanya jambo la makruh kama kulala na kuelekeza miguu upande wa kibla au kutema mate au kukojoa upande wa kibla, kisha watu wengine walipomuasa asifanye hivyo yeye akajibu (laiti dhambi zetu zote zingekuwa ni nyepesi kama lilivyo jambo hili) huyu nae anakhofiwa kupoteza imani yake. Hii ni kwa sababu amelizungumzia jambo ambalo ni makruh kama kwamba halina umuhimu wowote.

Iwapo mtumishi ataingia chumbani kwa bwana wake na akamsalimia kwa kusema (Assalamu alaykum) na ikawa mtu aliye pale akamwambia (nyamaza wewe mkosefu wa adabu, hayo ndio maneno gani ya kumuamkilia bwana wako) basi msemaji atakuwa kafiri.

Lakini kama lengo la kusema hivyo ni kumfunza namna mtumishi anavyotakiwa amsalimie bwana wake kwa maana ya kwamba angeweza kusalimia kimya kimya moyoni, basi bila shaka kwa hilo haitokuwa ukafiri.

Ikiwa mtu atamsengenya mtu mwengine kisha wale waliomnasihi akawajibu (Kwani jambo gani kubwa nililofanya mnalolipigia kelele!) naye huwa ni kafiri kwa mtizamo wa wanazuoni. Hii ni kwa sababu ameliunga mkono jambo la haramu badala ya kulipinga.

Ikiwa mtu atasema (Hata Allah akinipa pepo basi siwezi kuingia bila wewe) au (Kama nitaingizwa peponi na fulani, siingii) au (Allah akinipa pepo siitaki lakini kumuona yeye na uzuri wake ninataka) basi maneno ya aina hii yote ni kufur kwa mtizamo wa wanazuoni.

Kauli nyengine inayoambiwa na wanazuoni kwamba inasababisha ukafiri ni kusema kuwa imani inazidi na kupungua. Birgivi anasema juu ya hili kwamba ikiwa huko kushuka na kupanda atakusudia kwa muktadha wa **(Muuminun bih)** basi itakuwa ni kufur. Lakini kama atakusudia kwa muktadha wa (yaqin na quwwat sadik) basi haitokuwa kufur. Kuna mujtahid wengi ambao wamesema kuwa imani inazidi na kupungua.

Kufuatana na wanazuoni ni kufur kusema kuwa kuna vibla viwili. kimoja kiko Makka na kimoja kiko Jerusalem. Kufuatana na Birgivi ni kufur kusema kuna vibla viwili ila si kufur kusema kwamba siku za nyuma kibla kilikuwa Baytul muqaddas baadae kikabadilishwa na kuwa Makka.

Ikiwa mtu atamchukia au kumbughudhi mwanazuoni bila ya sababu inakhofiwa anaweza akawa kafiri.

Ikiwa mtu ataipenda ibada fulani ya makafiri ambayo iko kinyume na Uislam na akaitakidi kuwa ibada hiyo ni nzuri basi atakuwa amekufuru.

Iwapo mtu atasema kukaa kimya wakati wa kula ni katika ada nzuri za Majusi (waabudia juwa) au akasema kutokuwaingilia wanawake wakati wa hedhi au baada ya uzazi ni katika ada nzuri za Majusi basi atakuwa amekufuru.

Ikiwa mtu atamuuliza mwengine kama ni muumini au la, nae akajibu (Inshaallah… .) Itakuwa ni ukafiri kama atashindwa kuelezea alichokusudia.

Ikiwa mtu atafiwa na mtoto kisha mwengine akamwambia (Allah ana uhitaji wa mwanao) basi msemaji haya atakuwa kafiri.

Ikiwa mwanamke atavaa mkanda mweusi wa kitambaa kiunoni na atakapoulizwa akasema kuwa hiyo ni Zunnar (mikanda ya mapadri) basi atakuwa kafir na ataharamika kwa mumewe.

Imeelezwa kwamba mtu kusema (Bismillah) anapoanza kula chakula cha haramu ni kufuru. Anasema Birgivi itakuwa ni kufuru ikiwa hicho chakula ni haramu kwa nafsi yake kama nyama ya mnyama aliekufa mwenyewe na pombe. Sheria hii itahusika pale mtu atakapojua kuwa anachokila ni kitu haramu kwa nafsi yake. Kufanya hivyo atakuwa amelifanyia istihzai jina la Allah. Kama ilivyoelezwa na maimam wetu ikiwa mtu atapiga Bismillahi wakati wa kula chakula alichokiiba, chakula chenyewe hakitokuwa haramu ila wizi ndio haramu.

Ikiwa mtu atamlaani mwenzie na kumwambia (Allah aichukue roho yako ukiwa katika ukafiri) hili wamekhitilafiana wanazuoni kama litamfanya msemaji awe kafiri au la.

Na ikiwa mtu yeye mwenyewe atakubali akiambiwa kafiri basi hiyo ni kufur; lakini pia wanazuoni wamekhitilafiana kwa hili. Ama kumwambia mwengine kuwa ni kafiri basi hilo linaambiwa kuwa kufur. Hapa pia kuna hali mbili.

Ikiwa kumwita kafiri kunakusudiwa ukafiri wenyewe hasa basi hilo ni kufur lakini.

Ikiwa kumwita hivyo kunakusudiwa kuwa adhabu zake zitakuwa kali kutokana na makosa yake basi hiyo haitakuwa kufur. Anasema Birgivi kwamba (Tunafahamu umuhimu wa kauli hii ya wanazuoni. Na kisa cha kweli cha Hadhrat Musa „alaihis-salaam" ndani ya kur´an ni dalili ya hili.)

Ikiwa mtu atasema (Allah anajua kuwa mimi sikufanya hili) hali ya kuwa mwenyewe anajua fika kuwa amefanya jambo hilo, basi huo ni ukafiri. Sababu kusema hivyo ni kumsingizia ujinga Allah.

Ikiwa mtu atamuoa mwanamke bila ya kuwa na shahidi kisha akasema Allah na mtume "sallallahu alayhi wasallam" wake ndio mashahidi wao basi wote watakuwa wamekufuru. Sababu ni kwamba Mtume "sallallahu alayhi wasallam" hajui mambo ya ghaib.

Ikiwa mtu atadai kwamba anao uwezo wa kujua kilipo kitu kilichopotea au kuibiwa basi atakuwa kafir. Aidha kama atasema ana majini yanayompa habari basi kwa mara nyengine tena atakuwa kafiri. Mitume "sallallahu alayhi wasallam" na majini hawajui ghaib. Ni Allah pekee ndie ajuae ghaib na ila wapo na wale anaowatambulisha.

Ikiwa mtu atataka kuapa kwa jina la Allah na mwenzie akamwambia (sitaki kiapo cha jina la Allah. Nataka kiapo kiapwe kwa

vitu kama talaka, kuacha huru mtumwa au heshima) basi mtakaji haya atakuwa kafiri.

Iwapo mtu atamwambia mwenzie (Umbo lako linanikumbusha malaika wa mauti) basi atakuwa amekufuru kwa sababu malaika wa mauti ni kiumbe kitukufu.

Iwapo mtu atasema (Ni raha kubwa mtu kuwa husali) basi huyo huwa kafir. Aidha ikiwa mtu ataambiwa na mwenziwe asali yeye akajibu (Kwangu mimi kusali ni jambo zito) naye pia huwa kafiri.

Yeyote atakaesema (Allahu taala aliye mbinguni ni shahidi wangu) amekufuru kwa sababu amemtaja Allah katika kuwepo mahali na Allah ametakasika na mahali.

Mtu ambae atamuita Allahu taala. (Baba) basi atakuwa amekufuru.

Iwapo mtu atasema Mtume “sallallahu alayhi wasallam” alikuwa akiramba vidole vyake baada ya kula mwengine akasema (hio ni tabia chafu) basi huyu atakuwa nae amekufuru.

Atakaesema (Mtoaji riziki ni Allah lakini na harakati za binaadamu ni za lazima) hii ni kauli ya shirk. Harakati za binaadamu pia huumbwa na Allah.

Ikiwa mtu atasema ni bora kuwa Nasrani kuliko kuwa myahudi (au kusema kuwa bora kuwa mkiristo wa kimarekani kuliko kuwa mkomunisti) nao ni ukafiri. Ni vyema kusema myahudi ni muovu zaidi kuliko Nasrani au mkomunisti ni muovu zaidi kuliko mkiristo.

Kusema kwamba bora kuwa kafiri kuliko kufanya khiana ni ukafiri.

Yeyote atakaetoa sadaka kwa mali ya haramu kisha akategemea kupata thawabu, na yule aliyepokea akamtakia rehema kwa Allah hali ya kuwa anajua kuwa sadaka ile imetokana na haramu, kisha mtoaji nae akaitikia Amin, wote wawili wanakuwa makafiri.

Iwapo mtu atasema (Mimi kwenye madarsa nikafanye nini) au (Hayo maneno ya wanazuoni nani atayafuata) au akaitupa chini kwa makusudi karatasi iliyoandikwa fatwa au akasema (Haya maneno ya wanazuoni hayana maana) basi atakuwa kafiri.

Ikiwa mtu atakosana na mwenzie na akamwambia waende kwenye mahakama inayohukumu kwa searia za Allah na yeye akasema (Mimi siendi huko labda nibururwe na polisi) au akasema (Mambo ya Uislam ninayajuaje mimi) basi msemaji huyu huwa kafir.

Iwapo mtu atasema neno la kufur, yeye na yeyote atakaecheka kwa neno hilo basi atakuwa kafir. Haitokuwa kufuru kucheka kama itakuwa si kwa kukusudia ila kwa kughilibiwa na kicheko na kushindwa kukizuia.

Imeelezwa kwamba ikiwa mtu atasema (Hakuna sehemu yoyote ambayo Allah hayupo) au akasema (Allah yuko mbinguni) basi hayo ni kufur.

Ikiwa mtu atadai kwamba roho za mashekhe zipo kila wakati na zinajua yanayoendelea basi atakuwa kafiri.

Yeyote atakaesema (Sina habari na Uislam(siutaki)) basi atakuwa kafir.

Yeyote atakaesema kuwa (Lau Adam „alaihis-salaam" asingekula ngano, basi tusingekuwa kwenye mashaka haya) basi atakuwa kafiri. Wanazuoni wametofautiana katika jambo la kusema (Lau Adam „alaihis-salaam" asingekula ngano, basi tusingekuwa duniani sasa) kuwa ni kufuru au la.

Ikiwa mtu atasema Adam alikuwa akitengeneza vitambaa hivyo mwengine akasema (Basi sisi ni watoto wa mtengeza vitambaa) huyu msemaji wa pili atakuwa kafir.

Iwapo mtu atatenda dhambi ndogo kisha akaambiwa na mwenziwe alete toba yeye akasema (Kwa dhambi gani niliyofanya hata nilete toba!) basi atakuwa kafiri kwa hilo.

Ikiwa mtu ataambiwa na mwenzie waende kwa mwanazuoni au wasome vitabu vya elimu za kiislam nae akajibu (Elimu za kiislam zimenihusu nini mimi) basi huyo atakuwa kafir. Hii maana yake ni kuzidharau elimu za dini. Mtu yeyote atakaevidharau, kuvitukana au kuvidhihaki vitabu vya tafsiri au fiq´h basi atakuwa kafiri. Makafiri wenye kuvihujumu vitabu hivi vilivyoandikwa na wanazuoni wa ahlu sunna huitwa wazandik.

Yeyote ambae atashindwa kutoa jawabu za maswala kama (Wewe unatokana na kizazi cha nani) au (Mila yako ni ipi) au (Ni nani imam wako wa madhehebu ya kiitikadi) au (Ni nani imam wako wa madhehebu ya kiamali), basi atakuwa ni kafir.

Ikiwa mtu atasema kuwa kitu fulani ni halal hali ya kuwa kitu hicho kinajulikana kwa uhakika kuwa ni haramu kama pombe na nguruwe, au akasema kuwa kitu fulani ni haramu hali ya kuwa kitu hicho kinajulikana kwa uhakika kuwa ni halali basi mtu huyo huwa kafir (Ni hatari kusema kuwa sigara ni haram).

Ni kufuru kutamani kwamba lau jambo fulani la haramu lingehalalishwa na ilhali jambo hilo liliharamishwa kwa umati zote na kwamba kuhalalishwa hakukubaliani na hekima. Mfano wa haya ni zinaa, liwati, kujilazimisha kula baada ya kushiba na kuchukua riba. Sio

kufuru kutamani kuwa pombe ingefanywa halali kwa sababu pombe haikufanywa haramu kwa umati zote. Ni kufuru kuzitumia aya za Quran kwa kufanyia mzaha. Mtu kumwambia mwenziwe mwenye jina la yahya (**Ya Yahya khudhil kitaaba)** atakuwa kafiri kwa sababu amezifanyia mzaha aya za Quran. Hukmu ni hiyo hiyo kwa yule asomae Qurankafuatana na ala za muziki, nyimbo au dansi.

Ni kosa kubwa kusema (Ndio kwanza nimefika, Bismillah.) Au akasema aonapo kitu kingi **(Ma khalakallah)** hali ya kuwa hajui maana yake.

Ni kosa kubwa mtu kusema (sikutukani sasa hivi. Wameeka dhambi katika jambo la kutukana.)

Ni kosa kubwa kusema (Uko uchi kama mguu wa Jibril) kwa sababu hii ni kuonesha dharau kwa Jibril.

Ni haram kuapa kwa jina la kitu chochote isipokuwa Allah. Mtu hatokua kafiri kwa kutenda tendo la haramu ila atakuwa kafiri kama atasema kuwa ni halali jambo ambalo limeharamishwa kwa dalili iliyo wazi kabisa.

Pia ikiwa mtu ataapa kwa kichwa cha mwanawe au kwa kichwa chake na kutumia jina la Allah mfano kusema (Wallahi kwa kichwa cha mwanangu) inakhofiwa kuwa inaweza kuwa ni ukafiri.

## HUKUMU ZA UISLAM

Maamrisho na makatazo ya Uislam kwa ujumla wake huitwa **(Ahkam Islamiya)** au **(Uislam)** nao una hukmu nane. **Fardh, wajib, sunna, mustahab, mubah, haram, makruh, na mufsid.**

Fardh ni amri ya Allah iliyothibitishwa kwa dalili isiyo na mjadala yaani imeelezwa wazi kwa aya ya Quran. Mtu mwenye kulikataa au kutokulipa umuhimu jambo lenye sifa hiyo basi huwa kafiri. Mfano wa mambo haya ni imani, Quran, kutia udhu, kusali, kutoa zaka, kuhiji, na kukoga janaba.

Fardhi ziko aina tatu nazo ni Fardhi daim, Fardhi muwakkat, na Fardhi kifaya, Fardhi daima ni kuhifadhi, kujua maana na kuamini nguzo zote sita za imani **(amantubillah)** na kudumu nayo imani hiyo kila wakati. Fardhi muwakat ni zile ibada zote tulizoamrishwa na tukawa tunazitekeleza wakati wake unapofika kama vile sala, kufunga Ramadhani na kujifunza ueledi wa sanaa au biashara ambayo mtu anaifanya. Farditikadihi kifaya ni ile amri ambayo ikiwa itatokea mtu mmoja kuitekeleza basi itatosheleza kwa wale waliopo bila kujali idadi yao. Mfano wake ni kujibu salamu, kukosha na kumsalia maiti,

kujifunza elimu za nahw  na sarf na kuzihifadhi na kusoma elimu za sayansi na dini zaidi ya uhitaji wa sanaa au biashara anayojishughulisha nayo mtu.

Vile vile kuna Fardhi tano ndani ya fardhi. Fardhi hizi ni ilmul fardh, amalul fardh, mikdarul fardh, itikadi fardh, ikhlas fardh na inkaru fardh. Inkaru fardhi ni kufur.

Wajib ni lile jambo ambalo Allah ameliamrisha ila dalili ambayo imeliamrisha jambo hilo ina mitizamo katika kufahamu kwake. Jambo kama hili kulikataa kwake haiwi kufuru ila kuliacha kwake kulitekeleza inapelekea kuingia motoni. Mfano wa haya ni kusoma dua ya kunuti katika sala ya witri, kuchinja mnyama katika siku za idi ya kuchinja, kutoa zakatul fitri katika idi ya Ramadhani na kuleta **sijdati tilawa** wakati wa kisomo. Kuna wajib nyengine nne na fardh moja ndani ya wajib. Ilm wajib, amal wajib, iitiqad wajib, mikdar wajib na ikhlas fardhi. Ni haramu kufanya riya katika jambo la fardhi au wajib.

Sunna ni lile jambo ambalo Mtume “sallallahu alayhi wasallam” amewahi kutokea kuliacha kulifanya mara mbili tatu. Mtu kuliacha kulifanya jambo hili hatoadhibiwa. Kuliacha jambo hili bila udhuru tena kwa kuendelea kutamfanya mtu apate itab na kukosa thawabu za jambo hilo. Mfano wake ni kutumia mswaki wakati wa udhu, kusoma adhana na ikama, kuswali sala na jamaa, kulisha chakula cha harusi na kumtahiri mtoto wa kiume. Kuna aina tatu za sunna.

Sunnat muakkada (iliyopewa nguvu), Sunnat ghayru muakkada (isiyopewa nguvu) na sunnatul kifaya (ya kutosheleza) Mfano wa sunnat muakkada ni. Suna ya sala ya asubuhi, suna za kabliya na baadiya za sala ya adhuhuri, suna ya sala ya magharibi na suna ya baadia ya sala ya isha. Hizi ni sunnat muakkada. Kuna wanazuoni wanaosema kuwa sunna ya sala ya asubuhi ni wajib. Sunna hizi haifai kuziacha bila udhuru. Asiezipenda huwa kafiri.

Sunnat ghayri muakkada ni sunna za sala ya laasiri na sunna ya kablia ya sala ya isha. Hizi hata kama zitaachwa mara nyingi basi hailazimu kitu. Kuziacha kikamilifu bila ya udhuru wowote husababisha mtu kupata itab na kukosa shafaa siku ya kiama.

Kama inavyozungumzwa katika **(Halabi)** na **(Quduri)** kwamba matendo ya ibada yako aina mbili **(Faraidh)** na **(Fadhail)**. Yale matendo ya ibada ambayo si fardhi wala wajib huitwa (**Fadhail)** au **(Naafila)**. Sunna zinazosaliwa pamoja na sala tano huitwa naafila na hukamilisha mapungufu yanayotokea katika sala za fardhi. Hii haina maana kwamba sala ya sunna ina uwezo wa kuchukua nafasi ya sala ya fardhi.

Sala ya sunna haiwezi kumuokoa mtu na adhabu ya kuacha sala ya fardhi. Sala ya sunna iliyosaliwa na mtu alieacha sala ya fardhi bila ya udhuru haikubaliki. Sunna iliyo sahihi lazima isaliwe na nia yake. Bila ya nia sala ya sunna haitokuwa sahihi. Kwa hivyo yule mtu ambae kwa miaka kadhaa hakuwa akisali, wakati anasali sala za sunna za nyakati nne, atie nia ya sala ya kadha ya wakati ule pamoja na nia ya sala ya sunna ya wakati ule. Akitia nia kwa mtindo huo atakuwa amelipa sala ya wakati ule na pia amesali sala ya sunna, hivyo sunna itakuwa haikuachwa.

Sunnat kifaya ni ile sunna ambayo akiifanya mtu mmoja basi jukumu la wengine waliobakia nalo huondoka. Mfano wake ni kuitikia salamu, kukaa itikafu na kupiga Bismillahi wakati wa kuanza kufanya jambo.

Ikiwa mtu atakula bila kupiga Bismillahi madhara matatu atayapata: 1- Shetani ataungana nae katika kula hicho chakula. 2- Chakula kitamsababishia maradhi mwilini. 3- Chakula kitakuwa hakina baraka.

Iwapo atapiga Bismillahi wakati wa kula atapata faida tatu: 1- Shetani hatopata fungu katika chakula. 2- Chakula anachokula kitakuwa ni dawa mwilini. 3- Chakula kitakuwa na baraka. Ikiwa mtu atasahau kupiga Bismillahi anapoanza kula, basi wakati wowote atakapokumbuka ataisema.

Mustahabbu ni yale mambo ambayo Mtume “sallallahu alayhi wasallam” aliyafanya mara mbili tatu tu katika uhai wake. Mtu ambae hatolifanya jambo hilo hatopata adhabu yoyote duniani wala akhera na wala hatokosa shafaa siku ya kiama. Mfano wa haya ni sala za nafila, funga za nafila, kutekeleza umra, hija ya nafila na sadaka ya nafila.

Mubah ni jambo lililoruhusiwa na ambalo likifanywa kwa nia njema linaweza kumpatisha mtu thawabu ila likifanywa kwa nia mbaya linaweza kumpatisha mtu dhambi. Kuliacha hakuleti madhara yoyote. Mfano wa haya ni kutembea, kukaa, kununua nyumba, kula aina zote za vyakula halali na kuvaa aina zote za nguo ambazo ni halali

Haramu ni lile jambo ambalo Allah amelikataza wazi wazi kupitia aya za Quran. Mtu mwenye kulikana jambo hilo au akalichukulia wepesi basi huwa kafiri. Ikiwa mtu atafanya jambo la haramu lakini halikani kuwa ni haramu huyo hatokuwa ni kafiri, bali atakuwa Fasik. Ibni Abidin “rahmatullahi alaih” amesema maneno yafuatayo kuhusu mtu fasik kuwa imam katika sala (usisali nyuma ya imam ambae ni fasik. Fasik maana yake ni muislam mwenye kufanya dhambi kubwa kama kuzini, kulewa na kula riba. Madhambi madogo endelevu nayo

hugeuka yakawa makubwa. Ikiwa katika mji kuna msikiti zaidi ya mmoja unaosaliwa ijumaa basi inatakiwa kusali katika ule msikiti ambao imam wake ni salih. Ni wajibu kumfanyia khiyana na kumdharau mtu fasik. Hafai kuwekwa imam hata kama atakuwa na ilmu nyingi. Kumpa uimamu maana yake ni kumuheshimu na kumutukuza. Ikiwa mtu ni fasik tena mpinga madhehebu basi itakuwa ni Makruh muharram kumfanya imam. **(Taqwa)** ni kuacha yale ya haram. **(Waraa)** ni kuacha mambo ambayo yanatiliwa wasi wasi kuwa ni halali au haramu. Kuacha la halali kwa kuogopa kuingia kwenye jambo lenye shaka huitwa **(Zuhd)**. Wakati mtu anaishi katika nchi za makafiri, akisilimu ni wajibu ahamie nchi za kiislamu.

Kuna aina mbili za haramu. **(Haramu li ainihi)** na **(Haramu li ghayrihi).** Haramu li ainihi ni jambo ambalo kwa nafsi yake ni haramu mfano kujiiua, kuzini na kufanya livati, kunywa pombe, kucheza kamari, kula nguruwe na wanawake kutembea bila stara inayostahiki. Ikiwa mtu atapiga Bismillahi wakati wa kuanza kufanya jambo lolote miongoni mwa haya, au akakanusha uharamu wake au akawa haupi umuhimu uharamu wake basi huyo atakuwa kafiri. Lakini ikiwa mtu atafanya matendo haya hali ya kuwa anaamini kuwa ni haramu na anaogopa adhabu ya Allah basi huyo hatokuwa kafiri bali atastahiki adhabu.

Haram li ghayrihi ni mambo ambayo yenyewe binafsi si haramu ila yamepatikana kwa njia haramu mfano kuingia shambani kwa mtu ukachuma tunda na kulila, kumuibia mtu nyumbani kwake au pesa zake kisha ukazitumia. Ikiwa mtu atapiga Bismillahi wakati wakuanza kufanya mambo haya, au akasema kuwa ni halali basi hatokua kafiri. Mtu yeyote atakae chukua kitu cha mtu mwengine chenye uzito wa punje ya ngano basi siku ya kiama Allah atachukua kutoka kwa mtu huyo thawabu zenye thamani ya rakaa mia saba zilizosaliwa jamaa na kukubaliwa na kumlipa huyo mwenziwe. Inafaa kujiweka mbali na aina zote mbili za haramu. Kuna thawabu nyingi katika kujiepusha na haramu kuliko katika kutenda ibada.

Makruh maana yake ni jambo ambalo linaharibu thawabu ya jema lililotendwa. Kuna aina mbili za Makruh. Karahati tahrimiyya (Makruh tahrimy) na Karahati tanzihiyya (makruh tanzihy).

Karahati tahrimiyya ni kuacha kitu ambacho ni wajib na hii iko karibu na haramu. Karrahat tanzihiyya ni kuacha jambo la sunna nayo iko karibu na halali. Ikiwa mtu atafanya karahat tahrimiyya kwa makusudi basi anakuwa mja asie mtiifu na anapata dhambi, na

anastahiki adhabu. Kama atafanya hilo kwenye sala basi atalazimika kusali tena. Na ikiwa atafanya kwa kusahau basi ataleta sijdatu sahwi mwisho wa sala na wala hatoirejea sala yake. Mtu aliefanya karahatu tanzihiya hatoadhibiwa siku ya kiama lakini atakosa shafaa kama atafanya kwa kuendelea. Mfano wa haya ni kula nyama ya farasi, kula mabaki ya chakula alichokula paka na panya na kumuuzia zabibu mtengeneza pombe.

Mufsid ni yale mambo yenye kuziharibu amali kwa kikamilifu. Mfano wake ni kuharibu imani, sala, nikah, hajji, zaka na mauzo.

Muislam ambae anatekeleza fardhi, wajib na sunna na kuacha haram na makruh basi atalipwa mema huko akhera. Ikiwa mtu atafanya haram na makruh na kuacha fardhi na wajib basi huyo atanukuliwa kuwa ni mtu muovu. Thawabu za kujiepusha na haram ni nyingi kuliko thawabu za kutekeleza fardhi. Thawabu za kutekeleza fardhi ni nyingi kuliko zile za kuacha makruh. Na zile za kuacha makruh ni nyingi kuliko zile za kufanya sunna. Miongoni mwa mambo halali kuna yale yanayoitwa khayrat na **(Hasanat)** ambayo mtu hupata thawabu kwa kuyafanya ila thawabu zake ni chache zikilinganishwa na zile za sunna. Kufanya jambo lenye kupatisha thawabu hali ya kuuelewa na kuukusudia wema wake huitwa **(Qurubat)** (kujikurubisha).

Allah kwa rehema zake kwa watu amewapelekea dini ambayo ni chanzo cha furaha na utulivu. Dini ya mwisho ni hii iliyoshushwa kwa Mtume “sallallahu alayhi wasallam” Muhammad “sallallahu alayhi wasallam”. Dini zilizopita nyuma wafuasi wake waovu walizibadilisha. Mtu yeyote ikiwa ataishi sawa na mafunzo ya dini hii, ikiwa anafanya hayo kwa kujua au la, ikiwa ni muislam au kafiri, basi atapata maisha mazuri yasiyo na matatizo hapa duniani. Mfano wa haya ni wale makafiri wa marekani na watu wa ulaya ambao wanaishi kwa misingi inayokubaliana na uislamu. Ila makafiri hawatapata malipo huko akhera kwa wema wanaoutenda hapa duniani. Mema hayo yanapofanywa na muumini kwa kutegemea malipo ya Allah basi atapata raha za milele huko akhera.

## JENGO LA UISLAM

Uislam umejengwa juu ya nguzo tano. Nguzo ya kwanza ni kusema neno la shahada na kujua na kuamini maana inayobebwa na neno hilo. Nguzo ya pili ni kusimamisha sala mara tano kwa siku katika nyakati zake zilizopangwa. Nguzo ya tatu ni kufunga siku zote katika mwezi mtukufu wa Ramadhan. Nguzo ya nne ni kulipa zaka na ushuru mara

moja kwa mwaka baada ya kukamilia masharti yake. Nguzo ya tano ni kutekeleza ibada ya hija kwa mwenye uwezo. Kutekeleza mambo haya na kuacha yale Allahu taala aliyoyakataza yaitwayo haram ndio huitwa kuabudu. Kwa mtu ambae masharti yake hayajakamilia au kwa yule ambae ameshakwenda kufanya hija akafanya mara ya pili basi inakuwa ni nafila kwake. Haijuzu kufanya jambo la nafila ambalo litapelekea kufanyika jambo la bid'a au la haram. Imam Rabbani "rahmatullahi alaih" katika barua yake ya 29, 123 na 124 na Abdalla Dahlawi "rahmatullahi alaih" katika barua yake ya 26 ya kitabu kiitwacho **(Maqamati Mazhariyya)** hawakuruhusu kufanya nafila ya hajji na umra. Afifudyn Abdalla bin Asad Yafii "rahmatullahi alaih" (698-768 hijria, 1298-1367 miladia, aliezaliwa Yemen na kufia Makka) katika kitabu chake kiitwacho **(Nasr ul mahasin il ghaliya)**, wakati akizieleza daraja za Zuhud katika maqamati ashara (daraja kumi) anasema (Mwanazuoni mkubwa na walii Imam Nawawy wakati alipoulizwa Unafanya aina zote za sunna lakini umeacha ndoa ambayo ni moja kati ya sunna muhimu. Alijibu Nina wasiwasi nisije nikafanya mambo mengi ya haramu kwa kutekeleza hiyo sunna moja) Imam Yahya Nawawy alifariki Damascus mwaka 676 hijria (1277 milady) Profesa Habibu Rahman, mkuu wa chuo cha **(Jamia Habibiyya)** huko Pakistan wakati alipokwenda hija mwaka 1401hijria (1981 miladia) na akaona imam wa kiwahabi akisalisha kwa kutumia kipaza sauti, yeye alijitenga na kusali peke yake. Hapo alikamatwa akatiwa pingu na kupelekwa kituoni. Wakati alipohojiwa kwa nini hakujumuika katika sala ya jamaa alijibu kwamba haijuzu kwa imam mwenye kusalisha jamaa kutumia kipaza sauti. Kwa jawabu hilo alizuiliwa kutekeleza hija na akatolewa katika nchi.

Jambo la mwanzo linalomlazimikia mtu ni kujifunza misingi ya imani yake. Zamani ilikuwa ni rahisi kujifunza dini kutoka kwa wanazuoni kwa sababu walikuwepo wengi. Ila katika zama zetu hizi za mwisho wanazuoni hawapo tena. Wajinga na majahil walionunuliwa na Waingereza wameenezwa kila pahala leo wakibeba jina la wanazuoni. Njia pekee ya kujifunza imani sahihi leo ni kusoma vitabu vya wanazuoni wa ahli sunna. Kuvipata vitabu hivi ni neema kubwa itokayo kwa Allah. Maadui wa kiislam wanaeneza vitabu vingi vya dini ili kuwapoteza vijana, hivyo ni shida kupata vitabu sahihi. Vijana wamezongwa na aina kadhaa ya michezo ya kipuuzi hivyo hawana muda wa kutafuta na kusoma vitabu sahihi. Leo imeshuhudiwa kwamba vijana wengi wanafikiria michezo tu na wala hakuna njia ya kuwasaidia. Kuna wajibu mkubwa kwa wazee kuwaokoa watoto wao

na janga hili. Wanalazimika kuwafahamisha umuhimu wa kujifunza imani yao na kuwazoesha kusoma vitabu vya dini. Na hili litawezekana kwa kuwakinga watoto wao na kutumia muda wao kwenye mambo ya kipuuzi. Tumeshawaona baadhi ya watoto walioathirika ambao husahau hata kula kwa ajili ya michezo miharibifu. Ni muhali kwa mtoto kama huyu kusoma vitabu vyake vya shule na kupasi masomo yake. Wazazi wawahimize watoto kusoma vitabu. Kwa mfano kitabu kiitwacho **(Maadili ya Uislam)** inafaa kisomwe. Mtu atakaesoma kitabu hiki hatajifunza imani yake tu bali pia atajifunza mbinu wanazozitumia maadui wa Uislam. Ikiwa wazee watalidharau jukumu lao hili basi kizazi kisichofuata dini na cha wapagani kitajitokeza ambacho kitakuwa ni hatari kwa nchi na taifa letu

Jambo jengine ambalo wazazi wanatakiwa kulipa umuhimu ni vazi la stara. (Jambo hili limeelezewa kwa upana katika kitabu kiitwacho Endless Bliss). Tunawaona vijana wakicheza michezo ya hatari hali ya kuwa sehemu iliyo juu ya magoti iko wazi. Ni jambo muhimu la fardhi kwa mtu kusitiri utupu wake. Mtu ambae atalipuuza jambo hili anakhofiwa kupoteza imani yake. Watu wanakwenda msikitini kwa ajili ya kupata thawabu za kusali na kusikiliza mawaidha. Hata bila ya kusali na kusikiliza mawaidha kitendo cha kwenda msikitini peke yake kina thawabu. Ila sehemu ambayo inatembelewa na watu wasiositiri utupu wao haiwezi kuwa ni msikiti, bali huo ni mkusanyiko wa fisk (uchafu). Imeelezwa na wanazuoni wote kuwa ni haramu kwenda kwenye mikusanyiko ya fisk. Watu wanaokwenda katika misikiti kama hiyo huwa wanakwenda kwenye mkusanyiko muovu na badala ya kupata thawabu huwa wanapata dhambi. Wakati watu wasio na stara stahiki wanapoingia misikitini huwasababishia dhambi waislam. Ni dhambi kubwa kutokujisitiri inavyostahiki. Pia ni dhambi kubwa kuangalia sehemu zijulikanazo kuwa ni utupu wa mtu mwengine. Hivyo muislam anaekwenda katika misikiti kama hiyo hupata dhambi na ghadhabu za Allah badala ya kupata thawabu.

## MLANGO WA SALA

Sala ina fardhi kumi na mbili. Saba ziko nje ya sala na tano zimo ndani ya sala.

Fardhi zilizo nje ya sala ni hizi zifuatazo: Kujitahirisha na hadath, kujitahirisha na Najas, kusitiri utupu, kuelekea kibla, kuingia wakati, niya na takbira ya ufunguzi. Fardhi zilizo ndani ya sala ni hizi zifuatazo: Kusimama, kisomo, kurukuu mara moja kwa kila rakaa, kusujudu mara mbili kwa kila rakaa, kukaa kwa ajili ya tashahud. Fardhi zilizo ndani ya

sala huitwa **Ruknu** (nguzo).Katika sijda ni fardhi kugusisha paji la uso na viganja vya mikono kwenye sakafu.

Kutahirika na hadathi ni kutia udhu kwa asie na udhu, na kukoga kwa alie na janaba na kutayammam ikiwa maji yatakosekana wakati wa uhitaji wa kutia udhu au kukoga.

Kuna mambo matatu ya lazima kupatikana katika kutahirika na hadathi: Kuchukua tahadhari wakati wa kustanji na kufanya istibraa (itaelezwa mbele), kutokuacha sehemu yoyote ya fardhi katika kuosha viungo husika na kupaka kichwa. Kujitahirisha na najsi kuna mambo matatu. Usafi wa kiwiliwili, usafi wa nguo na usafi wa sehemu ya kusalia.

Kusitiri utupu nako kuna mambo matatu. Kwa mwanamme kwa madhehebu ya Hanafi ni kusitiri sehemu iliyoanza chini ya kitovu hadi sehemu iliyoanza chini ya magoti. Ni sunna kufunika miguu wakati wa sala.

Kwa mwanamke ambae si mtumwa, asioneshe sehemu yoyote ya kiwiliwili chake isipokuwa uso na viganja. Kufuatana na mapokeo ya baadhi ya wanazuoni nyayo nazo zinaweza kuonekana.

Kwa mwanamke ambae ni mtumwa atajifunika kuanzia juu ya matiti kifuani hadi chini ya magoti yake. (Wanawake wanaotembea vichwa wazi na miguu wazi au wakavaa nguo za kubana huwa wanapata dhambi. Wanaume wenye kuwaangalia wanawake hao pia hupata dhambi. Wale wenye kufanya dharau juu ya amri hii ya kujisitiri hao watakua ni makafiri walioritadi.

Kuna mambo matatu katika kuelekea kibla. Kuelekea kibla.

Kutokugeuka kifua chako na upande wa kibla hadi kumalizika swala.

Kunyenyekea kwa kuwepo mbele ya mamlaka ya Allah.

Kuingia wakati nako kuna mambo matatu ya kuyakamilisha. Kujua wakati unapoingia. Kujua wakati unapotoka. Kutokuichelewesha sala ikaingia wakati wa karaha.

Nia inapatikana kwa kujua na kupitisha katika moyo wako kuwa unatekeleza sala ya fardhi, wajibu, sunna au nafila na kuuweka moyo mbali na mambo ya kidunia. Kusali sala ya witri ni wajibu kufuatana na Imam Adham na ni sunna kufuatana na maimam wawili (Imam Abu Yusuf na Imam Muhammad) na imam Malik na Shafii. (Wakati wa dharura inajuzu mtu kuacha witri kwa kufuata madhehebu ya Malik)

Takbira ya ufunguzi inatimia kwa wanaume kunyanyua mikono yao hadi kwenye mabega na kuuhudhurisha moyo.

Kisimamo kinatimia kwa mambo matatu. Kusimama kuelekea kibla, kuangalia sehemu ya kusujudu na kutulia kwa kutokwenda kushoto na kulia.

Kiraa kinakamilia kwa mambo matatu. Kutoa sauti katika sala ya Jahar na kujisikilizisha mwenyewe tu katika sala ya siri. Kuisoma Quran sahihi na kwa mazingatio. [Wakati ukiwa ndani ya sala, takbira na dua pamoja na adhana lazima zote ziwe kwa lugha ya kiarabu. Haya inabidi watu wajifunze kutoka kwa mahafidh wanaojua. Quran iliyoandikwa kwa herufi za kilatini haiwezi kusomwa sahihi. Inakuwa na makosa na mapungufu. Ni sahihi kuitafsiri Quranla si sahihi kuifanyia tarjuma. Quran zilizoandikwa na watu wasio na dini na wale wasio na madhehebu wakaziita Quran za lugha za wenyeji, hizo haziko sahihi, tena ni mbovu. Kila muislam ana wajibu wa kujifunza dua na sura hizi kwa kiarabu na kuzisoma sahihi. Sala huwa sahihi iwapo kisomo kitakuwa sahihi. Katika **(Targhibu salat)** anasema (Ikiwa mtu kisomo chake ndani ya sala kitakuwa si sahihi kufuatana na wataalam nane lakini kikawa sahihi kufuatana na mtaalam mmoja basi sala yake sio fasid.)]

Rukuu inakamilika kwa mambo matatu: Kurukuu hali ya kuwa umeelekea kibla, kupinda mgongo vyema (ipatikane kama herufi kubwa L iliyogeuzwa) mgongo na kichwa kuwa katika usawa mmoja, na kupatikane utulivu (tumaanina) katika rukuu.

Kuna mambo matatu ambayo yanakamilisha sijda: Kusujudu kwa mtindo ulioelekezwa katika sunna. Kusujudu kwa kuelekea kibla na kikomo na pua viguse chini (sakafuni.) Kupatikane utulivu (tumaanina) katika sijda lau kwa muda mfupi. (Inaruhusika kwa mtu ambae si mgonjwa kusujudu juu ya kitu kilichonyanyuka kutoka juu ya ardhi kisichozidi sentimita ishirini na tano, ingawaje ni makruh kufanya hivyo) Mtume “sallallahu alayhi wasallam” hakuwahi kusujudu juu ya kitu kilichonyanyuka kutoka juu ya ardhi wala masahaba hawajawahi kufanya hivyo.

Kuna masharti matatu katika kukamilisha kitako cha mwisho (kitako cha atahiyyatu): 1- Kwa mwanamme kukalia mguu wa kushoto na mguu wa kulia kuukunja na kwa mwanamke kukaa kikao cha tawaaruk nacho ni kukalia matako na miguu kupindwa kulia. 2- Kusoma Atahiyyatu kwa vizuri. 3- Kusoma sala ya mtume “sallallahu alayhi wasallam” katika hii atahiyatu ya kikao cha mwisho

# MLANGO WA KUKOGA

Kuna fardhi tatu za kukoga katika madhehebu ya Hanafi, nne katika madhehebu ya Malik na mbili katika madhehebu ya Shafii.Na katika madhehebu ya hanbali ni moja. Kufuatana na madhehebu ya Hanafi:

1- Kuosha mara moja ndani ya mdomo. Ni fardhi kupatikana kwa maji baina ya meno na ndani ya tundu za meno. (kufuatana na madhehebu ya Hanafi haijuzu kufanya tiba ya kujaza jino ila kwa dharura. Inaruhusika kutia meno ya kubandika ambayo atakuwa akiyatoa wakati wa kutia udhu. Ikiwa atalazimika kufanya tiba ya kujaza jino basi wakati wa kukoga, kutia udhu na kusali itabidi anuie kuwa anatekeleza kwa kufuata madhehebu ya Shafii au Malik.

2- Kutia maji puani.

3- Kuosha mwili mzima mara moja. Ni fardhi kuosha sehemu zote za kiwiliwili ambazo zinafikika na hazina uzito kuoshwa. Iwapo atakua na uzito wa kimaumbile (sio wa kutengeneza) kuzifikia baadhi ya sehemu za mwili huyo atasamehewa na josho lake litakuwa sahihi.

Imeelezwa katika kitabu kiitwacho **(Durrul mukhtar)** kwamba chakula kilichobakia baina ya meno au ndani ya tundu ya jino bovu havitodhuru kwa sababu maji yanaweza kupenya na kufika chini yake. Ila iwapo chakula kilichoganda sehemu hizo kitakuwa ni kigumu basi kitazuia maji kupenya. Anasema **(Ibn Abidyn)** katika kitabu kiitwacho khulasatul fatawa: Maji yatapenya kwenye chakula kilichoganda na kurowesha sehemu iliyo chini. Lakini kama maji yatashinidwa kupenya basi josho hilo halitokuwa sahihi kwa rai ya wanazuoni. Hayo pia yameelezwa katika kitabu kiitwacho **(Hilyatul mujalli)**. Chakula ambacho kimechakuliwa na kuganda kikawa kigumu kitazuia kufika kwa maji, na kwa vile hapa hapana dharura wala uzito josho halitosihi. Chakula hicho kinalazimu kichokolewe kwanza.

Katika kitabu kiitwacho **(Halabi swaghir)** mwandishi anasema: Ikiwa chakula kimeganda baina ya meno, mtu anapokoga josho lake litakuwa sahihi hata kama atadhani kwamba maji hayakupita hapo, kwa vile maji ni kitu chenye kuteleza yatakuwa yamepenya tu. Kuwepo kwa fatwa hio imeandikwa katika kitabu cha **(Hulasa)**. Baadhi ya wanazuoni wengine wanasema kuwa udhu hautosihi ikiwa chakula ni kigumu. **(Zahire)**. Lililo sahihi zaidi ni hili kwa sababu maji hayatofika chini na wala hakuna dharura wala uzito wowote.

Katika **(Darul muntaka)** anasema: Iwapo kutakuwa na chakula ndani ya jino lenye tundu kuna wanazuoni wanaosema josho linasihi

kuna na wale wanaosema halisihi. Kilicho bora ni kukichokoa chakula hicho. Katika kitabu kiitwacho **(Merakil felah)** kwenye maandishi ya pembeni ya **(Tahtawi)** anasema: Kukiwa na chakula kwenye pachiko za meno au kwenye tundu, josho linasihi kwa sababu maji ni mepesi na yana uwezo wa kupenya humo mote. Ikiwa hayo mabaki ya chakula yamekuwa magumu kutokana na kuchakua basi yatazuia josho.Na hivyo ndivyo ilivyoandikwa katika **Fathul kàdir**.

Katika **Bahrur raik** anasema kuwa josho litakuwa sahihi iwapo chakula kimebaki kwenye tundu au pachiko za meno.Kwa sababu maji ni mepesi na yanaweza kupenya kila sehemu. Katika kitabu kiitwacho **(Tajnis)** pia imeandikwa hivyo hivyo. Sadru shehid Husammadin yeye anasema kuwa josho halitosihi na inalazimika kukichokoa hicho chakula ili maji yanyunyizike ndani. Kukichokoa chakula na kukosha humo ndani ni lenye kupendeza.

Katika **(Fatawa hindiya)** anasema chakula kilicho katika tobo za meno na pachiko zake hakizuwii josho kuwa sahihi. Katika **(Zahidi)** pia imeandikwa hivyo hivyo. Ila kukichokoa na kunyunyizia maji ni bora zaidi. Katika **(Kadihan)** yeye anasema josho halitosihi na hayo pia yameandikwa katika (**Natifi)**. Ni lazima kukichokoa chakula.

Katika **(Majmuat zuhdiyya)** anasema ikiwa kutakuwa na mabaki ya chakula katika pachiko za meno na vikazuia kufika kwa maji basi josho halisihi. Pia imeandikwa hivyo hivyo katika **(Halebi)**. (Hii ni kwa sababau katika hali ya kawaida hakuna uzito kukisafisha hicho chakula. Katika tiba ya jino lililojazwa au kuzibwa haiwezekani kuondoa hicho kilichozibiwa. Hapa uzito unapatikana). Hapa kuna uzito. Na ikiwa mtu atafanya jambo mbalo litaleta uzito basi inakuwa ni udhuru kwake wa kuweza kufuata madhehebu mengine. Lakini haiwi udhuru kuacha fardhi. Haifai kufata madhehebu mengine kwa ajili ya kuacha fardhi. Ili lipatikane hili, dharura (udhr) na uzito (haraj) lazima vipatikane pamoja. Kama itaulizwa je kulitibu jino kwa njia ya kulijaza ili kuondoa machungu na kulifanya lising'olewe sio dharura? Tunajibu ili jambo liwe dharura hapatakiwi iwepo njia ya kufata madhehebu mengine.

Wakati wa kuoga josho la wajibu, kusema kuwa (hukmu za kukosha meno hizo hizo zitatumika katika kuosha sehemu ya nje ya jino lililojazwa) haitofaa. Tahtawi katika maandishi ya pembeni ya **(Imdat)** anasema: Mtu akivaa hofu (soksi za Ngozi) baada ya kutia udhu, udhu wake unapotenguka basi utengukaji unakuwa uko kwenye zile hofu na wala sio miguuni.) Kufananisha fatwa hii iliyotajwa katika vitabu vya fikhi na swala la jino lililojazwa haiwi sahihi na inakuwa ni uzushi wa mtu binafsi. Pia si sahihi kufananisha hukmu ya ndevu zilizosokotana

sana katika udhu na hukmu ya jino lililojazwa katika kuoga. Hii ni kwa sababu hata kama hailazimiki maji kufika kwenye maoteo ya ndevu wakati wa kutia udhu, wakati wa kukoga yana ulazima yafike. Kuna wanaosema kuwa kwa vile wakati wa kutia udhu si lazima kuosha ngozi iliyo kwenye maoteo ya ndevu basi na wakati wa kukoga ni hivyo hivyo. Hawa huwa hawakoshi chini kwenye maoteo ya ndevu wakati wa kukoga. Josho lao hawa si sahihi kwa hivyo na sala zao pia si sahihi.

Si sahihi vile vile kufananisha jino lililojazwa na kidonda kilichofungwa dawa au mguu uliovunjika ukafungwa P.O.P. au bendej. Kwa sababu hivi kuviondoa huwa ni uzito au dhara na wala hakuna rai ya kufata katika madhehebu mengine. Hivyo uhitaji wa kukosha chini yake unaanguka (unakuwa haupo)

Baada ya kung'oa jino lenye kuuma uwezekano wa kuweka jino la bandia linaloweza kutolewa na kurejeshwa upo lakini wengine ndio huamua kujaza au kuziba. Kwa vile hili wanalifanya kwa hiari yao baada ya kuwa uwezo wa kutia meno yanayoweza kutoka upo, basi hii haiitwi kuwa ni dharura. Hata kama itaitwa kuwa ni dharura, haiifanyi hukumu ya kufika maji chini yake iondoke kwa sababu kuna nafasi ya kuweza kutumia hukumu ya madhehebu nyengine. Wale ambao wanasema dharura ipo na wakaamua kufuata rai ya madhehebu ya Shafii au Malik basi huwa hakuna mwenye haki ya kuwaambia kitu.

**Dharura** ni zile hali ambazo hazimo ndani ya uwezo wake binaadam Mfano wa haya ni amri na makatazo ya Uislam, hali za maumivu ya hali ya juu, hali za kupoteza maisha au kiungo na hali ya kuwa huna chaguo jengine. Ikiwa jambo linalofanywa litakuwa ni kikwazo kwa fardhi kufanyika au haram kuachwa basi hilo huitwa uzito. Maamrisho na makatazo ya dini huitwa hukmu za kiislam na hizi anatakiwa azitekeleze mtu kufuatana na maelekezo ya imam wa madhehebu yake. Iwapo mtu amefanya jambo, na ikawa katika kutekeleza amri za Uislam inakuwa ni uzito kufata kauli za wanazuoni wateule wa madhehebu yake, basi anaweza akafata kauli za wanazuoni wengine wa madhehebu yake hata kama si wateule. Na ikiwa hili pia litashindikana basi atafuata hukmu kutoka katika madhehebu mengine. Na ikiwa kufuata madhehebu mengine pia inakuwa ni uzito basi hilo jambo litatizamwa udharura wake.

1- Jambo likiwa na uzito na ikiwa dharura ipo basi hali ya fardhi huanguka.

2- Ikiwa hakuna dharura ya kufanya jambo litakalosababisha uzito (kama kupaka rangi ya kucha) au ikawa yako mambo mengine yanayoweza kufanyika lakini mtu akachagua kufanya lile litakaloleta

uzito, basi ibada ya mtu huyo haitokuwa sahihi. Inabidi aitekeleze fardhi kupitia njia isiyo na uzito. Iwapo kutakuwa na dharura au hakukuwa na dharura, ikiwa uzito utaleta mashaka basi inafaa kufata madhehebu mengine. Hayo yameandikwa katika **(Fatawil hadithiyya)**, **(Hulasatut tahkik)** na kitabu cha Tahtawy kiitwacho **(Merakil falah)** katika maandishi ya pembeni na katika kitabu cha Molla Halil Esirdin "rahmatullahi alaih" kiitwacho **(Maafuwat)**. Molla Halil alikufa mwaka 1259 hijria (1843 miladia). Kwa hivyo mtu ambae anafata madhehebu ya Hanafi kama ataamua kuziba jino badala ya kuweka meno ya kubandika anaweza kufuata madhehebu ya Malik au Shafii wakati wa kukoga josho la wajib. Kwa sababu katika madhehebu haya mawili si lazima kutia maji mdomoni au puani wakati wa kukoga josho la wajib. Kufuata madhehebu mbili hizi ni rahisi tu. Inabidi apitishe nia moyoni wakati wa kukoga, kutia udhu na kusali kuwa anafuata madhehebu ya Shafii au Malik na kama atasahau baadae akikumbuka tu atie nia hiyo. Italazimika kwa mtu huyu josho lake, udhu wake na sala yake vifate masharti ya madhehebu aliyochagua kuifuata. Kwa madhehebu ya shafi, mtu huyu udhu wake utatenguka akigusana ngozi kwa ngozi na mwanamke ambae si maharimu wake. Vile vile ndani ya sala atalazimika kusoma suratul fatiha nyuma ya imam. Ili kumfata malik itaelezewa katika kurasa za mbele. Kufata madhehebu haina maana ya kubadilisha madhehebu. Ni kutekeleza ibada fulani kwa kuzingatia fardhi na mufsid zilizotajwa katika madhehebu mengine. Yale mambo ya wajib, sunna na makruh yaliyo katika ibada hiyo ataendelea kufuata madhehebu yake.

Wakati rai za kifikhi za wanazuoni kuhusu jambo hili la kujaza jino zipo, tunasikia kuna watu ambao wanafuata rai zisizo njema za watu wasio na madhehebu. Wanasema kwamba fatwa ya kuwa kupata tiba ya kujaza jino ni jambo lenye kufaa imeandikwa katika toleo la mwaka 1332 hijria(1913 miladi) la Majmua ya Sabilul Rashad. Kwanza tunapenda kusema kwamba majmua hii imejaa maandishi ya wana mageuzi wa dini na wale wasio na madhehebu. Mhariri wa Majmua hii Ismail Hakki ni mmasoni wa kisiri. Huyu ni miongoni mwa wale walioathirika na kudaganywa na Mufti wa Cairo mwanamageuzi Muhammed Abdul. Huyu Ismail Hakki alipata elimu yake ya sekondari huko Izmir kisha akasoma Chuo cha ualimu kilichopo Istanbul. Ufahamu wake juu ya elimu na utamaduni wa kiislam ni wa chini. Alipendeza mbele ya wapinzani hivyo akapewa ualimu wa madrasa na akaanza kueneza fikra za kimageuzi za Muhammed abdul katika darsa zake na vitabu vyake. Mmoja kati ya wale aliowatia sum u na kuwapotoa ni mwanafunzi wake aitwae Ahmed Hamid Akseki Huyu

alitafsiri kitabu kiitwacho **(Talfikil madhahib)** kilichoandikwa na Mmisri asie na madhehebu aitwae Rashid Ridhaa. Ismail Hakki aliandika sifa nyingi katika utangulizi wa kitabu hiki, jambo ambalo limedhihirisha mtizamo wake uliokuwa umejificha.

Huyu Ismail Hakki aliandika maneno mengi juu ya tiba ya waya wa kukazia meno juu ya kuwa waya wa dhahabu unajuzu au haujuzu na akaandika maneno mengi juu ya tafauti za wanazuoni kuhusu hilo na kuwa waya wa fedha ungefaa zaidi na kuwa waya wa dhahabu ungeweza kutumika katika dharura na kwamba haya yameandikwa katika sherhe ya kitabu kiitwacho **(Siyar Kabir)**, na akaeleza kuwa tiba ya kukaza meno kwa waya ni dharura. Lakini alichoulizwa yeye haikuwa swala la tiba ya kukaza meno kwa waya uliotengenezwa kwa fedha au dhahabu bali aliulizwa juu ya kusihi kwa josho la mtu alie na jino lililojazwa ndani au kufunikwa juu. Ismail Hakki badala ya kujibu alichoulizwa, alileta maelezo marefu juu ya jambo ambalo watu tayari wanalifahamu na kukwepa kujibu swali alilotakiwa kujibu. Mtindo huu katika maydani za ilmu unaitwa Ujanja. Kuandika mawazo yako binafsi na ukajaribu kuyaonesha kuwa ni fatwa ya wanazuoni. Isitoshe hiyo, kuandika mawazo ya wanazuoni juu ya josho la wajibu na akaingiza baadhi ya mawazo yake binafsi na kuonesha kuwa ni ya hao wanavyuoni. Mfano anasema katika kitabu kiitwacho **Bahar** imesemwa (sehemu ambayo ni uzito kuifikia si lazima kuipaka maji), wakati kilichoandikwa ndani ya kitabu hicho ni (sehemu za kiwiliwili ambazo ni uzito kuzifikia). Hii ni kufananisha baina ya kitu alichokifanya binaadamu kuwa dharura na kile kitu ambacho kipo kwa binaadamu ambacho ni dharura. Kufananishwa ruhusa ya mwanamke kutokukosha kichwa ikiwa patakuwa na dhara, iliyopo ndani ya kitabu cha **(Durul mukhtar)** kuichukua na kuifananisha na tatizo la tiba ya kujaza jino pia sio sahihi. Hii ni kwa sababu dhara inayozungumzwa katika jambo la mwanamke kukosha kichwa ni maradhi yapatikanayo kichwani wakati jambo la kujaza jino analifanyisha mtu mwenyewe. Ndio maana **(Durul mukhtar)** imeandika mbali maudhui yanayohusu kujuzu au kutokujuzu kwa josho la mtu mwenye chakula kilichobaki ndani ya tundu ya jino bovu.

Hakumalizia hapo lakini aliendelea kuwazulia wanazuoni wa kiislam kwa kusema (Si sharti katika josho la wajib kwa maji kufika chini ya jino lililozibwa kwa fedha au dhahabu. Wanazuoni wa fikh wamekubaliana kwamba kuna dharura katika jino hilo kwa hivyo hailazimiki kufikisha maji ndani). Hakuna hata mwanazuoni mmoja wa kihanafi alieliona jambo hilo kuwa ni dharura. Uhakika ni kwamba tiba ya aina hiyo

haikuwepo katika zama zao. Ushahidi alioutumia katika tarjama ya **(Sherhe ya siyer kebir)** kilichozungumzwa humo ni kutia jino la bandia la dhahabu baada ya jino kung'oka au kutumia waya wa dhahabu kwa kuyashikilia meno. Hakuna maelezo yanayohusu kujaza au kuziba jino. Hayo ameyaongeza yeye Ismail Hakki. Viongozi wa dini ambao ni wamasoni, waovu na wasio na madhehebu imegundulika kwamba wanatumia kila aina ya hila kwa ajili ya kuwadanganya na kuwagawa waislam.

Imam Muhammad "rahmatullahi alaih" anasema: Jino lilotikisika linaweza kufungwa likazuwiwa lisitoke kwa waya wa fedha au dhahabu. Hakusema kwamba jino linaweza kujazwa au kuzibwa kwa dhahabu. Hayo yameengezwa na kina Ismail Hakki.

Haya maandishi yenye hila na uwongo yaliyoandikwa na Ismail Hakki wa Izmir yalijibiwa na mufti na watu wenye elimu wa wakati huo. Na wakaweka wazi uhakika ulivyo. Mmoja kati ya walimu hao thamini ni mwalim wa Bolvadin Yunuszade Ahmed Vehbi efendi "rahmatullahi alaih". Mtaalam huyu aliyekuwa mpana katika elimu ya dini alithibitisha kuwa wanazuoni wameafikiana kwamba mwenye kujaza jino, josho lake la wajib halitokuwa sahihi.

Uongozi wa jarida la **(Sabilu rashad)** walifahamu kwamba yaliyoandikwa na huyu Mtu wa Izmir ni hila na maneno ya kuunganisha kiasi ya kwamba ili kumuunga mkono, katika toleo la pili 1329 hijria (1911 miladia) la kitabu cha fatwa kiitwacho **(Majmua jadida)** walihisi uhitaji wa kuandika fatwa isemayo (Josho litakuwa sahihi.) Fatwa hii haikuwemo katika toleo la kwanza la kitabu hiki (1299 hijria). Fatwa hii iliingizwa katika toleo la pili na Musa Kasim ambae alikuwa sheikhul islam wa waharibifu hao. Kwa hivyo katika Sabilu Rashad , maneno ya mwanamageuzi yanathibitishwa na maneno ya mmasoni. Hakuna hata mwanazuoni mmoja aliesema kuziba jino au kujaza jino ni katika mambo ya dharura. Haya yameandikwa na wanamageuzi wa dini, watu wasio na madhehebu, wamasoni na wale waliodanganywa na kununuliwa na mawahabi.

Katika maandishi ya pembeni ya kitabu cha **(Merakil falah)** Ahmed Tahtawi "rahmatullahi alaih" anasema Ikiwa unamfuata imam wa madhehebu tafauti na yako, ili sala yako iwe sahihi, basi imam huyo asiwe na jambo ambalo kwa madhehebu yako wewe linabatilisha sala. Kama analo basi wewe uwe hulijui. Kauli yenye kutegemewa ni hii. Kauli ya pili ni hii isemayo (Ikiwa imam analolifanya ni sahihi kwa madhehebu yake, itakuwa sahihi maamuma kumfuata hata kama itakuwa ni kinyume na madhehebu yake binafsi.) Ibn abidin pia

ameandika hivyo. Kufuatana na kauli za Tahtawi na Ibn abidin “rahmatullahi alaih” mtu wa madhehebu ya Hanafi ambae hana jino lililozibwa au kujazwa, kumfata katika sala imam wa madhehebu nyengine ambae ana jino lililozibwa au kujazwa kutakuwa kuna kauli mbili. Kauli ya kwanza itakuwa ni kwamba sala ya huyo maamuma wa kihanafi haitosihi kwa sababu sala ya imam huyo kufuatana na madhehebu ya Hanafi haisihi. Katika kauli ya pili huyu imam kama anafuata madhehebu ya shafi au Malik basi maamuma wa kihanafi akimfata basi sala yake ni sahihi. Imam Hinduvani “rahmatullahi alaih” pia ijtihad yake imepita hapo. Katika madhehebu ya Malik pia ni hivyo. Imam salih ambae ameziba au amejaza jino, kama haikujulikana kuwa hafati madhehebu ya Shafii au Malik, basi itafaa kwa maamuma wa madhehebu ya Hanafi kumfuata. Pia si jaiz kumuuliza ili kutaka kujua kuwa anafuata dhehebu hizo mbili au la, kwani hiyo ni kufanya tajasus(kumchunguza). Kauli hii ya pili pamoja na kwamba ni dhaifu lakini kama tulivyoelezea huko juu kutumia kauli dhaifu katika hali ya uzito inajuzu. Katika kitabu cha **(Hadika)** imeandikwa kwamba kauli dhaifu inaweza pia kutumika katika kuepusha fitna. Yule asiyeyapa madhehebu umuhimu na akawa hafanyi ibada zake kwa kufuata vitabu vya fikh basi huyo si katika Ahli sunna. Aliyekuwa si ahli sunna ima ni mtu wa bid’a au ni yule murtad aliepoteza imani. Hatusemi kwamba watu wasizibe au wasijaze meno, ila tunachofanya ni kuwaonesha njia sahihi ndugu zetu ili ibada zao ziwe sahihi.

Kukoga kuko aina kumi na tano. Tano ni fardhi, tano ni wajib, nne ni sunna na moja ni mubah. Kukoga kwa fardhi ni katika mambo yafuatayo: Mwanamke anapomaliza hedhi au nifasi, kufanya tendo la jimai, kutokwa na manii kwa ladha, kuota na kuona manii mahali ulipolala au kwenye chupi. Ni fardhi kukoga kabla ya kutoka wakati wa sala ambayo haijasaliwa.

Yaliyo wajibu kukoga ni haya yafuatayo: Maiti ni wajibu kukoshwa maiti, mtoto anapopata ukubwa, wakati mke na mume wamelala wakayaona manii na wasiyajue yamemtoka nani kati yao basi ni wajibu wote wawili kukoga, ikiwa utayaona manii kwenye nguo yako na usiyajue yamekutoka wakati gani basi ni wajibu kukoga, mwanamke kama atazaa na ikawa hakutoka damu basi ni wajibu kukoga (akitoka damu ni fardhi kukoga).

Mambo abayo ni sunna kwako kukoga ni siku ya Ijumaa na siku ya Iddi. Wakati wa kuhirimia kwa nia yoyote ile na kabla ya kutoka kwenda Arafa. Ni mustahab kukoga kwa kafiri anapoingia uislam. Ikiwa

alikua na janaba wakati akiwa kafiri basi ni fardhi kwake kukoga na kama hakuwa na janaba basi ni mustahab.

Kuna mambo matatu ya haramu katika kukoga:

1- Wanaume kwa wanaume au wanawake kwa wanawake wanapokoga pamoja ni haramu kuonana sehemu zao baina ya kitovu na magoti.

2- Kufuatana na kawli, wanawake wa kiislam kuonekana na wanawake wa kikafir wakati wanakoga. (hukmu ni hiyo hiyo hata kwa wakati mwengine.)

3- Kufanya israfu katika kutumia maji.

Sunna za kukoga kufuatana na madhehebu ya Hanafi ni kumi na tatu:

1- Kustanji kwa maji. Yani kujisafisha kwa maji dhakari na matakoni.

2- Kuosha viganja viwili vya mikono.

3- Kuondoa najisi ya uhakika ikiwa ipo katika mwili.

4- Kusukutua na kupandisha maji puani. Hata kama itabakia sehemu ndogo tu kavu isiyopata maji basi josho halitokuwa sahihi. Mwanzo wake atie udhu wa sala.

5- Kutia nia ya josho la wajib.

6- Kujisugua viungo vilivyomiminiwa maji.

7- Kuanza kichwa, kwenda ubavu wa kulia kisha ubavu wa kushoto katika kujimiminia maji.

8- Kupitisha maji baina ya vidole vya mkono na mguu.

9- Kutokuelekeza uso wako au mgongo wako kibla wakati wa kukoga.

10- Kutokuzungumza mazungumzo ya kidunia.

11- Kusukutua na kupandisha maji puani mara tatu.

12- Kuosha kuanzia upande wa kulia.

13- Kutokukojoa katika sehemu unayokoga ikiwa maji yanatuwama hapo hapo. Mbali ya hizi tulizoziorodhesha bado ziko na suna nyengine.

Kufatana na kitabu cha **(Alfikh ala l madhahibil arbai)** mtu ambae analazimika kukoga ni haramu kwake kufanya yale mambo yote ambayo ni haramu kwa mtu ambae hana udhu, na hii ni kufuatana na madhehebu yote manne. Mfano mtu mwenye janaba hafai kusali sala ya fardhi wala sunna, na hii ni kufuatana na dhehebu zote nne. Ikiwa hatopata maji au akiwa na sababu ya maradhi basi atatayammam. Si haram kwa mwenye janaba kufunga funga ya fardhi au sunna.

Kukamata msahafu au kusoma Quran ni haram. Kukamata msahafu bila udhu pia si halali. Kuingia msikitini ni haram. Inajuzu kuingia msikitini kwa kukimbia adui, au kusoma aya mbili tatu kwa ajili ya kutolea hukmu, kuingia msikitini kwa ajili ya kuchukua kamba au ndoo ya kisima au ikiwa hakuna njia nyengine kupita mara moja. Kusoma aya fupi kwa nia ya dua mfano kupiga bismillahi. Kabla ya kuingia msikitini atatayammam.

## DUA YA TAWHIDI

**Ya Allah ya Allah. Lailaaha illallah Muhammadun Rasulullah. Ya Rahman ya Rahim Ya afuwwu ya Karim fa`fuanny warhamny ya arham-ar-rahimyn. Tawaffany musliman walhiqny bissalihyn. Allahummaghfirly wa li-aabai wa ummahaaty wa li-abai wa ummahati zawjati wa li-ajdady wa jaddaty wa li-abnai wa banaty wa li-ikhwaty wa akhwaaty wa li-amaamy wa ammaty wa li-akhwali wa khaalaty wa li-ustadh Abdulhakim-i Arwasi wa li kaafatil muuminina wal- muuminati. Rahmatullahi taala alayhim ajmain.**

## YANAYOHUSU HEDHI NA NIFASI

Uchache wa siku za hedhi ni tatu na wingi wake ni siku kumi. Nifasi haina muda katika uchache wake. Wakati wowote ikikatika huwajibika kukoga na kuanza kusali na kufunga. Wingi wake ni siku arubaini. Ikiwa hedhi itatoka kwa uchache chini ya siku tatu na ilipoanza akadhani kuwa ni hedhi na kuacha kusali, basi inabidi azilipe sala hizo. Wala hawajibiki kukoga. Na iwapo itakatika damu baada ya kukamilika siku tatu basi atakoga na kusali sala ya wakati uliopo. Baada ya kukamilika siku kumi atalazimika kukoga na kuanza kusali hata kama damu haijakatika. Nifasi nayo ikikamilika siku arubaini basi ni wajibu kukoga na kuanza kusali hata kama damu haijakatika. Katika siku za hedhi na nifasi maji maji yoyote yanayotoka (yawe manjano au machafu) hupewa hukumu ya damu.

Iwapo ndani ya siku kumi za hedhi au siku arubaini za nifasi damu itakatika kwa siku moja au mbili, akadhani kuwa imemaliza hivyo akakoga na kuanza kufunga, kisha ndani ya muda wake ikaanza tena basi funga hizo atatakiwa azilipe. Itakapokatika atatakiwa akoge tena. Ikiwa hedhi itakatika kabla ya muda wake wa kawaida lakini siku tatu zimeshapita, basi atakoga na kuanza kusali, ila hatofanya tendo la ndoa hadi siku zake za kawaida zimalizike. Hukmu ya nifasi pia iko kama hivyo. Ikiwa damu itaendelea zaidi ya ada yake lakini ikawa haijazidi siku kumi basi hiyo itahisabika kuwa ni hedhi. Ikiwa itaendelea zaidi ya

siku kumi, basi zile siku zilizopita ada yake hazitokuwa ni hedhi hivyo atalazimika kuzilipa sala alizoziacha. Hukmu ya siku arubaini za nifasi inafanana na hukmu ya siku kumi za hedhi.

Ikiwa damu ya hedhi au nifasi itakatika ndani ya siku ya mwezi wa Ramadhani baada ya kupita muda wa kuanza funga (imsak) atatakiwa ajizuie kula na kunywa kuanzia wakati huo wa damu ilipokatika ila siku hii haitohesabiwa kuwa ameifunga na atatakiwa aje ailipe kama nyengine. Na iwapo damu itaanza katika muda kama huo tulioutaja basi atatakiwa ale na anywe hata kama itakuwa ni baada ya laasiri. Kwa ujumla iwapo mwananmke ataiona damu imeanza kutoka basi ataacha kusali na kufunga. Iwapo damu itakatika kabla ya siku tatu atasubiri hadi kipindi cha sala kiliopo kikaribie kumalizika, ikiendelea basi hatosali na kama haitoendelea atatia udhu na kusali kabla kipindi kupita. (kukoga si lazima kama tulivyosema kabla) na kama damu itaanza tena basi ataacha kusali. Kama itakatika basi atasubiri tena hadi kipindi cha sala iliopo muda wake kukaribia kwisha na atatia udhu na kusali. Damu hizi zitokazo katika kipindi hichi kilicho kifupi kuliko siku tatu hazilazimishi kukoga. Ikiwa damu itakatika baada ya siku tatu, vile vile atasubiri karibu na wakati wa mwisho wa kipindi cha sala kiliopo kama haikutoka atakoga, atatia udhu na kusali na kama itarejea tena basi ataacha kusali. Ikiwa damu itaendelea kwa siku kumi, baada ya hapo atakoga na kusali hata kama bado damu inaendelea. Nifasi nayo ni hivyo hivyo na kila inapokatika ni lazima kukoga, hata kama itakatika katika siku ya mwanzo kabisa. Na katika siku ya mwezi wa Ramadhan ikiwa damu itakatika kabla ya wakati wa kuanza funga (imsak) basi nae atanuia na kuifunga siku hiyo. Na iwapo damu itatoka tena kabla ya wakati wa funga kumalizika basi siku hiyo haitohisabiwa na atatakiwa kuilipa.

Ikiwa ataharibu mimba kabla ya wakati, iwapo alichokizaa tayari kinaweza kupambanuliwa baadhi ya viungo kama vidole, pua, mdomo na nywele basi hukmu yake itakuwa sawa na aliyezaa mtoto wa kawaida. Na ikiwa alichokizaa kitakuwa bado hakiwezi kupambanuliwa sehemu zake basi huyo hatokuwa na nifasi. Ikiwa damu itatoka kwa siku tatu au zaidi hiyo itakuwa ni hedhi. Hata hivyo kama damu itaanza kutoka kabla siku kumi na tano tangu kumalizika hedhi iliyopita au ikiwa itaanza kutoka baada siku kumi na tano tangu kumalizika hedhi iliyopita lakini kutoka kwake ikawa chini ya siku tatu;basi hali hizo mbili hazitohesabiwa kuwa ni hedhi. Hiyo itakuwa kama kutokwa na damu ya pua. Atasali na kufunga na wala halazimiki kukoga ili kufanya tendo la ndoa.

[Mwanazuoni mkubwa Muhammed Birgiwi “rahmatullahi alaih” ameandika kitabu chenye thamani sana kinachozungumzia hali za hedhi na nifasi katika madhehebu ya Hanafi. Kitabu hiki kiitwacho **(Zuhrul mutaahilina)** kimeandikwa kwa kiarabu na Sayyid Muhammed amin ibni Abidin alikieleza kwa upana zaidi kitabu hiki na kuandika kitabu kiitwacho **(Manhalul waridina).** Imam Birgivi “rahmatullahi alaih” alikufa mwaka 981 (1573) huko Taun. Hiki ni kitongoji kilichoko huko Odemish, Anatolia. Ibni Abidin “rahmatullahi alaih” alikufia Sham mwaka 1253 hijria (1836 miladia). Katika kitabu cha **(Manhalul waridina)** anasema Ni fardhi kwa kila muislam kujifunza elimu ya ibada. Hivyo mume na mke wanawajibu kujua mambo ya hedhi na nifasi. Waume wanatakiwa wawafunze wake zao na kama wao hawajui basi wawaruhusu kwenda kujifunza kwa wanawake wenzao. Mke ambae hakupewa ruhusa na mumewe basi anaweza kutoka bila ya ruhusa ili kwenda kujifunza. Elimu hii mahsus inayowahusu kina mama kwa sasa imesahauliwa na walimu wenye kuijua hawapo tena. Walimu wa leo hawawezi kutafautisha damu ya nifasi, hedhi na istihadha. Vitabu vyenye kuelezea haya kwa urefu havipo. Hata vikiwepo wanaosoma wanapata uzito kufahamu kwa sababu haya si mambo mepesi kuyafahamu. Elimu hii ya damu ya wanawake ni muhimu sana katika kuyaendea mambo mengi ya dini kama udhu, sala, kusoma Quran, funga, itikafu, kubaleghe, kuolewa, kuachwa, eda na mengineyo. Ili kuifahamu elimu hii nimetumia nusu ya umri wangu na ndugu zangu ninaowafunza ninajitahidi kuwaelezea kwa ufasaha na uwazi.

Hedhi ni ile damu inayotoka kwenye utupu wa mbele wa mtoto wa kike, mwenye afya alietimiza miaka minane au mwanamke baada ya kipindi cha kusafika kutoka katika hedhi iliyopita. Damu hii kwa uchache hutoka kwa siku tatu. Hii huitwa **(Damu sahihi)**. Siku kumi na tano au zaidi zinazopatikana baada ya siku za kawaida za hedhi na zikawa baina ya hedhi mbili na ambazo hazina damu inayotoka huitwa **(Kusafika sahihi)**. Siku kumi na tano au zaidi zinazopatikana baada ya muda wa kawaida wa hedhi na zikawa baina ya hedhi mbili na ikapatikana ndani yake damu inayotoka hii huitwa **(Kusafika kwa hukmu)** au **(Kusafika fasid)**. Ikiwa kipindi cha kusafika na damu kitakuwa chini ya siku kumi na tano basi nayo pia huitwa **(Kusafika fasid)**. Kusafika sahihi na kusafika kwa hukmu huitwa kusafika kamili. Damu inayoonekana kabla na baada ya siku kumi na tano za kusafika kamili na ikadumu kwa muda wa siku tatu basi hizo ni hedhi mbili katika vipindi vyake. Ukiiacha rangi nyeupe, rangi yoyote iwayo au hata uchafu uchafu, hiyo inaisabiwa kuwa ni damu ya hedhi.

Mtoto wa kike anapoanza kutokwa na hedhi huwa ndio amevunja ungo (amekua), yani ametoka kwenye utoto na kuwa mwanamke. Siku hedhi inapoanza hadi siku inapomalizika ndio huitwa **siku za ada** (yaani kawaida yake huyo mwanamke) Siku za ada zinaweza kuwa ni tatu hadi kumi. Kwa madhehebu ya Shafii na Hanbal ni moja hadi kumi na tano.

Damu ya hedhi hailazimiki kutoka kwa kuendelea. Ikiwa itaanza kutoka kisha ikakata, na baadae ikaanza kutoka tena, muda wa hapo katikati kama utakuwa ni chini ya siku tatu basi inakubalika kuwa ni kipindi cha kutokwa na hedhi. Na ikiwa damu itakata kwa zaidi ya siku tatu lakini ikarudi kabla ya siku kumi pia itahisabiwa kuwa ni kipindi cha hedhi kufuatana na mapokezi ya Imam Muhammad "rahmatullahi alaih" kutoka kwa Imam Abu Hanifa "rahmatullahi alaih". Imam Muhammad "rahmatullahi alaih" pia anayo riwaya nyengine aliyopokea. Kufuatana na imam Abu Yusuf "rahmatullahi alaih" kipindi cha kuzuia kikiwa chini ya siku kumi na tano basi kitahesabiwa kuwa chote ni mwendelezo wa hedhi ile iliyoanza. Mtoto wa kike kapata damu siku moja kisha akazuia kwa siku kumi na nne zilizofata kisha akafuatisha siku moja ya kupata damu. Mwanamke kapata damu siku moja kisha akazuia kwa siku kumi, ikafuatwa na siku moja ya damu. Mwananmke kapata damu kwa siku tatu zikafuatwa na siku tano za kusafika kisha ikafuata siku moja ya damu. Kufuatana na Imam Abu Yusuf siku za ada kwa huyu mtoto wa kike zitakuwa ni siku kumi. Ama kwa huyu mwanamke wa mwanzo idadi ya siku zake za ada ndio itakuwa hedhi, na zile siku zozote zitakazozidi siku zake za ada basi huwa ni istihaadha. Na kwa huyu mwanamke wa pili siku zote tisa kwake ni hedhi. Kufutana na riwaya ya kwanza ya Imam Muhammad "rahmatullahi alaih" kwa huyu mwanamke wa kwanza siku tisa tu ndio zitakuwa hedhi. Na kwa riwaya ya pili ya Imam Muhammad kwa huyu mwanamke wa pili, siku tatu ndio zitakuwa hedhi. Zilizobaki sio hedhi. Sisi katika kufasiri kitabu chetu (**Multaka**) maalumati yaliyo chini yote tumefuata rai ya kwanza ya Imam Muhammad. Siku maana yake ni masaa ishirini na nne. Ni mustahab kwa mwanamke ambae hajaolewa katika siku zake za hedhi na kwa mwanamke alieolewa siku zote kuweka kitambaa au pamba iliyotiwa manukato katika mdomo wa utupu wake wa mbele. Ni makruh kukiingiza kitambaa hicho chote ndani ya utupu wake. Ikiwa mtoto wa kike atakuwa anaendelea kuona tone la damu kwenye hichi kitambaa kwa miezi kadhaa, basi siku kumi zitakuwa ndio hedhi na ishirini zitakuwa ni istihaadha. Damu hii huitwa **(Istimraar)** na ataendelea kufuata hivyo ilivyotajwa hadi itakapokatika. Ikiwa mtoto wa kike ataona damu siku tatu kisha ikazuia kwa siku moja;

kisha akaiona kwa siku moja kisha ikazuia kwa siku mbil; kisha akaiona kwa siku moja ikazuia siku moja kisha akaiona tena kwa siku moja, siku kumi hizi zote atahisabiwa kuwa yumo ndani ya hedhi. Ikiwa ataiona siku moja na siku inayofuata asiione na ikaendelea kwa mtindo huo kwa muda wa siku kumi kwa mwezi, basi atasita kusali na kufunga katika siku ambazo anaona damu na atakoga na kusali katika siku ambazo hapati damu. **(Masail sharhi wikaya)**. Mfano wa damu zifuatazo haziwi hedhi bali huitwa istihadha au damu fasid. Damu ambayo itatoka kwa muda mchache usiofikia siku tatu, yaani masaa sabini na mbili hata kama itapungua dakika tano. Damu itakayomtoka mtoto wa kike anaeanza kukua na ikapita siku kumi. Au kwa mwanamke ambae ameshapata hedhi kabla, ikapita siku zake za ada bali pia ikapita siku za kiwango cha juu ambacho ni siku kumi. Damu itakayomtoka mja mzito, mwanamke mzee au mtoto alie chini ya miaka tisa. Umri wa kumaliza hedhi wa mwanamke ni miaka hamsini na tano. Ikiwa mwanamke ambae ada yake ni siku tano, hedhi yake ikaendelea hata asubuhi ya siku ya kumi na moja jua lishachomoza nusu akaona damu lakini lilipofikia kuchomoza kwa thuluthi mbili tu damu ile ikakatika, hata kwa muda huu mfupi siku hii pia itahisabiwa kuwa kapata damu kwa hivyo damu yake itahisabiwa kuwa imeendelea kwa siku kumi na moja ambazo ni zaidi ya kiwango cha juu. Kwa mwanamke huyu hukmu ya hedhi yake itakuwa ni zile siku tano za ada yake tu na zile zilizozidi zitakuwa ni istihaadha. Hivyo huyu atakoga na atasali kadha zile sala zilizo katika siku zilizo juu ya ada yake.

Mwanamke ambae anapata istihaadha huwa na udhuru hivyo anaendelea kufanya ibada kama ilivyo kwa mtu mwenye tatizo la kushindwa kuzuia mkojo au atokwae na damu za pua endelevu.

Kufuatana na kauli ya Imam Muhammad ikiwa mtoto wa kike; mwenye kupata ukubwa kwa mara ya kwanza; atapa damu kwa siku moja tu kisha akapitisha siku nane, kisha kapata tena kwa siku moja, basi siku hizo zote kumi zitahisabiwa kuwa ni hedhi. Lakini iwapo atapata damu siku moja kisha ikasita kwa siku tisa na ikarejea katika siku ya kumi na moja hiyo haitohesabiwa kuwa ni hedhi. Hiyo damu ya hizo siku mbili itakuwa ni istihaadha. Hii ni kwa sababu kama tulivyoelezea damu inayoonekana baada ya siku kumi, haizifanyi siku safi za kabla yake kuwa za hedhi. Katika mfano huu lau kama angeona damu siku ya kumi na siku ya kumi na moja, basi zile siku safi za katikati nazo zingehisabiwa kuwa ni hedhi na ile damu ya siku ya kumi na moja tu ndio ingehisabiwa kuwa ni istihaadha.

Damu ya istihaadha ni dalili ya maradhi na inapoendelea kwa muda mrefu huwa ni hatari na inapasa kuonana na daktari. Idadi ya siku za hedhi kwa kila mwezi hufanana na idadi ya siku safi kwa kila mwezi pia hufanana. Mwezi mmoja ina maana ni siku inayoanza hedhi moja hadi ile siku inayoanza hedhi ya mwezi unaofuata. Kila mwanamke anatakiwa ahifadhi kwa moyo ni siku ngapi ndani ya mwezi anakuwa katika hedhi na siku ngapi anakuwa msafi. Ada ya hedhi kwa mwanamke haibadiliki kwa miaka mingi. Itakapobadilika basi anatakiwa aijue hiyo ada yake mpya.

Kitabu kiitwacho **(Manhadul waridina)** kinaeleza yafuatayo juu ya mabadiliko ya ada ya hedhi. Ikiwa mwanamke ataona damu sawa sawa na miezi iliyopita kwa idadi ya siku na wakati ilipokuja basi huyo huambiwa hedhi yake iko sawa. Hedhi ambayo haiko sawa inaweza ikatokana na mabadiliko aina tafauti ambayo yanaelezwa hapo chini. Ikiwa itaonesha mababdiliko hata kwa mara moja basi hiyo inakubalika kuwa imebadilika. Hivyo ndivyo fatwa zilivyoeleza. Mtu ambae hedhi yake ni ya siku tano, ikiwa ataona usafi kamili kisha akaona hedhi kwa siku sita basi huyo huambiwa ada yake imebadilika. Siku za usafi pia hubadilika. Hii ikitokea hata kwa mara moja ina maana ada imebadilika. Ikiwa mtu atakuwa anapata damu siku tano na usafi siku ishirini na tano halafu akabadilika akawa anapata damu siku tatu na usafi siku ishirini na tano au akapata damu siku tano na usafi siku ishirini na tatu basi hali ya mwanzo itakuwa ni kubadilika siku za damu na hali ya pili itakuwa kubadilika siku za usafi. Iwapo damu itapita siku kumi, hapo huwa imepatikana damu fasid. Ikiwa siku tatu au zaidi za hiyo damu fasid zitakutana na siku zake za ada, na siku za mwisho zilizobaki za ada zikakutana na siku za usafi mpya, siku ambazo zitakutana na ada yake ya zamani zitakuwa ndio ada yake mpya. Ikiwa ada yake ni siku tano, na damu ikaanza siku saba za mwisho za kipindi cha usafi na ikaendelea kwa siku kumi na moja basi hiyo nayo ni damu fasid kwa sababu imezidi siku kumi. Kuna siku zaidi ya tatu (ziko siku nne) ambazo zimo ndani ya ada yake ya zamani. Siku moja ya ada yake ya zamani (yaani siku ya tano ya ada ya zamani) imeangukia ndani ya siku za usafi. Kwa hivyo idadi ya siku zake za hedhi imebadilika na kuwa siku nne badala ya tano, lakini muda wa kuja hio hedhi haukubadilika. Wacha tutoe mifano zaidi kwa mabadiliko haya ya ada:

Ikiwa siku za damu zimetafautiana kiidadi na siku zilizopita na zikazidi siku kumi na moja, na iwapo siku tatu au zaidi hazikuangukia ndani ya ada yake ya zamani, hapa huambiwa muda wa kutokea hedhi umebadilika. Hakuna mabadiliko ya idadi ya siku za hedhi, na itaanza

kuhesabiwa ile siku damu ilipoanza kutoka. Ikiwa mwanamke hedhi yake ni siku tano na akawa hakuona damu ndani ya hizi siku tano au hakuona damu ndani ya siku tatu za mwanzo wa ada yake, kisha akapata damu kwa muda wa siku kumi na moja, idadi ya siku zake za hedhi itakuwa ile ile tano lakini kipindi cha kuanza hedhi kitakuwa kimebadilika, na hapa kitahesabiwa kuanzia siku ya mwanzo aliyoona damu. Iwapo siku tatu au zaidi za hii damu zitaangukia ndani ya siku zake za ada yake, hapo hizo tu ndio zitahesabiwa kuwa ni hedhi na zilizobaki zitakuwa ni damu fasid. Ikiwa atapata damu kwa muda wa siku tano kabla ya ada na akawa asipate damu yoyote ndani ya kipindi chake cha ada, kisha akapata damu siku moja tu iliyofuata mara tu baada ya siku zake za ada, kufuatana na imam Abu Yusuf hizo siku tano za usafi zilizo katikati ndiyo hedhi na ada yake haikubadilika. Ikiwa atapata damu katika siku tatu za mwisho za ada yake kisha ikaungana na siku nane zaidi (jumla zikawa kumi na moja), basi hizo siku tatu za mwanzo tu ndio hedhi na hapo idadi ya siku zake za hedhi itakuwa imebadilika. Iwapo hizo siku tatu zitafuatwa na siku ambazo kwa ujumla hazitozidi kumi kisha zikaja siku za usafi sahihi, basi hizo siku zote alizoona damu zitakuwa ni hedhi. Lakini Ikiwa usafi uliofuata ni usafi fasid basi ada itakuwa haikubadilika. Ikiwa ada yake ni siku tano lakini akapata damu kwa siku sita, kisha akapata usafi kwa siku kumi na nne na kisha ikafuata damu kwa siku moja basi ada yake haikubadilika. Wacha tutoe mifano kumi na moja ya mwanamke ambae ada yake ina siku tano za hedhi na siku hamsini na tano za usafi:

1- Ikiwa atapata hedhi siku tano kisha akasafika siku kumi na tano kisha akapata tena damu kwa siku kumi na moja, wala hakuna damu aliyoipata baina ya ada yake ya kawaida na iliyopita (hedhi yake kikawaida inatakiwa ije siku ya hamsini na tano baada ya ile hedhi yake aliyoipata ya siku tano.) Siku tano za mwanzo za siku kumi na moja za damu, zitahisabiwa ndiyo hedhi ya pili. Hivyo kipindi cha kuja hedhi kimebadilika lakini idadi ya siku za hedhi haikubadilika.

2- Ikiwa atapata damu kwa siku tano kisha akapata usafi siku arubaini na sita kisha akapata damu siku kumi na moja katika suala hili ni siku mbili za mwisho tu katika siku kumi na moja ndio zinaingia katika kipindi alichotakiwa apate hedhi yake ya pili (siku tisa zitaingia ndani ya kipindi alichotakiwa kuwa safi, 46+9). Lakini kwa vile siku mbili ni chache kuliko siku za uchache wa hedhi (ambao ni siku tatu), hivyo hedhi yake itahisabiwa ni siku tano za mwanzo za hizo siku kumi na moja za damu. Hivyo idadi ya siku za hedhi haikubadilika lakini wakati wa kuanza hedhi umebadilika.

3- Ikiwa atapata hedhi siku tano na akapata usafi siku arubaini na nane kisha akapata damu kwa siku kumi na moja basi siku saba za mwanzo (damu fasid) kati ya siku kumi na moja zitaungana na siku arubaini nane kukamilisha idadi ya siku za usafi, (48+7) na siku tano za mwisho zitakuwa ni za hedhi iliyokuja katika wakati sahihi na idadi sahihi.

4- Ikiwa atapata hedhi siku tano kisha akapata usafi siku hamsini na nne. Akapata tena damu kw asiku moja , akazuia kwa siku kumi na nne na akapata damu kwa siku moja nyengine. Katika suala hili kwa vile kuzuia kwake kwa pili kulikuwa ni chini ya siku kumi na tano, hiyo inazingatiwa kwamba alikuwa bado yumo ndani ya kipindi cha damu, hivyo ni kama kwamba siku zote kumi na sita (1+14+1) alikuwa yumo kwenye damu. Siku moja ya mwanzo ya damu itaungana na siku hamsini na nne kukamilisha siku zake za kawaida za usafi. Siku tano za mwanzo kati ya siku kumi na nne zitakuwa ndio siku zake za hedhi (hata kama alikuwa mkavu.) Kwa hivyo hapa hapana mabadiliko ya idadi ya siku wala wakati wa hedhi.

5- Ikiwa atapata siku tano za damu na siku hamsini na saba za usafi. Kisha akapata siku tatu za damu na siku kumi na nne za usafi kisha damu ikarejea kwa siku moja. Katika suala hili siku tatu ni siku za kawaida za ada. Siku kumi na nne zitahisabiwa kuwa ni siku za damu na kwa vile zimezidi siku kumi na moja ada yake itakuwa imebadilika kwa idadi ya siku.

6- Ikiwa atapata siku tano za damu na siku hamsini na tano za usafi. Kisha akapata siku tisa za damu kisha akapata usafi sahihi. Katika suala hili siku tisa zitakuwa ni hedhi na idadi ya siku za ada itakuwa imebadilika. Kuna zaidi ya siku tatu ndani ya kipindi cha ada na baada ya kipindi cha ada.

7- Ikiwa atapata siku tano za damu kisha siku hamsini za usafi zikafuatwa na siku kumi za damu, basi hizi siku kumi ni za hedhi. Muda wa ada ya usafi umekuwa siku hamsini. Lakini ada ya damu haikubadilika siku wala wakati.

8- Ikiwa atapata hedhi siku tano na usafi siku hamsini na nne kisha akapata damu siku nane, hizi siku nane zitakuwa ni hedhi ambayo ndani yake zaidi ya siku tatu zimo ndani ya ada. Kuna mabadiliko ya siku moja katika idadi ya siku za usafi na siku za hedhi.

9- Ikiwa atapata hedhi siku tano na usafi siku hamsini na damu ikaja tena kwa siku saba, hizi siku saba itakuwa ndio hedhi ila siku za ada zilizomo ndani yake ni chini ya tatu. Hivyo ada ya damu itakuwa

imebadilika muda wa kuanza na idadi ya siku. zake na ada ya usafi itakuwa imebadilika idadi ya siku zake.

10- Ikiwa atapata hedhi kwa siku tano kisha akapata usafi kwa siku hamsini na nane na kisha akapata hedhi kwa siku tatu, hizo siku tatu zitakuwa ndio hedhi. Mbili zimo ndani ya wakati wa ada na moja baada yake. Siku za ada zimebadilika idadi yake na wakati wa kuanza.

11- Ikiwa atapata hedhi kwa siku tano na usafi kwa siku sitini na nne kisha akapata damu kwa siku saba au kumi na moja. Katika suala la siku saba hiyo itakuwa ndio hedhi na imebadilika idadi ya siku na muda wakuja kwake wa ada. Katika suala la siku kumi na moja siku tano za mwanzo ni hedhi na zilizobaki ni damu fisadi. Idadi ya ada haikubadilika, muda wa kuja umebadilika. Idadi ya siku za ada ya usafi pia zimebadilika.

Imepokewa kutoka kwa imam Fakhrudin Uthman Zeylai "rahmatullahi alaih" (743hijri, 1343 miladi, Egypt) katika kitabu chake **(Tabyinul haqaiq)** na katika maandishi ya pembeni ya kitabu hiki yaliyoandikwa na Ahmad bin Muhamad Shilby "rahmatullahi alaih" (1031 hijria, 1621 miladia, Egypt): Ikiwa atapata damu siku moja kabla ya ada yake na kisha usafi wa siku kumi na akapata tena damu kwa siku moja, kufuatana na Imam Abu Yussuf "rahmatullahi alaih" hedhi yake itaanza siku ya mwanzo ya siku kumi (alizo mkavu) na itaendelea kwa kiasi ya muda wa siku za ada yake, hivyo siku yake ya mwanzo na ya mwisho ya hedhi zitakuwa hazina damu. Damu ilipatikana kabla ya ada na baada ya siku kumi kwa hivyo kipindi cha usafi fasid kilicho kati kati chote kitahisabiwa kuwa ni kipindi cha damu. Ila kwa mtizamo wa imam Muhammad "rahmatullahi alaih" kipindi hiki chote hakitakuwa na siku itakayohesabiwa kuwa ni hedhi. Ikiwa mwanamke ada yake ni siku tano za hedhi na ishirini na tano za usafi:

1- Ikiwa atapata damu siku moja kabla ya ada yake lakini siku ya mwanzo ya ada yake akawa msafi. Kisha damu ikaanza tena na ikaendelea kwa zaidi ya siku kumi;kufuatana na Imam Abu Yusuf siku tano za mwanzo za ada ni hedhi. Ilesiku kabla ya ada na zile zilizofuata baada ya ada ni damu fisadi. Kufuatana na imam Muhammad siku tatu zilizomo ndani ya muda wake wa ada ndio hedhi yake (hizi ni siku ya pili, ya tatu na ya nne ya ada kwa sababu siku ya mwanzo ya ada alikuwa msafi) Siku ya tano aliyotokwa na damu itakuwa nje ya siku zake za ada.

2- Ikiwa damu itaanza siku yake ya mwanzo ya ada kisha siku ya pili ikakata baadae siku inayofuata ikaanza tena na kuendelea kupita siku

kumi basi kwa makubaliano ya wanazuoni siku zake tano za ada ndio itakuwa hedhi.

3- Ikiwa siku tatu za mwanzo wa ada atapata damu kisha ikakata kwa siku mbili kisha ikaendelea kwa siku zaidi ya kumi; kufuatana na Imam Abu Yusuf siku zake tano za ada yake zitakuwa ni ndio hedhi na kufuatana na Imam Muhammad siku tatu tu za ada yake ndio itakuwa hedhi (kwa sababu kufuatana na Imam Muhamad siku ya mwanzo na ya mwisho ya hedhi lazima iwepo damu).

Katika **(Bahr)** na **(Durrul muntaka)** imesemwa (ikiwa damu itapitiza muda wa ada lakini ikamalizika kabla ya siku kumi, na muda wa usafi uliofuata ukatimia siku kumi na tano, basi siku zilizozidi nazo ni hedhi na hapo huambiwa idadi ya siku za ada imebadilika. Ikiwa damu itatokea alau mara moja ndani ya siku kumi na tano basi zile siku za ziada juu ya ada yake katika hali hii zitahesabiwa kuwa ni damu fasid. Na baada ya kutambulika kuwa zile siku za ziada zilikuwa ni damu fasid, atalazimika kulipa sala alizoziacha. Ikiwa damu itakatika baada ya muda wa ada, kabla ya siku kumi kumalizika basi ni mustahabu kusubiri hadi karibu na kumalizika wakati wa sala wa kipindi kiliopo, kisha atakoga na kusali sala ya kipindi hicho. Baada ya hapo anaweza kufanya tendo la ndoa. Ikiwa wakati anasubiri, kukampita kukoga na kusali hadi wakati wa kipindi cha sala ile ukatoka, hapo itajuzu kufanya tendo la ndoa hata bila ya kujitoharisha.

Ikiwa mtoto wa kike anaona damu kwa mara ya kwanza au mwanamke ambae anaona damu baada ya kupitiwa na siku kumi na tano tangu kupita ada yake, damu hiyo ikakata  kabla siku tatu, basi katika mifano hii miwili atatakiwa asubiri hadi karibu na mwisho wa wakati wa kipindi cha sala kiliopo na kisha atatia udhu tu(bila kulazimika kukoga) na atasali sala ya kipindi kile na atalipa sala alizoziacha ndani ya hicho kipindi kisichotimia siku tatu. Ikiwa itaanza tena, basi atajizuia kusali na ikikata basi atasubiri mwisho wa wakati wa kipindi cha sala iliopo atatia udhu na kusali sala ya wakati ule na atalipa sala aliyoiacha kama ipo. Ataendelea kufanya hivyo hadi siku tatu zitakapokamilika Katika muda huu tendo la ndoa haliruhusiwi hata kama atakoga.

Katika mifano hiyo ikiwa damu itaendelea zaidi ya siku tatu lakini ikakatika kabla ya muda wa ada, tendo la ndoa halitaruhusika hadi muda wa ada utakapokamilia, hata kama atakoga. Lakini kama hakuona tone la damu hadi mwisho wa kipindi cha sala basi atakoga na kusali. Atafunga vile vile. Ikiwa atabakia kuwa msafi kwa muda wa siku kumi na tano, basi ile siku ya mwisho ilomalizika damu itakuwa

ndiyo ya ada yake mpya. Lakini kama damu itajitokeza tena basi ataacha kusali. Na ile siku aliyoifunga atatakiwa aje ailipe baada ya kumalizika Ramadhan. Ikiwa damu itakatika tena atakoga karibu na mwisho wa kipindi cha sala na atasali sala ya wakati ule na atafunga vile vile. Ataendelea kufanya hivyo hadi siku kumi zitakapomalizika. Baada ya siku kumi atasali bila ya kukoga hata kama ataona damu na kufanya tendo la ndoa kwake itakuwa ni halali hata bila ya kukoga. Hata hivyo ni mustahab kukoga kabla ya kufanya tendo la ndoa. Ikiwa damu itakatika kabla ya alfajiri, lakini ikawa muda uliobaki unatosha kukoga na kuvaa nguo tu na haubaki muda wa kuweza kusema (Allahu akbar) basi huyo hatolazimika kulipa sala ya Isha iliyopita. Na ataifunga siku hiyo. Lakini kama palibakia muda wa kuweza kusema (Allahu akbar) basi atatakiwa kuilipa sala ya Isha ya usiku huo. Ikiwa damu yake itaanza kabla ya wakati wa kufutari basi hapo hapo funga yake itaharibika na atatakiwa kuja kuilipa. Ikiwa damu itakuja ndani ya sala basi sala yake itaharibika na kama ni sala ya fardhi hatotakiwa kuilipa lakini kama ni sala ya sunna atailipa. Ikiwa atalala na kuiona damu ndani ya kitambaa chake (au pamba) baada ya kuamka basi anahesabiwa kuingia katika hedhi kuanzia huo wakati alipoiona hiyo damu. Ikiwa ataamka asubuhi na kuona kitambaa chake (au pamba) kiko safi, basi huyo anahesabiwa alisafika wakati akiwa usingizini (na wala sio wakati alipokiona hicho kitambaa kisafi). Katika masuala haya mawili wote wana wajibika kulipa sala ya Isha ya usiku huo. Kwa sababu sala inategemea kipindi cha usafi (na wala sio kupata hedhi). Ikiwa mwanamke atapata hedhi kabla ya kusali sala ya kipindi kilichoingia basi hatolazimika kuilipa.

Lazima kuwe na kipindi cha usafi uliokamilika baina ya hedhi mbili. Ikiwa kipindi hiki kitakuwa ni kusafika sahihi basi hizo damu mbili za kabla na baada ya kipindi hicho kwa makubaliano ya wanavyuoni. huwa ni hedhi. Siku za kusafika zinazoonekana ndani ya siku kumi za hedhi nazo huhesabiwa kuwa ni siku za hedhi. Damu itakayoonekana baada ya siku kumi ni istihaadha (damu fisadi) nayo huisabiwa imo ndani ya kipindi cha usafi. Ikiwa mtoto wa kike atapata hedhi siku tatu kisha akasafika kwa siku kumi na tano. Akapata tena damu ya siku moja, na akapata usafi wa siku moja kisha akapata damu kwa siku tatu, katika suala hili zile siku tatu za mwanzo na hizi za mwisho zitakuwa ndio hedhi mbili. Kwa vile ada yake itakuwa siku tatu, hedhi ya pili haikuanza na ile siku moja pekee aliyopata damu. Kupata damu hiyo siku moja kunakifanya kipindi chote cha usafi kuwa ni fasid. Molla Husraw “rahmatullahi alaih” katika sherhe ya **(Ghurar)** anasema.

Iwapo binti atapata damu siku moja akazuia siku kumi na nne, akapata damu siku moja akazuia siku nane, akapata damu siku moja akazuia siku saba, akapata damu siku mbili akazuia siku tatu, akapata damu siku moja akazuia siku tatu, akapata damu siku moja akazuia siku mbili, hatimae akapata damu siku moja, katika mtiririko huu wa siku arubaini na tano zile siku kumi pekee zilizofuata siku kumi na nne za usafi ndio hedhi na zilizobaki ni Istihaadha. (damu fasid) kufuatana na imam Muhammad. Baada ya siku kumi hizo hakuna kipindi cha usafi kamili kilichopatikana na kwa hivyo hakuna hedhi iliyoanza. Kwa vile hakuna hedhi nyengine iliyoanza, siku za usafi zilizofuata haziisabiwi kuwa ni siku za muendelezo wa damu kwa sababu hazimo ndani ya kipindi cha hedhi. Kufuatana na Imam Abu Yusuf 'siku kumi' za mwanzo na 'siku kumi' za nne ambazo zina siku za usafi mwanzo na mwisho hizo ndio zitakuwa hedhi. Na kufuatana na Abu Yusuf siku za usafi fasid zilizofuata, zinahesabiwa kuwa zimo ndani ya mwendelezo wa damu. Kwa hivyo kwa mfano huu baada ya siku kumi za mwanzo za hedhi siku ishirini ni za usafi na siku kumi za mwisho ni za hedhi.

Ikiwa damu itaendelea kwa siku kumi na tano bila kukatisha **(Istimrar)** basi itahesabiwa kufuatana na ada. Kufuatana na ada zitahesabiwa siku za usafi kutoka katika mwezi uliopita zilipomalizikia hapo itahesabiwa kuwa hedhi ndio imeanza na itapewa siku kufuatana na ada yake

Ikiwa damu ya kuendelea (istimrar) itapatikana kwa mtoto wa kike anaeanza hedhi basi kufuatana na **(Manhalul waridina)** hali zifuatazo zitazingatiwa

1- Ikiwa damu itaendelea, siku kumi za mwanzo itakuwa ni hedhi na siku ishirini zilizobaki itakuwa ni siku za usafi.

2- Ikiwa istimrar imetokea baada ya kwamba mtoto wa kike ameshawahi kuona damu sahihi na usafi sahihi basi atahisabiwa kama mwanammke ambae ada yake inajulikana. Mfano kama atapata damu siku tano na akapata usafi wa siku arobaini, basi hizo siku tano zitakuwa ndio hedhi na siku arobaini itakuwa kipindi cha usafi.

3- Ikiwa atapata kipindi cha usafi fasid kisha akapata damu fasid, hivyo vyote viwili havitohesabiwa kuwa ni ada. Ikiwa usafi fasid utatokana na kuwa siku zake zilipungua chini ya kumi na tano basi damu ya mwanzo itakayoonekana itazingatiwa kama ni damu inayoendelea (istimrar). Ikiwa atapata damu siku kumi na moja na usafi siku kumi na nne kisha akapata damu ya istimrar katika suala hili hiyo damu ya mwanzo kwa vile imezidi siku kumi ni fasid kwa hivyo siku ya

kumi na moja ya damu itahisabiwa ndani ya kipindi cha usafi. Pia siku tano za mwanzo za damu ya istimrar nazo zitaingizwa katika kipindi cha usafi. Baada ya hizi siku tano siku kumi zinazofuata zitakuwa ni hedhi na ishirini zitakuwa ni usafi na ataendelea kwa mtindo huo. Iwapo kipindi cha usafi kitatimia ila tu kikawa kimechanganya na siku za damu ndani yake basi pia kitahisabiwa kuwa ni usafi fasid, na ikiwa siku za usafi zikijumlishwa na siku za damu hazizidi thelathini, basi hiyo damu ya mwanzo itakubalika kuwa ni damu ya istimraar. Na hali ni hiyo hiyo kama atapata damu siku kumi na moja na akapata usafi siku kumi na tano kisha akapata damu ya kuendelea (istimraar). Siku ya mwanzo ya siku kumi na sita za usafi (siku ya 11 ya damu) kwa vile ilikuwa ni ya damu hiki kipindi kinakuwa cha usafi fasid. Siku nne za mwanzo za damu ya istimraar zitaingia ndani ya kipindi cha usafi fasid(ili kukamilisha siku ishirini). Ikiwa jumla inazidi siku thalathini, siku kumi za mwanzo zitakuwa ni hedhi na siku zitakazoendelea hadi kufikia damu ya istimraar zitakuwa ni siku za usafi, baada ya damu ya istimraar siku kumi itakuwa hedhi na ishirini ni usafi. Na iwapo itapatikana hedhi siku kumi na usafi siku ishirini kisha ikaja damu ya istimraar basi hesabu yake itakuwa kama hivyo.

4- Ikiwa atapata damu sahihi na usafi fasid, siku za damu sahihi zitakuwa ndio ada yake. Kisha siku za usafi zitahesabiwa kwa kukamilisha siku thalathini. Mfano kapata damu siku tano, usafi siku kumi na nne kisha akapata damu ya kuendelea (istimrar). Siku tano za mwanzo zitakuwa ndio za damu na siku ishirini na tano zitakuwa za usafi. Ili kukamilisha siku za usafi ziwe ishirini na tano, tutachukua siku kumi na moja kutoka kwenye siku za damu ya istimrar. Baada ya hapo ataendelea kwa mtindo wa siku tano za hedhi na siku ishirini na tano za usafi. Ikiwa atapata damu siku tatu kisha usafi siku kumi na tano, ikarejea damu kwa siku moja kisha usafi siku kumi na tano kisha damu ya istimrar hapa siku tatu za mwanzo ni hedhi na siku zote zilizopo kabla istimrar (15+1+15) zitakuwa ni usafi fasid. Hivyo hedhi yake ni siku tatu na siku thelathini na moja ni za usafi. Ila ndani ya kipindi cha istimraar siku tatu atahisabu hedhi na siku ishirini na saba atahesabu usafi. Lau kama usafi wa pili ungekuwa ni siku kumi na nne basi kufuatana na Imam Abu Yusuf hizo zingehesabiwa ni siku za damu. Hivyo siku mbili kati ya hizo zingehesabiwa kuwa ni hedhi (zinajumuika na ile moja) kisha siku kumi tano zinazofuata (mbili kutoka istimrar) zitakuwa za usafi. Hapa ada itahesabiwa ni siku tatu za hedhi na siku kumi na tano za usafi.

Mwanamke mwenye kusahau ada yake huitwa **(Muhayyira)** au **(Dhalla)**.

**(NIFASI)** ni damu ya uzazi. Vile vile kama mwanamke ataharibu mimba kitakachotoka kama mikono na miguu yake tayari inatambulika basi damu yake pia itakuwa nifasi. Hakuna muda mfupi maalum kwa nifasi. Wakati wowote damu itakapokatika basi atakoga na kuanza kusali. Hata hivyo hawezi kufanya tendo la ndoa hadi siku zake za ada zimalizike. Wingi wake ni siku arobaini. Ifikapo siku ya arubaini atakoga na kuanza kusali hata kama damu haijakatika. Damu ambayo itatoka baada ya siku arubaini itakuwa ni istihaadha. Ikiwa mwanammke katika uzazi wake wa mwanzo atapata damu siku ishirini na tano, basi ada yake itakuwa ni siku ishirini na tano. Ikiwa mwanamke huyu katika mimba ya pili atapata damu siku arubaini na tano basi nifasi yake ni siku ishirini na tano na siku ishirini zilizobaki ni istihaadha. Atasali kadhaa siku ishirini alizoziacha hivyo idadi ya siku za nifasi nayo lazima itambulike. Ikiwa atapata damu kwa muda wa siku thelathini na tano hiyo idadi ya siku zake za ada itakuwa imebadilika kutoka ishirini na tano na kuwa thalathini na tano na hizo siku zote zitakuwa ni nifasi.

Ikiwa ndani ya mwezi wa Ramadhan damu itakatika mara tu baada ya alfajiri kuingia basi siku hiyo atatakiwa ajizuie kula na kunywa lakini hatohesabiwa kuwa amefunga na atatakiwa kuja kuilipa baadae. Na ikiwa hedhi itaanza wakati wowote ule baada ya alfajiri kuingia hata kama itaanza baada ya alasiri basi atatakiwa ale na anywe.

Kufuatana na madhehebu yote manne ni haramu kwa mwenye hedhi na nifasi kusali, kufunga, kuingia msikitini, kushika msahafu na kusoma, kutufu na kufanya tendo la ndoa. Funga atazilipa lakini sala hazilipi, atasamehewa. Katika kila kipindi cha sala kama atatia udhu na kukaa juu ya msala akaleta tasbihi na adhkaar basi atapata thawabu sawa na za sala iliosaliwa vizuri.

Katika kitabu cha **(Jawhar)** anasema (Mwanamke ana wajibu wa kumwambia mumewe hedhi yake ikianza. Ikiwa mume atamuuliza na yeye asimwambie basi hio ni dhambi. Na iwapo ni msafi akamwambia mumewe kuwa yumo ndani ya hedhi hiyo pia ni dhambi kubwa. Mtume "sallallahu alayhi wasallam" anasema **(Amelaaniwa mwanamke ambae anamficha mumewe siku inayoanza hedhi yake na siku inayomalizika)** Katika siku za kawaida au katika hedhi ni haramu kumuendea mwanamke kinyume na maumbile (kwenye duburi). Ni dhambi kubwa sana. Amelaaniwa mwenye kumfanyia hivyo mkewe. Na yule mwenye kumfanyia mwanamme **liwati** basi atakuwa amefanya dhambi kubwa zaidi. Kufuatana na surat Anbiya hilo

limeitwa ni tendo la kikhabithi. Katika sherhe ya **(Birgivi)**, amesema mtume "sallallahu alayhi wasallam" **(Ikiwa mtawakuta wawili wanafanya liwati basi waueni wote).** Baadhi ya wanazuoni wamesema kwamba wote wawili wanachomwa moto. Wenye kufanya liwati wote wanakuwa na janaba. Mwenye kusafishwa tumbo kwa kupitishwa kitu kwenye duburi yake hapati janaba lakini funga yake itakuwa imeharibika (fayziyya).]

Ikiwa wakati wa sala umeshaingia na mwanamke akapata hedhi kabla ya wakati huo kutoka basi sala hiyo halazimiki kuilipa. [Soma kitabu cha **(Saadatin abadiyya)** mlango wa kukoga.]

## YANAYOHUSU UDHU

Fardhi za udhu ni nne kufuatana na Hanafi, saba kufuatana na Malik na sita kufuatana na Shafii na Hanbali:

1- Kuosha uso.

2- Kuosha mikono hadi kwenye visugudi.

3- Kupangusa robo ya kichwa.

4- Kukosha miguu pamoja na vifundo.

Udhu ni aina nne. Fardhi, wajib, sunna na mandub.

Ni fardhi kutia udhu katika hali nne. Kusali pamoja na sala ya jeneza, kushika msahafu na kusujudu sijda ya kisomo.

Ni wajibu kutia udhu kwa ajili ya tawafu ya ziara.

Ni sunna kutia udhu kwa kusoma Quran uliyoihifadhi, kutembelea makaburi na kabla ya josho la wajib.

Ni mandub kukoga kabla ya kulala na baada ya kuamka, baada ya kusengenya na kusema uongo na baada ya kusikiliza muziki wenye kusisimua shahawa. Baada ya mambo hayo maovu ataleta istighfar na toba kisha ni mandub kutia udhu.

Ni mandub kutia udhu wakati wa kwenda kwenye majlis za elimu. Na ikiwa una udhu kisha ukafanya jambo ambalo ni lazima kutia udhu kwalo, mfano ukasali, basi ni mandub kutia udhu tena (hata kama udhu haujatenguka) na kama hajatenda ibada inayolazimu udhu basi ni makruh kutia udhu tena.

## YANAYOHUSU MAJI

Maji ni aina nne Mutlaq, mukayyad, mashkuk na mustaamal.

1- Maji Mutlaq ni maji ya mvua , bahari, chemchem mto na kisima. Maji haya yana sifa za kusafisha kitu kilicho kichafu na yanaweza kutumika kwa mahitaji yoyote.

2- Maji mukayyad ni kama maji ya tikiti, maji ya zabibu, maji ya mauwa na mengine kama hayo. Maji haya pia yanaweza kusafisha kitu kichafu ila hayatofaa kwa kutilia udhu au kukogea.

3- Maji mashkuk ni maji yaliyobaki baada ya kunywewa na punda au nyumbu ambae baba yake ni punda.

Maji haya yanafaa kukoga na kutilia udhu. Ana hiyari ya kutanguliza chochote kati ya hayo mawili.

4- Maji mustaamal ni yale yaliyotumika na ni jambo wametofautiana wanazuoni juu ya kuitwa kwake Mustaamal kuwa ni baada ya kuwa yameshaanguka juu ya sakafu au mara tu baada ya kuuacha mwili unaokoshwa. Lililo makini zaidi ni kwamba mara tu baada ya kuuacha mwili unaokoshwa. Kuna kauli tatu juu ya hili. Kufuatana na Abu Hanifa “rahmatullahi alaih” maji hayo ni Najasat ghalidha (najsi nzito), kufuatana na Imam Abu Yusuf “rahmatullahi alaih” ni Najasat hafifa (najsi nyepesi) na kufuatana na Imam Muhamad “rahmatullahi alaih” maji hayo ni safi. Kauli hii ndio sahihi zaidi.

Masharti ya wajib kwa udhu ni tisa:

1- Kuwa muislam.

2- Kuwa baleghe.

3- Kuwa na akili.

4- Kuwa huna udhu.

5- Maji ya kutilia udhu kuwa safi.

6- Kuweza kutia udhu.

7- Kutokuwa na hedhi.

8- Kutokuwa na nifasi.

9- Kuwa ndani ya wakati kwa kila sala [Sharti hili ni kwa wale wenye udhuru.]

Sunna za udhu zimetajwa ishirini na tano:

1- Kusoma Audhu.

2- Kusoma Bismillahi.

3- Kukosha viganya viwili.

4- Kukosha pachiko za vidole.

5- Kusukutua.

6- Kupandisha maji puani.

7- Kutia nia. Kwa madhehebu ya Hanafi si fardhi kutia nia wakati wa kuosha uso, ni sunna lakini kwa shafii ni fardhi. Kwa Maliki ni fardhi wakati wa kukosha viganja.

8- Kuelekea kibla.

9- Kutia vidole kwenye ndevu kama ni nyingi.

10- Kupangusa ndevu.

11- Kuanza kulia katika kuosha.

12- Kutumia kidole kidogo cha mkono wa kushoto na kukipitisha baina ya vidole vya mguu wa kulia kwa kuanzia kidole kidogo na vinavyofuata.

13- Kupangusa kichwa chote kizima.

14- Kupangusa masikio na shingo kwa maji yaliyobaki katika kupangusa kichwa.

15- Kukosha kwa mpangilio.

16- Kukosha kwa kuendeleza bila kukatiza.

17- Kuanzia mbele wakati wa kupangusa kichwa

18- Kutumia mswaki.

19- Kufikisha maji pembeni ya macho na kwenye nyusi.

20- Kusugua wakati wa kukosha.

21- Kutia udhu hali ya kuwa umesimama sehemu iliyo juu kidogo.

22- Kuosha viungo mara tatu.

23- Kulijaza birika baada ya kumaliza kutia udhu.

24- Kuto kuzungumza mambo ya kidunia wakati wa kutia udhu.

25- Kudumu na nia wakati wa kutia udhu.

## YANAYOHUSU KUTUMIA MSWAKI

Kutumia mswaki kuna faida kumi na tano ambazo zimeainishwa hapo chini kutoka kitabu kiitwacho **(Sirajul wahhaj).**

1- Kusababisha kupata shahada wakati wa kufa.

2- Kusafisha meno na ufizi.

3- Kukata nyongo.

4- Inasaidia kusafisha kifua kwa kutoa makohozi.

5- Kuondoa maumivu mdomoni.

6- Kuondoa harufu mbaya.

7- Allah anampenda mtu anaetumia mswaki.

8- Inaipa nguvu mishipa ya damu ya kichwani.

9- Shetani hupata huzuni.

10- Macho yake huingia nuru.

11- Huongeza mema na mazuri.

12- Inakuwa mtu katekeleza sunna.

13- Mdomo huwa safi.

14- Anakuwa mfasaha wa maneno.

15- Rakaa mbili zinazoswaliwa na mtu alietumia mswaki ni bora kuliko rakaa sitini zinazoswaliwa na mtu asietumia mswaki.

**Yaliyo mustahabu katika udhu ni mambo sita yafuatayo:**

1- Nia iliyo moyoni kuitamka kwa mdomo.

2- Maji yaliyobaki masikioni kupangusia shingo.

3- Kutokukosha miguu hali ya kuwa umeielekeza kibla.

4- Kunywa maji yaliyobakia katika udhu ikiwezekana akiwa ameelekea kibla katika hali ya kusimama.

5- Kudondoshea maji kidogo nguo yako baada ya udhu.

6- Kujipangusa maji kwa kitu kisafi.

Ibn Abidin wakati alipokuwa akielezea mambo yanayotengua udhu alisema yafuatayo (Jambo ambalo si makruh katika madhehebu yake mtu na likawa ni fardhi kwa madhehebu nyengine, basi huwa ni mustahab kulifanya jambo hilo.) Anasema Imam Rabbani katika barua ya 286 (Kwa vile katika madhehebu ya Malik ni fardhi kusugua viungo vinavyokoshwa, basi na sisi (Hanafi) inabidi tusugue. Ibn Abidin wakati anaelezea talaka rejea anasema (Kwa yule alie katika madhehebu ya Hanafi ni bora kufuata yaliyo katika madhehebu ya Maliki. Hii ni kwa sababu Imam Malik ni kama mwanafunzi wa Imam Hanafi. Wakati pasipopatikana fatwa ya jambo fulani katika madhehebu ya Hanafi basi wanazuoni wao walichukua fatwa ya Malik. Madhehebu ya Maliki ndiyo yaliyo karibu zaidi na madhehebu ya Hanafi.)

**Mambo yaliyo makruh kwenye udhu:**

1- Kupiga maji kwa nguvu kwenye uso.

2- Kuyapuliza maji ya kutilia udhu.

3- Kukosha chini ya mara tatu.

4- Kukosha zaidi ya mara tatu.

5- Kutemea mate maji ya kutilia udhu.

6- Kupenga mafua ndani ya maji.

7- Kumeza maji wakati wa kusukutua.

8- Mgongo kuelekea kibla.

9- Kufumba macho.

10- Kufumbua macho kwa upana.

11- Kuanza kuosha upande wa kushoto.

12- Kupenga mafua kwa mkono wa kulia.

13- Kutia maji ya kusukutua kwa mkono wa kushoto.

14- Kutia maji puani kwa mkono wa kushoto.

15- Kupiga miguu chini.

16- Kutia udhu kwa maji yaliyopashwa kwa jua.

17- Kuto kukwepa kutumia maji mustaamal.

18- Kuzungumza mambo ya kidunia.

**Mambo yenye kubatilisha udhu:**

1- Kinachotoka utupu wa nyuma.

2- Kinachotoka utupu wa mbele.

3- Minjoo au kijiwe kikitoka mbele au nyuma.

4- Kusafishwa tumbo kupitia utupu wa nyuma.

5- Dawa aliyoitia mwanamke ndani ya utupu wa mbele ikitoka.

6- Ikiwa dawa iliyotiwa masikioni itatokea mdomoni udhu utatenguka lakini kama itatokea puani au masikioni udhu hautenguki **(Hindiyya)**.

7- Ikiwa pamba aliyoitia mwanamme katika mrija wa mkojo itarowa na kuanguka. (Ikiwa sehemu ya pamba itakuwa nje ya mrija wa mkojo na ikawa kavu basi udhu hautotenguka ikiwa haitoanguka)

8- Ikiwa kipande cha pamba kitaanguka na sehemu iliyo nje ikawa imerowa.

9- Kutapika mdomo ukajaa. Kutoa makohozi hakutengui udhu hata kama yatajaa kinywani. Maji yanayotoka mdomoni wakati wa kulala ni masafi hata kama yatakuwa manjano.

10- Machozi yanayotokana na maradhi yatatengua udhu ila yale ya kulia au yanayotokana na sababu kama vitunguu hayatengui udhu.

11- Damu, usaha au maji ya manjano yakitoka puani yatatengua udhu hata kama hayakutoka nje ya tundu ya pua. Mafua ni kitu kisafi wala hayatengui udhu yanapotoka.

12- Ikiwa mate yaliyotemwa yatakuwa na damu nyingi.

13- Ikiwa atatafuna kitu chenye damu na damu ikaingia mdomoni na menoni mwake basi udhu utatenguka. Ikiwa damu haikuingia mdomoni au menoni basi udhu hautenguki.

14- Ikiwa damu itatoka katika sehemu yoyote ya mwili na ukaiona damu ile imeenea sehemu ile basi kwa madhehebu ya Hanafi udhu utatenguka. Ila kwa madhehebu ya Malik na Shafii udhu hautenguki.

15- Kupanda mnyama bila soji na ukawa umelala hali ya kuwa anateremka mlima.

16- Ikiwa utakuwa na shaka kwamba umetia udhu au hukutia basi dhana yako iwe hukutia.

17- Ikiwa mume atamkumbatia mkewe wakiwa uchi basi udhu wao utatenguka.

18- Ikiwa utasahau kukosha moja ya viungo vya udhu na usiweze kukijua ni kipi.

19- Mahali penye kijipu pakitoka usaha, damu, au maji manjano kwa kutumbuliwa au chenyewe kikipasuka

20- Ikiwa atakuwa na kidonda ambacho kina usaha , damu au maji manjano ndani yake, ikiwa uchafu huo utaingia sehemu ambayo haina kidonda au ukachafua kitambaa kilichofungwa juu ya kidonda basi udhu wake utatenguka.

21- Ikiwa utalala na kuegemea kitu basi ikiwa kitu ulichokiegemea kikiondoshwa utaanguka kwa usingizi basi udhu wako utatenguka.

22- Wakati wa sala ambayo ina rukuu na sijda ukicheka hadi ukajisikia wewe mwenyewe na mtu alie ubavuni kwako udhu utatenguka. Ikiwa kicheko chako hakitokuwa kikubwa cha kusikilikana na mtu alie ubavuni kwako basi udhu hautotenguka. lakini sala itakuwa imebatilika.

23- Kupata kifafa na kuzimia kunatengua udhu.

24- Ikiwa usaha, damu au maji ya manjano yatatoka sikioni kisha yakagusa sehemu ambayo ni wajibu kuguswa na maji wakati wa josho la lazima basi udhu utatenguka.

**Ulaya wamejifunza kwetu kukoga chooni**
**Kabla ya hapo nyumba zao haziingiliki kwa harufu mbaya.**

**Usafi duniani umeenezwa na waislam**
**Hivyo binaadamu wameokoka na adui mkubwa.**

## DUA ZA UDHU

Wakati wa kuanza kutia udhu atasema (**Bismillahi-l-adhim walhamdulillahi ala dinil islam wa ala tawfiqil iman. Alhamdulillahi lladhy jaalal maa tahuran wajaalal islami nuuran).**

Wakati akitia maji ya kusukutua atasema (**Allahumma asqiny min hawdhi nabiyyika kaasan la adhmau baadaha abadan).**

Wakati wa kupandisha maji puani atasema **(Allahumma arihny rayhatal janna warzukni min naimiha wala turihny rayhata nnar).**

Wakati wa kuosha uso atasema **(Allahumma bayyidh wajhy binurika yawma tabyadhu wujuhu awliyaika wala tusawwid wajhi bidhunuby yawma taswadu wujuh aadaika).**

Baada ya kukosha mkono wa kulia atasema **(Allahumma aatwiny kitaby biyaminy wahasibny hisaban yasira).**

Na atakapokosha mkono wa kushoto atasema **(Allahumma la tuutwiny kitaby bishimaly wala min warai dhahry wala tuhasibny hisaban shadyda).**

Wakati wa kupangusa kichwa atasema **(Allahumma harim shaari wabashari alannar. wa adhillini tahta dhilli arshika yawma la dhili illa dhilluka).**

Wakati akipangusa masikio atasema **(Allahummaj-alny minalladhyna yastamiunal kalama fayatabiuna ahsanaha).**

Wakati anapangusa shingo atasema **(Allahumma aatik rikaabaty min annar wahfadh mina salassil wannar).**

Wakati anakosha mguu wa kulia atasema **(Allahumma thabit kadamayya alasirrat yawma tadhillu fihil akdaam).**

Wakati anakosha mguu wa kushoto atasema **(Allahumma la tatarud kadamayya ala sirati yawma tatarud kullu akdami aadaika. Allahummaj-al saayi mashkuran wa dhanbi maghfuran wa amali makbulan wa tijarati lan tabur).**

Baada ya kukamilika udhu atasema **(Allahummaj-alny mina tawwabin waj-alny minal mutatahirin waj-alni min ibadika swalihin. waj-alny mina lladhyna la khawfun alayhim walahum yahzanun).**

Baadhi ya watu husema hali ya kuwa wanaangalia mbinguni **(Subhaanakallahumma wabihamdika ash-hadu anlaailaaha illa anta wahdaka la sharika laka wa anna Muhammadan abduka wa rasuuluka).**

Baada ya hapo atasoma **(Innaa anzalnahu)** mara moja, mbili au tatu kwa kuanza na **(bismillahi).**

Ni lazima kuwasomesha watu wake wa nyumbani elimu ya dini kwa sababu siku ya kiama mtu ataulizwa juu ya mkewe.

# MLANGO WA KUTAYAMMAM

Kufuatana na madhehebu ya Hanafi kutayammam inasihi hata kama wakati wa sala haujaingia lakini kwa madhehebu matatu yaliobaki haisihi. Fardhi za kutayammam ni tatu:Yale yaliyolazima kwa tayammum ya udhu ni sawa na yale ya tayammum ya kukoga ila kuna tafauti katika nia. Kwa hivyo tayammum ya moja kati ya hili haiwezi kutumika kwa jengine.

1- Ni sharti kutia nia.

2- Kupiga viganja viwili kwenye dongo lililo safi na kupangusa uso wote.

3- Kupiga tena viganja viwili kwenye dongo na kupangusa mikono miwili. Kiganja cha kushoto kitaupangusa mkono wa kulia pande zote na kiganja cha kulia kitaupangusa mkono wa kushoto pande zote. Hii ni katika nguzo.

Dalili ya kuwa kutayammam ni fardhi iko katika Suratu Nisaa aya ya 43 na Suratul Maida aya ya 6. Kufuatana na Malik na Shafii haijuzu kutayammam kabla ya wakati wa sala kuingia na tayammam moja haisaliwi zaidi ya sala moja ya fardhi.

Haijuzu kufanya tayammam kwa vitu sita vifuatavyo ila kama patapatikana dongo juu yake. Chuma, shaba, fedha , dhahabu, bati, na bronzi. Ukiachilia vitu hivi, vitu vyengine ambavyo vikipigwa moto vinayayuka basi vinafaa kwa tayammam. Kigae ambacho kinayayuka kikipigwa moto na kaure ila tu sharti viwe katika hali ya dongo.

Ikiwa sehemu ilikojolewa na ikawa imeshakauka, sehemu hiyo inafaa kusali ila dongo lake halifai kwa tayammam.

Ili kuweza kufanya tayammam lazima kwanza mtu awe ametafuta maji asiyapate, akamuuliza muislam alie muadilifu na akampa jawabu la ukweli juu ya kutokupatikana kwa maji katika sehemu husika.

Masharti ya kutayammam ni matano:

1- Kutia nia. 2- Kupangusa sehemu husika. 3- Kutayammamu kwa kutumia udongo au ikiwa kitu chenyewe si udongo basi pawe na dongo au vumbi juu yake. 4- Dongo au kitu chenye dongo kiwe safi. 5- Iwe haiwezekani kutumia maji kwa uhakika kwa hukmu. [Kuwa na uchovu miguuni na mikononi baada ya maradhi ni udhuru. Uzee nao pia ni udhuru. Hawa husali kwa kukaa kitako.]

Sunna za tayammam ni saba.

1- Kusoma Bismillahi. 2- Kupiga viganja kwenye dongo safi. 3- Kupeleka viganja mbele na nyuma mara moja juu ya sehemu uliyopiga. 4- Kutanua vidole. 5- Kutoa vumbi kwenye viganja kwa kuvipiganisha(kama kupiga makofi). 6- Kuanza na kupangusa uso. 7- Kupangusa kila sehemu ya mkono pamoja na visugudi.

Sharti za kutafuta maji ni nne:

1- Kuwa mkazi wa sehemu hiyo.

2- Kuelezwa kuwa maji yanapatikana.

3- Kuwa na dhana yenye nguvu kuwa maji yanapatikana.

4- Kuwa hupo kwenye sehemu ya hatari.

Ikiwa mtu atakuwepo pahali na maji yakawa yanapatikana kwa umbali uliozidi meli moja basi ataruhusiwa kufanya tayammum. Na ikiwa masafa hayafiki meli moja na ikawa muda uliobaki wa sala unatosha kwa yeye kuyafuata maji basi haijuzu kutayammam.

Na ikiwa atatafuta maji asiyapate, kisha akatayammam na kusali na baadae akayaona maji je atarejea sala yake? Hili ni suala lenye tofauti kati ya wanazuoni. Kauli iliyo sahihi zaidi ni kwamba hatorejea sala yake.

Ikiwa mtu atakua ameroa na hakupata maji ya kutilia udhu wala kitu cha kufanyia tayammam basi atalikausha dongo kisha atafanyia tayammam. Ikiwa kikundi cha watu wamefanya tayammam ila mwenzao mmoja akafanikiwa kuyapata maji basi hawa wote tayammam yao itakuwa batil.

Na ikiwa wataletewa kima cha maji na wakaambiwa mmoja wenu anaweza kutia udhu basi tayammam yao wote itakuwa imebatilika. Na kama wataambiwa nyote tieni udhu na ilhali maji yanatosha kwa mmoja wao tu, basi wote tayammam yao itakuwa sahihi.

Ikiwa mtu atakuwa na janaba na ikawa maji hayapatikani ila msikitini basi kwanza atafanya tayammam kwa nia ya kukoga ili aweze kuingia msikitini. Na kama atafika msikitini na asikute maji basi atahitaji kufanya tayammum nyengine ili asali.

Ikiwa mtu wakati amekaa msikitini atapata ndoto na kutokwa na manii, basi kwanza atafanya tayammam, kisha ndio atanyanyuka na kutoka msikitini.

Ikiwa mtu atakuwa hana mikono basi anaweza akafanya tayammam. Ila kama nae mtu wa kumsaidia kustanji (kujisafisha mbele

na nyuma) basi atalazimika kusafishwa. Ikiwa hana mtu wa kumsafisha basi atakuwa amesameheka.

Ikiwa mtu hana miguu wala mikono kufuatana na Imam Abu hanifa na Imam Muhammad Shaybany huyo atasameheka kusali, ila Imam Abu Yusuf yeye anaona mtu huyu lazima asali.

Haijuzu kutayammam kwa ajili ya kuwahi sala ya ijumaa, yaani ikiwa mtu hana muda wa kutosha kutia udhu ili kuwahi sala ya ijumaa hivyo akaamua kutayammam basi haijuzu. Kwa sababu sala ya ijumaa inayo mbadala wake nayo ni sala ya adhuhuri. Kufuatana na kitabu kiitwacho **(Durrul Muhtar)** haijuzu kutia udhu kwa maji ya tende yaitwayo Nabidh.

Ikiwa mtu yuko safarini na akatokwa na manii ndani ya ndoto, atafanya tayammum na kusali sala ya asubuhi. Akaendelea na safari yake hata wakati wa adhuhuri ulipokaribia mwisho akasali sala ya adhuhuri. Akaendelea na safari na akayapata maji wakati wa mwisho wa sala ya laasiri, je atazisali tena sala zake za asubuhi na adhuhuri?

Jambo hili lina tafauti ya wanazuoni na kuna wanaosema atazirejea na kuna wasemao hatozirejea. Suala hili linaweza kutizamwa kufuatana na Sahibi Tartib.

Ikiwa mtu ana maji yake kwenye mnyama wake aliepanda kisha mnyama akampotea hivyo akafanya tayammam. na akaanza kusali. Ikiwa atasikia sauti ya mnyama wake wakati ana sali basi tayammam yake itabatilika.

Ikiwa mtu anasafiri na wenzie juu ya mnyama na ikiwa kama atashuka mnyama wake wenzie hawatomsubiri, basi atafanya tayammum juu ya mnyama wake na kusali sala ya Imaa.

Ikiwa kuna hatari njiani au kutokana na baridi mtu akikoga atapata maradhi basi itajuzu kutayammam.

Wakati mtu anaposafiri inafaa abebe jiwe au jasi ambalo ataweza kulitumia kwa tayamaum kama huko njiani itakuwa vitu vyote vimerowa.

Ikiwa mtu anasali sala ya Idi na udhu wake ukatenguka, ikiwa akienda kutia udhu sala itampita au itakuwa shida kwenda sehemu ya kutilia udhu kutokana na msongamano wa watu uliopo, basi anaweza kufanya tayammam na kusali. Hii ni kauli ya Imaam Adham. Ama kauli ya maimamu wawili ni kwamba akatie udhu.

Katika kitabu kiitwacho **(Marakil falah)** maandishi ya pembeni ya Tahtawy yanasema (Maradhi ni udhuru unaomruhusu mtu

kutayammam. Ikiwa mtu ni mzima lakini akakhofia kwamba kama atatia udhu ataumwa basi huo si udhuru. Wale maulamaa waliokubalisha kwamba ikiwa mtu anaogopea akifunga ataumwa inajuzu kuacha na kulipa, basi pia wamejuzisha kutayammum kwa kuogopa kuumwa. Maradhi ni ya aina nne. Kudhurika kwa maji. Kudhurika kwa harakati ya aina yoyote. Hawezi kutumia maji mwenyewe. Hawezi kufanya tayammum. Kupata dhara kunaamuliwa na uzoefu wake yeye mwenyewe au kwa kuelezwa na daktari bingwa, muislam na muadilifu. Ikiwa hakupatikana muadilifu, basi yule ambae ufasik wake hauko dhahiri pia atafaa. Mtu ambae hawezi kutia udhu mwenyewe, ikiwa atapatikana mtu wa kumtia udhu basi atamtia na ikiwa atakosekana basi atafanya tayammam. Kufuatana na Imam Adham si lazima kuajiri mtu kwa jambo hili. Na ikiwa hawezi kufanya tayammum basi atakujalipa sala baadae. Mke na mume pamoja na kwamba hawana ulazima kusaidiana kwenye kutia udhu na kusali, mume anaweza kuomba msaada kutoka kwa mkewe. Ikiwa mtu hana uwezo wa kupata maji ya moto na akakhofia kuwa maji ya baridi yatamtia maradhi basi anaweza kutayammam. Ikiwa nusu au zaidi ya viungo vya udhu vina vidonda, basi atafanya tayammum. Ikiwa nusu ni vidonda atakosha, na sehemu za vidonda atapangusa. Ikiwa kupangusa pia kutaleta dhara atapangusa juu ya kitambaa na ikiwa pia italeta dhara basi asipanguse. Ikiwa sehemu zinazolazimu kukosha katika mikono na miguu zimekatika na uso pia una vidonda hatoweza kufanya tayammam hivyo atasali bila ya udhu na sala hatoirejea. Ikiwa uso ni mzima basi atakoshwa. Ikiwa hana mtu wa kumsaidia basi uso wake ataupangusa pahala penye dongo. Iwapo mtu hana mkono mmoja, au una vidonda au umekatika atatia udhu kwa mkono mmoja. Na iwapo mikono yake yote miwili iko hivyo atapangusa uso wake sehemu yenye dongo. Iwapo amefunga kidonda kwa kitambaa , bendeji, plasta, P. O. P., ubao, au amepaka krim kwa ajili ya tiba na haiwezi kuondoshwa na kwamba ngozi haiwezi kufikiwa basi atapangusa juu ya sehemu kubwa ya hicho kitu pamoja na ngozi iliyo pembeni mwake. Na kama inawezekana kuviondoa basi itabidi aviondoe ili akoshe ngozi. Vitu hivi havina ulazima kurejeshwa baada ya kutia udhu wala havina muda maalum unaoruhusika kuwepo kwake. Inaruhusika mguu mmoja ulio mzima kuukosha na mwengine wenye kitambaa ukapangusa. Ikiwa kitu kilichofungwa juu ya kidonda kitaanguka kabla ya kidonda kupoa, udhu hautoharibika. Pia udhu hautoharibika kama kitambaa (bandeji n. k. ) kitabadilishwa baada ya kwisha kupangusa juu yake. Ikiwa atakuwa amejipaka malham (cream) na kama itakuwa dhara kuyaondosha kwa ajili ya udhu basi atakosha

juu yake na isipowezekana kukosha juu yake basi atapangusa juu yake na iwapo kupangusa pia haiwezekani basi ataacha. (kwa vile madhehebu nyengine pia zinasema hivi, basi hapana uwezekano wa kufuata madhehebu mengine.) Haya malham ni kama kibanzi kilichofunika kufuatana na Ibn Abidin “rahmatullahi alaih” na hakifanani na jino lililozibwa au lililojazwa. Kwenye suala la jino ni tafauti kwenye madhehebu ya Shafii na Maliki hivyo uwezekano wa kufata upo. Mtu ambae atapoteza akili au kuzimia kwa sababu zisizo mikononi mwake, ikiwa atapitwa na vipindi sita vya sala basi hatolazimika kulipa sala hizo. Ikiwa mtu atashindwa kusali hata kwa kutumia njia ya im’aa (kuashiria), kwa wingi wowote sala hizo zitakavyokuwa, hatoziandika sala hizo katika wasia kuwa zilipwe ila atakapoweza yeye mwenyewe atazilipa.

Amesema Ibn Abidin “rahmatullahi alaih” ni makruh kwa mtu asie mgonjwa, kuoshwa au kupanguswa viungo vyake na mtu mwengine kwa ajili ya udhu. Inajuzu kuletewa maji au kumiminiwa maji na mtu mwengine wakati mwenyewe anajikosha. Ikiwa mgonjwa anachafua nguo zake na kitanda chake kila wakati au ikawa kuna uzito kuvibadilisha basi atasali hata kama ana najisi. Ikiwa ubao, bendeji au kitambaa kitaanguka baada ya kidonda kupoa basi udhu utakuwa umeharibika. Ikiwa kidonda kitapoa na ikawa bado kitambaa , bendeji, P. O. P., au ubao bado haujatolewa basi pia udhu utakuwa umebatilika ikiwa uwezo wa kutolewa bila ya dhara upo.

Allahu taala anawapa maradhi na machungu waja wake ili awasamehe madhambi yao au awaengezee neema zake huko akhera. Ibada zao zina kuwa na uzito na mashaka. Hivyo anawapa wepesi na mafanikio katika shughuli zao za kidunia na kuwaongezea riziki. Wakati wanaodharau ibada zao hawapi wepesi na baraka kama hizo. Watu kama hawa chumo lao linakuwa ni la kutumia ujanja, utapeli na ulaghai na wanaishi maisha ya anasa na fakhari ambayo hayachukui muda mrefu. Baada ya muda mfupi tu wanamalizikia gerezani au hospitali na kuishi maisha mabaya yenye idhlali. Bila ya shaka na adhabu zenye kuwasubiri akhera ni zenye kuumiza zaidi.

## ISTINJAA, ISTIBRAA NA ISTINQAA

Istinjaa ni kusafisha utupu baada ya kwenda haja. Istibraa ni kusubiri hali ya kuwa unatembeatembea au kufanya harakati nyengine ili kutoa nafasi kwa kibofu cha mkojo kutoa vitone vya mkojo vilivyobaki (kabla ya kutia udhu). **Istinqaa** ni kule kujitosheleza ndani ya moyo wako kuwa umesafika.

Kuna aina nne za istinjaa.

Iliyo fardhi. Ikiwa kuna najsi nzito juu ya nguo, kiwiliwili au pahala pa kusalia, iliyozidi dirham moja (gramu nne na sentigramu nane) basi ni fardhi kuiondoa najsi hiyo kwa maji.

Iliyo wajib. Ikiwa kutakuwa na najsi katika nguo au sehemu ya kusalia inayofikia uzito wa dirham moja basi ni wajibu koiondoa.

Na ikiwa ina uzito chini ya dirham moja basi ni sunna kuiondoa.

Mustahab. ni ile hali ya kuwa kuwa najsi chahe sana na ni mustahab kuiondoa. Mandub. ni ile hali ya kwamba mtu katokwa na upepo hali ya kuwa yuko majimaji katika sehemu zake za chini. Ni mandub kujikosha.

Na kama atakuwa ni mkavu basi kujikosha katika hali hii itakuwa ni bid'a.

Sunna za istinjaa: Baada ya kujisafisha kwa kujipangusa kwa kijiwe au kidunza cha dongo, hapo inakuwa ni sunna kujikosha kwa maji.

Ikiwa najsi haikuweza kuondolewa kwa kijiwe au kidunza cha dongo na iliyobakia ikazidi dirham moja na ikawa imetapakaa katika duburi yake basi itakuwa ni fardhi kukosha kwa maji. Baada ya kumaliza atajipangusa maji kwa kitambaa au kwa mkono. ikiwa hana kitambaa.

Jambo ambalo ni mustahab wakati wa kustanji ni kuweka idadi ya vijiwe katika witri (tatu, tano, saba).

[Kwa mtu ambae ana tatizo la kutokuweza kuzuia mkojo anatakiwa achukue kitambaa chenye ukubwa wa (12 x 12) cm, akikunje kwenye ncha moja na afunge kamba yenye urefu wa nusu mita. Kitambaa kitazungushwa kwenje ncha ya dhakari na kamba itafungwa kwenye ncha ya kitambaa. Ncha ya kamba iliyo upande wa kitambaa itazungushwa mara mbili na kukazwa. Ncha ya pili itazungushwa fundo na kufungwa kwa pini kwenye chupi. Wakati wa kuhitaji kujisaidia, pini itafunguliwa na fundo litaondoshwa. Hapo kamba ikivutwa basi kitambaa kitajiachia kwa wepesi. Baadhi ya wazee dhakari zao zinakuwa zimelegea sana kiasi ya kwamba haiwezekani kuzizungushia kitambaa. Basi katika hali hii watatafuta mfuko wa plastik na kuitia dhakari na hasua zao ndani ya mfuko na kuufunga. Mtu anayefuata madhehebu ya Hanafi ambae hawezi kuzuia mkojo na ambae hana udhuru, basi atanuia kufata madhehebu ya Malik wakati wa kuanza kutia udhu au kukoga kisha atasali. Katika kitabu cha **(Alfikh alal madhahibil arbai)** kilichoandikwa na mwanazuoni wa Egypt, profesa

wa Azhar Abdulrahman Jaziri “rahmatullahi alaih” (alikufa 1384 hijria) anasema (Kufuatana na kauli ya pili ya Maliki, iwapo mtu atakuwa mgonjwa au kutokana na uzee, akitokewa na sababu ya kutengua udhu, huhisabiwa kuwa na udhuru na udhu wake hautenguki. Wale wafuasi wa madhehebu ya shafii na Hanbali wanaweza kufuata kauli hii.) Iwapo mfuasi wa madhehebu ya Hanafi ataponyokwa na mkojo ndani ya sala, na ikawa hali hairuhusu basi atafuata kauli hii ya Malik. Atatia nia na ataendelea na sala yake hali ya kuwa ni mwenye udhuru.]

## NAMNA YA KUTEKELEZA SALA

Sala ina mambo manne. Fardhi, wajib, sunna, mustahabu. Kufuatana na madhehebu ya Hanafi kunyanyua mikono hadi usawa wa masikio ni sunna. Kuelekeza viganja upande wa kibla ni sunna. Wanaume. kufikisha kidole gumba kwenye ndewe ya sikio na wanawake kunyanyua hadi mabegani ni mustahabu.Kusema **(Allahu Akbar)** ni fardhi. Baada ya kuleta takbira kufunga mikono ni sunna. Kuweka mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto ni sunna. Mwanamme kufunga mikono chini ya kitovu na mwanamke juu ya kifua ni sunna. Ni mustahabu kwa mwanamme kukizungushia kiganja cha mkono wa kushoto, vidole vya kiganja cha mkono wa kulia.

Ni sunna kwa imam, maamuma na mtu mwenye kusali peke yake kuleta dua ya Subhaanaka. Ni sunna kwa imam au mwenye kusali peke yake kusoma Auduhu. Kusoma Bismillahi pia ni sunna. Kusoma Suratul fatiha ni wajib na kusoma aya tatu au aya moja yenye urefu wa aya tatu baada ya suratul fatiha ni wajib. Ni Fardhi kusoma aya moja ya Quran wakati umesimama katika sala za sunna na katika kila rakaa ya witri na wakati mtu anasali pekee katika rakaa mbili za sala ya fardhi.

Katika rukuu ni fardhi kupinda mgongo na ni wajib kubakia katika hali hiyo kwa kiasi cha kusema **(Subhanallah)** mara tatu. Kusema **(Subhanallahil adhim)** mara tatu ni sunna na kusema mara tano au saba ni mustahabu. Baada ya kusimama kutoka kwenye rukuu na katika kikao baina ya sijda mbili, kutulia kwa kiasi cha muda wa kuweza kusema **(Subhanallah)** mara moja ni fardhi kufuatana na kauli ya Imam Abu Yusuf. Na kwa kauli ya pande mbili ni wajib, lakini pia wapo waliosema ni sunna ila kauli iliyo sahihi zaidi ni hii ya wajib.

Katika sijda ni fardhi kugusisha kichwa chini (sakafuni) na ni wajib kubakia hivyo kwa kiasi ya muda wa kuweza kusema **(Subhanallah)** mara moja. Kusema **(Subhana rabiyal aala)** mara tatu ni sunna na kusema mara tano au saba ni mustahabu.

Anasema ibn Abidin “rahmatullahi alaih” wakati mtu anasujudu kwanza magoti yafike chini, kisha mikono, kisha pua na mwisho paji la uso. Vidole gumba vya mikono vitakuwa usawa wa masikio. Kwa madhehebu ya Shafii viganja vitakuwa usawa wa mabega. Ni fardhi kwa vidole vya miguu kugusa chini alau kimoja. Sehemu ya kusujudia inatakiwa iwe ngumu ili kichwa kisizame ndani yake. Busati, mkeka, mashuke ya ngano au mtama yaliyotandikwa chini yanaweza kusaidia. Meza, sofa au ndani ya gari vyote vinakubalika kuwa sawa na chini (sakafuni) Juu ya mnyama, au soji na vitu mfano wake vilivyotandikwa juu ya mnyama, havihisabiwi kuwa ni chini. Vitu vilivyofungwa pande mbili kama kwenye matawi ya mti na vikawa vinaninginia hewani kama pembea hivyo havihisabiwi kuwa ni chini (sakafu). Kusujudia kitu chenye kuteleza kama chembe za mchele, na ngano haitokuwa sahihi, ila kama vitakuwa ndani ya gunia basi itafaa. Ikiwa sehemu unayosujudia itakuwa juu zaidi ya usawa wa magoti kwa nusu ziraa, yaani vidole kumi na mbili (sentimita ishirini na tano) sala itasihi ila ni makruuh. Wakati wa kusujudu visugudi viwe mbali na mwili, sehemu ya kitovu iachane na mapaja na ncha za vidole vya miguu zielekee kibla. Ni sunna wakati wa kusujudu na wakati wa kurukuu kugusanisha visigino vya miguu.

Wakati mwanamke anaposali mikono yake atainyanyua mpaka kwenye mabega. Viganya vyake asivitoe nje ya mikono ya nguo yake Ataweka mikono juu ya kifua, kiganja cha kulia juu ya kiganya cha kushoto. Wakati wa kurukuu pia atapinda kwa wastani tu. Nyonga haitokuwa usawa mmoja na kichwa. Katika rukuu na sijda hatanui vidole vyake, anavibana. Viganja vyake vitakuwa juu ya magoti. Magoti ambayo ambayo atayapinda. Wakati wa sijda mikono yake ataigusisha chini karibu na tumbo lake. Tumbo lake litagusana na mapaja. Wakati wa atahiyyatu miguu yake ataivutia kulia na kukaa chini. Vidole vya mikono atavinyoosha kwenye magoti. Vidole vikamatane. Ni makruh kuswali jamaa wao wenyewe au katika jamaa ya wanaume. Kwao si fardhi kusali sala ya Ijumaa au sala ya Idi. Katika siku za Idi ya kuchinja wao wataleta **(Takbira)** kimya kimya baada ya sala ya fardhi. Si mustahab kuchelewesha sala ya asubuhi. Ndani ya sala hatosoma kwa sauti.) Imekamilika tarjuma ya Ibn Abidin. Anasema Hamawy “rahmatullahi alaih” katika sherhe ya **(Ashbaah)** wanawake kunyoa nywele, kukata au kuzitoa kwa dawa ni makruh tahrimy. (Inajuzu kuzifupisha nywele zao zisivuke masikio ila la muhimu wasifanane na wanaume) Ni karaha kwa mwanamke kusoma adhana na ikama. Asisafiri bila ya kuwa na mumewe au maharim wake. Kwenye hija

hafungui kichwa chake na hata kama atakuwa kwenye hedhi basi anaweza kufanya sai baina ya swafaa na marwa. Tawafu atafanya mbali na Kaaba. Hasomi hutba kwa sababu sauti yake ni sehemu ya utupu wake inayohitaji kuhifadhiwa. Atavaa mesti wakati wa hija. Mwanamke habebi jeneza, anaportadi hauliwi. Ushahidi wake katika kesi za hukmu ya kisasi au hadd haukubaliwi. Hakai itikaf msikitini. Inajuzu kupaka hina mikononi na miguuni ila kupaka rangi ya kucha haifai. Kwenye urithi , kwenye Ushahidi na katika kumpa matumizi jamaa alie fakiri yeye huwa nusu ya mwanamme. Mwanamke muhsina haitwi mahakamani bali hakim au wakili atamfuata nyumbani. Mwanamke kijana, hasalimiani wala kutoa pole kwa mwanamme asie maharim wake, hamtakii rehema anaekwenda chafya wala yeye akinenezwa hatojibu. Hawi pekee na mwanamme asie maharim yake katika chumba. Tarjama ya Hamawy imemalizika hapa.

Kukaa kikao cha kwanza ni wajib, kukaa kikao cha mwisho ni fardhi. Ni wajibu kusoma atahiyyatu katika kikao cha mwisho.

Katika sala za fardhi na za wajib, na sunna za kabla ya adhuhuri na Ijumaa na sunna za baada ya Ijumaa ni sunna kumswalia mtume "sallallahu alayhi wasallam" katika tashahud ya mwisho tu. Katika sala nyengine(mfano sunna za rakaa nne za adhuhuri na laasiri) ni sunna kumswalia mtume "sallallahu alayhi wasallam" katika tashahud ya mwanzo na ya mwisho. Kutoa salamu ni wajib na kugeuka ukaangalia mabega mawili wakati wa salamu ni sunna. Kuangalia kwa mazingatio ni mustahab.

Ili sala ikubaliwe kwa ukamilifu wake inategemea (kujiepusha na maasi) kufanya hushui na taqwa na kuacha mambo ya kipuuzi na kuacha uvivu na uzushi. Hushuu ni kuogopa shani yake Allah alie mtukufu na taqwa ni kuvihifadhi viungo vyake tisa na haramu na makruh, kuacha mambo ya kipuuzi, kuacha mazungumzo na shughuli ambazo hazina faida duniani wala akhera, kuacha uvivu wakati wa swala na kuacha shughuli zote unaposikia adhana na kukimbilia sala ya jamaa.

Ndani ya sala inalazimu kuyalinda mambo sita. Ikhlas, tafakkur, khofu, rajaa, ruuyati taqsir na mujahada.

Ikhlas ni kufanya ibada kwa ajili ya Allah pekee. Tafakkur ni kuzingatia yaliyo ndani ya sala. Khofu ni kuogopa shari yake Allah alie mtukufu. Rajaa ni kuwa na tamaa ya kupata rehema za Allah. Ruyati taksir ni kuyaona mapungufu yake.Mujahada ni mapambano dhidi ya nafsi na shetani.

Wakati adhana inaposomwa anatakiwa mtu ahisi kama ndio israfil amepuliza baragumu, anaposimama kutia udhu ahisi kama ndio amesimamishwa kutoka kaburini, anapokwenda msikitini ahisi kama anakwenda kwenye uwanja wa hukumu, wakati wa kupanga safu baada ya ikama ahisi kama ndiyo yuko kwenye safu za uwanja wa hukumu (kwenye uwanja wa hukumu watu watakuwa katika safu mia na ishirini. Safu themanini ni za umati wa mtume "sallallahu alayhi wasallam" wetu na safu arobaini ni za umati mwengine.) Wakati anamfuata imam na ikasomwa fatiha basi azingatie kama pepo iko kuliani kwake na moto uko kushotoni kwake, nyuma yake yuko Israil na mbele yake liko kaburi lake, upande wake wa pili iko nyumba ya Allah na chini ya miguu yake liko daraja la siraat. Afikirie kama atapata maswala mazito yatakayomshinda kujibu, afikirie kama ibada zake zitakuwa ni taji huko akhera, na kama zitakuwa rafiki safarini mwake na mwenza kaburini, au zitakuwa hazikutakabaliwa hivyo arembewe nazo kama nyambwe la tambara usoni mwake.

**Ewe dunia, huna shukurani kwa neema yoyote.**
**Kila lililo zuri huharibika kwa haraka ya pupa.**

## ADHANA YA MUHAMMAD

Maelezo yanayofuata yamefanyiwa tarjama kutoka **(Durrul mukhtar)** na sherehe yake **(Ibn Abidin)**:

Ikiwa muislam mwenye akili atayasoma maneno yaliyokwishatajwa katika vitabu vya fik-h kwa mtindo wake uliotajwa hiyo ndio adhana. Ni lazima kupanda juu ya mnara na kusomwa kwa kiarabu hali ya kuwa amesimama. Ikiwa itatarajumiwa kwa lugha nyengine basi haitoitwa adhana hata kama maana yake ni hiyo hiyo. Adhana hutumika kutambulisha kuingia wakati wa sala tano. Kwa wanaume kutoka nje ya msikiti sehemu iliyonyanyuka na kuisoma ni sunna iliyopewa nguvu. Kwa wanawake kusoma adhana na ikama ni makruh. Wao kuzisikilizisha sauti zao kwa wanaume ni haramu.

Muadhini anatakiwa apate pahala paliponyanyuka na asome adhana kwa sauti ya juu ili kuwasikilizisha majirani. Haijuzu kupaza sauti bila kiasi. Wakati wa kusoma akbar ima atasimama kwa sukun au ataunganisha na kuendelea kwa kutia fatha na hatotia dhama mwisho. Haijuzu kuongeza mada, irabu au herufi ili iwezeshe kusoma kwa kughani bali pia haijuzu kusikiliza adhana kama hiyo. Katika neno Salat na Falah atageuka kushoto na kulia. Miguu na kifua chake vitakua thabit kuelekea kibla. Kama itakuwa inasomwa juu ya mnara basi

muazini atasoma hali ya kuwa ameligeukia kuba la mnara. Mnara wa mwanzo ulijengwa na Hadhrat Muawiya. Katika msikiti wa mtume "sallallahu alayhi wasallam" kulikuwa na kitu kilichonyanyuka. Bilal alikuwa kipanda hapo na kuadhini. Mtume "sallallahu alayhi wasallam" sallallahu alayhi wasallama alimuamrisha kutia vidole vyake masikioni. Ikiwa atazungumza katikati yake basi ni wajibu kurejea adhana. Inajuzu adhana kusomwa kwa pamoja na zaidi ya mtu mmoja. Kusoma sehemu ya adhana na kuiacha sehemu haijuzu. Kusoma adhana hali ya kuwa umekaa ni makruh tahrimy. Ni sunna muadhini kuwa ni mtu salih, kujua sunna na wakati wa adhana, kuendelea kusoma kila siku na kusoma kwa kutafuta radhi za Allah bila kupokea. Kusoma kwa kupokea ujira pia inajuzu. Adhana ya mtoto ambae bado hajawa mpambanuzi haisihi kwa sababu sauti yake ni sawa na ndege au ala ya mziki. (kusoma adhana na ikama kwa vipaza sauti si sahihi. Mtu fasik kusoma adhana au kupaaza sauti baada ya imam haaminiki, hivyo ni makruh kusoma kwake. Ni wajib kwa muadhini kujua kuwa anaadhini wakati sahihi na kwa watu waliobaki ni wajib kujua kuwa wanasali katika wakati sahihi. Mtu atakaesali hali ya kuwa hana hakika ya wakati kuingia basi sala yake haitosihi hata kama itadhihirika kwamba alisali katika wakti sahihi. Kufuata kalenda zilizotayarishwa na makafiri na mafasik sio sahihi. Kalenda zinazotumika katika nchi zitambulikanazo kama Darul harb ni wajibu kumuuliza muislam mwema mwenye utaalamu juu ya usahihi wake.) Ikiwa mtu atakuwa anasikia adhana kutoka misikiti tafauti kwa wakati mmoja basi ataijibu ile iliyoanza mwanzo na ikiwa ni ya msikiti anaoswali jamaa kwa kawaida basi atatoka kwenda zake kuwahi jamaa. Anatakiwa aijibu adhana hata kama atakuwa anasoma Quran. Halazimiki kuijibu adhana kama atakuwa anasalia maiti, yuko chooni, anakula, yuko msikitini au wako kwenye darsa ya dini. Adhana isiyo ya kiarabu na ile inayosomwa kwa kughani sana haziendani na sunna. Atakaesikia adhana kama amekaa ni sunna kusimama na kama anatembea ni sunna kusita.Katika mlango wa viapo wakati ikielezwa nadhiri imeandikwa (Ni wajibu kwa serikali kujenga msikiti katika kila kitongoji, Na kama serikali haikujenga basi watu wenyewe wana wajibu wa kujijengea.)

Hivyo kama kila kitongoji kitajengwa msikiti basi kila mtu atasikia adhana kutoka katika msikiti wao na patakuwa hapana haja kwa muadhini kupaaza sauti sana au kutumia vipaza sauti. Vipaza sauti ni bid'a iliyosababishwa kuachwa kwa sunna za adhana. Ni dhambi kubwa kutumia bid'a hii wakati wa kusoma adhana na wakati wa kusali. Hii inasababisha kuharibika kwa ibada. Ndio maana idara ya mambo ya

dini na tunu za kiislam katika maamuzi yake nambari 737 ya tarehe 1/12/1954 kifungu cha 15 kinasema (Ni marufuku kuweka vipaza sauti katika mihrab. Ikiwa sauti ya imam haitasikilikana basi mmoja wa waadhini au mtu alie mbali zaidi apaaze sauti baada yake. Imeelezwa katika kitabu cha **(Alfikhi alal madhahibil arbai)** wakati ikielezewa sijda ya kisomo kwamba Quran na adhana inayosomwa kwenye vipaza sauti, redio na santuri kwamba hizo sio sauti halisi za wasomaji bali ni sauti zilizozalishwa kwa mawimbi ya usumaku na kielektronia. Pia imeelezwa kwa kirefu katika **(Saadati abadiyya)** wakati zikielezewa nyimbo na vyombo vya mziki. Adhana iliyoamrishwa katika uislam ni ya sauti ya muislam aliye salih na wala sio sauti ya bomba. Mmoja kati ya wanazuoni wa uhakika wa zama zetu hizi Hamdi Efendi wa Elmali "rahmatullahi alaih" anasema katika tafsir yake juzuu ya tatu ukurasa wa 2361 (Inafahamika kwamba amri ya kunyamaza na kusikiliza imehusishwa na kisomo (qiraat) Qiraa ni kitendo cha kukusudia, ambacho mtu mwenye akili na nutki, hutoa kinywani mwake na katika makhraj yake sauti zenye makusudi na mafahamu maalum. Hata kitendo cha Jibril basi sio qiraa bali ni kumsomesha mtume "sallallahu alayhi wasallam" ili afanye qiraa. Kitendo cha Allah ni tanzil na uumbaji wa qiraa. Kwa hivyo sauti zinazotokana na vitu visivyo na uhai haziitwi qiraa kama ambavyo haziitwi kiraa sauti zinazoakisi (zinazorudia) baada ya msemaji. Na kutokana na sababu hii ndio maulamaa wakaamua kwamba sauti inayoakisi baada ya msemaji (echo) sio kiraa na wala haihitaji kufanyiwa jambo lolote kwa mfano sijdatu tilawa. Kama ambavyo kutalii kitabu kimya kimya haiitwi qiraa basi ni hivyo hivyo kusikiliza sauti zinazoakisi (echo) kutoka kwenye vitu vinavyotoa sauti au ala za mziki haiitwi kusikiliza qiraa. Kwa hivyo msomaji anaposoma na ikawa sauti yake inaakisiwa na redio au kipaza sauti basi hicho kinakuwa sio kiraa wala amri ya kusikiliza na kunyamaza haihusu katika hali hii. Quran ambayo inalazima kunyamaza na kuisikiliza ni Quran inayosomwa na wala sio Quran inayorushwa kwenye vyombo vinavyoakisi sauti. Pamoja na kwamba kusikiliza kwake si wajib wala si mustahab lakini mtu asije akafikia maamuzi kwamba haifai kusikiliza au ni wajibu kuacha kusikiliza. Kwani kurusha Quran kwenye vyombo vya sauti na kusikiliza Quran hiyo ni mambo mawili tafauti. Ni wazi kwamba kuirusha Quran kwenye vifaa vya sauti (redio n. k.) au pamoja na ala haitofaa. Pamoja na kuwa kusoma Quran ni kujikurubisha kwa Allah, lakini kuisoma katika sehemu yenye kuiondoshea utukufu wake ni kosa. Lakini kama itasomwa ukasikia sio kosa, kutokusikiliza ndio litakuwa kosa. Mfano mtu akisoma Quran bafuni atapata dhambi ila kutokusikiliza si jambo la thawabu. Vile vile kuwa si wajibu kusikiliza

kuran kwa sauti iliyoakisiwa au kutolewa na vyombo, haizalishi wajibu wa kutokusikiliza. Kwa sababu pamoja na kwamba sio kiraa halisi, ni mfanano wa kiraa. Imetokana na maneno ya Allah. Hivyo pamoja na kuwa si wajibu wala si mustahabu kusikiliza, lakini inajuzu na ni bora kufanya hivyo tena haifai kabisa kutokuonesha heshima kwake. Vile vile ikiwa muislam ataiona karatasi ya Quran ipo katika sehemu isiyofaa basi asiiache tu lakini aichukue na kuiweka sehemu inayostahili kukaa.

Katika vitabu vingi vya fikhi mfano **(Kadihan)** vinasema (Kusoma adhana ni sunna. Ni miongoni mwa tunu na ishara ya Uislam. Iwapo itatokea katika kitongoji kuwa adhana haisomwi basi vyombo vya dola vitumike kuwalazimisha watu wa kitongoji hicho kusoma adhana. Muadhini anatakiwa azijue nyakati za sala na upande wa kibla. Kusoma adhana mpaka ukamaliza hali ya kuwa umeelekea kibla ni sunna. Adhana zimewekwa ili kutambulisha kuingia kwa wakati wa sala na wakati wa kufutari. Asiezijua nyakati hizi na mtu fasiki wakisoma adhana itakuwa ni sababu ya fitna. Mtoto asiefikia umri wa upamabanuzi, mlevi, mwendawazimu, mwenye janaba na mwanamke ni makruuh kwao kusoma adhana. Ikitokea basi muadhini atatakiwa aadhini tena. [Ni jambo la thawabu kusoma, kusomesha na kusikiliza maulidi. Lakini mwanamke kuwasikilizisha sauti yake wanaume wasio maharimu zake kwa kusoma maulidi, kuadhini, kuimba au kuzungumza kusiko na faida ni haram kwake na kwa wasikilizaji. Mwanamke anatakiwa asome kwa wanawake wenziwe tu na asiitoe sauti yake kwenye redio, vinasa sauti, televisheni n. k.] Ni makruuh kusoma adhana hali ya kuwa umekaa au bila ya kuwa na udhu au kuisoma hali ya kuwa uko juu ya mnyama mjini. Pamoja na haya hailazimiki kwa adhana hiyo kurejewa. Adhana husomwa juu ya mnara au nje ya msikiti, sio ndani ya msikiti. Kuyabadilisha maneno kwa kuyavuta ili upate kughani ni makruuh. Adhana isomwe kwa lugha ya kiarabu tu. Katika **(Hindiyya)** anasema kwamba (Muadhini kutoa sauti zaidi ya uwezo wake ni makruuh.) **(Ibn Abidin)** "rahmatullahi alaih" anasema (Ili adhana iweze kusikilikana mbali ni sunna kwa muadhini kuwa katika sehemu iliyonyanyuka. Inajuzu kwa muadhini zaidi ya mmoja kusoma adhana moja) Kufuatana na maneno haya ya wanazuoni inafahamika kwamba kuadhini, kukimu na kuswalisha kwa vipaza sauti ni bid'a. Kufanya bid'a ni dhambi kubwa. **(Mwenye kufanya bid'a ibada zake hazikubaliwi)**. Sauti inayotoka katika kipaza sauti pamoja na kuwa inafanana na sauti ya binaadamu lakini sio sauti ya binaadamu. Ni sauti iliyopatikana kwa mwenendo wa vifaa vya kisumaku (magnet). Si sauti

ya binaadamu aliyesimama sehemu iliyonyanyuka. Kuvipachika vipasa sauti juu ya mnara kuelekea kushoto, kulia na nyuma ni sababu ya kufanya muelekeo wa kutoka sauti usiwe kibla jambo ambalo pia ni dhambi. Hakuna haja ya kufikisha sauti mbali sana kwa kutumia sauti za kimetalika za vipaza sauti kwa sababu kila kitongoji ni wajibu kujenga msikiti. Kila msikiti utasoma adhana na kila nyumba itasikilikana. Pamoja na haya waadhini zaidi ya mmoja kusoma adhana moja pamoja inajuzu. Hii huitwa Adhani jawq. Sauti ya binaadamu yenye mvuto itasikilikana kutoka mbali na kuathiri moyo na roho, na kuengeza imani ya watu. (Adhana ya muadhini na kisomo cha imam kinatosha kwa kuwasikilizisha walio karibu na msikiti na wale walio msikitini. Hakuna haja kujilazimisha kutoa sauti kubwa kuwasikilizisha walio mbali. Hapa inadhihirisha kuwa hakuna uhitaji wa kutumia vipaza sauti). Kwa kumalizia, sauti zinazotoka katika bomba la kipaza sauti siyo adhana. **(Adhana ya Muhammad)** ni ile inayotoka katika kinywa cha muadhini. Mwanazuoni Abu Nuaym Isfahan katika kitabu chake **(Hilyatul awliyaa)** ameandika hadithi isemayo **(Sauti ya adhana inayotoka kwenye ala (kifaa) ni adhana ya shetani. Mwenye kusoma adhana hiyo ni muadhini wa shetani)**.

Katika hadithi sharifu tunasoma **(Kiyama kitakapokaribia, Quran itasomwa kutoka katika zumari)** na **(Itafika zama Quran itasomwa kutoka katika zumari. Hii haitosomwa kwa ajili ya kutaka radhi za Allah bali kwa kujifurahisha)** na **(Kuna watu wengi ambao wanalaaniwa na Quran wakati wanapoisoma)** na **(Itafikia wakati waadhini watakuwa ndio watu duni kabisa)** na **(Itafikia wakati Quran itasomwa kutoka katika zumari. Allah atawalaani watu hao).** Zumari maana yake ni ala yoyote. Kipaza sauti pia ni zumari. Inafaa waadhini waziogope hadithi hizi na kuacha kuadhini kwa vipaza sauti. Baadhi ya watu majahil wa dini wanasema kwamba vipaza sauti vina faida. kwa sauti kufika mbali. Mtume "sallallahu alayhi wasallam" anasema **(Fanyeni ibada zenu kwa namna mlivyoniona mimi na masahaba wangu tunafanya. Kufanya kinyume na nilivyofanya mimi ni bid'a. Watu wa bid'a kwa uhakika wataingia motoni. Hawa ibada zao hazitotakabaliwa)**. Kusema kuwa tunaengeza kitu chenye faida kwenye ibada sio jambo sahihi. Hayo ni maneno ya uongo ya maadui wa dini. Badiliko lolote kuwa lina faida au halina litajulikana na wanazuoni walio katika daraja ya **(Mujtahid)**. Mujtahid hawafanyi mabadiliko kwa nafsi zao. Wanaweza kufahamu ikiwa nyongeza au mabadiliko ni bid'a au sio bid'a. Kusoma adhana kwa ala imetajwa kuwa ni bid'a kwa kauli moja. Njia yenye kuwafikisha watu kwenye

radhi na mapenzi ya Allah ni moyo. Kimaumbile moyo ni kama kioo kilicho safi. Ibada zinazidisha usafi wa moyo na kuupiga msasa. Bid’a na dhambi nyengine zinautia moyo kiza. Inaufanya moyo usiweze kupokea nuru inayokuja kwa njia ya mapenzi. Watu wema huifahamu hali hii na huhuzunika. Hawataki kufanya maovu na hutaka kuongeza ibada. zaidi. Hutaka kuongeza zaidi kusali, mbali ya sala tano za fardhi za siku. Kufanya maasi kunaifanya nafsi ipate ladha na ivutiwe. Bid’a zote na dhambi zote zinaipa nguvu nafsi, ambayo ni adui wa Allah. Kusoma adhana kwa kipaza sauti ni mfano wa hilo. Anasema Rauf Ahmed ambae alikuwa ni khalifa wa Abdulla Dahlawy katika kitabu chake **(Durrul maarif)** kwenye utangulizi (Kusoma Quran karim au visomo vyengine kwa ala ni haramu) Kusoma adhana kwa kipaza sauti ni mfano wa hilo.

[Anasema Shafii katika **(Mukaddimatul hadhramiyya)** na **(Anwar)** (Kwa maamuma walio nje ya msikiti, ili waweze kumfata imam alie ndani ya msikiti kwa madhehebu ya shafii kuna sharti tatu: 1- Awe katika nafasi ambayo inamuwezesha kumuona imam. 2- Aweze kumsikia imam. 3- Masafa baina yao yasizidi ziraa 300 x 0,42 (mita 126).

Kumfata imam alie mbali ambae anaonekana kwenye televisheni haijuzu kwa madhehebu ya Hanafi na Shafii. Mambo ambayo hayakuwa ibada wakati wa Salafi salih kuyachanganya na ibada baada yake ni **(Bid’a)**. Adhana na sala kuichanganya na vipaza sauti, redio na televisheni ni bid’a itakayowapeleka motoni wenye kuifanya. Inafahamika hivyo kutoka katika Suratu nisaa aya ya 114. Sauti inayosikilikana kwenye vipaza sauti na redio sio adhana yenyewe ni mfanano wake tu. Kama ambavyo kilicho kwenye kioo au karatasi ni mfanano tu na wala sio mtu mwenyewe.]

**MAMBO YA WAYJIBU KATIKA SALA:** Kwa aliye nyuma ya imamu kutokusoma chochote zaidi ya “Subhanaka…….” (dua ya ufunguzi). Kwa imam au kwa anaesali pekee kusoma suratul fatiha mara moja katika rakaa mbili za sala ya fardhi na katika sala nyengine katika kila rakaa. Kusoma sura (dhammy) katika sala za fardhi za rakaa tatu na rakaa nne, ndani ya rakaa mbili za mwanzo na katika sala nyengine katika kila rakaa. Katika sala za fardhi za rakaa nne na rakaa tatu, kuisoma suratul Fatiha katika rakaa mbili za mwanzo. Kutoka fardh moja kwenda fardh nyengine. Kuisoma suratul fatiha kabla ya sura nyengine. Kukaa kikao cha tahiyatu ya mwanzo. Kufuatisha sijda moja baada ya nyengine. Kusoma tahiyatu katika kikao cha mwisho. Kumaliza sala kwa tamko la salamu. Kusoma kunuti katika sala ya witri. Kusoma takbira za ziada katika sala ya Idi. Kusoma kwa siri sehemu

zinazohitajika na kusoma dhahiri sehemu zinazohitajika. Kutulizana katika nguzo (tumaanina). Kuleta sijda ya kisomo anaposoma au kusikia kutoka kwa imam. Kuleta sijadatus sahwi. Kusimama moja kwa moja kutoka katika kikao cha tahiyyatu ya mwanzo bila kupinda. Kumfata imam katika kila hali. Ikiwa huna udhuru kufuatana na moja ya kauli, kusali sala za fardhi na jamaa. Kuleta takbira kuanzia baada ya sala ya asubuhi ya siku ya arafa hadi siku ya nne baada ya sala ya alasiri.

**SUNNA ZA SALA:** Kufuatana na madhehebu ya Hanafi sunna za sala ni:

Kunyanyua mikono katika takbira ya ufunguzi na katika takbira ya kunuti ya witri. Wanaume watanyanyua hadi kwenye ndewe za masikio na wanawake watanyanyua hadi usawa wa mabega. Kuelekeza kibla viganja katika takbira ya ufunguzi na takbira ya kunuti ya witri. Katika kisimamo kufunga kwa kuvibana vidole vya mkono wa kulia kwenye kiganja vya mkono wa kushoto. Kwa wanawake kuweka kiganja cha kulia juu ya kiganja cha kushoto. Kwa wanaume kuweka mikono chini ya kitovu na kwa wanawake kuweka mikono juu ya kifua. Kusoma dua ya ufunguzi katika rakaa ya mwanzo ya kila sala. Hii ni kwa imamu, maamuma au mwenye kusali peke yake. Kusoma audhu na bismillahi baada ya **(subhanaka)**. Vile vile kwa imam na kwa yule anaesali peke yake kusoma bismillahi mwanzo wa suratul fatiha. Kusema amin mwisho wa suratul fatiha baada ya kusema (**waladhaalyn)**. Hii ni kwa imam, maamuma na hata anaesali peke yake. Kuleta takbira wakati wa kwenda kwenye rukuu. Wakati wa rukuu kuweka viganja kwenye magoti na kuchanua vidole. Kusema (**subhanarabbiyal adhim)** mara tatu kwenye rukuu. Katika rukuu nyonga na kichwa kuwa katika usawa mmoja. Imam na anaeswali peke yake kusema **(samiallahu liman hamida)** wakati wa kutoka rukuu kuja kisimamo. Baada ya kusimama kusema **(Rabbana lakal hamdu)**. Kusema **(Allahu akbar)** wakati wa kwenda sijda kutoka kisimamo. Kusema **(Subhana rabbiyal aala)** mara tatu ndani ya sijda. Kusema **(Allahu akbar)** wakati wa kutoka kwenye sijda ya kwanza na wakati wa kwenda sijda ya pili. Kuvibana vidole vya mkono pamoja wakati wa sijda. Kwa wanaume katika sijda magoti watayaweka chini na mapaja yao hayatoshikana na tumbo lao wakati wanawake mapaja yao yatagusana na tumbo. Kusema **(Allahu akbar)** wakati wa kunyanyuka kutoka sijda ya pili. Wanaume kupinda mguu wa kulia na kuukalia mguu wa kushoto. Kumsalia mtume "sallallahu alayhi wasallam" kwenye kikao cha mwisho.Kugeuza kichwa kulia na kushoto wakati wa kutoa salamu. Katika tahiyatu kuweka mikono kwenye ncha za magoti

na kuviwachia vidole katika hali yake.Katika sijda kuelekeza kibla viganja na ncha za vidole Ukifika kwenye sijda kuweka viganja vya mikono usawa wa masikio. Kusujudu juu ya viungo saba.Katika sala za fardhi za rakaa nne kusoma fatiha tu katika rakaa mbili za mwisho. Kusoma adhana kufuatana na sunna ya mtume “sallallahu alayhi wasallam”. Kwa wanaume kusoma ikama katika sala ya jamaa au ya pekee.

**MAMBO MUSTAHAB YA SALA:** Mambo yaliyo mustahabu kwa madhehebu ya Hanafi:

Wakati muadhini anaposema **(hayya-ala-salah)** maamuna kusimama mara moja. Kwa wanaume kugusa ndewe za masikio kwa dole la gumba la mkono wakati wa takbira ya ufunguzi na kunut ya witri. Kukamata kiganya wakati wa kufunga mikono. Kutizama sehemu ya kusujudia wakati wa kisimamo. Katika rukuu na sijda kuleta tasbihi mara tano au saba. Katika rukuu macho kutizama miguuni. Kuambatanisha miguu pamoja katika rukuu. Wakati ukirudi kwenye kisimamo kuipambanua tena miguu. Kufikisha pua kabla paji la uso katika sijda.Katika sijda, macho kutizama pembe mbili za pua. Wakati wa kutoa salamu kuangalia bega. Kwa yule aliye kushoto ya imam kuwanuia imam, maamuma na malaika wenye kuhifadhi matendo wakati wa salam. Kwa aliye kuliani kwa imam kuwanuia malaika wenye kuhifadhi matendo na maamuma wakati wa salam. kiwa hakuna mtu kushotoni kwake na kuliani kwake basi atawanuia malaika. Kuacha kwenda myayo na kukohowa. Wakati wa kukaa tahiyyatu atizame juu ya mapaja. Baada ya sala, imam ageuke uso uwaangalie maamuma.

**ADABU ZA SALA:**

1. Kwa mtu aliesali pekee au pamoja na jamaa kusema **(Allahumma anta salaam waminka salaam tabaarakta yaa dhaljalali wal ikram)**. Kisha kusema mara tatu **(Astaghfirullahal adhimaladhy laailaha illa huwal hayyul kayyum wa atubu ilayhi)** Hii inaitwa dua ya **(Istighfari)**. Inajuzu kusoma bila ya udhu.

2. Baada ya hapo kusoma **(Ayatul kursy).**

3. Kusema **(Subhanallah)** mara thelathini na tatu.

4. Kusema **(Alhamdulillah)** mara thalathini na tatu.

5. Kusema (**Allahu akbar)** mara thalathini na tatu.

6. kusema mara moja **(Lailaaha illallahu wahdahu la sharikalah lahul mulku walahul hamdu yuhyi wayumitu wahuwa ala kulli shay’in qadir.)**

7. Kunyoosha mikono mbele na kuvielekeza viganya mbinguni, ndio kibla cha dua, kuomba dua kwa mazingatio.

8. Ikiwa anasali na jamaa asubiri dua.

9. Kusema **(Amin)** mwisho wa dua.

10. Kupangusa uso baada ya dua.

11. Baada ya hapo kusoma **(Ikhlas)** kumi na moja kwa kuanza na bismillahi kwa kila moja yao. Hii imeandikwa katika **(Barika)**, juzuu ya kwanza ukurasa wa mwisho. Kisha atasoma (**Kul audhu**) mara moja moja, kisha atasoma **(astaghfirullah)** mara sitini na saba ili kukamilisha sabini na tasema **(Subnallahi wabihamdih subhanallahil adhim)** mara kumi. Kisha asome aya ya **(Subhana rabbika)**. Haya yameandikwa katika kitabu kiitwacho **(Maraakil falah)**. Katika hadithi sharif inasema **(Kila dua inayosomwa baada ya sala tano za fardhi hukubaliwa)**. Dua inatakiwa iombwe na moyo ulio wazi na iwe kimya kimya. Ni makruh kuomba dua baada ya sala tu au nyakati fulani tu au kuomba kwa maneno uliyoyahifadhi na ukawa unayakariri tu kama mashairi. Baada ya dua ni sunna kupangusa mikono usoni. Mtume "sallallahu alayhi wasallam" alikuwa akiomba dua wakati wa kutufu, baada ya chakula na wakati wa kulala. Katika dua hizi alikuwa hanyanyui mikono wala hapangusi uso. Dua na dhikri nyengine yoyote ni bora kama inafanywa kimya kimya. Inapendeza kuomba dua na kuleta dhikri hali ya kuwa una udhu. Mfumo wanaoufanya watu wa tarika wa kugeukageuka na kucheza, kupiga makofi, kutumia ala za mziki kama dufu, firimbi na gitaa katika dhikri ni haram. Hapa inafahamika kwamba ni bora kwa imam na maamuma kuleta dua pamoja kimya kimya. Pia inajuzu kuleta dua kila mmoja kwa wakati wake au kunyanyuka na kuondoka bila kuleta dua. Katika fatwa ya **(Hindiya)** anasema. (Ni makruh kwa imam kukaa baada ya sala ambayo ina sunna ya baadia. Anatakiwa asogee kushoto, kulia au nyuma na asali sala ya baadia mara moja. Katika sala ambazo hazina sunna ya baadia ni makruh, tena ni bid'a kwa imam kubaki ameelekea kibla. Anaweza akawaelekea maamuma, akaelekea kushoto au kulia bali pia anaweza kunyanyuka na kwenda zake.)

**DUA BAADA YA SALA:** Alhamdulillahi rabbil alamin. Asssalatu wassalamu ala rasulina Muhammad wa alihi wa sahbihi ajmain. Ya Rabbi, tutakabalie sala yetu. Tujaalie mwisho mwema. Turuzuku neno la shahada wakati wa pumzi zetu za mwisho. Waghufirie na uwasamehe maiti wetu. Allahummaghfir warham wa anta khayrurahimin. Tawaffani musliman walhikny bi swalihin. Allahummaghfirly wa li-walidayya wa li-lustadhya wa li-lmuuminina

wal muuminati yawma yakumul hisabi. Ewe mola nihifadhi na shari za shetani, adui na nafsi yenye kuamrisha maovu. Tujaalie mema nyumbani mwetu na uturuzuku rizki yenye kheri na ya halali. Wape salama na mema waislam na uwape maovu maadui wa waislam. Wape msaada wako wale waislam wenye kupigana jihadi na makafiri. Allahumma innaka afuwwun tuhibbul afwa faafuanny. Ya Rabbi! Wape shifaa wagonjwa wetu na uwaondoshee matatizo yao wale walio na matataizo. Allahumma inni as-aluka sihhat wal-afiyata wal-amanata wahusnalhulk waridhaa bilqadar bi-rahmatika ya arhama rahimin. Baba na mama yangu, watoto na jamaa zangu , rafiki na ndugu zangu katika dini wote uwape maisha marefu na maadili mema, akili iliyo sawa na siha na afya, uwajaalie na uongofu na kutenda yaliyo sawa. Amin, Walhamdulillahi rabbil alamin. Allhumma swalli alaa…, Allahumma barik alaaaa…, Allahumma rabbana atina… Walhamdu lillahi Rabbil alamin. Astaghfirullah, astaghfirullah, astaghfirullaha, astaghfirullah-al-adhim al-karim al-ladhi la ilaha illa huw-al-hayyal-qayyum wa atubu ilayhi.

**MAMBO YALIYO KARAHA KWENYE SALA:**

1- Kugeuza shingo na kuangalia kushoto au kulia.

2- Kuchezea kitu kilicho juu yake.

3- Kuipangusa kwa mikono sehemu ya kusujudia bila ya sababu maalum.

4- Kwa wanaume, kuweka mikono kifuani wakati wa kisimamo. au kuweka usawa wa kifua wakati wa sijda.

5- Kudatisha vidole.

6- Kukaa hali ya miguu kupita baina yake bila ya udhuru.

7- Kunyanyua mguu wakati wa sijda.

8- Kusali hali ya kuwa umevaa nguo ambazo huwezi kuzivaa mbele ya mkubwa wako.

9- Kusali hali ya kutizama uso wa mtu mwengine.

10- Kusali nyuma ya moto.

11- Kuwa na mchoro au picha mwilini au kwenye nguo ya kusalia.

12- Kwenda myayo bila sababu.

13- Kusali na viganja vimo ndani ya mikono ya shati.

14- Kukaa hali ya kuwa miundi imenyooka kama mbwa.

15- kufumba macho.

16- Katika sala ya jamaa kusali safu ya nyuma hali ya kuwa nafasi ipo katika safu ya mbele. Ikiwa ubavuni kwake kutakuwa na mtu basi

ni makruh tanzih na kama atakuwa peke yake basi ni makruh tahrim na hivyo atakuwa ameacha wajib. Sala hiyo atalazimika kuirejea.

17- Kusali hali ya kuelekea kaburi bila ya kuwa na kizuizi baina yake na kaburi.

18- Kusali ukaelekeza mkono kusikokuwa upande wa kibla.

19- Kusali hali ya kuilekea najsi.

20- Mwanamke na mwanamme kusimama ubavu kwa ubavu hali ya kuwa wanasali sala tafauti.

21- Kusali hali ya kuwa unahitaji kwenda kujisaidia.

22- Kutanguliza mikono wakati wa kwenda sijda bila ya udhuru.

23- Ndani ya nguzo moja kujikuna sehemu mara mbili. (Ikiwa atanyanyua mkono na kujikuna mara tatu basi sala yake itabatilika)

24- Kufika kwenye rukuu kabla imam.

25- Kunyanyuka kutoka kwenye rukuu kabla ya imam.

26- Kufika kwenye sijda kabla ya imam.

27- Kunyanyuka kutoka kwenye sijda kabla ya imam.

28- Kunyanyuka ukawa umekamatia kitu bila ya udhuru.

29-Wakati wa kunyanyuka kutoka kwenye sijda kunyanyua magoti kabla mikono.

30- Kupangusa vumbi lililo usoni na machoni.

31- Kuacha kusoma sura inayofuata sura uliyoisoma katika rakaa iliyopita.

32- Kusoma sura moja ndani ya rakaa ya kwanza naya pili au kuisoma sura mara mbili ndani ya rakaa moja.

33- Kusoma sura iliyo kabla ya sura uliyosoma katika rakaa iliyopita.

34- Kusoma aya tatu zaidi kupita kisomo cha rakaa iliyopita.

35- Kutegemea kitu wakati wa kuinama au kunyanyuka hali ya kuwa huna udhuru.

36- Kupunga nzi.

37- Kusali mabega, mikono au miguu ikawa wazi.

38- Kutokuwa na stara wakati unasali nje.

39- Kusali sehemu wanayopita watu.

40- Kufanya tasbihi kwa vidole wakati wa rukuu na sijda.

41- Imam kuwa ndani ya mihrab kiasi ya kwamba kama litashushwa bazia basi yeye yote atabaki ndani.

42- Imam kuwa sehemu ya juu au chini ya maamuma wake kwa dhiraa moja (takriban nusu mita) na akawa yuko pekee katika usawa huo.

43- Imam kusimama sehemu nyengine isiyokuwa mihrab.

44- Kusema amin kwa sauti wakati wa sala.

45- Kukamilisha kisomo cha kwenye kisimamo ndani ya rukuu.

46- Kukamilisha kisomo cha ndani ya rukuu kwenye kisimamo.

47- Kusimama kwa mguu mmoja bila ya udhuru.

48- Kutikisika kushoto na kulia.

49- Kuviuwa vidudu visivyongata kama chawa.

50- Kunusa kitu ndani ya sala.

51- Kusali kichwa wazi. Mahujaji watasali kichwa wazi baada ya kuhirimia.

52- Kusali hali ya kuwa mikono iko wazi.

53- Kusali na miguu iko wazi (Wanawake kusali miguu iko wazi kwa kauli moja ni kiraha na kwa kauli nyengine ni kwamba sala haisihi.) Imesemwa katika Ibn Abidin ukarasa wa 439 kwamba ni makruh kuviacha viatu na vitu vyengine nyuma ya msikiti. Ni sunna kuviweka upande wa kushoto **(Barika)**.

Ni makruh kuleta uradi na dua baina ya sala ya fardhi na sunna ya baadia. Haya yameandikwa katika **(Targhibu salaat)**.

**MAMBO YENYE KUHARIBU SALA:** Mambo ambayo huharibu sala yakifanywa kwa makusudi au kwa kusahau katika madhehebu ya Hanafi yatatajwa hapa hamsini na tano.

1- Kuzungumza mambo ya kidunia.

2- Kucheka mpaka ukajisikia mwenyewe.

3- Kufanya matendo yajulikanayo kuwa ni mengi.

4- Kuliwacha jambo la fardhi bila udhuru.

5- Kuacha fardhi bila ya hiyari.

6- Kulia kwa sauti kwa jambo la kidunia.

7- Kukohoa au kukwaruza koo bila ya udhuru.

8- Kutafuna ubani.

9- Ndani ya nguzo moja kujikuna sehemu moja mara tatu au kunyanyua mikono ukapiga makofi.

10- Kupeana mkono na mtu.

11- Kutokuisoma takbira ya ufunguzi kwa sauti alau ya kujisikia wewe mwenyewe.

12- Kutokusoma kwa sauti alau ya kujisikia wewe mwenyewe.

13- Wakati mtu akikwita ukasema **(la haula wala kuwwata illa billahil-ali-yil adhim) au (subhanallah)** au **(La ilaha illallah).** Kama atasema kwa lengo la kutambulisha kuwa yumo ndani ya sala basi sala

yake haibatiliki. Lakini kama atakusudia kumuitikia aliemwita basi sala yake itabatilika.

14- Kuitikia salam kwa makusudi.

15- Kupata ladha ya kitu kilicho mdomoni kama sukari, kisha ukameza maji yake.

16- Wakati anasali sehemu ya wazi, akafungua mdomo na akadondokewa na maji, theluji au mfano wa hivyo na kisha akameza.

17- Kuvuta hatamu ya mnyama mara tatu(wakati uko juu ya mnyama)

18- Kunyanyua mkono mara tatu au kuua mdudu kama chawa kwa kumfikicha.

19- Kuvuta nywele tatu ndani ya nguzo moja.

20- Kutamka neno lenye sauti tatu.

21- Wakati uko juu ya farasi unasali kufuatana na maelekezo ya kiislam, mguu wako ukamchochea mara tatu.

22- Kumchochea mara moja kwa miguu yote miwili.

23- Kunyanyuka kabla imam.

24- Kutembea urefu wa safu moja bila udhuru.

25- Kuchana ndevu au nywele.

26- Mwanamke na mwanamme kusimama ubavu kwa ubavu ndani ya safu wakawa wanamfata imam wakiwa hawako ubavu kwa ubavu au kuna pazia baina yao basi sala haitobatilika. Ni haram kwa wanawake kutoka kwenda msikitini au majiani bila ya stara ya kisheria. Hivyo ibada wanayoifanya haiwi ni thawabu bali ni dhambi.

27- Kumkosoa au kumsaidia kisomo imam anaeswalisha wengie (asie imam wako.)

28- Ikiwa mwanamke alifika na sehemu ikawa iko wazi akasimama na kufuata jamaa baadae wakaja wanaume wakaanzisha safu kiasi ya kwamba wakajaza na kumfikia huyu mwananmke. Basi wale wanaume waliosimama ubavuni kwake kuliani na kushotoni na yule alie nyuma yake sala zao zitabatilika.

29- Kumkumbatia mtoto.

30- Kula au kunywa.

31- Kumeza kitu chenye ukubwa wa mbaazi ambacho kilibakia menoni.

32- Kuzileta ncha mbili za ukosi pamoja kwa mikono miwili au au kuivua kofia kwa mkono mmoja au kuivua na kuivaa tena.

33- Kusema **(Innaa lilahi wa innaa ilayhi rajiun)** baada ya kusikia habari mbaya.

34- Kusema **(Alhamdulillah)** baada ya kusikia habari nzuri.

35- Kufuatana na moja ya kauli, kusema (**Alhamdulillah)** baada ya kwenda chafya.

36- Kusema **(Yarhamukallah)** baada ya kumsikia mwenda chafya alie karibu na wewe.

37- Kusema **(Yahdikumullah)** baada ya kumsikia mwenda chafya.

38- Mwanamme kuja na akambusu mwanamke mwenye kusali.

39- Kuomba mambo ya kidunia kama dhahabu na fedha, kwenye dua iliyo ndani ya sala.

40- Kifua chako kugeuka kikaacha usawa wa kibla. Kuna njia mbili za kujua usawa wa kibla. 1. Njia ya pembe (angle) ya kibla. 2. Njia ya saa ya kibla. 1. Ikiwa utachorwa mstari katika ramani baina ya mji husika na Makka, mstari huo ni mstari wa kibla. Tafauti yake na upande wa kusini ndio huwa pembe (angle) ya kibla. 2. Mtu yeyote atakaelielekea jua katika wakati ulioandikwa saa ya kibla katika kalenda basi atakua ameelekea kibla. Kadusi anaelezea juu ya Rub I daira (Wakati mshale wa Rub i daira ukipelekwa muelekeo wa arc ya kibla, pembe inayooneshwa na Kamba katika arc ya urefu, hio ndio Fadhli dair (H) ya wakati wa kibla wa Istanbul. Wakati saa ikielekezwa juu na mshale wake ukaelekea upande wa jua, ukichorwa mstari kwenye pembe inayofanyika baina ya mshale unaoonesha saa na namba kumi na mbili, mstari huo huonesha upande wa kusini.)

41- Miguu yote miwili kutokugusa chini wakati wa sijda.

42- Kuisoma Quran kwa makosa ambayo yataharibu maana yake.

43- Mwanamke kumnyonyesha mtoto.

44- Kubadilisha sehemu baada ya kuambiwa na mtu.

45- Kumpiga mnyama uliepanda mara tatu.

46- Kufungua mlango.

47- Kuandika kwa uchache herufi tatu.

48- Kuvaa kaftan.

49- Kukumbuka sala zako za kadha ikiwa ni chache kuliko sita.

50- Ikiwa unasali ndani ya chombo au juu ya mnyama ukageuzwa upande usio wa Kaaba.

51- Kumpakia mnyama wakati uko mgongoni kwake.

52- Kurtadi kwa moyo wako.

53- Kupata janaba au hedhi.

54- Kwa imam kumsogeza mtu mwengine pahala pake baada ya kudhania udhu wake umetenguka.

55- Kusoma Quran katika kubadilisha herufi zake hadi maana yake ikabadilika. Amesema Ibn abidin wakati akielezea sunna za sala (Kumfuata aliye nje ya sala kunaifanya sala isiwe sahihi. Imam na muadhini kutoa sauti kubwa kuliko inavyohitajika ni makruh. Wakati imam na muadhini wanapoleta takbira kwa kuanza sala basi na nia yao pia iwe ni ya kuanzia sala na wala wasilete takbira kwa nia ya kuwasikilizisha maamuma tu. Sala yao haitokuwa sahihi na wale waliomfuta pia sala yao haitokuwa sahihi. Iwapo sauti ya imam inatosha basi ni makruh kwa muadhini kupaaza sauti baada yake na ni bid'a iliyo mbaya. Inapendeza kupaaza sauti pale inapohitajika ila, kama atafanya hivyo kwa nia ya kughani basi sala yake huyo muadhini itakuwa batil.) Hivyo kwa imam na muadhini kutumia vipaza sauti kunaifanya sala ya wanaowafuata na sala zao wenyewe kuwa batil. Hii ni bid'a mbaya na ni dhambi kuifanya. Kumfuata Imam anaesali sehemu nyengine ukawa unamuona ndani ya televisheni sio sahihi. Haya yameandikwa na wanazuoni wa India huko Mlappuran katika jarida la **(Almuallim)** la mwezi wa Rabiul awal mwaka 1406 sawa na Disemba 1985 toleo namba 12.

**Yasiyoharibu sala:** Kujaza safu ya mbele kwa kutembea hatua moja au mbili, kusema Amin lakini sio kwa kumjibu mtu, kumuitika mtu salamu kwa ishara ya macho, iwapo mtu akakuuliza rakaa ya ngapi ukamuonesha kwa vidole, haya yote hayabatilishi sala.

Maana ya kilugha sala ni: Kwa allah maana yake ni kurehemu, kwa malaika maana yake ni kutakia maghfira na kwa binaadamu maana yake ni kuomba dua. Maana ya sala kwa istilaha ni kufanya vitendo maalum vyenye nguzo maalum. Vitendo maalum ni vile vinavyofanyika kabla ya kuingia ndani ya sala na nguzo maalum ndio hizo tunazozifanya ndani ya sala na hivi kwa pamoja ndio vinafanya hio sala yenyewe.

Siku moja mtume "sallallahu alayhi wasallam" alimwambia Sayyidna Ali "karramallahu wajhahu" **(Ewe ali, tekeleza fardhi, wajib, sunna na mustahab za sala).** Mmoja wa Mashaba katika Ansar akasema Ewe mtume "sallallahu alayhi wasallam" wa Allah, Hadhrat Ali tayari anayajua yote haya. Tueleze faida za fardhi, wajib, sunna na mustahab za sala ili tuzitekeleze vyema. Bwana mtume "sallallahu alayhi wasallam" akasema **(Enyi umati wangu na masahaba wangu! Sala ni yale mambo ambayo Allah anaridhika nayo. Ni yale mambo ambayo malaika wanayapenda. Ni mwenendo wa mitume "sallallahu alayhi wasallam". Ni nuru ya maarifa. Ndiyo amali njema kuliko zote. Ni nguvu ya kiwiliwili. Ni baraka ya riziki. Ni nuru ya roho.**

**Ni sababu ya kukubaliwa dua. Ndio inayompoza malaika wa mauti. Ni taa ya kaburini. Ni jawabu kwa Munkar na Nakir (malaika wenye kusaili watu). Ndio dari itakayofunika juu yako siku ya kufufufliwa. Ndio pazia baina yako na Jahannam. Itakupitisha kama umesa kwenye daraja la siraat. Ni taji kichwani kwako huko pepeoni. Ndio ufunguo wa pepo).**

## FADHILA ZA SALA YA JAMAA

Mtu amabae atasali rakaa mbili za jamaa atapata fadhila zaidi kuliko mwenye kusali rakaa ishirini na saba akiwa pekee.

Kufuatana na mapokeo mengine rakaa moja ya sala ya jamaa ni bora kuliko rakaa elfu za sala ya pekee. Thawabu za kusali sala ya jamaa ni nyingi. Wacha tutaje baadhi yake:

1- Waumini wanapokusanyika pamoja , mapenzi baina yao huongezeka.

2- Wale wasiojua hupata fursa ya kujifunza kutoka kwa wanaojua.

3- Kwa kawaida baadhi ya watu sala zao hutakabaliwa na wengine hazitakabaliwi. Katika sala ya jamaa wale ambao hawakutakabaliwa pia hutakabaliwa kupitia za wale waliotakabaliwa.

Katika hadithi sharif tunasoma **(Enyi umati wangu, mimi nimekuekeeni njia mbili. Quran na sunna. Mwenye kufuata zisizokua njia mbili hizi basi si katika umma wangu.)** Anasema Abdulghani Nablusi katika kitabu kiitwacho **(Hadika)** ukarasa wa 99 (Allahu taala ametambulisha sehemu ya Uislam kupitia Quran na sehemu kupitia sunna za bwana mtume “sallallahu alayhi wasallam”). Sunna za mtume “sallallahu alayhi wasallam” ni yale aliyoyaamini, aliyoyasema, aliyoyafanya, tabia zake na yale mambo yaliyofanywa au kusemwa mbele yake akayanyamazia (kuonesha ameyakubali) Hadithi sharifu hii inaonesha dalili ya pili miongoni mwa dalili za sharia.

## UIMAM NDANI YA SALA

Wenye kumfata imamu wanagawika mafungu manne, Mudrik, Muktadi, Masbuk na Lahik.

1- Mudrik ni yule mwenye kuleta takbira ya ufunguzi pamoja na imam.

2- Muktadi ni yule ambaye hakuiwahi takbira ya ufunguzi ya imam.

3- Masbuk ni yule aliyejiunga wakati imam ameshasalisha rakaa moja au mbili.

4- Lahik nu yule ambae ameleta takbira ya ufunguzi pamoja na imam lakini akapata dharura ya kutengukiwa na udhu, akaenda akatia udhu na kuja kuwahi tena jamaa. Huyu kama ilivyokuwa awali atasali bila kiraa na ataleta tasbih katika rukuu na sujudu. Ikiwa hatoleta mazungumzo ya kidunia wakati anakwenda kutia udhu tena, huwa kama yuko pamoja na imam. Ila inabidi sehemu anayokwenda kutia udhu iwe karibu. Ikiwa itakuwa sehemu ya mbali basi wako walosema kuwa sala yake itafisidika.

Ikiwa mtu atakuja na akamkuta imam yuko kwenye rukuu, hivyo akafanya haraka ili amuwahi imam, na katika haraka zake akaleta takbira ya ufunguzi wakati anaelekea kwenye rukuu, basi huyo hakumfuata imam. Ikiwa imam yuko kwenye rukuu. maamuma anatakiwa atie nia na kuleta takbira ya ufunguzi akiwa amesimama. Kisha aende rukuu na kuleta tasbihi zake hali ya kuwa imam bado yuko rukuu, hapo ndipo atakuwa ameipata hiyo rakaa. Amma ikiwa wakati yeye anakwenda rukuu imam ananyanyua mgongo kusimama, basi huyo atakuwa hakuiwahi rakaa.

## KUTULIA KATIKA NGUZO

Katika sehemu tano ndani ya sala ikiwa mtu ataacha taadil arkan (kutulia katika nguzo) kwa makusudi bila ya kusahau basi kufuatana na Imam Abu Yusuf “rahmatullahi alaih” sala yake itabatilika. Kufuatana na mashekhe wengine wawili haitobatilika. Ila kwa vile ameacha wajibu kwa makusudi, kutokana na nuksan jabry inabidi aisali tena sala yake.

**Kuacha taadilul arkan kuna madhara ishirini na sita.**

1- Kunasababisha ufakiri.

2- Anachukiwa na ulamaa wa akhera.

3- Anapoteza sifa ya uadilifu hivyo ushahidi wake haukubaliki.

4- Sehemu aliyosali itatoa ushahidi dhidi yake siku ya kiama .

5- Ikiwa mtu atamuona mtu anasali bila ya kutunza utulivu nae asimwambie basi nae hupata dhambi.

6- Anawajibika kuisali tena sala hiyo.

7- Anakuwa ni mwizi wa sala.

8- Inasababisha kufa bila imani.

9- Sala aliyoisali inakuwa kama nyambwe bovu ambalo atarembelewa usoni siku ya kiama.

10- Anakosa rehema za Allah.

11- Anakuwa amemtovukia adabu Allah wakati yuko mbele yake.

12- Atakosa thawabu nyingi zinazopatikana ndani ya sala.

13- Inapelekea kukosa thawabu za ibada nyengine.

14- Inapelekea kustahiki moto wa Jahannam.

15- Wasiojua wakimuona nao watamfuata anavyofanya. Ndio maana alim wa dini anapofanya makosa hustahiki adhabu zaidi.

16- Huwa amemkhalifu imam.

17- Sunna zilizopo katika kuondoka sehemu moja kwenda nyengine ndani ya sala itakuwa kaziacha.

18- Anapata ghadhabu za Allahu adhimu shaan.

19- Anakuwa amemfurahisha shetani.

20- Anakuwa mbali na pepo.

21- Anakuwa karibu na moto.

22- Anakuwa ni katili wa nafsi yake.

23- Anaichafua nafsi yake.

24- Anawaumiza malaika walio kuliani na kushotoni kwake.

25- Anamghadhibisha mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allah sallallahu alayhi wasallam.

26- Analeta dhara kwa viumbe wote. Kutokana na dhambi zake mvua na mazao yanaweza yakakosekana au mvua kubwa zikanyesha na kusababisha gharika.

## SALA YA SAFARINI

Imeelezwa katika **(Nimeti islam)** kwamba inajuzu wakati wowote na pahala popote kusali kitako katika sala za sunna hata kama uwezo wa kusimama unao. Wakati wa kurukuu atapinda mwili wake na wakati wa kusujudu uso wake ataugusisha chini. Ikiwa hana udhuru maalum basi thawabu za sala inyosaliwa kitako ni nusu ya thawabu za sala inayosaliwa wima. Sunna za sala tano na sala ya tarawehe ni miongoni mwa sala za nafila. Wakati mtu yuko njiani, yaani nje ya mji au kijiji inajuzu kwa madhehebu ya Hanafi kusali sala za nafila juu ya mnyama. Hailazimu kuelekea kibla au kurukuu na kusujudu. Atasali kwa ishara (imaa). Hii ina maana kwamba atapinda kidogo kwa ajili ya rukuu na atapinda zaidi wakati wa sujudu. Kuwepo kwa najsi nyingi juu ya mnyama hakuzuii sala. Kwa mtu aliyechoka inafaa kusali hali ya kuwa anamuegemea mtu mwengine, mkongojo (fimbo) au ukuta. Si sahihi kusali hali ya kuwa yeye mwenyewe anatembea. Kwa sala za fardhi na wajib inajuzu kusali juu ya mnyama iwapo tu atakuwa na udhuru. Udhuru ni kama kuogopa kukimbiwa na wenziwe kama atashuka juu ya mnyama, kuogopa kuibiwa mali na mnyama wake,

chini kuwa na tope au kutokuweza kupanda tena mnyama. Ikiwezekana atamsimamisha mnyama na kuelekea kibla. Kama haikuwezekana basi atasali kuelekea mwelekeo wowote. Hali ni hiyo hiyo kama atakuwa anasali ndani ya kitu kama sanduku kubwa lililowekwa juu ya mnyama. Ikiwa mnyama atasimamishwa na pakatandikwa chini ya hilo sanduku basi litahisabika kaba sofa na hivyo hukumu yake itakuwa ni sawa na mtu anaesali chini. Atalazimika kuelekea kibla na kusali chini.

Kusali ndani ya meli ni kama vile ambavyo alivyofunzwa Sayyidna Jaffar na mtume “sallallahu alayhi wasallam” wakati akienda uhabeshi. Wakati meli inatembea, pasipo na uzito sala za fardhi na wajibu husaliwa. Sala ya jamaa pia inaweza kusaliwa. Kusali kwa ishara (imaa) haito juzu, lazima rukuu na sijda zifanyike. Pia ni lazima kuelekea kibla. Ataanza kusali kwa kuelekea kibla na kama meli itageuza upande basi naye atajigeuza. Ni wajibu katika meli, kuisafisha sehemu ya kusalia kutokana na najsi. Kufuatana na madhehebu ya Hanafi, inajuzu kusali kitako hata sala ya fardhi katika meli yenye kutembea hata kama huna udhuru.

Meli iliyotia nanga baharini lakini ikawa inayumba sana kutokana na mawimbi basi hukumu yake ni kama yenye kutembea. Na ikiwa haiyumbi sana basi itapewa hukumu ya meli iliyosimama. Haijuzu kusali sala ya fardhi kwa kukaa katika meli iliyosimama bandarini. Ikiwa uwezo wa kushuka nchi kavu upo basi ashuke nchi kavu na kusali. Na kama kutakua na hatari ya kuibiwa mali yake au kukimbiwa na chombo basi atasali wima humo ndani ya chombo. Maelezo ya **(Nimeti islam)** yamemalizikia hapa.

Anasema **(Ibn Abidin)**: kusali ndani ya mkokoteni wa maringi mawili ambao hauwezi kusimama wenyewe bila ya kufungwa na mnyama basi hukumu yake, wakati mnyama anatembea au amesita, ni sawa na kusali juu ya mnyama. Mkokoteni wa maringi manne ni kama kochi wakati mnyama hatembei. Na wakati anatembea ataswali kwa kufata hukmu kama iliyotajwa kabla, atamsimamisha mnyama na kusali hali ya kuelekea kibla. Na kama haikuwezekana kumsimamisha basi atasali kwa hukmu ya kusali ndani ya meli yenye kutembea. Ikiwa mtu atakuwa katika safari na ikawa hawezi kukaa chini wala kuelekea kibla basi atafuata rai ya Shafi na Malik ya kuchanganya sala mbili baada ya kuwasili. Haijuzu kwa mgonjwa ambae anaweza kukaa chini, kusali kwa ishara (imaa) juu ya kiti au kochi. Aliye ndani ya basi au ndege atasali kama aliye ndani ya gari. Mtu huhesabiwa kuwa ni msafiri ikiwa baada ya kutoka nje ya mipaka ya mji au kijiji akawa

amenuia kufanya safari ya siku tatu, yaani farsah 18 (meli 54 sawa na kilomita 104). Kufuatana na Ibn Abidin meli moja ni dhiraa 4000 na dhiraa moja ni sawa na vidole 24. Kidole kimoja ni sawa na sentimita mbili. Kwa hivyo kufutana na Shafii na Malik farsah 16 ni sawa na meli 48 na ni sawa na kilomita 80.

**Njoo tusali, tufute uchafu wa moyo**
**Bila kusali, huwezi kumkaribia Allah**

**Wakati sala ikisaliwa, dhambi zote hupukutik**
**Bila kusali, mja hawezi kukamilika**

**Sala imesifiwa sana , ndani ya Quran karim**
**Bila ya sala, amesema, sitompenda mja.**

**Katika hadithi sharif, alama ya imani**
**Bila ya sala, haiwezi kuonekana**

**Kuacha sala, ni dhambi kubwa**
**Haitoshi toba, bila kuilipa**

**Mwenye kuibeza sala, hupotewa na imani**
**Hawi muislam bila ya kutekeleza sala**

**Sala husafisha moyo, huzuia maovu**
**Hupati nuru, bila ya kusali.**

## FADHILA ZA TAKBIRA YA UFUNGUZI

Mtu yeyeote ambae ataleta takbira ya ufunguzi pamoja na imam basi hupukutika dhambi zake kama majani ya mti yanavyopukutika katika msimu wa kipupwe.

Siku moja wakati mtume “sallallahu alayhi wasallam” akiswalisha sala ya asubuhi, mmoja wa masahaba hakuiwahi takbira ya ufunguzi na kutokana na hilo akamuachia huru mtumwa. Kisha akamueleza mtume “sallallahu alayhi wasallam” kilichotokea na kutaka kujua kama kumwachia kwake huru mtumwa kutamfikisha thawabu za kuwahi takbira ya ufunguzi. Mtume “sallallahu alayhi wasallam” akamgeukia sayyidan Abubakar “radiyallahu anhuma” akamuuliza **(Wewe unasemaje juu ya hii takbira ya ufunguzi?)** Akasema Sayyid-na Abubakar „radiyallahu anhuma” (Ewe mjumbe wa Allah, lau kama nitakuwa na ngamia arobaini na wakawa wote wamebeba vito vya thamani. na vyote nikavitoa sadaka kwa masikini. Basi sihisi kwamba nitakuwa nimezifikia thawabu za kuwahi takbira ya ufunguzi pamoja na imam. Kisha mtume “sallallahu alayhi wasallam” akasema **(Je wewe Umar, unasemaje juu ya hii takbira ya ufunguzi)** Akasema Sayyid-na

Umar “radiyallahu anhu” (Ewe mjumbe wa Allah, lau kama nitakuwa na ngamia waliojaa katika ardhi ya Makka na Madina na wakawa wote wamebeba vito vya thamani. na vyote nikavitoa sadaka kwa masikini. Basi sihisi kwamba nitakuwa nimezifikia thawabu za kuwahi takbira ya ufunguzi pamoja na imam). Kisha mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allah akasema **(Je wewe Othman unasemaje kuhusu hii takbira ya ufunguzi)** Akasema Sayyidna Othman „radiyallahu anhuma” (Lau kama nitasimama kusali rakaa mbili za sala ya usiku na nikakhitimisha Quran nzima ndani yake , basi sihisi kwamba nitakuwa nimezifikia thawabu za kuwahi takbira ya ufunguzi pamoja na imam.) Kisha mtume “sallallahu alayhi wasallam” akasema **(Ewe Ali, wewe unasemaje juu ya hii takbira ya ufunguzi)**. Hazrat Ali karramallahu wajhahu akasema. (Ewe mjumbe wa Allah, lau kama jeshi la makafiri litajaa mashariki na magharibi na likawa linawaua waislam. Kisha Allah akanipa nguvu nikapigana jihadi na kuwaua wote. Basi sihisi kuwa nitakuwa nimepata thawabu zenye kufikia kuiwahi takbira ya ufunguzi pamoja na imam.)

Kisha akasema mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allah **(Enyi masahaba wangu na umati wangu! Lau kama mbingu saba na ardhi saba zingelikuwa karatasi, na bahari zote zikawa wino, na miti yote ikawa kalamu na malaika wote wakawa ni waandishi na wakaandika hadi siku ya kiama, basi wasingeweza kuziandika thawabu zinazopatikana kwa kuwahi takbira ya ufunguzi pamoja na imam).**

Na kama utajiuliza. malaika walioumbwa na Allah wana wingi gani basi jawabu lako litakuwa ni kwamba siku ambayo mtume “sallallahu alayhi wasallam” alipopandishwa miraji aliwaona malaika wakizizunguka pepo, moto, na baytul mamur na wakienda zao. Mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allah akauliza **(Ewe ndugu yangu Jibril, hawa malaika wanaozunguka baytul maamur wakishazunguka hawarudii tena. Huwa wanakwenda wapi?)** Akasema Jibril „alaihis-salaam” (Ewe kipenzi cha Allah, Mimi tangu niumbwe hadi hivi leo, malaika wanaizunguka nyumba hii. Na kwa yule ambae ameshazunguka mara moja, zamu yake haitokuja tena hadi siku ya kiama).

Wakati mja anaposoma Audhu na Bismillahi ndani ya sala, Allah humpa thawabu sawa na wingi wa nywele zilizo mwilini mwake. Wakati anaposoma Suratul Fatiha anampa thawabu sawa na hija iliyokubaliwa. Na wakati anaporukuu anampa thawabu sawa na alietowa sadaka dhahabu mia. Na anapoleta sunna ya kusoma tasbih mara tatu ndani ya rukuu basi Allah anampa thawabu sawa na aliesoma vitabu vinne na sahifa mia zilizoshushwa kutoka mbinguni.

Na anaposema **(Samiallahu liman hamidah),** basi Allah anamzamisha kwenye bahari ya rehema zake. Na anapokwenda kwenye sijda anampa thawabu sawa na idadi ya binaadam na majini. Wakati yuko kwenye sijda akaleta sunna ya kuleta tasbih mara tatu, kuna fadhila nyingi ambazo huwa anapewa. Miongoni mwao ni hizi:

Anapata fadhila zenye uzito sawa na arshi na kursiyyi. Allah anampa maghfira yake mja huyo. Malaika Mikail “alaihis-salaam” atakuwa akimtembelea kaburini hadi siku ya kiama. Siku ya kiama malaika Mikail “alaihis-salaam” atambeba kwenye mbawa zake, atamtakia shufaa na kumchukua kumuingiza peponi.

Wakati anapokaa kitako cha mwisho atampa mja huyo thawabu za fakiri mwenye subira.

Fakiri mwenye subira ataingia peponi miaka mia tano kabla ya tajiri mwenye shukrani. Matajiri watakapowaona basi watatamani nao wangekuwa masikini duniani.

**Malaika wa hesabu watakuja kaburini**
**Wakuulize kama ulisali sawa sawa**

**Ulidhani umeokoka kwa kuondoka duniani**
**Wakwambie adhabu yako leo itayari.**

## YANAYOHUSU PEPO TUKUFU

Kuna pepo nane zenye milango minane. Kila mlango una ufunguo wake. Ufunguo wa kwanza ni sala tano. Wa pili ni Bismillahi sharif. Sita iliyobaki imo ndani ya suratul Fatiha. Pepo nane ni hizi:

1- Dari jalal. 2- Dari karar. 3- Dari salam. 4- Jannatul huda. 5- Jannatul maawa. 6- Jannatul aden. 7- Jannatul Firdaus. 8- Jannatul naim.

Dari jalal: hii inatokana na nuru nyeupe.

Dari karar: Hii inatokana na yakuti nyekundu.

Dari salam: hii inatokana na zabarjad ya kijani.

Jannatul huda: hii inatokana na marjan

Jannatul maawa: hii inatokana na fedha.

Jannatul aden: hii inatokana na dhahabu.

Jannatul Firdaus: hii inatokana na dhahabu na fedha.

Jannatul naim: hii inatokana na yakuti nyekundu.

Waumini watakaoingia pepeoni watakaa huko milele na hawatatoka. Mahuri waliomo humo, hawapati damu ya hedhi wala

nifasi na wala hawatokuwa na vitiba viovu. Kila aina ya chakula na kinywaji wanachotaka kitakuwa tayari mbele yao. Hakuna kazi ya kupika au kuchuma kutoka mtini. Ndege wataruka juu ya vichwa vyao hali ya kuwa wamekaa kwenye makasri yao wakiwatazama. Lau kama itamjia mtu katika akili akasema (Kama duniani ungekuwa unanijia karibu kama hivi basi ningekukamata nikakuchoma), basi hapo hapo atashushiwa sahani ya ndege ambae ndio kwanza amechomwa. Baada ya kuiweka mifupa pembeni kama itamjia katika akili kuwa awe ndege kama alivyokuwa mwanzo basi hapo hapo atakuwa ndege na kuanza kuruka. Dongo la peponi limeumbwa kwa misk na nyumba zake zimejengewa fedha na dhahabu.

Watu wa peponi watapewa nguvu za wanaume mia na kila mmoja atapewa mahuri sabini na wanawake wawili wa duniani kwa uchache.

Ndani ya pepo kuna mito minne, inayoanzia sehemu moja na kuelekea sehemu tofauti na yenye ladha tofauti. Mmoja una ladha ya maji safi, wa pili una ladha ya maziwa safi, wa tatu una ladha ya mvinyo wa peponi na wa nne una ladha ya asali safi.

Katika pepo kuna villa refu ambazo waumini watakuwa wanazipanda na kuwapeleka wanakotaka. (Hizi kwa mfano wa leo ni kama ndege na ngazi zenye kutembea.)

Kwenye pepo kuna mti uitwao Tuba. Mti huu mizizi yake iko juu na matawi yake yako yananinginia kuelekea chini. Ni kama mfano wa jua na mwezi.

Watu wa peponi watakula na kunywa wanachotamani lakini hawatohisi haja ndogo wala kubwa. Watakuwa mbali na mahitaji hayo ya kibinaadamu.

Kisha Allahu talaa atawahutubia waja wake na kusema **(Enyi waja wangu, mnataka nini zaidi nikupeni. Furahieni mazuri na matamu yenu)**. Waja nao watasema (Ewe mola wetu, umetuokoa na adhabu ya moto na ukatuingiza peponi. Umetupa mahuri, ghilman na wildan. Umetupa neema ambazo jicho halijawahi kuona, sikio halijawahi kusikia wala akili haijawahi kufikiria. Tutake nini tena kutoka kwako!) Allahu talaa atawaambia **(Enyi waja wangu, bado mnatakiwa mtake kitu kutoka kwangu).** Waja watajibu (Ewe mola wetu, baada ya kutupa yote haya, hatuna uso wa kuomba chengine. Hata cha kukiomba pia hatukijui.) Allah atawauliza **(Mlipokuwa duniani wakati jambo likikutatizeni mlikuwa mnafanya nini)**. Watajibu waja (Tulikuwa tukiwauliza wanazuoni) Allah atawaambia **(Basi na hapa fanyeni hivyo hivyo. Na chochote watakachokwambieni basi nitakupeni)**.

Wanazuoni watasema mmesahau Jamalullah (uzuri wa Allah). Wakati mlipokuwa duniani mlikuwa mkitamani sana kuona Jamalullah na mlikuwa mkisema (Huko akhera mola wetu ambaye ametakasika na kuwepo pahali, atatuonesha Jamalullah (uzuri wake)). Hilo ndilo mnalotakiwa mliombe hivi sasa. Hapo tena wataomba ruuyatu jamalih (kuuona uzuri wake). Allah alietakasika na kuwepo kwake pahali atawaonesha jamalih na hilo litabakia akilini mwao kwa maelfu ya miaka.

Wakati muumin yuko ndani ya kasri lake kutakuwa na matunda yamemzunguka na mengine madirishani mwake. Wakati atakapofikiria kunyanyuka ili achume tunda kutoka tawini, basi tawi litasogea alipo na atachuma. atakapoanza kulila kabla ladha haijafika kooni, tayari tunda jengine litakuwa limeshaota pale lilipochumwa la mwanzo. Wakati atakapolitia mdomoni ataliona ni tamu lililowiva. Na Allah tayari atakuwa ameshaumba jengine.

**Ikiwa ni mwenye akili Sali, sababu ndio mhimili wa furaha**

**Fahamu kwamba sala ndio miraji ya muumini.**

## SALA ZA KADHA

Kuna fadhila nyingi kwa sala zilizosaliwa kwa wakati wake:

1- Inatia nuru ya uso

2- Inafanya umri uwe na baraka.

3- Inasababisha kupokelewa dua

4- Inaleta kheri.

5- Waumini wote humpenda mtu huyo.

Kuacha sala kwa maana ya kuiahirisha ukaisali baada ya wakati wake kutoka bila ya udhuru kuna madhara kumi na tano. Matano ya duniani, matatu wakati wa kufa na matatu kaburini na manne baada ya kufufuliwa. Ama matano ya duniani ni:

1- Inaondoa nuru ya uso.

2- Inaondoa baraka katika umri.

3- Dua haikubaliwi.

4- Dua atakayomuombea nduguye muumin haikubaliwi.

5- Hapati thawabu za amali zake nyengine.

Dhara za wakati wa kufa ni hizi:

1- Anakufa hali ya kuwa ana njaa.

2- Anakufa na kiu.

3- Anakufa asie tosheka. Chakula chochote atakachokula hakitomuondolea njaa na chochote atakachokunywa hakitomuondolea kiu.

Dhara za kaburini ni hizi:

1- Kaburi litambana mpaka mifupa yake itapandiana.

2- Kaburi lake litazungukwa na moto.

3- Nyoka mkubwa aitwae Aqra ataingia kaburini mwake. Huyo nyoka atakuwa na bakora mkononi mwake. Bakora hiyo atakapopigwa mja mara moja itampeleka hadi chini ya ardhi. Kisha atarudi tena ili apigwe nyengine. Na atendelea kupata adhabu hiyo hadi siku ya kiama.

Dhara za siku ya malipo:

1- Hesabu yake itakuwa nzito.

2- Atastahiki kupata ghadhabu ya Allah.

3- Ataingia moto wa Jahannam.

4- Kwenye paji lake la uso itaandikwa mistari mitatu:

Mstari wa kwanza utasema (amestahiki ghadhabu ya Allah.

Mstari wapili utasema hakutekelza haki ya Allah.

Mstari wa tatu utasema kwa vile hakutekeleza haki ya Allah, leo yuko mbali na rehema zake.

Sala ni nguzo ya dini. Yeyote mwenye kusali anakuwa amesimamisha nguzo ya dini. Kwa muda huo hufanyika kivuli cha kumfunika.

Ikiwa mtu ataacha kipindi cha sala kwa makusudi na kisha asiilipe sala hiyo basi kufuatana na madhehebu matatu imetolewa fatwa ya kumuuwa. Kufuatana na madhehebu ya Hanafi hafai kuuliwa ila atakuwa amefanya dhambi kubwa kabisa. Ataendelea kuwekwa jela hadi atakaposali. Ikiwa ataacha sala kwa kutokuipa umuhimu na kutokuamini ndio wadifa wa mwanzo wa muislam basi huyo huwa kafiri.

Ikiwa mtu ataacha sala kwa makusudi kisha akasali kadha basi ataekwa ndani ya Jahannam kwa muda uitwao hukba (miaka themanini na nane). Ili kuokoka na adhabu hii inalazimu kuleta toba na kuomba. Msamaha.

(Siku moja ya akhera ni sawa na mwaka wa hapa duniani. Hivyo kisia itakuwaje miaka kadhaa ya akhera).

Anasema Muhammad Amin ibni Abidin “rahmatullahi alaih” katika kitabu kiitwacho **(Raddul muhtar)**. Dini zote zilizoshushwa kutoka mbinguni zimeamrisha kusali. Adam akisali laasiri, Yakubu akisali

magharibi na Yunus akisali isha. kama ambavyo kuzikubali fardhi na haram zote ni sharti ya imani basi vile vile kukubali kuwa kusali ni wadhifa na ni deni pia ni wajibu wa imani. Ila kitendo chenyewe cha kusali si sharti ya imani.

Kwa kila muislam mwanamke na mwanamme ambae ana akili na amebaleghe basi ni sharti asali sala tano kila siku. Sala tano zilifaradhishwa katika usiku wa Miraji. Katika hadithi inayopatikana katika **(Mukaddimatu salat)** na **(Tafsiri mazhar)** na **(Halabiyyi Kabir)** inasema **(Jibril alaihis-salaam alinisalisha karibu na mlango wa Kaaba kwa siku mbili. Sote tulisali asubuhi wakati alfajiri ilipochomoza, adhuhuri wakati jua lilipotenguka, alasiri wakati urefu wa kivuli umekipita kitu husika, magharibi wakati jua lishazama** [sehemu yake ya juu imeshapotea] **na isha anga lilipoingia kiza. Na siku ya pili sala ya asubuhi tuliisali wakati anga limepata mwangaza, adhuhuri kivuli kilipofika mara mbili ya kitu husika, laasiri mara tu baada ya hapo, magharibi wakati wa kufungua saumu na isha wakati usiku umeshagawika sehemu moja kati ya tatu. Kisha akasema hizi ndizo nyakati za sala kwako na kwa mitume "sallallahu alayhi wasallam" iliyopita. Umati wako watasali sala tano, kila moja baina ya hizi nyakati mbili tulizosali).** Imeamrishwa kila siku kusali sala tano. Kuanza kumuamrisha mtoto kusali akiwa na umri wa miaka saba na afikapo miaka kumi mzazi anatakiwa kumpiga kwa mkono kama hatosali. Haijuzu kumpika zaidi ya mara tatu au kumpiga kwa bakora. Na kwa namna hiyo hiyo hupigwa katika kuhimizwa funga na kukatazwa kunywa pombe. Yule ambaye hatoamini kuwa sala ni fardhi, yaani ndio wadhifa wa mwanzo wa muislam, basi huyo huwa kafir. Yule ambae anaamini kuwa ni fardhi ila akawa haitekelezi labda kutokana na uvivu wake basi huyo hawi kafiri bali anakuwa **(Fasik)**. Atatiwa gerezani hadi atakapoanza kusali, hatosamehewa wala hatoonewa huruma. Ikiwa hatoanza kusali basi ataachwa gerezani hadi afe. Kuna pia waliosema kuwa atapigwa hadi atoke damu. Kufuatana na madhehebu ya Shafii na Malik ikiwa mtu ataacha kipindi cha sala kwa uvivu, pamoja na kuwa hawi kafiri, lakini adhabu yake ni kifo. Kufuatana na madhehebu ya Hanbal ni kafiri anaefaa kuuliwa. Pia rai hii inapatikana kwa baadhi ya wanazuoni wa Shafii. Mtu amabae atasali na jama anafahamika kuwa ni muisalm. Kwa sababu katika dini nyengine sala ilikuwa ikisaliwa kwa mtu peke yake, haisaliwi kwa jamaa. Hija pia wakifanya. Kwa vile sala ni ibada inayofanywa kwa kiwiliwili tu, haiwezekani kufanyiwa na mtu mwengine. Iwapo mtu atakuwa na udhuru, kwa mali yake na amri yake anaweza akatolewa zaka na mtu

mwengine kwa sababu zaka ni ibada ya mali tu. Kwa vile hija inafanyika kwa mali na kiwiwliwili, hivyo kwa amri yake na mali yake mtu anaweza kufanyiwa hija na mtu mwengine. Kama mtu amefikia umri wa kuwa hatoweza tena kufunga hadi kufa kwake basi kwa kila siku ya funga atatoa fidia ya mali na kumpa maskini mmoja. Haijuzu kutoa fidia kwa ajili ya sala. Iwapo mtu hawezi kusali kama akiacha wasia basi ili kulipa deni la sala, itakuwa vyema ikitolewa fidia kutoka katika mali aliyoiacha. Ikiwa mali aliyoiacha haitoshi kulipia deni la sala basi deni hilo inajuzu kulihaulisha. Katika funga ni wajibu kulipa.

Katika kipindi cha kiangazi, kwa wakazi wa upande wa kaskazini, ambako alfajiri inafika hata kabla ya anga kuingia kiza, wakati wa isha na alfajiri haupatikani, hivyo kufuatana na madhehebu ya Hanafi sala mbili hizi kuzisali si lazima. Mujtahid mkubwa, imama Shafii yeye amesema kuwa ni lazima kuzisali sala hizi. Wengi wa wanavyuoni wanaona kuwa si fardhi kwa watu wa maeneo hayo kuzisali sala hizo za isha na asubuhi. Kulipa kadha pia si lazima kwa sababu sala hizi wakati wake hauingii. Kusali kabla ya kuingia wakati wake si fardhi. Lakini funga haiko hivyo. Mwezi ukionekana katika nchi basi funga huanza.

Iwapo mtu anapotekeleza fardhi au kuacha la haramu kutakuwa na **(Haraj)** (uzito) katika madhehebu yake, basi anaweza kuondoa uzito huo kwa kufuata madhehebu nyengine. Haraj maana yake ni kupatikana uzito katika kulifanya jambo au kushindikana kabisa kufanyika. Iwapo hakuna njia isiyo na haraj katika madhehebu nyengine na ikawa hili jambo lenye haraj pia lina dharura basi kutekeleza fardhi hiyo au kuacha haram hiyo kunasamehewa. Lakini kama itakuwa hakuna dharura, basi atatakiwa kutafuta njia ya kuiondoa hiyo haraj.

Mtu ambae atakuja katika sala ya asubuhi hali ya kuwa amechelewa basi hatosali sunna. Kuacha sunna ili usipitwe na wakati ni lazima. Na ikiwa ataiwahi jamaa basi anaweza kusali nyuma au nje ya msikiti. Ikiwa hakuna sehemu kama hiyo basi asisali ubavuni mwa msikiti. Ataacha kusali sunna kwa sababu inafaa kuacha sunna ili kuepuka kutenda makruh.

Sala ambazo hazikusaliwa kutokana na udhuru huitwa **(Fawait)**. Zile ambazo hazikuachwa kwa udhuru, bali ziliachwa kwa uvivu hizo huitwa **(Matrukat)**. Maulamaa wa fik-hi walipotaja sala za kadhaa walitaja Fawait hawakutaja sala zilizoachwa, kwa sababu kuacha sala bila ya udhuru ni dhambi iliyo kubwa. Dhambi hii haisamehewi kwa

kusali kadha. Inalazima kuleta toba au kuhiji hija mabruur. Kusali sala ya kadha kunaondosha dhambi la kutokuitekeleza ile sala lakini haiondoshi dhambi ya kupitisha sala kutokana na wakati wake. Toba inayoletwa kabla ya kusali kadha pia haikubaliki kwa sababu moja kati ya sharti ya toba ni kuachana na lile kosa ulilolitenda.

Kuna dharura tano zinazokubalika kuipitisha sala baada ya wakati wake: Iwapo yuko katika vita na haiwezekani kusali hata kitako au juu ya mnyama hata kwa kuelekea upande usio wa kibla. Msafiri amabae anakhofia kuibiwa na wezi au kuvamiwa na majambazi au wanyama wakali. Iwapo mkunga anakhofia kwamba mzazi au mtoto anaezaliwa atadhurika . Kusahau. Kulala. Sala inakubaliwa kuwa imewahiwa kwa kuwahi kuleta takbira ya ufunguzi kufuatana na madhehebu ya Hanafi. Kufuatana na madhehebu ya Shafi kwa kuiwahi alau rakaa moja.

Ni fardhi kulipa fardhi na ni wajib kulipa wajib. Kulipa sunna kunampa mtu thawabu za sunna. Ni lazima kufuatanisha mpangilio wa sala tano na sala ya witri wakati wa kuzitekeleza kila siku na wakati wa kusali kadha. Ila ikiwa wakati wa sala unakaribia kutoka hili si lazima kulifuata. Hii ina maana kwamba haiwezekani kuacha sala ya wakati uliopo kwa ajili ya kusali kadha. Ikiwa atasahau kuwa kuna sala iliyomfutu au sala zilizomfutu zinafika sita basi sharti ya kufuatanisha inaondoka na zitakapopungua chini ya sita sharti hairejei tena. Sala ambazo hazikusaliwa kwa mpangilio pamoja na kuwa zinakuwa fasid, idadi yake ikiwa sita, utakapotoka wakati wa sala ya tano basi sala zote huwa sahihi. Mfano, mtu asie sali sala ya asubuhi, hata baada ya kukumbuka akawa hakusali kadha na akaendelea kusali sala za adhuhuri, alasiri, magharibi, isha na witri basi sala hizi zote hazitakuwa sahihi. Ila jua litakapochomoza zote zitakuwa sahihi.

Ni wajibu mtu kuharakisha kulipa sala iliyomfutu. Anaweza akacheleweshа kulipa kwa ajili ya kuwatafutia watoto mahitaji ya lazima, kusali sala za sunna zinazokwenda na fardhi, kusali sala ya dhuha na tahiyatul masjid. Anasema Ibn Abidin katika suna za udhu (maana ya jaiz ni kwamba si jambo lililokatazwa. Hivyo hata jambo ambalo ni makruh tanzih ni jaiz). Hivyo kutokufanya jambo ambalo ni jaiz, na kutokuchelewesha kulipa fardhi na wajib kwa ajili ya sala hizo za suna. Kulipa funga ya Ramadhani hakuna haraka.

Wale waliosilimu ambao wanaishi katika nchi za makafiri hawatolipa ibada zilizowapita katika umri wao kama sala, zaka na saumu. Kwani hawakuwa na habari nazo. Ila kutokujua mambo ya halal na haramu si udhuru kwa watu wanaoishi katika nchi za kiisalm. Mtu akiritadi (akiacha Uislam) kisha akarudi katika Uislam hatotakiwa

kulipa zile sala alizoziacha kipindi alipokuwa kafiri kwa sababu Uislam hauwaamrishi ibada makafiri. Ikiwa mtoto ambae hajabaleghe alisali sala ya isha kisha akalala, na akabaleghe usingizini basi asubuhi akiamka atalazimika kuilipa sala ya isha. Hii ni kwa sababu ile sala alioisali kabla ya kubaleghe ilikuwa ni sunna na alilazimika kuanza kusali baada ya kubaleghe akiwa usingizini. Kwa sala ambazo hazikusaliwa wakati mtu akiwa na afya, anaweza kuzilipa wakati ni mgonjwa hali ya kuwa ametayamam au anasali kwa ishara. Iwapo msafiri analipa sala za rakaa nne alizoziacha wakati akiwa mukimu (si msafiri) basi atalipa rakaa nne. Iwapo mtu ameacha sala ya rakaa nne akiwa safarini, ambapo husaliwa rakaa mbili basi atakapolipa wakati ameshárudi katika safari yake ataisali rakaa mbili. Wakati anasali sala ya adhuhuri ni wajibu kwenye nia kupitisha kuwa anasali sala ya adhuhuri ya wakati ule au hata kupitisha tu kuwa anasali sala ya adhuhuri. Kama kutakuwa na kadha zaidi ya moja basi atapitisha katika nafsi kuwa ni kadha ya mwanzo au ya mwisho ya adhuhuri anayoilipa. Ila katika Ramadhani kama unadaiwa zaidi ya siku moja si lazima kupitisha katika nia siku halisi unayoilipa kwa sabau sharti hilo halipo katika funga.

Wakati analipia sala zilizokuwa Matruk inalazimu asidhihirishe kwa watu kwa sababu kuacha sala bila udhuru (matruk) ni dhambi na kudhihirisha dhambi pia ni dhambi. Kufanya dhambi usiku kisha ukaja ukaihadithia mchana ni dhambi. Tarjama ya Ibn Abidin inamalizikia hapa.

Inafahamika kwamba katika madhehebu ya Hanafi kulipa sala iliyomfutu mtu ni lazima. Katika madhehebu ya Shafi ni hivyo hivyo. Mmoja wa wanazuoni wa Shafii Shamsudin Muhamad Ramly anasema (Mtu mwenye sala zilizomfutu kwa udhuru, kusali sala ya tarawehe mwezi wa Ramadhani na kuziacha sala zilizomfutu baada ya Ramadhani inajuzu lakini kwa sala zilizoachwa bila ya udhuru haliwezekani hilo na ni lazima kulipwa haraka. Wanazuoni wa Shafii wanaeleza kwa uwazi kuwa ni dhambi kuacha kulipa sala zilizoachwa bila ya udhuru na badala yake ikawa anasali sala za sunna kama tarawehe na kwamba ni lazima kulipa badala ya kusali sala hizi sa suna. Pia katika madhehebu ya Hanafi ni hivyo hivyo.

Sala iliyoachwa kwa udhuru kufuatana na madhehebu ya Hanafi imeambiwa inaweza kucheleweshwa kwa ajili ya kusali suna ila ni vyema kutokuzichelewesha sala za kadha kwa ajili ya sunna hizo. Kwa sababu katika Uislam jaiz maana yake ni kwamba haikukataziwa. Ibn Abidin anasema kufuatana na kauli isemayo inafaa kufanya israfu kwa

maji yenye kuchuruzika maana yake ni makruh tanzih. Sala iliyoachwa kwa udhuru inalazimika kuharakisha kuilipa na ile iliyoachwa bila ya udhuru inalazimika kusaliwa badala ya sunna. Anasema Ibn Abidin "rahmatullahi alaih" (Kukosha mara tatu wakati wa udhu ni suna iliyokokotezwa. Ikiwa kuna shida ya maji, maji yakiwa baridi sana au kukiwa na uhitaji mwengine wa maji basi si makruh kuacha suna hii) Inafahamika kwamba ni lazima kulipa sala iliyoachwa haraka na ni lazima kuzisali sala hizi katika sunna za sala nyengine ukiachia suna ya asubuhi. Utekelezaji wa sala ya kadhaa badala ya sunna unaelezewa katika mlango wa umuhimu wa sala.

## KUANGUKA KWA SALA KWA MAITI

Kuanguka kwa sala kwa maiti maana yake kuondoka kwa deni la sala. Kwa ajili ya hili hutolewa kafara. Ili kutolewe kafara inabidi kabla mtu hajafa aandike wasia na aache pesa zitakazotosha. Yani theluthi ya mali aliyoacha isiwe ni chache kuliko kiwango cha kafara. Kafara inatolewa na walii. Walii ni yute mtu aliemuusia au warithi wake. Katika uislam kuna mawalii aina nne. Walii wa maiti, walii wa yatima, walii wa mwanamke wakati wa kuolewa na walii wa mtumwa. Huyu wa mwisho huitwa **(Maula)**. Mbali na hawa kuna na mawalii wa Allah. Hawa pia huitwa **(Awliyaa)**. Hawa ni vipenzi vya Allah. Ili kuweza kufikia penzi hili maneno, matendo na mwenendo wake mtu lazima uwe kama alivyofunza mtume "sallallahu alayhi wasallam". Haya anaweza kujifunza mtu kutoka kwa alim wa kweli. Na iwapo hakuna alim wa kweli basi ajifunze kutoka kwenye vitabu vya wanazuoni wa ahli sunna. Anasema **(Ibn Abidin)** "rahmatullahi alaih" (Sala iliyomfutu mtu kama ataweka wasia kuwa ilipiwe kafara basi kwa kila sala moja ya fardhi na wajib italipwa nusu pishi (lita 2. 1) yani dirham mia tano na ishirini (1750 gram) ya ngano au unga kutoka katika thuluthi ya mali aliyoiacha. Hii atawapa masikini wengi au hata mmoja. Kutoa thamani ya vitu hivyo kwa dhahabu au fedha ni bora zaidi. Iwapo mtu ameacha wasia lakini hakuacha mali au thuluthi ya mali yake haitoshi kulipia wasia huo, au hakuacha wasia lakini mmoja kati ya jamaa akataka kutabaruku kwa kumtolea kafara basi hesabu yake kwa siku itakuwa ni 1750 x 6 = 10500 gram. Hii ni kilo kumi na nusu kwa siku ambayo ni kilo 3780 za ngano kwa mwaka. (Au anaweza akalipa kwa thamani inayojulikana. Kilo kumi za ngano kwa kawaida thamani yake ni gram moja ya dhahabu hivyo kwa kutizama usawa wa thamani yake kwa sarafu za dhahabu atalipa sarafu 52.5 au kwa kupendeza zaidi sarafu 60. Kufuatana na uzito wa sarafu hizo (432 gram) anaweza akalipa kitu

chengine kama bangili au pete. Kwa kuzingatia kuwa sala alizozisali maiti zinaweza kuwa na mapungufu, basi atapunguza miaka kumi na mbili kwa mwanamme na miaka tisa kwa mawanamke kutoka kwenye umri alioishi, hapo atapata idadi ya miaka mabayo alilazimika kusali na kufuatana na madhehebu ya Hanafi kila siku ina sala sita zenye kulazimu kafara hivyo kwa mwaka ni kilo 3780 za ngano au kilicho bora zaidi ni kulipa thamani yake ambayo ni sarafu sitini za dhahabu. Hii atapewa fakiri hali ya kutia nia ya kafara ya sala kwa ajili ya maiti husika. Fakiri lazima awe mwenye akili, baleghe, alie mwema na mwanamme. Fakir atapokea na kusema nimepokea. Kisha fakiri atamrejeshea walii hiyo mali kwa kumpa zawadi. Walii anaweza kuitumia tena mali hiyo kwa kulipia kafara ya mwaka mwengine kwa kumpa fakiri huyo huyo au fakiri mwengine. Na kwa mtindo huo anaweza kuitumia mali hiyo kulipia kafara ya miaka yote anayodaiwa. Ikiwa aliazima dhahabu nyingi kuliko inayohitajika kwa mwaka basi idadi ya mizunguko itapungua. Ikiwa hakuna sarafu za dhahabu basi anaweza akaazima vitu kama bangili na pete kutoka kwa mwanamke atapima na kuweka kwenye kitambaa uzito ufikao (miaka aliyokua hakusali x 7.2 gram). Katika kitambaa kutakuwa na dhahabu ya miaka yote ambayo maiti hakuswali. Uzito huu ukizidishwa kwa sitini na kugaiwa kwa idadi ya mafakiri hapo itapatikana idadi ya mizunguko inayohitajika. Ikiwa dhahabu itakuwa chache kama nusu ya mfano uliopo basi namba ya mizunguko itakuwa mara mbili yake. Kwa mtu aliekufa katika umri wa miaka sitini, 60 x 48 x 7.2=20736 gram zitatolewa kupewa fakiri mmoja. kwa mwaka mmoja hutolewa sarafu sitini. Hivyo itafanyika mizunguko thalathini ya 100 gram ya dhahabu kwa masikini saba. Wakati mizunguko imemalizika, fakiri wa mwisho atampa walii hizo dhahabu kama zawadi ili nae apate akarejeshe alikoziazima. Kwa namna hiyo mizunguko inaweza kufanywa katika malipo ya funga, kiapo na ibada ya kuchinya. Lakini katika kiapo zaidi ya mafakiri kumi wanahitajika na fakiri mmoja hawezi kupewa zaidi ya nusu pishi kwa siku wakati kwenye sala mtu mmoja anaweza akapewa kafara zaidi ya moja kwa siku moja bali hata wakati mmoja. Deni la zaka la maiti haliwezi kuondoshwa ila kwa wasia wake. Ila kwa vile funga haishurutishi wosia, basi hata kwa zaka kama walii atatabaruku kwa kutoa kwa maiti wake itakuwa vyema. Baada ya kumalizika mizunguko yote mrithi atatoa zawadi ya mali kwa mafakiri.

Iwapo wosia wa kafara alioutoa maiti unazidi theluthi ya mali, basi walii hawezi kutoa zaidi ya theluthi ya mali bila ya ruhusa ya warithi. Iwapo theluthi itatosha kwa wasia lakini maiti akawa na deni basi

itabidi kwanza madeni yalipwe hata kama mwenye kudai ataruhusu ilipwe kafara. Kwanza itatakiwa alipwe haki yake. Akishalipwa haitojuzu kutoa zawadi kwa ajili ya kulipa kafara kwa sababu malipo yanayokubaliwa kwenye kafara ni yale yanayotoka na zawadi iliyotolewa na warithi. Ikiwa mtu ataweka wasia kulipwa kafara kwa sala ambazo hakuzisali umri wake wote , na ikawa umri wake haujulikani, basi wasia huo utakuwa batil. Lakini ikiwa thuluthi ya mali. inazingatiwa kuwa ni zaidi ya kima kinachohitajika kwa sala alizoziacha katika umri wake, hii ina maana kwamba ametoa usia kwa mali ambayo haitimii theluthi ya mali yake na hapo wasia wake utakuwa sahihi. Walii au warithi hawalazimiki kutoa cha kwao kwa ajili ya kulipia kafara hata kama maiti ameusia. Lazima thuluthi ya mali atakayoacha maiti kama wasia iweze kukidhi malipo ya kafara na aseme kwamba zitumike kutolea kafara ya sala. Kama atausia kuwa sehemu ya theluthi itumike kuzungushia katika malipo na sehemu nyengine wagaiwe warithi au watu wengine basi atakuwa ameacha wajib na hili ni dhambi. Kwa hivyo kuusia kuwa sehemu ya theluthi itumike kwa kuzungushia na nyengine zitumike kwa hitima na halili sio sahihi.

Pia haijuzu kutumia pesa nyengine kwa ajili ya kumlipa msomaji wa Quran. Mtoaji na mpokeaji wote watapata dhambi. Inajuzu kusomesha watu Quran kwa ujira ila hakuna aliejuzisha malipo ya kusoma Quran. Ikiwa maiti atausia kuwa sala hizi zisaliwe kadhaa na mrithi wake basi haitokuwa sahihi. Inawezekana kwa mtu kusali au kufunga na kisha thawabu zake akazitoa hadiya kwa maiti. Mtu alie katika maradhi ya kifo haitojuzu kulipia fidia sala zake mwenyewe. Tarjama ya Ibn Abidin imemalizikia hapa.

Anasema Ahmed Tahtawi “rahmatullahi alaih” katika maandishi ya pembeni ya kitabu **(Merakil Falah)** kwamba kuhusu kuanguka saumu iliyokuwa haikufungwa kwa kulipia fidia, ni jambo lililothibitishwa kwa nass. Na kwa vile sala ni muhimu kuliko funga, jambo la kuwa sala nayo inahitaji kulipwa wanazuoni wetu wamekubaliana. Kiongozi wa dini anayesema kuangusha sala halina asili katika dini basi atakuwa amethibitisha ujinga wake. Wanazuoni wetu wamelipinga hili kwa kauli moja.

Wakati mgonjwa yuko kitandani na ikawa hawezi kusali hata kwa ishara, sala hizi asizoweza kuzisali hata kama ni chache chini ya tano basi halazimiki kuandika wasia. Na kwa mfano huu ikiwa msafiri au mgonjwa atashindwa kufunga, na asipate ukaazi au siha ya kuweza kulipa, huyu naye hatoandika wasia. Inawezekana kuandika wasia kwa zakatul fitri, nafaka ya mke, makosa ya hija baada ya ihram, hija,

sadaka za nadhiri na mengineyo. Iwapo maiti hakuandika wosia basi mrithi wake au mtu yoyote yule kufanya tabaruu kwa ajili yake inshallah itafaa. Ikiwa mtu atausia hija, yule mwenye kumfanyia ana weza akaondokea kwenda safari ya hija kutoka katika huo mji wa maiti au kutoka pale ambapo theluthi ya mali yake itatosheleza. Lakini ikiwa anamfanyia hija kwa pesa alizo tabaruu yeye mwenyewe basi anaweza akaondokea mji wowote. Si sahihi kwa mtu yeyote kumsalia au kumfungia maiti kwa ujira au bila ya ujira. Hadithi zinazokubalisha jambo hili ni mansuh (zimefutwa hukmu yake) Kupitia sadaka zitakazotolewa kama kafara, Allah atamsamehe maiti madeni yake. Katika kitabu cha Shafii kiitwacho **(Anwar)** anasema (Kutoa fidya kwa sala ambazo maiti hakuzisali si wajibu na hata kama itatolewa basi haiziangushi hizo sala) Wafuasi wa Malik na Shafii wanaweza kufuata rai ya Hanafi na wakafanya mzunguko.

Ikiwa mali aliyousia maiti haitoshi kwa kafara au theluthi ya mali yake haitoshi kwa kafara, au hakuacha wosia kabisa, akitokea mtu na akatoa mali kidogo basi itatumika kwa njia ya kuizungusha ili kulipa deni lake lote. Atapewa fakiri kwa nia ya kulipa deni. Kisha yeye atampa zawadi mali hiyo walii au mtu mwengine. Ni sharti mali hiyo apewe na kuishika mikononi mwake kwanza. Kisha yeye anaweza akatoa tabaruu kwa nia ya kulipia deni la maiti, na hapo atapewa fakiri. Tarjuma kutoka maandishi ya pembeni ya Tahtawi inamalizika hapa.

## YANAYOHUSU SALA YA IJUMAA

Kuna masharti saba ya kuifanya sala ya Ijumaa iwe sahihi:

1- Sehemu inayosaliwa sala ya Ijumaa iwe ni kubwa kiasi ya kuitwa mji.

2- Kusomwa hutba.

3- Hutba kusomwa kabla ya sala.

4- Kuwepo mazun naib wa Imam au hata rais wa nchi.

5- Isaliwe ndani wa wakati wa sala ya adhuhuri.

6- Isaliwe jamaa. Kufuatana na imam Adham na Imam Muhammad “rahmatullahi alaih”, mbali ya imamu, wapatikane watu watatu wanaume balegh wenye akili. Kufuatana na Imam Abu Yusuf “rahmatullahi alaih” wanaume wawili wenye akili walio baleghe watatosha . Lililo sahihi zaidi ni la mashekhe wawili.

7- Isaliwe sehemu ambayo jamaa wanaweza kushiriki.

Katika fatwa ya **(Hindiyye anasema)** (mwanaume huru, asie mgonjwa, asie safarini, ni fardhi kwake kusali sala ya Ijumaa).

Sala ya Ijumaa si fardhi kwa wanawake, walio safarini na wagonjwa. Pia kwa wale wenye kuogopa dhuluma ya vyombo vya dola. au kukiwa na mvua kubwa pia si fardhi kwao. Amiri, kamanda au muajiri asiwazuie wale walio chini yake kwenda kusali sala ya Ijumaa. Ikiwa imam anaesalisha Ijumaa ni fasik, na ikawa uwezo wa kumzuia haupo basi ni lazima kumfuata imam huyu na kuto kuacha sala ya ijumaa. Katika sala nyengine inafaa akasali msikiti mwengine na asiswali nyuma ya imam fasik. Ni makruh kwa mwanamke yeyote kusali sala yoyote msikitini.

Mtu yeyote ambae ataiwahi sala ya Ijumaa katika rukuu ya rakaa ya pili basi kufuatana na imam Muhammad "rahmatullahi alaih" atakamilisha kwa kusali adhuhuri lakini kufuatana na imam Adham na imam Abu Yusuf "rahmatullahi alaih" hata kama atawahi tashahud tu basi atakamilisha sala ya Ijumaa. Wakati hatibu anahutubia, mtu yeyote atakaesali suna basi atasali rakaa mbili tu bila ya ziada. Na ikiwa ni sunna ya Ijumaa kuna khitilafu kati ya kuwa atasali rakaa mbili tu au atakamilisha nne. Lililo sahihi zaidi ni kwamba atakamilisha nne.

Yaliyo wajibu katika sala ya Ijumaa ni mambo matano:

1- Kuacha kila kitu baada ya kuadhiniwa.

2- Kuharakia kwenda msikitini.

3- Kutosali nafila wakati hatibu yuko juu ya min-bar.

4- Kutokuzungumza maneno ya kidunia

5- Kukaa kimya.

Yaliyo mustahab katika sala ya Ijumaa ni mambo sita:

1- Kutia manukato.

2- Kutumia mswaki.

3- Kuvaa nguo safi.

4- Kwenda msikitini mapema (Katika zama za masahaba walikuwa hawatoki msikitini baada ya sala ya asubuhi na wakisubiri hadi Ijumaa ikimalizika).

5- Kukoga.

6- Kumsalia mtume "sallallahu alayhi wasallam".

Yaliyo makruh katika sala ya Ijumaa ni mambo matano:

1- Kutoa salamu wakati hatibu yuko kwenye minbar.

2- Kusoma Quran.

3- Kumjibu anaepiga chafya **(Yarhamukallah).**

4- Kula na kunywa.

5- Kufanya lolote lililo makruh. [hatibu kurefusha hotuba pia ni makruh.]

Baada ya adhana ya kwanza ya Ijumaa inayosomwa juu ya mnara, imam atakuja karibu na minbar na atasali sala ya kablia. Kisha atakuja usawa wa minbar hali ya kuwa ameelekea kibla na atasoma dua kisha atapanda juu ya minbar na atakaa hali ya kuwaelekea maamuma na kusikiliza adhana ya pili. Kisha atasimama na kuanza hotuba.

Wale wanaoitwa wahabi si katika madhehebu ya ahli sunna. Hawa ni wasio na madhehebu. Hawa huitwa **(Wahabi)** au **(Najdy)**. Uwahabi umeanzishwa na waingereza Wameanzisha kupitia Muhammad Abdul-wahab ambae ni mnajdi asie na nasabu, kiongozi wa dini alie jahil. Ndani ya vitabu vyake wale waislam wasio wahabi amewaita makafiri na mushrik. Akasema hawa inajuzu kuwaua na kuwachukua wake zao, binti zao na mali zao kama ghanima Wakichukua viongozi wa dini majahil wasio na madhehebu kutoka kila nchi, wakiwapa pesa nyingi na kuwapeleka kwenye makao makuu ya kiwahabi waliyoyaita **(Rabitatul alamil islam)**. Hawa hutoa fatwa zisizokubalika na uislam (na wakadai kuwa ni fatwa za umoja wa wanazuoni wa dunia) na kuzieneza nchi zote za kiisalam. Kila mwaka hutoa bure fursa za kufanya hijja. Miongoni mwa waliyoyaandika ni kwamba ni faradhi kwa wanawake kusali sala ya Ijumaa. Wanawalazimisha wanawake na watoto wa kike kwenda sala ya Ijumaa. Wanasali sala hali ya kuchanganyika wanawake na wanaume. Miongoni mwa maandishi yao wameandika (Hutba za sala ya Ijumaa na sala ya Idi zisomwe kwa lugha ya wenyeji na zisisomwe kwa kiarabu. Fat-wa kama hizi zimejibiwa na wanazuoni wa kweli kwa kutumia dalili katika miji tafauti. Mfano wa fatwa hizo zilizo sahihi ni zile zilizotolewa India na wanazuoni mbali mbali wa ahli sunna. mfano Mufti wa Madrir allama hibrunnihrir wal fahama sahibut takrir wa tahrir mawlana Muhammad Tamim Muhammad Madrasy “nawwarallahu markadahu” anasema:

Kuisoma hutba yote kwa lugha ya wenyeji au kuisoma kwa kiarabu na tafsiri yake ni makruhu. Kwa sababu mtume “sallallahu alayhi wasallam” alisoma hutba kwa kiarabu Katika **(Bahrur raik)** wakati anaelezea sala ya Idi anasema: Ukiachia sala ya tarawehe na sala ya kupatwa mwezi, sala nyengine za nafila hazisaliwi jamaa. Sala za Idi mara zote zinasaliwa jamaa na hii inaonesha kuwa sala hizi si nafila bali ni wajibu. Inafahamika kwamba ibada ambayo mtume “sallallahu alayhi wasallam” aliendelea kuifanya kila wakati basi inakuwa ni wajib. Mwanachuoni Zabidy “rahmatullahi alaih” Allah amrehemu katika sherhe ya **(Ihya)** anasema (Amali ambayo mtume “sallallahu alayhi

wasallam” amedumu kuifanya inakuwa ni wajibu na haioneshi kuwa ni fardhi.) Mwanazuoni mufti Abusuud Efendi “rahmatullahi alaih” katika **(Fat-hullahil muumin)** (Mtume “sallallahu alayhi wasallam” anapodumu kufanya jambo basi hiyo inaonesha kuwa ni jambo la wajib). Anasema ibn abidin aktika sunna za udhu (Iwapo mtume “sallallahu alayhi wasallam” amefanya jambo kwa kudumu bila ya kuliacha basi hilo linakuwa ni sunnat muakkada (sunna iliyopewa nguvu). Pamoja na kutokuliacha akakataza lisiachwe basi hilo huwa ni wajib kwa sababau kutokukataza maana yake ni kuacha. Ndio maana Abusuud akasema kuwa lile ambalo aliliendeleza bila kuliacha ni wajib. Yote mawili kuachwa kwake bila ya udhuru ni makruh tahrimy kama ambavyo itaelezwa mwisho wa makruh za sala Mtume “sallallahu alayhi wasallam” sallallahu alayhi wasallama kusoma hotuba kwa kiarabu tu inaonesha wajibu wa kusoma hotuba kwa kiarabu. Kwa hivyo kusoma hotuba kwa lugha nyengine au kusoma kwa kiarabu na tarjuma yake ni makruh tahrimy. Katika hali ya kwanza hotuba huwa imeachwa kusomwa kwa kiarabu na katika hali ya pili imeachwa kuwa ya kiarabu pekee. Katika hali zote mbili limeachwa lile jambo ambalo mtume “sallallahu alayhi wasallam” alidumu kulifanya. Basi ni hivyo hivyo kuleta takbir ya ufunguzi kwa kiarabu na kusema Allahu akbar baina ya vitendo vya sala ni mambo mawili tafauti ambalo lolote kati ya haya mawili likiachwa basi inakuwa ni makruh tahrimy. Kwa vile mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allah alidumu kusema Allahu akbar, basi inakuwa ni wajibu kuisema na kutokuisema ni makruh tahrimy. Anasema Ibn abidyn katika **(Raddul Mukhtar)** (Makruh ni kuacha wajib au sunna. La kwanza ni makruh tahrimy na la pili ni makruh tanzihy) Na katika **Halaby Kabir** anasema (Kuacha sunna ni makruh tanzihy na kuacha wajib ni makruh tahrimy). Katika **(Fatawa sirajiyya)** anasema kuwa inajuzu kusoma hotuba kwa kiajemi. Kufuatana na kauli hii kusoma hotuba kwa lugha isiyokuwa ya kiarabu inafaa ila kutoa fatwa kwamba si makruh tanzihy wala tahrimy ni batil. Kwa sababu mwenye kitabu amesema “inakuwa sahihi”. Neno hili halimaanishi kuwa sio makruh. Anasema Ibn Abidin katika **(Raddul mukhtar)** kwamba (kusema sahihi, haimaanishi kuwa si makruh). Anasema Muhammad Abdulhay Luknawy “rahmatullahi alaih” katika **(Umdatur riaya)** (Kusoma hotuba kwa kiarabu si sharti. Kusema inajuzu kusoma kwa kiajemi au lugha nyengine jaiz ina maana kwamba sala itajuzu. Ina maana ili sala ya ijumaa iwe sahihi sharti la hutba litakuwa limetekelezeka. Ila haimaanishi kuwa hotuba haikuwa na jambo makruh. Kwa sababu mjumbe wa Allah na masahaba wake kila wakati na kila mahala walisoma hotuba kwa lugha ya kiarabu tu.

Kwenda kinyume nao ni makruh tahrimy. Matabiina na tabii tabiina wote kila wakati kila mahala walisoma hotuba kwa kiarabu tu. Hawakusoma kwa lugha isiyokuwa ya kiarabu wala hawakuleta tarjama yake. (Hali ya kwamba Asia na Afrika ilikuwa wanaowasikiliza hawajui kiarabu na wala hawakusikia au kufahamu kitu. Wala hawakufanya tarjama ili nao waweze kufahamu. Pamoja na kwamba hawa walikuwa ni waislam wapya ambao wanalazimika kufunzwa Uislam, lakini maimam hawakuona kuwa inajuzu kusoma hotuba kwa lugha isiyo ya kiarabu. Ili waweze kufahamu hotuba na Uislam vizuri waliwataka wajifunze kiarabu. Na sisi tunatakiwa tufanye kama wanazuoni hawa.)

Kwenda kinyume na hawa na kuzisoma hutba kwa lugha isiyo ya kiarabu ni **(Bid'a)** na ni makruh tahrimy. Kusema ya kwanza ni makruh tahrimy na ya pili ni makruh tanzihy si sahihi kwa sababu makruh tanzihy ni kuacha sunna. Mtume "sallallahu alayhi wasallam" sallallahu alayhi wasallama siku zote na kila pahala alisoma khutba kwa kiarabu tu hivyo hili ni jambo la wajib. Je kwa vipi kuacha wajibu huu iwe makruh tanzihy? Jambo lililo makruh tahrimy ni wajibu kuliacha. Mawlana Bahrul ulum "rahmatullahi alaih" katika **(Arkanul arbaa)** anasema (Jambo ambalo ni makruh tahrimy kuliacha ni wajib. Kulifanya jambo hili maana yake ni kuacha jambo la wajib.)

Mtu ambae kila wakati anafanya jambo ambalo ni makruh tahrimy basi mtu huyo huhesabiwa si muadilifu. Katika kuelezea wajibu katika sala Ibnu Abidin "rahmatullahi alaih" katika kitabu chake **(Raddul Mukhtar)** alimnukuu Ibn Nujaym kwa kusema (Kufanya makruh tahrimy ni dhambi ndogo. Kuifanya dhambi ndogo kwa kuendelea kunaondosha uadilifu). Hivyo wale wenye kusoma tarjuma za hutba nao pia ni watu wasio na uadilifu, mafasik. Ni makruh tahrimy kusali nyuma yao. Inasemwa katika **(Nurul izah)** na **(Ibn Abidin)** (Ni makruh kuwapa uimam mtoto wa zina, watu wa vijijini, na mtumwa ikiwa watakuwa hawana elimu au fasik na mtu wa bid'a hata kama atakuwa na elimu. Ni dhambi kwa watu hawa kuwafanya maimamu.) Allama Ibrahim Halabi "rahmatullahi alaih" katika kitabu cha **(Halabiyil Kabir)** anasema (Wenye kumfanya fasik imam basi wametenda dhambi kwa sababu tendo hilo ni makruh tahrimy.) Na katika **(Merakil falah)** anasema (Mtu yeyote ambae ni fasik, ni makruh kumpa uimamu hata kama atakuwa ni alim. Kwa sababu atafanya bezo katika utekelezaji wa mambo ya Uislam. Inafaa kwenda kinyume nae. Kumpa uimamu mtu kama huyu ni kumpa heshima. Ikiwa itashindikana kumuondoa katika uimamu basi ni wajibu kusali sala ya Ijumaa na sala nyengine katika

msikiti mwengine asio salisha yeye.) Allama Tahtavi “rahmatullahi alaih” katika kulieleza hili anasema (Kumpa uimamu mtu fasik ni makruh tahrimy).

Haitakiwi kuwa msaidizi katika tendo la imam kusoma hotuba kwa lugha isiyo ya kiarabu. Kusaidia katika hilo ni dhambi kwa sababu kusaidia dhambi yoyote nako ni dhambi. Anasema Ibn Abidin “rahmatullahi alaih” katika **(Raddul mukhtar)** (Haifai kusali nyuma ya imam fasik. Inalazimu imam mwengine ambaye si fasik. Ila haiko hivyo kwa sala ya ijumaa. Lakini ikiwa katika mji kunasaliwa ijumaa zaidi ya moja basi pia itakuwa ni makruh kusali nyuma ya imam fasik kwa sababu uwezo wa kusali nyuma ya imama mwengine upo. Hivyo pia ndivyo ilivyoandikwa katika **(Fathul kadir)**. Kwa hivyo asisali mtu nyuma ya imam anaesoma hutba kwa lugha isiyo ya kiarabu. Atafute imam anaesoma kwa lugha ya kiarabu tu na asali nyuma yake. Kwa maelezo zaidi soma kitabu kiitwacho **(Attahkikatu suniyya fi karahatil hutba bi ghayril arabiyya wa qiraatiha bil arabiyya maa tarjumatiha bi ghayril arabiyya).** Tarjuma ya allama Muhammad Tamim Madrisy imemalizika hapa.

Maelezo ya hapo juu yaliandikwa kwa kiarabu huko India mwaka 1349 hijria (1931 miladia) na kusadikishwa na kutiwa saini na waalimu kumi na tisa. Fatwa ya tarehe hii pamoja na fat-wa za wanazuoni wa India zilizo katika **(Diyobend),** (Bakiyatul salihat)**, (Madras)** na **(Haydar abad**) ambazo ni za kiarabu zilichapishwa huko Istanbul. Maelfu ya Wanazuoni na Shaykhul islam waliopata umaarufu wakati wa dola ya Uthman walifanya jitihada kutafuta njia ili watu wazifahamu hotuba. Kuzitafsiri hotuba za kiarabu hawakuona kuwa ni jaiz hivyo hawakutoa ruhusa hiyo. Waliamua kuwa kutolewe maelezo ya hutba baada ya sala ili watu wafaidike na hilo liliendelea kwa zaidi ya miaka mia sita. Kwa njia hiyo waislam waliweza kushikamana na dini yao bila kuacha mafunzo yake.

Katika sala ya Idi kuna takbira tisa. Moja ni fardhi, moja ni sunna na saba ni wajib. Takbira ya ufunguzi ni fardhi, takbira ya rukuu ya kwanza ni sunna na takbira saba za ziada ni wajib.

## KUSALI

Katika **(Nimatil Islam)** anasema kwamba ni fardhi kwa mtu ambae ana akili na ni baleghe kusali sala tano kila siku . Mtu hawezi kutekelezewa sala yake na mtu mwengine. Mtu anaweza kutoa hadiya thawabu za sala yake na ibada zake nyengine kwa mtu mwengine alie hai au alie kufa. [Watapewa thawabu kama alizopewa yeye bila ya yeye

kupunguziwa chochote.] Haijuzu kutoa hadiya thawabu na kumpa hasimu yako anaekudai ili aweze kukusamehe. Mtu mbaye anaamini kuwa sala ni fardhi na akawa hasali kutokana na uvivu basi huyo hatokuwa kafiri bali ni Fasik. [Imeelezwa kwamba kwa kila sala moja ataunguzwa kwenye Jahannam miaka sabini elfu]. Ataekwa jela hadi atakapoanza kusali. Mtoto akifikia umri wa miaka saba ataamrishwa asali. Ikiwa atafikia umri wa miaka kumi akawa hasali basi atapigwa kwa kutumia mkono. Hatopigwa zaidi ya makofi matatu wala hatopigwa kwa kiboko bakora). Kiboko kinatumika kupiga watu wazima wenye makosa kupitia uamuzi wa hakimu. Mume pia hatakiwi ampige mkewe kwa kiboko. [Haifai kukipiga kiumbe chochote kilicho hai kichwani, usoni, kifuani, na mbele tumboni.] Ni fardhi kwa mgonjwa kusali kwa kiasi ya uwezo wake.

## KUWA NA UDHURU

Ikiwa kitu chenye kutengua udhu kitakuwa kinatoka mwilini kwa kuendelea huo huitwa udhuru. Wasioweza kuzuia mkojo, uharo, ushuzi, damu ya pua au uchafu unaotoka kidondani, kutokwa na machozi kwa kuendelea kutokana na maumivu au uvimbe wa jicho na damu ya istihadha hawa huwa ni watu wenye udhuru. Vitu hii vitatakiwa kuvizuia kwa dawa, kuifunga sehemu husika, kusali kitako au kwa ishara. [Mwanaume mwenye kutokwa na mkojo atie pamba ndani ya tundu yake. Wakati wa kwenda haja , kipande cha pamba kitatoka chenyewe. Ikiwa mkojo unaomtoka ni mwingi basi utapenya kwenye kipande cha pamba na kutoka nje hivyo kusababisha udhu kutenguka. Mkojo hautakiwi upenye na kuchafua chupi, hivyo inabidi ajizonge kwa kitambaa. Ikiwa utakuwa ni mwingi basi anaweza kaengezea na pamba kwenye kitambaa. Mtu anaepitwa na mkojo anatakiwa abebe vitambaa vitatu hadi vitano kwa ajili ya kujizongea. Baadhi ya wanaume wazee na wale wagonjwa, dhakari yao inakuwa nyofu na haiwezi kuzongeka kwa kitambaa. Watu hawa watatia kitambaa ndani ya mfuko wa plastiki na wataziingiza dhakari zao pamoja na hasua (korodani) ndani ya mfuko na kuufunga. Ikiwa mkojo ulioingia kwenye kitambaa utafikia dirham moja (4.8 gram) kitambaa inabidi kibadilishwe. Udhu wa mtu mwenye udhuru hubatilika mara tu unapomaliza wakati wa sala iliyopo. Iwapo atapatwa na udhuru mwengine basi udhu wake utabatilika kabla ya kumalizika wakati wa sala kutokana na huo udhuru mwengine. Mfano kama alitia udhu kwa udhuru wa kutokwa na damu ya pua katika tundu moja, basi damu ikianza kutoka katika tundu ya pili udhu utatenguka. Kwa madhehebu

ya Shafi na Hanafi ili mtu ahesabiwe kuwa ana udhuru kile kitu chenye kuchuruzika kiwe kinachuruzika kwa kuendelea kwa kipindi kizima cha sala. Ikiwa inawezakana kutia udhu na kuwahi kusali bila ya kuchuruzika basi huyo haitwi kuwa ni mwenye udhuru. Ikiwa najsi iliyosababisha udhuru itadondoka kwenye nguo kwa ukubwa unaozidi dirham moja na ikawa inawezekana kuzuia isichafue tena basi inalazimu kuisafisha. Anasema katika **(Alfikhu ala l madhahibil arbaa)** (Katika madhehebu ya Malik kuna kauli mbili juu ya mgonjwa kuwa na udhuru: Kauli ya kwanza ni kuwa kitu chenye kutengua udhu kiwe kinaendelea kwa zaidi ya nusu ya kipindi cha sala na iwe haijulikani wakati gani inaanza na wakati gani inazuia. Kauli ya pili inasema pale inapoanza kuchuruzika tu hiyo najsi basi mgonjwa huambiwa yuko kwenye udhuru hata kama masharti mawili ya kauli ya mwanzo hayakupatikana. Udhu wake hautenguki. Ikiwa wakati itakaposita unajulikana basi kutia udhu wakati wa kusimama kusali ni mustahabu. Wale wafuasi wa madhehebu ya Hanafi na Shafii ambao hawana sifa za kuambiwa kuwa wana udhuru wanaweza kufuata kauli hii ya pili ya Malik.)]

Wakati wa kukoga josho la wajib ikiwa mtu atakhofia kuwa mgonjwa, au maradhi yake yataongezeka nguvu au muda kwa kutumia maji basi anaweza kutayamam Khofu hii inaweza ikawa inatokana na uzoefu wake au kwa kuambiwa na daktari muislam bingwa na mwadilifu. Daktari ambaye si fasik na asietambulikana kwa madhambi kauli yake pia inaweza kukubalika. Ikiwa ni baridi na mtu hana pa kukaa, hana pa kuchemsha maji au hana pesa za kulipia kwenye vyoo vya nje huyu anaweza kupata maradhi akitumia maji ya baridi. Kufuatana na madhehebu ya Hanafi kwa tayammum moja anaweza kusali fardhi anazotaka. Kwa madhehebu ya Shafi na Malik . atatakiwa kutayamam kwa kila fardhi.

Mwenye vidonda zaidi ya nusu ya viungo vya udhu nae hutayammam. Ikiwa vidonda havitimii nusu ya viungo basi atakosha sehemu zisizo na vidonda na atapangusa kwenye vidonda. Kwa vile wakati wa kukoga mwili mzima unahisabiwa kuwa ni kiungo kimoja, ikiwa nusu ya mwili una vidonda basi atafanya tayammum. Na ikiwa vidonda ni chini ya nusu ya mwili atakosha sehemu zisizo na vidonda na kupangusa kwenye vidonda. Ikiwa kupangusa kutampa madhara basi atapangusa juu ya kitambaa (bendej) naikiwa hilo pia litampa dhara basi ataacha kupangusa. Ikiwa kupangusa kichwa kutaleta dhara wakati wa udhu au kukoga basi ataacha kupangusa. Ikiwa mtu hawezi kutumia maji kutokana na matatizo aliyonayo kwenye viganja kama

vidonda, basi atatayammam kwa kupangusa uso na mikono kwenye dongo au hata ukuta wenye dongo chokaa na kadhalika. Ikiwa mtu hana miguu wala mikono na uso una vidonda basi atasali bila udhu. Yule ambae hana mtu wa kuweza kumtia udhu atatayammam. Mtoto, mtumwa au mfanyakazi alie nae wanalazimu kumsaidia. Pia anaweza kuomba msaada kutoka kwa watu wengine ila wao hawalazimiki kumsaidia. Mke na mume pia hawana ulazima kutiana udhu.

Ikiwa mtu amejifunga bendej (au plasta iliyo juu ya kitambaa au malham) kutokana na kutokwa na damu kwenye kidonda, tumvitumvi, jipu, mfupa uliovunjika au kukatika, ikiwa hatoweza kuikosha sehemu iliyoathirika kwa maji ya moto au ya baridi, au hata kupangusa juu yake kwa hivyo wakati wa kukoga au kutia udhu atapangusa zaidi ya nusu ya hiyo sehemu. Ikiwa itakuwa ni dhara kufungua bendej basi sehemu iliyo chini ya bendej hailazimiki kukoshwa. Kupanguswa kutafanywa juu ya sehemu zilizo nzima zinazoonekana pembeni ya bendej. Sio lazima kuwa na udhu wakati wa kufunga bendej. Ikiwa bendej litabadilishwa baada ya kupangusa basi si lazima kupangusa juu ya bendej jipya na hali ni hiyo hiyo kama atafungwa bendeji jipya juu ya kongwe.

## SALA WAKATI WA UGONJWA

Anasema katika **(Nimat-i islam**):

Mtu ambae hawezi kusimama au anaehisi kuwa akisimama maradhi yake yataongezeka basi atasali kwa kukaa na wakati wa kurukuu atapinda kidogo kesha atakaa sawa na kusujudu juu ya sakafu. Atakaa kama ambavyo itakuwa ni wepesi kwake. Inaruhusika kwao kupiga magoti, kukaa kwa kuzungusha miguu au kukaa kwa kukalia matako na kuweka mikono kwenye magoti. Maumivu ya kichwa , jino na jicho yote yanakubalika kuwa ni maradhi. Kuogopa kuonekana na adui pia inakubalika kuwa ni katika udhuru. Ikiwa udhu unatenguka pindi akisimama basi atasali kitako. Ikiwa ataweza kusali kasimama hali ya kuegemea kitu basi aegemee. Ikiwa mtu anaweza kusimama kidogo kisha nguvu zinamwishia basi wakati wa takbira ya kufungulia sala aanze amesimama na nguvu zikimwisha aendelee kwa kusali kitako.

Yule asiyeweze kusujudu kwa kupinda chini basi atasali wima kisha atakaa na kusali kwa imaa. Wakati wa kurukuu atapinda kidogo na wakati wa kusujudu atapinda zaidi. Ikiwa mwili haupindi basi atapindisha kichwa tu. Si lazima kusujudu juu ya kitu. Na kama watasujudu juu ya kitu kilichonyanyuliwa sala yao itakuwa sahihi lakini

italazimika kwamba kupinda kwao wakati wa kusujudu kuwe ni zaidi kuliko wakati wa rukuu. Ki uhakika ni kwamba hakuna haja kusujudu juu ya kitu kilichonyanyuliwa. Ikiwa ataweza kusali kwa kukaa huku ameegemea basi haitokuwa jaiz kusali kwa kulala. Mtume "sallallahu alayhi wasallam" sallallahu alayhi wasallam alimuona mgonjwa akisali kitako na mbele kaweka mto wa kusujudia. Mtume "sallallahu alayhi wasallam" aliuondoa ule mto. Akaja akamuona kaweka ubao wa kusujudia nao pia akauondoa, kisha akamwambia **(Ikiwa unaweza sujudu chini na ikiwa huwezi fanya imaa kwa kupinda zaidi wakati wa kusujudu kuliko wakati wa rukuu.)** Haya yametajwa kwenye **(Bahru raik)**. Katika surat Ali Imran aya ya 191 katika maana ya aya inasema (Sala kwa mwenye kuweza husali amesimama. atakaeshindwa atasali amekaa. Na atakaeshindwa zaidi atasali kwa kulala) Wakati Imran bin Huseyn alipokuwa mgonjwa mtume "sallallahu alayhi wasallam" alimwambia **(Sali hali ya kuwa umesimama. Usipoweza kaa kitako. Usipoweza Sali hali ya kuwa umelala ubavu au juu ya mgongo (kichalichali).** Hapa inafahamika kwamba yule mgonjwa asiyeweza kusimama atasali amekaa. Na asipoweza kukaa atasali amelala. Asiyeweza kukaa kwa aina yoyote ile basi atasali kwa kulala. Haijuzu kwa mtu ambae anaweza kusali hali ya kuwa amekaa chini, au kwa wasafiri kwenye ndege au basi kusali juu ya kiti na kuninginiza miguu chini. Yule ambae anashindwa kusali kwa kusimama akiwa kwenye jamaa basi na asali kwa kusimama nyumbani. Mambo ishirini yafuatayo ni katika udhuru za kutokuhudhuria jamaa: Mvua, baridi au joto kali, woga wa kuvamiwa nafsi au mali yake na adui, kuogopa kukimbiwa na wenzio mlio safarini pamoja, kiza kizito, fakiri anaeogopa kukamatwa na kutiwa jela kutokana na deni lake, kuwa kipofu, kutokuweza kutembea kwa kupooza, kuwa huna mguu mmoja, mgonjwa, mlemavu, tope, kutokuweza kutembea, mzee asiyeweza kutembea, kuogopea kuikosa darsa ya fikhi iliyo nadir kupatikana, kuogopea kukikosa chakula anachokipenda sana, msafiri akiwa katika harakati, kuwa na mgonjwa na ukawa huna wa kumuachia, usiku wenye upepo mkali na kuwa na uhitaji wa kwenda chooni. Yule ambaye anakhofia maradhi yake kuzidi au kuengezeka muda, yule ambae anaangalia mgonjwa na hana wa kumuachia na yule mzee ambaye hawezi kutembea hao wanapewa udhuru wa kutokuhudhuria sala ya Ijumaa pia. Kwenda msikitini kwa kutembea ni bora kuliko kwenda kwa kipando. Kusali kwa kukaa juu ya kiti msikitini haijuzu. Kufanya ibada kinyume na Uislam ulivyofahamisha ni **bid'a** nayo ni dhambi kubwa kufuatana na vitabu vya fikh.

Mgonjwa asiyeweza kuelekea kibla ataelekea upande ambao ni mwepesi kwake. Mgonjwa aliyelazwa juu ya mgongo ataekewa mto chini ya kichwa ili kinyanyuke na uso uelekee kibla japo kidogo. Ni vyema kwa magoti kupindwa. Ikiwa mtu hawezi kusali kwa imaa basi sala itakujalipwa kadhaa. Yule ambae ataumwa ndani ya sala basi ataendelea kwa namna atakavyoweza. Yule ambae alikuwa akisali hali ya kuwa kakaa akajihisi amepata nguvu, basi atasimama na kuendelea kusali wima. Yule ambae atapoteza fahamu hatoendelea na sala. Ikiwa fahamu zitamrudi kabla ya kumalizika vipindi vya sala tano basi atazilipa zote sala tano. Ikiwa fahamu zitarejea wakati kipindi cha sala ya sita kimeshaingia basi hatozilipa hizo sala.

Ni fardhi kuharakisha kulipa sala hata kama itakuwa ni kwa imaa. Ikiwa hatowahi kuzilipa kwa kufikiwa na wakati wa umauti basi si wajib kuacha wasia wa kutumia mali yake kuangusha hizo sala. Ikiwa atapata siha kwa muda wa kutosha kuweza kulipa basi hapo kuusia itakuwa ni wajib. Ikiwa hatousia, basi walii au hata mtu wa mbali kutumia mali yake kwa kuzifuta hizo sala itakuwa jaiz. Maandishi kutoka **(Nimatil islam)** yameishia hapa.

Katika hadithi tunasoma kuwa kuna mambo ishirini na nne yanayoleta ufakiri.

**1- Kukojoa wima bila dharrura.**

**2- Kula hali ya kuwa una janaba.**

**3- Kukidharau kipande kidogo cha mkate na kukikanyaga.**

**4- Kuchoma moto maganda ya kitunguu maji na kitunguu thomu.**

**5- Kutembea mbele ya wakubwa wako.**

**6- Kuwakata majina baba na mama.**

**7- Kujichokoa meno kwa kijiti cha ufagio au kijiti cha mti.**

**8- Kukosha mikono kwa tope.**

**9- Kukaa kizingitini.**

**10- Kutia udhu sehemu iliyokojolewa.**

**11- Kutia chakula katika vyombo visivyokoshwa.**

**12- Kushona nguo wakati ziko mwilini.**

**13- Kula kitunguu maji wakati una njaa.**

**14- Kujipangusa uso kwa skati.**

**15- Kuacha mabuibui katika nyumba.**

**16- Kuharakia kutoka msikitini baada ya kumaliza sala ya asubuhi.**

**17- Kwenda mapema sokoni na kuchelewa kutoka.**

**18- Kununua mkate kutoka kwa mtu masikini.**

**19- Kuwaombea dua mbaya baba na mama.**

**20- Kulala uchi.**

**21- Kutokufunika mitungi na vyungu.**

**22- Kuzima kitu kwa kupuliza kama mshumaa.**

**23- Kufanya jambo lolote bila kusema Bismillahi**

**24- Kuvaa suruali hali ya kuwa umesimama.**

Mtu yeyote ambae atasoma **(Inna aatayna)** wakati wa kulala na kisha akasema (Yarabbi niamshe kwa sala ya asubuhi) kwa idhini ya Allah ataamka sala ya asubuhi kwa wakati wake.

## UMUHIMU WA SALA

Katika kitabu cha **(Ashiatul Lamaat)** kuna hadithi nyingi zinazoelezea umuhimu wa sala. Kitabu hichi ni sherhe ya kifarsi ya kitabu kiitwacho **Mishkatul Masabih** kilichoandikwa na mmoja kati ya wanazuoni wakubwa wa India Abdulhak bin Seyfudin Dahlavi "rahmatullahi alaih". Chapa ya tisa ilichapishwa huko Luknov mwaka 1384 hijria (1964 miladia).

Sala maana yake ni dua rahma na istighfar. Imeitwa sala kwa sababu ya kujumuisha kwake maana zote hizi tatu

1. Abuhurayra „radiyallahu anh" anasema Amesema mtume "sallallahu alayhi wasallam" wa Allah (**Sala tano na sala ya Ijumaa hadi Ijumaa, na Ramadhan hadi RamadhanIi ni kafara kwa dhambi anazozifanya, zinakuwa ni sababu ya kusamehewa madhambi madogo. kwa wenye kujikinga na madhambi makubwa).** Madhambi madogo ambayo hayakuhusisha haki za waja wengine husamehewa. Baada ya kumalizika madhambi yote madogo basi kwa yale madhambi makubwa hupunguziwa adhabu zake. Ili kuweza kusamehewa madhambi makubwa ni lazima kuleta toba. Ikiwa hana madhambi makubwa basi huwa ni sababu ya kupandishwa daraja. Hadithi hii imo ndani ya kitabu **cha Muslim**. Sala ya Ijumaa huwa ni sababu ya kusamehewa wenye mapungufu katika sala nyengine. Ramadhani nayo huwa ni sababu ya kusamehewa mapungufu ya sala ya Ijumaa.

2. Anahadithia tena Abuhurayra „radiyallahu anh" kwamba mtume "sallallahu alayhi wasallam" wa Allah amesema **(Iwapo mto utapita mbele ya nyumba ya mtu na akawa anakoga mara tano kwa siku je kuna uchafu wowote utakao bakia katika mwili wake?)** Masahaba wakajibu kwamba **(hakuna uchafu unaobaki, ewe mjumbe wa Allah).** Akasema mtume "sallallahu alayhi wasallam" sallallahu alyhi wasallama **(Basi ni hivyo hivyo kwa sala tano. Mtu anaeswali sala**

**tano anafutiwa madhambi yake madogo na Allah) (Bukhari)** na **(Muslim)**.

3. Abdulla bin Masud „radiyallahu anh" anasema mtu mmoja alimbusu mwanamke. Yani mmoja kati ya Ansari alikuwa akiuza tende. Akaja mwanamke kununua tende. Yule Ansari zikamjia hisia za kinyama kwa yule mwanamke. Akamwambia nyumbani ziko nzuri zaidi. Alipofika nyumbani akamgusagusa na kumbusu. Yule mwanamke akamwambia (Ni nini unachokifanya. Muogope Allah). Yule Ansari akajuta na akaja kwa mtume "sallallahu alayhi wasallam" kumueleza alichokifanya. Mtume "sallallahu alayhi wasallam" hakumjibu kitu. Akasubiri wahyi kutoka kwa Allah. Kisha huyu mtu akaswali na Allah akateremsha aya ya 114 ya surat Houd yenye maana ya aya ifuatayo **(Salini katika ncha mbili za mchana na jua linapozama. Hakika mambo mazuri yanafuta maovu.)** Ncha mbili za mchana maana yake ni mwanzo na mwisho wa mchana. Hii ina maana sala ya asubuhi, adhuhuri na laasiri. Na sala zilizo usiku ni sala ya magharibi na isha. Aya hii inaelezea kuhusu kufutiwa madhambi madogo kutokana na kusali sala tano. Huyu mtu akauliza (Ewe mjumbe wa Allah, habari hii nzuri ni kwa ajili ya mimi tu au kwa watu wote). Akajibu mtume "sallallahu alayhi wasallam" wa **(Ni kwa umati wangu wote)**. Hadithi hii iko katika sahihi zote mbili.

4. Anasema Anas bin Malik „radiyallahu anh" kwamba alikuja mtu kwa mtume "sallallahu alayhi wasallam" wa akasema (Nimefanya kosa la kupewa adhabu iliyoandikwa (Had). Nifikishie adhabu ya Had). Mtume "sallallahu alayhi wasallam" hakumuuliza ni kosa gani alilofanya . Ukafika wakati wa sala na tukasali. Baada ya mtume "sallallahu alayhi wasallam" kumaliza sala, huyu mtu alinyanyuka na akasema (Ewe mtume "sallallahu alayhi wasallam" wa Allah, mimi nimefanya kosa la kupewa adhabu iliyoandikwa (Had). Nifikishie adhabu kwa namna Allah alivyoamrisha ndani ya Quran) Mtume "sallallahu alayhi wasallam" akamuuliza **(Wewe hukusali na sisi?)**. Akajibu ndiyo nimesali. Mtume "sallallahu alayhi wasallam" akamwambia **(Usihuzunike, Allah amesamehe kosa lako)**. Hadithi sharif hii imo katika vitabu viwili vya msingi. Huyu mtu alidhani amefanya kosa kubwa lenye kustahiki adhabu iliyoandikwa. Aliposali kosa lake lilisamehewa na hii inaonesha kuwa dhambi yake ilkuwa ni ndogo. Au hiyo adhabu iliyoandikwa (Had) aliyoizungumza ni adhabu ndogo ya kuadhiriwa tu. Katika suala lake la mara ya pili kuwa hakusema (nifikishie adhabu ya Had) inaashiria hilo.

5. Anasema Abdalla bin Masud „radiyallahu anh”: Nilimuuliza mtume “sallallahu alayhi wasallam” ni amali gani yenye thawabu zaidi akanijibu **(Sala inayosaliwa katika wakati wake)** au katika mapokezi mengine **(Sala inayosaliwa mwanzoni mwa wakati wake)**. Nikamuuliza kisha ni ipi. Akasema **(kuwatendea mema wazazi wawili)** Nikamuuliza kisha ni ipi. Akasema **(Jihadi katika njia ya Allah)** Hadithi hii inapatikana katika sahihi mbili. Katika hadithi nyengine, (**Bora ya amali zote ni kulisha chakula)**. Na katika hadithi nyengine **(kueneza salamu)**. Na katika hadithi nyengine **(Kusali usiku hali ya kuwa watu wote wamelala)**. Na katika hadithi nyengine **(Amali iliyo bora kabisa ni kutokumdhuru mtu kwa ulimi wala mkono)** Na katika hadithi nyengine **(Amali bora ni jihadi)** Pia zipo hadithi nyengine zilizosema **(Amali bora ni haji mabrur)**. Yani hija ilyofanywa bila makosa. Na **(Kumdhukuru allah)**. Ja wabu zilitolewa kufuatana na hali ya muulizaji au wakati suala lilipoulizwa. Mfano mwanzo wa uislam jihadi ilikuwa ndiyo amali bora. [Katika wakati wetu, amali bora ni kupambana na makafiri na watu wasio na madhehebu kwa kuwapa jawabu na kueneza madhehebu ya ahli sunna wal jamaa kwa maandishi na uchapishaji. Wale wenye kusaidia jihadi hii, na wale wenye kushiriki kwa mali zao, pesa zao na miili yao nao wanapata thawabu zao. Katika aya na hadithi, sala imeelezwa kuwa ni bora kuliko zaka na sadaka. Ila mtu alie katika hatari ya kifo akatoa kitu ili kuokoka na mauti basi ni bora kuliko kusali.]

6. Jabir bin Abdullah anasema, amesema mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allah **(mpaka ulio baina ya mja na kukufuru ni kuacha sala)** Hii ni kwa sababu sala ni pazia linalomzuia mtu kuwa kafiri. Pazia hili likinyanyuka basi mtu anaangukia kwenye ukafiri. Hadithi hii ipo kwenye **(Muslim)**. Hadithi hii inaonesha uovu wa kuacha sala. Wengi wa masahaba wamemtaja mtu anaeacha sala bila ya udhuru kuwa ni kafiri. Katika madhehebu ya shafii na Malik pamoja na kuwa wamesema hawi kafiri lakini wamesema kuwa ni wajibu auwawe. Kufuatana na madhehebu ya Hanafi anatiwa gerezani na kupigwa.

7. Ubada bin Samit „radiyallahu anh” anatoa habari kwamba amesema mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allah **(Allahu talaa ameamrisha kusali sala tano. Mtu yeyote atakaetia udhu wake mzuri na akasali kwa wakati wake na kafanya rukuu zake kwa hushui basi Allahu taala ameahidi kumsamehe madhambi yake. Asiefanya haya hakumpa ahadi. Akitaka atamuadhibu na akitaka atamsamehe.)** Hadithi hii ameitaja imam Ahmed, Abu Daud na Nisai. Hapa inafahamika kuwa sharti ya sala ni kuwa na hushui katika rukuu na sijda.

Allah hendi kinyume na ahadi yake. Mwenye kusali sala yake kwa usahihi, kwa hakika Allah humsamehe.

8. Anahadithia Abu Umama „radiyallahu anh” kwamba mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allah amesema **(Salini sala zenu tano. Fungeni mwezi wenu mmoja. Toeni zaka ya mali zenu. Watiini viongozi wenu. Ingieni pepo ya mola wenu.)** Inafahamika hapa kwamba, mwenye kusali sala tano, akafunga mwezi wa Ramadhani, akatoa zaka na akawatii wale ambao Allah amewapa ukhalifa katika ardhi katika waislam wenye kutekeleza amri za Uislam, basi huyu ataingia peponi. Imepokewa na Imam Ahmad na Tirmidhy.

9. Miongoni mwa masahaba mashuhuri Burayda Aslami „radiyallahu anhuma” anasema, amesema mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allah **(Ahadi iliyopo baina ya sisi na nyinyi ni sala. Mwenye kuacha sala ni kafir.)** Hapa inafahamika kwamba mwenye kusali ni muislam. Yule asieipa umuhimu sala, na akawa hasali kwa sababu haamini kuwa ni wadhifa wa mbele kwa muislam basi huyo ni kafiri. Hadithi hii imepokelewa na imam Ahmad, Tirmidhy na Ibn maja.

10. Anasema Abu Dhar-i Gifari„radiyallahu anh” Moja kati ya siku za msimu wa vuli, tulitoka pamoja na mtume “sallallahu alayhi wasallam”. Majani ya miti yalikuwa yakianguka. Mtume “sallallahu alayhi wasallam” akakata vitawi viwili. Vitawi vile majani yake yakadondoka haraka. Akasema Mtume “sallallahu alayhi wasallam” **(Ewe Abu dhari, Iwapo muislam atasali kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah . Basi dhambi zake hupukutika kama yanavyopukutika majani ya tawi hili.)** Imepokelewa na Imam Ahmad.

11. Kutoka kwa Zayd bin Khalid Juhaymy, amesema mtume “sallallahu alayhi wasallam” **(Muislam atakaposali rakaa mbili kwa usahihi na khushui basi hufutiwa madhambi yake.)** Ina maana madhambi madogo yote husamehewa. Imepokewa na Ahmad “rahmatullahi alaih”.

12. Kutoka kwa Abdalla ibn Amr bin As „radiyallahu anh”, amesema mtume “sallallahu alayhi wasallam” **(mtu yeyote atakaetekeleza sala basi sala hiyo inakuwa ni nuru na Burhan kwake siku ya kiama. na itamuokoa na Jahannam. Ikiwa hakuhifadhi sala zake basi nuru na Burhan haipatikani wala haokoki na moto. Atakuwa pamoja na Karun, Firaun, Haman na Ubey bin Khalaf.)** Hapa inafahamika kwamba mtu yoyote atakaesali na kutekeleza vyema fardhi, suna, wajib na adabu za sala basi sala hiyo huwa ni nuru kwake siku ya kiama . Na kama asipoendeleza basi atakuwa pamoja na makafiri hao waliotajwa majina.

Yaani ataingia kwenye Jahannam na kupata adhabu kali. Ubey bin Khelef alikuwa ni mmoja wa wakubwa wa makafiri wa Makka. Katika vita vya Uhud, Mtume "sallallahu alayhi wasallam" alimuuwa kwa mkono wake. Imepokewa na Ahmad, Bayhaki na Darimy.

13. Anasema mmoja wa matabii wakubwa Abdulla bin Shakik "rahmatullahi alaih" (Wamesema masahaba, miongoni mwa ibada, ni sala pekee ambayo ukiiacha unakuwa kafiri) imepokelewa na Tirmizi. Abdulla bin Shakak amepokea hadithi kutoka kwa Umar, Ali, Uthman na Aisha "radiyallahu anhuma". Amefariki 108 hijria.

14. Anasema Abu Derda "radiyallahu anh" dardaa. mmoja kati ya watu niwapendao alinambia **(Hata kama utakatwa vipande vipande na ukaunguzwa motoni, basi usikubali kumshirikisha Allah na usiache sala za fardhi. Mwenye kuacha sala za Fardhi kwa makusudi basi anatoka katika Uislam. Usinywe pombe. Pombe ndio ufunguo wa maasi yote.)** Inafahamika hapa kwamba kuacha sala kwa kuidharau na kutokuipa umuhimu kunamfanya mtu awe kafiri. Ikiwa hatosali kwa uvivu tu basi hatokuwa kafiri lakini atakuwa amefanya dhambi kubwa. Ikiwa itampita sala kwa sababu ya udhuru unaokubalika na uislam basi haitokuwa dhambi. Pombe humuondoa mtu akili. Mtu alieondokwa na akili anaweza kufanya ovu lolote.

15. Kutoka kwa Ali „radiyallahu anh" amesema mtume "sallallahu alayhi wasallam" (**Ewe Ali, mambo matatu usicheleweshe kuyafanya. Wakati sala ikifika Sali haraka. Maiti akishatayarishwa msalie haraka. Na iwapo atakapotokea mchumba wa uzani wake muozeshe binti haraka.)** Imepokewa na Tirmidhy "rahmatullahi alaih". Ili sala ya maiti isicheleshwe basi inafaa kusali hata katika nyakati ambazo ni karaha. Kusali.

[inafahamika hapa kwamba ni vyema kumuozesha binti kwa mtu wa uzani wake. Kuwa wa uzani wake haina maana kuwa tajiri au kuwa na mshahara mkubwa. Kuwa wa uzani ina maana mwanamme kuwa mwema, miongoni mwa ahli sunna, mwenye kusali, asiyelewa, kwa ujumla awe anafata Uislam na anaweza kuyakimu mahitaji ya nyumba. Wale wazee ambao wanataka mchumba awe tajiri tu na kumiliki nyumba basi hao wamewatelekeza binti zao na kuwatia hatarini. Binti nae pia lazima awe anasali, anavaa mavazi ya stara ya kisheria na hakai na wanaume wasio maharim zake.]

16. Kutoka kwa Abdulla bin Umar "radiyallahu anh", amesema mtume "sallallahu alayhi wasallam" (**Wale wanaosali mara tu baada ya kuingia wakati, basi wanapata radhi za Allah. Na wale wanaosali**

**mwisho wa wakati wa sala Allah anawasamehe).** Imepokewa na Tirmidhy “rahmatullahi alaih”.

Kwa madhehebu ya Shafii na Hanbali kusali mwanzo wa wakati wa sala kwa sala zote ni bora. Malik nae kauli yake imekaribiana na hii. Kwa madhehebu ya Hanafi, ni bora kuchelewesha sala ya asubuhi na isha, na sala ya adhuhuri iwapo joto litakuwa kali sana. [Kufuatana na kauli za maimamu wawili sala ya adhuhuri isaliwe kabla ya kuingia wakati wa sala ya laasiri. Sala ya laasiri na Isha kufuatana na imam Adham zisaliwe mara tu baada ya kuingia wakati wake, ndiyo ubora na umakini. Watu wachamungu wanakuwa makini katika mambo yao yote.]

17. Kutoka kwa Ummi Farwa „radiyallahu anha” amesema mtume “sallallahu alayhi wasallam” **(Amali iliyo bora ni sala inayosaliwa mwanzo wa wakati wake.)** Imepokewa na Ahmad, Tirmidhy na Abu Daud “rahmatullahi alaih”. Sala ndio ibada tukufu kulio zote na ikisaliwa mara tu wakati unapoingia inazidi utukufu.

18. Anasema Aisha „radiyallahu anhuma” (Hazijatokea mara mbili nikamuona mtume “sallallahu alayhi wasallam” amesali sala mwisho wa wakati wake.)

19. Kutoka kwa Ummu Habiba „radiyallahu anha”, amesema mtume “sallallahu alayhi wasallam” (**Mja muislam, ikiwa atasali sala zake za fardhi na akaengeza rakaa kumi na mbili za tatawuu (sunna), basi Allah atamjengea kasri katika pepo)** Imepokewa na **(Muslim)**. Inafahamika hapa kwamba sunna zinazosaliwa pamoja na fardhi kila siku, mtume “sallallahu alayhi wasallam” amezitaja kwa jina la tatawuu.

20. Mmoja wa matabii wakubwa, bwana Abdalla bin Shakik “rahmatullahi alaih” anasema: Nilimuuliza Aisha „radiyallahu anhuma” juu ya sala za tatawuu (nafila) za mtume “sallallahu alayhi wasallam akanambia (Rakaa nne za kabla na mbili za baada ya sala ya adhuhuri, rakaa mbili baada ya sala za magharibi na isha na rakaa mbili kabla ya sala ya asubuhi) Imepokewa na Muslim na Abu Daud “rahmatullahi alaih”.

21. Aisha „radiyallahu anha” anasema (Katika ibada ya nafila aliyoiendeleza sana mtume “sallallahu alayhi wasallam” ni sunna ya sala ya subuhi). Imepokewa na **(Bukhari)** na **(Muslim)**. Hapa Aisha amezitaja sala zinazosaliwa na fardhi tano kwa jina la nafila.

[Mwanazuoni mkubwa wa kiislam, mpambanaji mwenye nguvu wa ahli sunna dhidi ya wapotofu na wasio na madhehebu, muenezaji wa dini aliyoichagua Allah, mwenye kuvunja bid’a, mujahid imam Rabbany,

mujaddid alfu shani, Ahmad bin Abdulahad Faruki Sarhandy “rahamatullahi alaih” katika kitabu chake ambacho hakuna mfano wake katika maandishi ya kiislam **(Maktubat)**, juzuu ya kwanza barua ya 29 anasema:

Mambo ambayo Allah anayaridhia ni fardhi na nafila. Nafila hazina thamani zikifananishwa na fardhi. Kuisali sala moja ya fardhi kwenye wakati wake basi ni bora zaidi kuliko kusali sala za nafila kwa muda wa miaka elfu bila kupumzika. Hivyo ndivyo zilivyo aina zote za nafila kama sala, zaka, hija, funga, umra, dhikri na tafakur. Kutekeleza sunna na adab za ibada ya fardhi kuna thamani zaidi kuliko kutekeleza nafila nyengine. Siku moja amir-il muuminin Umar ul-Faruk „radiyallahu anh” alipokuwa akisalisha sala ya asubuhi kuna mtu hakumuona akauliza sababu ya kutokuwepo kwake. Akajibiwa kuwa huyo mtu yeye husali sana nafila za usiku. Pengine amechukuliwa na usingizi hivyo hakuweza kuja katika sala ya asubuhi. Akasema (Angelilala usiku kucha kisha akahudhuria sala ya asubuhi jamaa basi ingekuwa bora zaidi.) Inafahamika hapa kwamba wakati wa kutekeleza ibada ya fardhi, kuzichunga sunna zake na adab zake na kuacha makruh zake ni bora kuliko kuleta dhikri, tafakur na murakaba. Bila shaka kama haya yatafanywa pamoja na hizo adab na kuacha makruh basi faida kubwa inapatikana, lakini kama hayo yataachwa basi na haya pia yatakuwa hayana faida. Kwa mtizamo huo basi kutekeleza fardhi ya zaka hata kwa kutoa shilingi moja ni bora kuliko sadaka ya nafila ya shilingi elfu moja. Wakati wa kutoa hiyo shilingi moja kama utazingatia adab za kutoa mfano ukampa jamaa wa karibu basi hilo nalo lina fadhila zaidi kuliko hiyo sadaka ya nafila. [Hapa inafahamika kwamba kwa wale wanaotaka kusali sala za usiku basi ni lazima kusali sala za kadha. Maamrisho ya Allah huitwa **(Fardh)**, makatazo yake huitwa **(Haram)**, maamrisho ya mtume “sallallahu alayhi wasallam” huitwa **(Sunna)** na makatazo yake huitwa **(Makruh)** na haya yote kwa pamoja huitwa **(Ahkami islamiyya)**. Kuwa na tabia njema na kuwatendea mema watu ni fardhi. Miongoni mwa ahkam islamiyya ikiwa mtu ataikana lau moja au kutokuipenda basi atakuwa ni **(Kafir)**, **(Murtad)**. Mwenye kuziamini zote huwa **(Muislam)**. Muislam asietekeleza ahkamul islam kwa uzembe wake huwa ni **(Fasik)**. Fasik asietekeleza fardhi au asieacha haramu ataingia katika Jahannam. Hatopata ujira kwa suna anazozitekeleza. Mtu mwenye kuacha kutoa zaka ya shilingi moja basi hatopata thawabu za mamilioni anayoyatoa kama sadaka. Hapati thawabu kwa kujenga misikiti, hospitali, madrasa na anachotoa kwenye taasisi za kheri. Mtu ambae hakuswali sala ya isha basi sala

yake ya tarawehe haikubaliki. Ibada ambazo sio za fardhi wala wajib huitwa **(Nafila)**. Ibada za sunna ni Nafila. Kwa maelekezo haya basi, mtu mwenye kusali sala ya kadha huwa pia amesali sunna. Thawabu za kutekeleza fardhi na kuacha haramu ni nyingi kuliko za kutekeleza milioni ya Nafila. Mwenye kuacha fardhi au kufanya la haramu ataingia motoni. Ibada zake za nafila hazitomuokoa na moto. Mabadiliko yanayofanywa kwenye ibada huitwa **(Bid'a)**. Kufanya bid'a katika ibada ni haramu na ni sababu ya kuharibika kwa ibada. Hadithi sharif inasema **(mwenye kufanya bid'a hazikubaliki ibada zake)**. Mtu fasiki, mfano mwenye kumwachia binti yake au mkewe atembee bila ya stara ya kisheria, au mtu wa bid'a, mfano mwenye kutumia vipaza sauti kwenye ibada, haifai kusali nyuma yao, haifai kusikiliza hutuba zao wala kusoma vitabu vyao. Lakini ni vyema kuzungumza kwa upole na bashasha na kila mtu akiwa ni rafiki au adui. Haifai kuleta malumbano yasiyo na faida. Katika hadithi sharifu tunasoma kuwa **(Mjinga usimjibu)**. Ibada zinazidi kuutakasa moyo. Dhambi zinautia kiza moyo na kuufanya usipate mwangaza. Ni fardhi kwa kila muislam kujifunza nguzo za imani, fardhi na haramu. Kutokujua sio udhuru. Yani ni sawa na mwenye kujua ikawa hakutekeleza.] **(Maktubat)** ni kitabu kilichoandikwa kwa kiajemi. Hapa tumemaliza tarjuma yake. Imam Rabbani alikufa India mwaka 1034 hijria (1624 miladia).

Kufuatana na maelezo ya hapo juu inafahamika kwamba sunna za sala tano nazo ni nafila. Hizi kwa vile zinasaliwa na sala za fardhi kukamilisha mapungufu yake basi zina ubora zaidi. Ikiwa mtu anaamini umuhimu wa sala za fardhi na kujua kuwa ndio wadhifa wa mwanzo kwa muislam halafu akaacha kusali sala ya fardhi bila ya dharura maalum, basi huyo atakuwa amefanya dhambi kubwa. Atakuwa ndani ya moto pamoja na kina Firauni na Hamana. Sala za nafila yaani suna, hazitomuokoa mja na mzigo huu wa adhabu. Kwa hivyo ni fardhi kusali sala alizoziacha mtu. Kucheleweesha kulipa kadha pia ni dhambi. Hivyo ni wajibu kujiokoa na hizi dhambi zinazoengezeka kila siku. Kwa vile kusali kadha ni fardhi, thawabu zake ni nyingi kwa maelfu kuliko kusali sunna. Kutokana na hili, na kwa vile inaruhusika kuacha suna kwa dharura, kila muislam anatakiwa alipe sala alizoziacha bila ya udhuru badala ya sala za sunna za nyakati nne. Kwa vile sunna ya sala ya asubuhi imetajwa kuwa ni wajib na baadhi ya wanazuoni, hivyo haitofaa kulipa fardhi badala yake. Kwa mtindo huu sala za kadha zitasaliwa kila kipindi ili kujiokoa na mzigo wa madhambi. Baada ya sala za kadha kumalizika ataendelea kusali sala za sunna. za sala tano. Kwa sababu kuacha suna kwa kuendelea hali ya kuwa huna udhuru ni

dhambi ndogo. Yule ambae atazibeza na kuona kuwa suna hazina umuhimu basi huyo atakuwa kafiri.

Pamoja na kwamba ni fardhi kuharakisha kuisali sala ambayo haikusaliwa kwa wakati wake, kwa vile sala zilizompita mtu kwa udhuru hazina dhambi, basi kuichelewesha kidogo ukapata kusali suna kwa mujibu wa wanzuoni wa Hanafi hili wamesema linajuzu. Ila hii haina maana kwamba inajuzu pia kwa sala zilizoachwa bila ya udhuru. Vile vile kusema jaiz haina maana kuwa ni wajib au kuwa ni vizuri. Kuna vitu vingi ambavyo vimeambiwa kuwa ni jaiz lakini vinajulikana kuwa makruh. Mfano makafiri walio chini ya dhima inajuzu kuwapa **(Zakatul fitri) i**ngawa inajulikana kuwa ni makruh.

**Sali sala zako, mkono usiguse haramu,**
**Usitegemee Maisha marefu duniani!**
**Shikamana na sala tano ukiwa kijana!**
**Utavuna unachopanda kwenye shamba la peponi.**

**Watu wawili hawakumbuki mauti,**
**Hutenda haramu na kuacha sala!**
**Siku itafika, mikono haishiki,**
**Hautoweza sema, ulimi usiomtaja Allah!**

## KUTOA ZAKA

Dalili ya kufaradhishwa zaka ni aya ya arobaini na tatu na aya ya mia na kumi ya Suratul Bakara.

Haijuzu kuwapa zaka aina kumi na mbili za watu.

Mwenda wazimu, maiti kwa ajili ya sanda yake, Kafiri, matajiri, jamaa waitwao usul na furuu, mke, mtumwa, mukataba (huyu ni yule mtumwa ambae ataachiwa huru baada ya kumpa mmiliki wake kima fulani cha pesa), Mudabbara (mtumwa ambae atakuwa huru baada ya bwana wake kufa). Kuna hitilafu juu ya swala la mke kumpa mume zaka, ila lililo sahihi zaidi ni kuwa asimpe.

Na ikiwa mtu atatoa zaka kwa mtu anae mdhani ni wa mbali lakini baadae akagundua kuwa ni mwanawe, au alimpa mali akidhani ni muislam baadae akagundua kuwa ni kafiri kilicho sahihi zaidi ni kuwa hatolipa tena.

Zaka inawajibika kupewa watu wa aina nane:

1- Maskini kama inavyokubalika katika dini.

2- Fakiri ambae hamiliki nisab ya ibada ya kuchinja.

3- Muislam mwenye deni.

4- Mwenye kufanya kazi ya kukusanya mali(mshahara wake)

5- Mwenye uhitaji akiwa njiani kwa ajili ya jihadi au hija

6- Yule ambae atakuwa muhitaji akiwa ugenini, hata kama ni tajiri mjini kwake.

7- Mali anyoihitaji mtumwa kumpa mmiliki wake ili amuachie huru.

8- Makafiri waliopewa jina la muallafa kulub ambao kwa sasa hawapatikani.

Mtu ambae ana ziada juu ya kile cha kutumia nyumbani lakini ni chini ya mali ya kununulia nisab ya mnyama wa kuchinja basi huyo huitwa **(Fakiri)**. Mtu yeyote ambaye mshahara wake una mpa uzito kuendesha nyuma, bila ya kujali anapata kiasi gani, basi anajuzu kuchukua zaka na si lazima kwake ibada ya kuchinja na zakatil fitri. Mwenye kusoma au kusomesha elimu ya dini hata kama atakuwa na mali ya kutosha mahitaji ya nyumba kwa miaka arobaini, basi bado anaweza kuchukua zaka. Pesa za zaka hazitumiki kwa kujengea msikiti, jihadi au hija. Hazitolewi kwa ajili ya sanda ya maiti. Huwezi kumpa zaka mtoto mdogo wa Tajiri, mama yako, baba yako, watoto wako, na mke. Ni thawabu zaidi kuwapa zaka ndugu zako, mke wa mwanao, mume wa mwanao, baba na mama wa mkeo, baba mdogo, mjomba, shangazi na mama mdogo. Fakiri atapewa chini ya nisab. Ila kama atakuwa na mke na watoto basi atapewa zaidi ila isipite kiwango cha nisab kwa hisabu ya kila mmoja wao. Zaka hapewi mtu anaejulikana kufanya israf au kutumia kwenye haramu. Masayyid (watokanao na ukoo wa mtume "sallallahu alayhi wasallam") kwa sasa wanaweza kupewa zaka kwa sababu hawawezi kupata sehemu yao itokanayo na ghanima (mali iliotekwa kwenye vita vya kiislam).

Kuna masharti sita ya kuifanya zaka iwe fardhi:

1. Kuwa muislam.
2. Kuwa baleghe.
3. Kuwa na akili.
4. Kuwa huru.
5. Kumiliki mali halali iliyofikia nisab ya zaka.
6. Mali aliyonayo iwe imepita uhitaji wake na madeni yake.

[Mtu ambae tayari ameshawajibikiwa na zaka katika mali yake, asipotowa zaka, au mwenye deni la mtu akawa halilipi badala yake akawa anatoa sadaka na kutoa kwenye njia za kheri, basi hatopata thawabu bali atapata dhambi. Ni fardhi kwake kutoa zaka na kulipa deni lake. Katika **(Hadika)** juzuu ya pili ukurasa wa 635 na **(Barika)**

ukurasa wa 1369 anasema mtu ambae anatumia pesa zake katika mambo ya haramu na yule mwenye kufanya israfu haijuzu kuwapa zaka. Kwa sababu kusaidia haramu ni haramu.]

Isiwe kuna hali ya kwamba mwenye kutoa zaka bado atafaidika na kile alichokitoa. Mke na mume wakipeana zaka manufaa kwa mtoaji yanakuwa hayakukatika kikamilifu. Kama zilivyo ibada zote zaka vile vile inahitaji nia. Zaka lazima iwe ni ziada juu ya deni na mahitaji ya lazima na ni lazima ifikie **(Nisab)**. Nisab ya dhahabu ni mithkal 20 (96 gram, sarafu 13.3). Nisab ya fedha ni dirham 200 (672 gram). Ili kutoa zaka iwe fardhi, baada ya mali kufikia nisab, inalazimika ipitiwe na muda wa mwaka mmoja wa hijria. Kufanya hila ya kisheria kabla ya mwaka kukamilika ili kuzuia zaka isiwe fardhi kufuatana na imam Muhammad hilo ni makruh lakini kwa Abu yusuf sio makruh. Kwa sababu itakapokuwa fardhi kutokuitii ni dhambi na kuepuka dhambi ni kutii. Fatwa imekwenda na kauli ya Imam Muhammad.

**Mali ya zaka** maana yake ni mali yenye kuongezeka. Kuna aina nne ya mali za zaka. Wanyama wenye miguu minne wenye kulishwa kwenye mashamba ya malisho wakiwa majike na madume au majike watupu. Mali iinayouzwa nakununuliwa kwa ajili ya biashara. Dhahabu na fedha. Mazao ya chakula yanayotoka kwenye ardhi. Iwapo wanyama waliopo kwenye shamba la malisho ni madume watupu au nyumbu na punda hawa hawalazimu kutoa zaka. Ndama wanapopatikana pamoja na wanyama wakubwa basi nao wataingizwa katika hesabu ya zaka. Inajuzu kutoa thamani ya zaka kwa kulipa zaka ya ushur, kulipia kafara au kulipa zakatul fitri. Kwa madhehebu ya shafii hayo hayajuzu. Iwapo mali itaangamia baada ya kuwa wakati wa zaka umefika basi fardhi inaanguka. Ikiwa mtu ataiangamiza hapo fardhi haitoondoka.

Wakati muislam, baleghe mwenye akili, anapomiliki mali kwa njia ya halali, ikafikia nisab na ikapitiwa na mwaka, akatoa sehemu maalum ya hiyo mali na kumpa muislam mmoja au zaidi kutoka katika aina nane zilizoainishwa basi hio huitwa Zaka. Mtu anaepewa lazima awe muislam. Milki kamili maana yake ni kwamba inawezekana na inajuzu kutumiwa kwake. Mali inayonunuliwa baada ya kukubaliana inakuwa tayari umeimiliki ila kama bado hujaipokea hutoweza kuitumia, kwa hivyo huko si kumiliki kwa ukamilifu. Mali iliyopatikana kwa wizi , ujambazi au unyang anyaji, riba, rushwa, kamari, kupiga ala za muziki na kuimba, kuuza pombe huitwa mali ya kikhabithi. Mali hizi hazifai kutolewa zaka kwa sababu alizonazo hana umiliki mkamilifu. Inafaa zirejeshwe kwa wamiliki wao na kama wamekufa wapewe warithi wao

na kama hawapo basi wapewe mafakiri waislam. Iwapo **mali ya kikhabithi** zitachanganyika zenyewe au zikachanganyika na mali za halali hii huitwa Milki ya kikhabithi. Haifai kumpa mtu au kutumia milki ya kikhabithi na kwa vile hana umiliki mkamilifu basi haifai kutolewa zaka. Hii baada ya kutoa mfano wa ile mali ya habithi au kima chake kutoka katika mali yake ya halali au zaka yake akawalipa wenyewe hapo milki ya kikhabithi itakuwa halali kutumia na italazimu kuhesabiwa katika nisab ya zaka. Ikiwa hana mali ya halali basi ataazima na kulipa. Pamoja na kwamba **milki ya kikhabithi** ni haramu kutumia au kumpa mwengine kabla ya kulipa, ila ikiwa ataiuza au kumzawadia mtu basi yule aliyenunua au kupewa haitokuwa haramu kwake. Katika zoezi la kurejesha milki ya kikhabithi, iwapo wenyewe hawajui au imechanganyika kwa kuchukuliwa kima tofauti kwa watu tofauti basi mali hiyo ataitoa sadaka kwa mafakiri wa kiislam.

Ikiwa fakiri ataamua kumrejeshea aliyempa kama zawadi, basi inajuzu kupokea.

Dhahabu na fedha hazitumiki katika hali zake za uhalisi (isiyochanganywa). Ikiwa itakuwa halisi kwa asilimia hamsini basi inalazimu kutolewa zaka na itahesabiwa kufuatana na uzito wake. Ikiwa kuna kabila mbili sokoni na zinatumika kwa kutilia thamani ile ambayo iko safi zaidi (ina vichanganyo kidogo) huitwa **(Jayyid)** (nzuri) na ile yenye vichanganyo zaidi huitwa **(Dhuyuf)**. Iwapo halisi itakuwa chini ya nusu, na ikawa inatumika katika biashara, na thamani yake ikawa sawa na nisabu ya dhahabu au fedha basi ni lazima kutoa zaka yake.

Mazao yanyopatikana kutoka katika ardhi inayolimwa kwa maji ya mvua au mto, hata kama mazao yatakayopatikana yatakuwa kidogo au ikawa na matunda na mboga zenye kuharibika haraka, inalazimu zaka ya fungu moja kati ya kumi apewe mkusanyaji mwenye kazi hiyo. Yeye atauza na kupeleka pesa zinazopatikana kwenye **(Baytul mal)**. Ni farz kutoa wakati matunda yatakapopea, yatakapowiva au wakati yatakapovunwa. Ikiwa ardhi inamwagiliwa kwa mnyama au kwa chombo au mashine basi zaka ya mazao yake ni sehemu moja katika ishirini. Lazima itolewe kabla ya kutoa gharama zozote. Haijuzu kwa serikali kugawa hili fungu kwa kumpa mtoaji, kumsamehe au kulifuta. Asali inayotoka mlimani au kwenye ardhi ya ushru basi nayo hutolewa fungu moja kati ya kumi.

Kafiri aneishi chini ya dhima ya dola ya kiislam hapewi zaka, ila anaweza kupewa sadaka au kinacholipwa kafara na nadhiri na zakatul

fitri. Anasema katika **(Bahr)**. Kafiri asie kwenye dhima, iwe ni mwenye amani au vita na waislam, hapewi kutoka katika kinachotolewa kwa fardhi, wajib au nafila. Ni makruh kumpa fakiri ambae hana deni, kima kinachofika nisab au zaidi. Ikiwa huyu fakiri ana familia kumpa kima kwa wingi ambao kama itagawiwa kwa kila mmoja wao haitopita nisab basi itajuzu.

Inajuzu kuuza kitu na kupokea thamani kwa pesa. Pesa ni zile sarafu zisizo za dhahabu au fedha na zile noti, ambazo kiada zinatumika kulipia thamani na hazihitajiki kuoneshwa. Ikiwa hazikubaliki tena katika soko basi mauzo yanayolipiwa nazo hayatakuwa sahihi, kufuatana na Imam adham. Kufuatana na maimamu wawili, Abu yusuf na Imam Muhammad "rahmatullahi alaih" mauzo hayatakuwa batil lakini yatalipwa kwa pesa nyengine zenye thamani sawa. Iwapo mtu atakopa na baadae pesa zikawa zimetolewa sokoni basi kufuatana na Imam adham atalipa kwa pesa nyengine kwa kiasi cha pesa alizochukuwa na kufuatana na maimamu wawili atalipa kwa thamani sawa ya dhahabu au fedha. Kununua kwa kutumia pesa ambayo haiko sokoni inalazimika kuionesha kwanza. Mali iliyooneshwa wakati wa mauzo inakuwa tayari imeshaainishwa hivyo ni lazima kuitoa hiyo hiyo bila kubadilisha. Iwapo mtu atakwenda kwa mbadilisha pesa na akampa fedha yenye uzito wa dirham moja na wakakubaliana amlipe pesa zenye thamani ya nusu dirham ya fedha ile, na nusu dirham ya fedha ile iliyobaki atampa fedha iliyopungua uzito kidogo (isiyotimia nusu) basi mauzo hayo hayatakuwa sahihi. Hii ni kwa sababu kuuza fedha yenye uzito wa nusu dirham ukalipwa uzito chini ya huo ni riba. Na ikiwa atamwambia Nipe pesa kwa nusu ya hii na nipe nusu dirham ya fedha iliyopungua kidogo kwa nusu iliyobaki basi mauzo ya pesa yatakuwa sahihi. Na kama atamwambia Nipe pesa zenye uzito wa nusu dirham na unipe fedha yenye uzito wa nusu dirham iliyopungua kidogo, nami nikupe fedha yenye uzito wa dirham moja, basi mauzo hayo yatakuwa sahihi. Kwa sababu fedha yenyeuzito uliopungua nusu dirham itakuwa imeuzwa kwa fedha yenye uzito sawa nayo. Na pesa zitakuwa zimelipwa kwa fedha yenye uzito wa nusu dirham na kuzidi kidogo. Japokuwa pesa na fedha zilizotolewa zinatofautiana kiuzito , hakuwi na tatizo kwa sababu ni vitu viwili tafauti.

Anasema katika **(Beaiyus sanai)**. Mali inayotolewa zaka iwe ile ile au ya jinsi nyengine ya mali inayohusu kutolewa zaka (haitofaa kumpa maskini nguo, viatu, unga au mafuta badala ya dhahabu). Mali ya zaka ima itakuwa ni Ayn au Dayn. Mali ambayo ni Ayn hupimika kwa uzito au ujazo. (Volume) au ni kitu kisichopimika. Ikiwa ni kitu kisichopimika

basi itakuwa ni mnyama au vitu vya biashara. Ikiwa ni mnyama basi kufuatana na kiwango kilichotajwa na nass atatoa yule aliye katika hali ya wastani. Na ikiwa atatoa wa hali ya chini basi atalipia ile tofauti iliyopo na yule wa hali ya wastani, kwa kutoa dhahabu au pesa. Ikiwa atatoa thamani ya mnyama basi itatolewa kwa yule wa wastani. Na kama atatoa kwa thamani ya alie chini basi tafauti italipwa kwa fedha au dhahabu. Inajuzu kutoa kondoo mkubwa badala ya kondoo wawili wa wastani iwapo thamani itakuwa sawa, kwa sababu mali zisizokuwa za riba thamani zake zinaweza kuzingatiwa.

Katika vitu vya biashara hutolewa fungu moja ya mafungu arobaini kama ilivyotajwa kwenye nass. Ikiwa itatolewa kwa jinsi isiyokuwa yenyewe, ikiwa kile kizuri kikatolewa mbadala kwa cha hali ya kati au hali duni basi tofauti inalazimika kulipiwa. Hivi ni vitu ambavyo haviwezi kupimika kwa uzito au ujazo (volume). Hivi havina riba katika wingi wake. Mfano inajuzu kutoa nguo mbili za kawaida badala ya moja iliyo nzuri. Ikiwa atatoa kwa jinsi isiyo yake basi italazimika kulipa tofauti itakayojitokeza. Ikiwa kitu kinachotolewa zaka kinaweza kupimwa kwa uzito au ujazo basi hutolewa fungu moja katika arobaini. Na ikiwa itatolewa kwa mali nyengine ya kabila tofauti na inayohusu kutolewa zaka (siyo yoyote tu) basi itazingatiwa thamani yake iwe sawa. Na iwapo atalipia kwa mali nyengine ya kabila ile ile basi uzito ndio utakaozingatiwa na wala sio thamani kufuatana na kauli ya mashekhe wawili. Mfano ikiwa kilo mia mbili za ngano nzuri sokoni zina thamani ya dirham mia mbili, basi inafaa kutoa zaka kilo tano za ngano ya kawaida. Na iwapo dirham mia mbili za fedha iliyo Jayyid inalazimika kutolewa zaka, basi itajuzu kutoa dirham tano za fedha iliyo Dhuyuf. Kanuni hii pia inaweza kutumika katika kuondoa Nadhiri.

Fedha na dhahabu ni thamani kwa udhati wake. Vimeumbwa ili kutumika kuwa thamani. Havina matumizi ya moja kwa moja kwa mahitaji ya binaadamu. Ni njia ya kufanyia biashara kwa vitu vyengine. Vitu vyengine vimeumbwa viwe na thamani lakini pia vitumike kwa mahitaji mengine. Tarjuma kutoka **(Bedayi)** imemalizika hapa.

Vitu ambavyo binaadamu anavihitaji ili aweze kuishi kwa utulivu na kutekeleza Uislam wake basi hivyo huitwa vitu vya uhitaji, navyo hubadilika kutegemea na wakati na hali. Vile ambavyo si lazima kwa utulivu wa maisha lakini akawa binaadamu anavihitaji kwa hamu zake, kwa kujiremba au kujipatia heshima basi hivyo huitwa vitu vya mapambo. Dhahabu na fedha si katika vitu vya mahitaji. Ni vitu vya mapambo. Inajuzu kwa wanaume kutumia mapambo wakiwa nyumbani au njiani na kwa wanawake wakiwa nyumbani tu.

Inafahamika kwamba pesa zilizo sokoni ni mali ya biashara kila wakati. Zile ambazo zimetimia thamani ya nisab ya dhahabu ya thamani ya chini iliyo sokoni, basi zitalazimu kutolewa zaka. Kufuatana na maimamu wawili, nisab ya mali za biashara zitahisabiwa kwa kuzingatia dhahabu au fedha. Itatizamwa ile iliyo maarufu zaidi sokoni. Zaka itatolewa kwa moja ya arubaini ya kitu husika au thamani yake ya pesa. Fakiri atatumia hii kuwa ni mahitaji ya lazima. Pesa ni thamani inayotumika badala ya dhahabu na fedha. Inaweza ikatengenezwa kama sarafu kwa shaba na chuma au karatasi ya noti. Hivyo pesa za noti ni thamani inayolazimu kutolewa zaka. Ila hizi thamani yake si ya asili kama dhahabu na fedha. Thamani yake inategemea namna ilivyopewa na serikali husika Huzipa thamani na kuziondolea thamani na hapo huwa hazina thamani tena. Na zinatoka katika mali zenye kulazimu zaka. Anasema Ibn Abidin (Thamani ya mali ya biashara inaweza kuhesabiwa kwa kutumia pesa zilizochapishwa ikiwa ni za dhahabu au fedha ambazo kwa kawaida ndizo zinazotumika sana kwenye biashara. Ikiwa itahesabiwa kwa fedha na ikawa na thamani ya dirham mia mbili na arubaini, na ikihesabiwa kwa dhahabu thamani yake ikawa mithkal ishirini, na thamani zote mbili zikawa zimefikia nisab mali hii italazimu kuitia thamani kwa fedha. Hii ni kwa sababu kwa ajili ya zaka inabidi itolewe dirham sita za fedha au nusu mithkal ya dhahabu na hapa kwa vile thamani yake iko sawa na dirmah tano za fedha basi faida kwa masikini inakuwa ndogo. (kwa vile mithkal ishirini za dhahabu na dirham mia mbili za fedha zinaonesha nisab sawa basi na thamani yake ni sawa) Sarafu ya dhahabu yenye uzito wa mithkal moja huitwa **(Dinar)**. (Sarafu zote za dhahabu za uturuki ni mithkal mbili na nusu ambayo ni gram 7.2). Ni wajibu kulipa zaka kwa pesa (za fedha au dhahabu) ambayo ilitumika kuhisabia nisab yake. Hii ni kusema kwamba nisab ya pesa za noti lazima ihesabiwe kwa kutumia sarafu ya dhahabu ya thamani ya chini kabisa inayotumika sokoni kwa biashara. na zaka yake lazima itolewe kwa dhahabu. Kwa vile fedha haitumiki tena kama pesa hivi sasa. Zaka ya noti za karatasi italipwa kwa metali yaani dhahabu iliyotumiwa kuhesabia nisab yake. Fungu moja kati ya arobaini haliwezi kulipwa kwa pesa za karatasi (noti) kwa sababu hizo karatasi zenyewe haziwezi kutumika kwa mahitaji yoyote muhimu. Pamoja na kwamba zinaitwa karatasi, itakuwa ni is`raf kuitumia pesa ya karatasi kwa matumizi mengine ya karatasi;na kufanya israf ni haram. Haifai vile vile kulipa pesa za karatasi kwa zaka ya pesa za karatasi ili zitumike kama pesa. Ili kutumia kama pesa inabidi kitumike kitu chenye thamani ya uhakika ambacho ni dhahabu.

Dhahabu inaweza ikalipwa kama sarafu au katika hali nyengine. Dhahabu ipo na inapatikana kila mahala. Iwapo mtu hatopata dhahabu sehemu alipo, basi atamtumia pesa rafiki yake anayeishi mji mwengine ili amnunulie dhahabu huko na aitoe sadaka kwa niaba yake. Ni ruhusa kwake kulipa baadae. Kwa vile kutoa zaka kwa pesa za karatasi ni rahisi, mtu akiacha kutoa kwa dhahabu kama ilivyoelezwa na vitabu vya fik`hi na akaamua kutoa kwa pesa za karatasi ambazo thamani yake ni ya kupewa na ya muda, halitokuwa jambo sahihi. Kuacha kufanya ibada kwa kufuata vitabu vya fik`hi na kutekeleza kwa ufahamu binafsi wa aya za Quran ni jambo la watu wasio na madhehebu walio waovu. Kinachofaa kuwaambia watu hawa ni kwamba (Mimi ibada zangu sizifanyi kwa ufahamu wako wewe wa Quran au sunna, bali ninazifanya kwa ufahamu wa maimamu wa madhehebu). Vitabu vyenye kutoa mafunzo ya hao maimam wanne huitwa **(Vitabu vya fik`hi)**.

Mmoja kati ya wanazuoni wa chuo kikuu cha Azhar Abdulrahman Jazairy aliongoza jopo la wanazuoni walioandika kitabu kiitwacho **(Alfikh alal madhahibil arbai)**. Kitabu hichi kimekusanya maalumati kutoka katika madhehebu yote manne na kimechapishwa cairo mwaka 1392 hijria sawa na 1972 miladia kikiwa na juzuu tano. Chini ya kichwa cha habari kinachohusu kutoa zaka ya pesa za karatasi imeandikwa (Wanazuoni wa fik`h wameona kuwa ni lazima kuzitolea zaka pesa za noti. Kwa sababu hizi pesa hutumika kwenye biashara kwa niaba ya dhahabu na fedha. Hizi zinaweza kubadilishwa kwa dhahabu au fedha kwa wepesi kabisa. Haiingii akilini kuwa mtu alie na pesa nyingi za noti kuwa asitoe katika nisab ya dhahabu na fedha na kuwa asizitolee zaka. Kwa hivyo wanazuoni wa fik`h wa madhehebu matatu wamekubaliana kuwa pesa za noti nazo zinalazimika kutolewa zaka . Wanazuoni wa madhehebu ya Hanbali pekee ndiye waliokwenda kinyume na hili. Kufuatana na wanazuoni wa madhehebu ya Hanafi, pesa za karatasi (ni karatasi ya ahadi ya deni iliyoandikwa) zinaweza kubadilishwa wakati wowote kuwa dhahabu au fedha hivyo zaka yake inatakiwa ilipwe mara moja. Kwa sababu kulipa zaka ya deni lililofikia wakati wake ni fardhi ikiwa dhahabu na fedha zitapatikana. Ikiwa hazijapatikana zaka inakuwa ni fardhi ila kutoa huwa bado si fardhi. Anaweza akasubiri mpaka akazipata hizo dhahabu au fedha kisha akalipa kwa idadi ya miaka iliyopita. Vyenginevyo anaweza kulipa kwa kulipa dhahabu au fedha aliyonayo kwa kila mwaka. Huwezi kutoa zaka ya dhahabu, kwa kutumia karatasi ya ahadi ya deni kwa kulipia zaka yake, atatoa moja katika arubaini ya dhahabu au fedha yenyewe baada ya kulipwa hilo deni lake. Kwa kila mwaka uliopita atatoa hesabu yake mbali na

kuwapa mafakiri. Atanunua sarafu za dhahabu zenye thamani ya chini sokoni au kwa uzito wake atachukua pete au bangili na kutoa kwa masikini.

Haijuzu kutoa zaka kwa mtu unaemdai pesa kwa kumwambia tu kwamba umempa zaka ila zaka hiyo inafuta deni lake kwa hivyo akubali. Hapa kwa kuwa hapakupita makabidhiano inakuwa wewe hukutoa zaka wala yeye hakulipa deni. Inatakiwa kwanza mwenye kupewa zaka apewe na apokee kisha ndio alipe deni. Ikiwa mwenye kudai haamini kuwa mdaiwa atamlipa deni lake baada ya kumpa hiyo zaka basi kuna njia iliyopendekezwa katika juzuu ya sita ya **(Fatawa Hindiya)**. Anasema Mwenye kudai anaweza katafuta mtu anaemuamini na akamtaka mwenye kudaiwa awe wakili wake katika kupokea zaka yake na kuitumia kwa kulipia deni. Baada ya kupewa uwakala yule mtu atakapopokea ile zaka tayari itakuwa ni mali ya huyo masikini. Hapo atamrejeshea huyo mtoaji kwa niaba ya masikini ili kulipa deni lake. Ikiwa mtu atakuwa na deni kwa zaidi ya mtu mmoja na ikawa mmoja wao anataka kumpa zaka ili alipie deni lake yeye, kwanza atampa fakiri zaka kiasi ya lile deni. Kisha atamsamehe deni lake . Kisha fakiri atatoa ile mali kama hadiya na kumpa huyo tajiri. Au fakiri anaweza kuazima mali kutoka kwa mtu na akampa zawadi huyu tajiri. Kisha Tajiri akaitumia mali ile kumpa zaka masikini, kisha akamsamehe na deni lake. Masikini ataichukua mali ile na kuirejesha alikoiazima. Pesa za zaka (na za kulipia nadhiri) hazitumiki ka mambo ya khayrat. Ili kuweza kufanya hivyo unaweza ukampa zaka fakiri kisha yeye akatumia kwa khayrat hizo. Hapa inafahamika kwamba ili kuweza kutoa zaka ya pesa za karatasi, baada ya kuzihisabu na kuzijua kima chake utaangalia thamani yake kwa sarafu za dhahabu. Kisha kufuatana na uzito wa hizo sarafu, utaazima mapambo ya dhahabu yenye uzito sawa na zile dhahabu halafu utatoa zaka kwa fakiri anaestahiki miongoni mwa watu wa karibu. Hapo fardhi ya zaka ya hizo pesa za karatasi itakuwa imekamilika. Baada ya hapo huyu fakiri aliepokea vitu vya dhahabu kwa ajili ya zaka atampa zawadi vitu hivi yule tajiri, nae atavirejesha kwa mwenyewe. Baada ya hapo yule tajiri atachukua zile pesa zilizotakiwa kutolewa kama zaka atampa huyo masikini na nyengine anaweza akafanyia mambo ya khayrat. Ikiwa huyu fakiri anataka kupata sehemu katika mambo ya kheri anaweza akamuuzia hizo dhahabu huyo tajiri kisha akampa uwakala na pesa za kumfanyia hayo mambo ya kheri.

Mmoja kati ya magwiji wa elimu za madhehebu manne mwanazuoni mkubwa Sayyid Abdulhakim Arsawi “rahmatullahi alaih”

anasema (Thamani ya pesa za karatasi ni thamani ya kupewa (si ya asili) Ikiondolewa inakuwa haipo na inakuwa haina thamani. Kutokana na hilo haijuzu kutoa zaka na zakatul fitri kwa kutumia pesa za noti. Zile zaka ambazo zilitolewa kwa kutumia pesa za karatasi inahitaji zilipwe kadha kwa kutumia njia ya kuzungusha. Ukiachilia zaka, ibada nyengine za mali zinalipiwa kadha kwa njia ya kuzungusha.)

Anasema katika **(Durrul mukhtar)**. (Wale waislam wapinzani walioasi serikali na kuinyakua dola, na wale masultani dhalim katika waislam, watakapochukua zaka ya wanyama na mazao na wakatoa kwa wale watu ambao Allah ameamrisha , basi hicho walichokichukua kitahesabika kuwa ni zaka. Na ikiwa watazitumia kwenye maeneo mengine basi hiyo sio zaka. Wale ambao zilichukuliwa kwao mali hizi basi watawajibika kutoa tena zaka hizi kwa kuwapa wanaostahili. Ikiwa watakusanya zaka ya vitu vya biashara au pesa basi haitosimama kama zaka.) kufuatana na mtizamo wa wengi kati ya wanazuoni. Na huo ndio mtizamo wa fatwa. Ama wengine wanaona kwamba itasimama kama zaka kwa sababu hao masultani dhalim ni waislam, na ikiwa kile walichokikusanya ni milki ya hao waliotoa, watazingatiwa masikini, kwa hivyo kile watakachopewa kwa nia ya zaka kitakuwa ni zaka. **(Ibn abidin)** anasema (pesa zinazotolewa kama kodi, ushuru na zenye majina mengine kama haya nazo zinaingia katika hukumu hii Ni sahihi wale waliosema kuwa hata kama itatiwa nia, haziwezi kuhisabiwa kama zaka. Hii ina maana kwamba hawa madhalimu hawana haki ya kukusanya mali hizo. Hivyo ndivyo fatwa inavyosema na yameandikwa hayo katika maandishi ya pembeni ya **(Tahtawy)**. Kama inavyofahamika hapa, zaka ya wanyama na ushur (mazao) itakuwa sahihi kama serikali inayokusanya ni ya waislam na itaigawa kwa watu stahiki kufuatana na vitengo vinne vya idara ya hazina **(Baytul mal)** Kufuatana na rai ya wanazuoni wengi, ushuru unaolipwa kwa serikali hauhisabiwi kuwa ni zaka ya pesa au mali. Kuna kauli ya wanazuoni kuwa itahisabiwa kuwa ni zaka ikiwa serikali ni ya waislam na hicho kinachotolewa kitatolewa kwa lengo la zaka. Ila chanzo cha ripoti hii ni dhaifu.

**Njoo ndugu yangu, usikatae, kuwa na insaf.**
**Umri wangu thamini , usiufanyie israfu**

**Ulinde moyo na matamanio ya nafsi**
**Kama jino lako, nje na ndani kuwa safi**

**IKiwa dhahabu itachanganywa na shaba**
**Je ataipenda sonara alieinunua?**

**Usijigambe kwa kuwa muhitimu wa chuo**
**Usizungumze bila kuzangatia**

**Pata mtu mwenye maarifa umsikilize,**
**Kwa hilo utapata kuifikia haki**

**Zamia kwenye bahari ya uhakika**
**Toa vito vilivyomo na uwe muwazi**

**Usidanganywe na wenye vyeti vya dini**
**Njia sahihi wameshakuonesha salafi**

## MLANGO WA FUNGA

**Yaliyo fardhi katika funga ni mambo matatu:**

1- Kutia nia.

2- Nia itiwe baina ya wakati wa mwanzo na wakati wa mwisho.

3- Kujizuia na mambo yanayotengua funga katika wakati unaostahiki funga, nao ni wakati wa kujizuia alfajiri hadi jua linapotua. Wakati wa imsak ni ule weupe wa alafajiri sadik (ya kweli) unapoonekana juu ya mstari wa ufuk dhahiri. Ikiwa mtu atajizuia na mambo yenye kufunguza hadi jioni bila ya kutia nia ya kufunga, huyo hatokuwa amefunga na atalazimika kuja kuilipa hiyo siku.

**Mambo yanayomfanya mtu afaradhikiwe na funga ni saba:**

1- Kuwa muislam. 2- Kuwa baleghe. 3- Kuwa na akili. 4- Kwa wale walio katika nchi za makafiri (darul harb)kupata taarifa kuwa funga ni fardhi. 5- Kuwa mkaazi. 6- Kutokuwa kwenye hedhi. 7- Kutokuwa kwenye nifasi.

Mambo sita yanaharibu funga:

Kula chakula, Kunywa kitu miongoni mwa vitu vinavyonywewa, Kufanya tendo la jimai, Hedhi, Nifasi, Kutapika matapishi yanayojaza kinywa. Kusema uongo, kusengenya, kubeba maneno na kuapa kiapo cha uongo na mfano wa vitu kama hivi huwa havifunguzi ila vinaondosha thawabu ya funga.

Watu sita wameruhusika kula katika siku ya funga:

1- Mgonjwa. 2- Msafiri. 3- Mwenye hedhi. 4- Mwenye nifasi. 5- Mwanamke mja mzito asipoweza kufunga. 6- Mwanamke anaenyonyesha ikiwa atakhofia mtoto kudhurika. 7- Mtu aliye mzee sana tena dhaifu.

Ni lazima kutia nia ya kufunga kila siku. Katika **(Hindiye)** anasema (nia hutiwa moyoni. Kuamka kula daku maana yake ni kuwa na nia).

Nia ziko za aina mbili. Aina ya kwanza ni ile inayotiwa kila siku kwa funga za Ramadhani, sunna au nadhiri muayyan. Hii hutiwa katika wakati ulio baina ya kuzama jua kwa siku iliyopita na wakati uitwao dahwai kubra wa siku inayotaka kufungwa. **(Dahwai kubra)** ni nusu ya mchana wa kisheria, yaani ni nusu ya muda wa kufunga wa siku nao hupatikana kwa.

$$\text{Fajr} + \frac{24 - \text{Fajr}}{2} \text{ Or Fajr} + 12 - \frac{\text{Fajr}}{2} = 12 + \frac{\text{Fajr}}{2}$$

Hii ni kusema wakati wa dahwai kubra ni nusu ya namba yenye kuonesha wakati alfajiri kufuatana na adhana. Ni kabla ya Zawal (kati ya siku) kwa urefu wa tofauti kati ya mchana wa kisheria na mchana wa jua kufuatia saa za kawaida. Hiyo tofauti ni sawa na nusu ya hissa-I-fajr ambayo nayo ni muda baina ya kuchomoza jua na alfajiri au wakati wa kujizuia. Kwa kuchelewa unaweza ukatia niya hadi wakati wa Dahwai kubra ikiwa hujala au hujanywa chochote baada ya wakati wa imsak(kujizuia)kuingia. Hairuhusiwi kutia nia baada ya wakati wa Dahwai kufika. Ikiwa atatia nia kabla ya imsak basi atatia nia ya kufunga kesho na kama atatia nia baada ya imsak atatia nia ya kufunga leo.

Aina ya pili ni kwa ajili ya kulipa kadha, kafara au nadhiri Mutlaq. Hizi funga tatu zinahitaji nia ya aina moja. Wakati wake ni kuzama kwa jua hadi kabla ya alfajiri sadik, yaani kabla weupe haujadhihiri mbinguni. Hairuhusiki kutia nia baada ya alfajiri kwa hizi funga tatu. Imeandikwa na Ibn Abidin katika sehemu ya mwisho ya mlango alioelezea sala ya kadha kwamba, wakati unalipa Ramadhan, masiku kadhaa ambayo hukuyafunga katika Ramadhan ya mwaka fulani, huhitajiki kuzitaja siku kwa majina yake au mpangilio wa zilivyoandamana. Kuna daraja tatu za funga kutegemea na watu wenye kufunga. Funga ya watu wasiosoma, funga ya watu waliosoma na funga ya manabii na maawliyaa. Wakati watu wasiosoma wanapofunga hujizuia na kula, kunywa na kufanya tendo la ndoa ila wanafanya makosa mengine. Waliosoma huepuka makosa. Manabii na mawalii hujizuia na yale yote yenye kutia shaka wakati wa kufunga.

Kuna aina tatu za Idi kufuatana na watu wanaoshereheka. Idi ya wasiosoma , Idi ya waliosoma na Idi ya manabii na maawliyaa. Idi ya watu wasiosoma huwa kwa kufungua na kula chakula cha asubuhi, na jioni hula na kunywa kila wanachokitaka na kusema hii ni Idi yetu. Idi ya watu waliosoma hufutari jioni kisha hukaa wakitafakari wakasema ikiwa mola wetu ametutakabalia funga yetu basi hii ndio Idi yetu, lakini

ikiwa hakututakabalia basi itakuwaje hali yetu. Idi ya manabii na mawalii ni ruuyatullah. Wao wamestahiki kupata rehema zake Allah.

**Aina za sikukuu kwa maumini wote ni tano:**

1- Iwapo malaika wa mkono wa kushotoni mwenye dhamana ya kuandika maovu, hatopata hata mambo matano ya kuandika.

2- Iwapo katika sakratul mauti malaika wema watakuja kumpa habari njema na kumwambia wewe ni mja wa peponi.

3- Iwapo kaburi lake atalikuta kuwa ni bustani miongoni mwa bustani za peponi.

4- Ikiwa siku ya kiama atafunikwa chini ya kivuli cha Arshurahmani pamoja na manabii, mawalii na wema wengine.

5- Ikiwa ataweza kutoa jawabu sahihi kwa masuala saba na akaweza kuvuka daraja la sirat, ambalo ni jembamba kuliko nywele na kali kuliko upanga, lenye kiza kizito na minyanyuko elfu, mishuko elfu na tambarare elfu. Masuala hayo saba ni kuhusu imani, kuhusu sala, kuhusu funga, kuhusu hija, kuhusu zaka, kuhusu haki za waja na kuhusu josho na kwenda haja.

Iwapo mtu alietia nia ya Ramadhan kabla ya imsak ataharibu Ramadhan yake kwa makusudi basi atalazimika kulipa na kutoa kafara. Hakuna kafara katika funga za nafila na za kadha.

Kafara ni. Kumuachia huru mtumwa, na kama asipoweza. Kufunga siku sitini kwa kufuatanisha, zilizo nje ya Ramadhani na zisizokuwa siku za haramu kufunga(siku za haramu kufunga ni siku ya mwanzo ya Idil fitry na siku nne za mwanzo za Idil udh-hia). Kisha atatakiwa pia kuzilipa siku alizofungua kufuatana na idadi yake. Na kama asipoweza. Atalisha fakiri sitini milo miwili kwa siku moja au atamlisha fakiri mmoja milo miwili kwa siku sitini au atampa kila maskini kiwango kinachototolewa kwa fitri.

Na kwa kila siku aliofungua atalipia siku moja.

Watu watano hawalazimiki kulipa kadha. Mgonjwa, msafiri, mwanamke anaenyonyesha, aliye mzee sana na dhaifu na yule ambae anahofia kuangamizwa na njaa au kiu. Hawa udhuru wao utakapoondoka watalipia siku moja kwa siku moja.

Katika yawmu shaka (siku inayotiliwa shaka kuwa ni Ramadhani au la) kuna aina ya nia zinazoweza kutumika.

Inaruhusika ingawaje ni makruh kutia nia ya kufunga siku ya Ramadhan au funga nyengine ambayo ni wajib au kufunga siku ya mwezi wa Ramadhan au funga nyengine ambayo ni nafila au isio wajib.

Nia nyengine ni ile ambayo haina makruh ni ile ya kunuia funga mutlaqa tu au funga ya shaaban, yaani funga ya nafila.

Haitojuzu nia ya mtu atakaesema “ikiwa Ramadhan nimefunga na ikiwa si Ramadhan basi sikufunga”

Ikiwa mtu atatia nia baada ya kuwa alfajri imeingia, kisha akala kabla ya kuingia mchana basi kwa rai ya Imam adham huyu halazimiki kafara, ila kwa rai ya maimamu wawili analazimika kafara. Kwa sababu amekula ndai ya wakati ambao bado anayo nafasi ya kutia nia ya funga. Lau kama atakula baada ya adhuhuri basi kwa maafikiano halazimiki kafara.

Iwapo mtu atakula siku moja moja kwenye Ramadhani tatu tofauti je atalipa kafara moja kwa zote au kila moja ina kafara yake?. Kuna hitilafu katika kuliendea suala hili ila lililo na nguvu zaidi ni kwamba atakuwa na kafara mbali kwa kila Ramadhani. Na iwapo mtu atakuwa anadaiwa funga na akabaki asiilipe hadi mwaka ukapita basi mtu huyo atakuwa ni mja wa dhambi.

Na iwapo mtu atakuwa anafunga funga ya kafara na ikaingia Ramadhani au sikukuu ya udh-hia, atalazimika kuja kuanza tena upya baada ya Ramadhani au Idi hiyo na zile siku alizozifunga mwanzo hazitahesabiwa.

Iwapo mtu ambae hakutia nia ya safari amekula kisha baadae ndio akatia nia ya safari, basi atalazimika kafara pamoja na kulipa. Safari haihalalishi kufungua saumu. Mtu aliefunga kama ataanza safari haifai kufungua. Msafiri ikiwa atatia nia ya kufunga usiku au wakati wowote kabla ya Dahwa I kubra, basi sio halali kwake kula siku hiyo. Na ikiwa atakula basi atatakiwa alipe bila kafara.

Kilicho halali kwa msafiri ni kutokuanza kuifunga siku tangu mwanzo. Ikiwa mtu atapoteza fahamu katika mwezi wa Ramadhan, basi atakuja lipa pale fahamu zake zitakaporudi. Iwapo atakuwa hana fahamu mwanzo hadi mwisho wa Ramadhani basi funga hiyo kwake itakuwa imeanguka na hatolazimika kuilipa.

Ikiwa mtu atasahau kuwa amefunga, akafungua saumu basi funga yake haikuharibika. Pale atakapokumbuka kuwa amefunga akadhani kuwa funga yake imeharibika na akaendelea kula basi atalazimika kulipa bila kafara. Lakini ikiwa baada ya kukumbuka akajua kuwa Ramadhani yake haikuharibika lakini akaamua kuendelea kula, huyo atalazimika kafara pamoja na kulipa.

Iwapo mtu aliyefunga atameza jasho lake, au akatafuna uzi wenye rangi na akameza ile rangi au akameza mate ya mtu mwengine au mate yake mwenyewe ambayo yalikwisha toka nje au akameza chakula kilicho katika pachiko za meno ambacho ukubwa wake ni kama punje ya mbaazi au akaingizwa dawa kwa sindano chini ya ngozi basi funga yake itaharibika na atalazimika kulipa bila kafara.

Iwapo mtu atameza kipande cha karatasi, gao la chumvi, chembe ya ngano au mchele basi funga itaharibika na atalazimika kulipa bila kafara. Kwa sababu gao la chumvi kwa kawaida haliliwi kama dawa wala kama chakula, kama ilivyo kwa dongo. Ama ikiwa atakula chumvi kidogo basi hiyo italazimu na kafara. Hayo yametajwa katika **(Ashbah).** Hii ni kwa sababu kima kidogo cha chumvi hutumika kama chakula na kama dawa vile vile.

Mtu ambae anafanya kazi kwa kutafuta maisha hali ya kuwa amefunga na akajua kuwa atapata maradhi basi haitofaa kufungua hadi atakapokua mgonjwa. Ikiwa atafungua basi atawajibika kulipa na kafara. Ili kuepuka kafara, kwanza atameza karatasi. Iwapo mwanamke mwenye uja uzito au mwenye kunyonyesha akajihisi kudhoofu na kupata uzito anaweza akafungua na atalazimika kulipa tu. Mtu asiye na udhuru na akaamua kuwa anakula kula ovyo tu katika mwezi wa Ramadhan huwa ni Murtad. (Fevziyye).

Iwapo mtu atatafuna tu chembe ya ufuta basi funga yake haitoharibika, lakini ikiwa ataimeza hali ya kuwa ameichakua au bila ya kuichakua basi funga yake itaharibika na atalazimika kulipa.

Funga ziko za aina kumi na tano. Tatu ni fardhi, tatu ni wajib, tano ni haram, na nne ni suna.

Funga za fardhi ni Ramadhan, funga za kadha na funga za kafara.

Funga za wajib ni nadhiri muayyan, nadhiri mutlak na kuikamilisha funga ya nafila uliyoianza.

Funga za haram ni siku ya kwanza ya Idil fitri na siku nne za Idil udh-hia.

Funga za sunna ni masiku meupe ya kila mwezi, funga ya nabii Daud, Jumatatu na Alkhamisi, siku ya Ashuraa, siku ya Arafa na siku nyengine tukufu. Masiku meupe ni tarehe 13, 14, 15 katika kila mwezi wa hijria. Funga ya Daudi ni kufunga siku moja na ukala siku moja.

**Kuna faida kumi na moja za kufunga:**

1- Huwa ni ngao ya moto.

2- Hupelekea kukubalika ibada nyengine.

3- Huwa ni dhikri ya kiwiliwili.

4- Inavunja kiburi.

5- Inaondoa kujivuna.

6- Inazidisha hushui.

7- Huwa ni thawabu katika mizani.

8- Kuridhiwa na Allah.

9- Akifa na imani huingia peponi mapema.

10- Huutia moyo nuru.

11- Huitia akili nuru.

Katika siku ya ishirini na tisa ya Shaaban jua linapozama, ni wajibu kuutafuta mwezi wa mwandamo wa Ramadhani upande wa magharibi. Iwapo mtu muadilifu, yaani asietenda madhambi makubwa, muislam wa ahli sunna, akiuona mwezi kwenye hali ya hewa iliyofunga atampa habari hakimu au walii. Ikiwa atakubali basi Ramadhani itaanza kila pahali. Katika sehemu isiyo na hakimu au walii iwapo muislam atauona mwezi basi Ramadhan itaanza katika sehemu hiyo tu. Kauli ya mtu wa bid'a na mtu fasik haitokubalika. Katika hali ya hewa iliyo safi basi ni lazima watu wengi watoe habari. Iwapo mwezi haukuonekana, shabani itakubalika kuwa ni siku thalathini kisha siku itakayofuata Ramadhani itaanza. Ramadhan haianzi kwa hesabu za kiastronomia wala kalenda. Katika vitabu vya **(Bahar)** na **(Hindiyya)** na **(Kadihan)** vinasema (Mtu alieshikiliwa mateka katika nchi za kikafiri ikiwa hajui Ramadhani kuanza kwake akafunga kwa kutumia kalenda, inaweza kutokea akaanza mapema kabla ya siku moja, akachelewa kwa siku moja au akaanza sawa sawa. Katika hali ya kwanza , atakuwa siku ya mwisho ya Ramadhani ameila sikukuu, na siku aloanza Ramadhani haikuwa Ramadhani. Katika hali ya pili, siku ya mwanzo ya Ramadhani atakuwa ameikosa, na siku ya mwisho atakuwa amefunga siku ya sikukuu. Katika hali zote mbili atakuwa amefunga siku ishirini na nane na atatakiwa kulipa siku mbili. Na katika hali ya tatu ambayo amefunga na kwa bahati ikatokea sawa, siku ya mwanzo na siku ya mwisho alizofunga zilikuwa na shubha. Siku za Ramadhani zinazofungwa hali ya kuwa kuna subha huwa hazisihi funga yake hivi huyu naye atalipia siku mbili. Hapa inafahamika kwamba wale wanaofunga kwa kufuata kalenda badala ya kutizama mwezi, wanawajibu wa kufunga siku mbili baada ya Ramadhani kwa nia ya kulipa. Suala la kutumia mahesabu kutafuta siku Ramadhani inapoanza, limezungumzwa kwa kirefu katika kitabu kiitwacho **(Saadati abadiya)**.

Ibni abidin “rahmatullahi alaih” anasema (Katika hali ya hewa iliyofunga, hata kama adhana itasomwa basi haifai kufungua mpaka pawe na ithibati kuwa jua limetua. Mtu yeyote atakaefutari kabla ya wakati wa kuonekana nyota nyingi basi atakuwa ameleta jambo mustahabu la kuharakisha futari. Wakati jua limeshazama na watu wakawa wanafutari katika sehemu fulani, wale walio maeneo ya juu, mfano juu ya mnara hawatakiwi kufutari ila baada ya kuhakikisha kuzama kwa jua. Katika vitabu vya astronomi, Katika jadweli ya **(Tamkin)** inaonesha kwamba wakati wa Tamkin hubadilika kutegemea na mnyanyuko. Wakati inapopangwa jadweli ya wakati wa sala huwa panatumika wakati wa Tamkin wa sehemu moja tu iliyo juu. Iwapo jadweli itatayarishwa bila ya kuzingatia wakati wa Tamkin basi wakati wa kuzama jua utatangulia kwa baadhi ya dakika. Wakati unaoonesha jua limezama kwenye jadweli, kiuhalisia jua litaonekana bado kuzama. Hivyo wale wanaofungua kwa kufuata kalenda zinazotayarishwa bila kuzingatia wakati wa Tamkin, funga zao zinakuwa ni batil.

## SHARTI ZA KUCHINJA NI TATU:

1- Kuwa muislam, baleghe mwenye akili.

2- Kuwa mkaazi.

3- Kuwa na mali yenye kutosha nisab ya kuchinja.

Kufuatana na nguzo, wanyama wanaochinjwa ni mbuzi na kondoo, ng’ombe na ngamia. Wanaweza kushirikiana watu saba kwa ng’ombe au ngamia mmoja. Akijitokeza mtu wa nane naye akasema anashiriki basi uchinjaji huo utakuwa fasid. Nisab ya kuchinja ni sawa na nisab ya fitra.

Anasema Ibn abidin “rahmatullahi alaih” iwapo yeyote kati yao hisa yake itakuwa chini ya moja katika saba basi wote itakuwa uchinjaji wao haukusihi. Hivyo inasihi kushirikiana na watu chini ya saba. Pamoja na kuwa kuingia katika ushirika baada ya mnyama kununuliwa ni sahihi, lakini lililo bora zaidi ni kuingia ushirika kabla kununuliwa mnyama. Mtu anaweza kushiriki kwa kununua hisa moja hadi sita kati ya hisa saba za mnyama Kisha watagawana nyama kufuatana na hisa zao. Ikiwa mmoja kati ya washirika atakufa basi warithi wake watawataka washirika wake wachinje kwa niaba yake na yao kwa sababu inajuzu katika Uislam kuchinja kwa niaba ya maiti. Ikiwa warithi hawakusema hivyo, hisa ya yule mtu haitohisabiwa kuwa ni ibada ya kuchinja hivyo wale wote walioshirikiana katika mnyama yule ibada yao haitosihi. Ikiwa mshiriki mmoja ni kafiri, au ikiwa mtu atashiriki kwa kupata nyama tu (sio kwa ibada) basi ibada ya washiriki wote wa mnyama

huyo haitosihi. Kwa sababu kila mshiriki analazimika kuwa na nia ya ibada ya kuchinja. Nia ya kafiri ni batil. Kutia nia ya kupata nyama ya kula pia haikidhi nia ya ibada ya kuchinja. Ikiwa mmoja atatia nia ya ibada ya kuchinja kwa ajili ya mwaka uliopo na wengine wakatia nia kwa ajili ya mwaka ujao, basi wale waliotia kwa ajili ya mwaka ujao nia yao itakuwa batili, na kuchinja kwao kutakuwa ni tatawwuu na watalazimika kuigawa nyama kama sadaka kwa masikini. Nia ya mtu wa kwanza ni sahihi ila hatoweza kula ile nyama kwa sababu hukumu ya kwamba nyama itolewe kama sadaka itakuwa imeenea kwa mnyama wote. Nia ya ibada ya kuchinja si lazima iwe kwa kuchinja kwa wajib, bali inaweza kuwa kwa sunna na nafila. Inaweza kuwa kwa ajili ya aina tofauti za wajib. Inaweza kuwa vile vile ni kwa ajili ya akika kwa ajili ya mtoto au mtu mzima. Akika ni kichinjo cha shukurani kwa ajili ya kuruzukiwa mtoto. Pia inawezekana kuchinja kwa ajili ya chakula cha harusi inayofanyika kwa njia za kisheria. Nayo pia ni sunna na shukrani. Ni bora kwa washirika wote kuwa na nia ya kuchinja kwa ajili ya Idil udh-hia. Kuchinja kwa ajili ya akika kufuatana na madhehebu ya Hanafi si sunna, ni mustahab au mubah. Mambo ya mustahab ni mambo ya kujikurubisha. Mubah vile vile kama itafanywa kwa lengo la kushukuru basi litakuwa na kujikurubisha. Kuna ada nyingi ambazo kama zitakwenda na nia basi huwa ni ibada. Mambo ambayo ni mubah yakifuatana na nia huwa ni utiifu. Suala la Akika limezungumzwa kwa kirefu katika kitabu kiitwacho **(Ukudud duriyya)** na **(Durrul muhtar)**.

## NGUZO ZA HIJA NI TATU:

1- Kutia nia ya hija wakati wa kuvaa ihram.

2- Kusimama arafa

3- Kufanya tawafu ya ziara.

Wakati wa mwanzo wa kusimama arafa ni tarehe tisa Dhul-hija baada ya jua kutenguka hadi siku ya pili wakati sawa na wa asubuhi. Kusimama arafa siku moja kabla au siku moja baada ya hija haitosihi. Mawahabi husherehekea sikukuu siku moja kabla, hata bila ya kuuona mwezi. Wenye kusimama arafa nje ya wakati wake hazitosihi hija zao.

Kuna aina saba za tawafu:

Tawafu ya ziara.

Tawafu ya umra (hizi mbili ni fardhi).

Tawafu kudum (ya utangulizi). Nayo ni sunna.

Tawafu ya kuaga.

Tawafu ya nadhiri nayo ni wajib.

Tawafu ya nafila.

Tawafu ya tatawuu ambayo ni mustahab.

Ni fardhi kutia nia kwa kuhirimia hija. Ni suna kuvaa vazi linaloitwa ihram. Ni wajib kuvaa nguo isiyoshonwa.

Kuna masharti manane kwa mtu kuweza kuhiji:

1- Kuwa muislamu.

2- Kuwa baleghe.

3- Kuwa na akili.

4- Kuwa na siha.

5- Kutokuwa mtumwa

6- Kuwa na mali iliyozidi mahitaji ya lazima.

7- Kufika wakati wa hija. Wakati wa hija ni arafa na siku nne za sikukuu. Muda wa njiani pia unaingizwa kwenye hesabu.

8- Ikiwa inatimia masafa ya Safari, basi inatakiwa kwa mwanamke asafiri na mumewe au maharimu wake (mwenye kukamilisha masharti haya nane, ni fardhi kwake kwenda kutekeleza hija, mara moja katika umri. Ikiwa atafanya zaidi ya mara moja hizo zinazofuata zitakuwa ni nafila. **(Ibada za nafila)** ni zile ambazo si fardhi wala sunna ila anazifanya mtu mwenyewe kwa mapenzi yake. Thawabu za ibada ya fardhi ikifananishwa na ile ya nafila ni sawa na mto na tone la maji lililo pembeni yake kwa uchache wake. Wanazuoni wa kiislam hawakuruhusu kwenda tena hija kwa watu ambao wako mbali na mji wa Makka. Abdulla Dahlawi qaddasallahu ruhahu katika barua ya sitini na tatu anasema(wakati uko safarini kwa ajili ya hija inakuwa ni uzito kutekeleza ibada sawa sawa. Hivyo Imam Rabbani katika barua yake ya 123 na 124 hakuridhia watu kwenda umra au hija ya nafila. Ikiwa hija ya nafila itamzuia mtu kutekeleza fardhi au kumzuia mwanamke na stara ya sheria basi itakuwa ni haram. Kwenda hija kama hio ni dhambi badala ya thawabu. Kwenda umra nako kuna hukumu kama hiyo.

Zaka hutolewa baada ya kukamilika nisab na kupitiwa na mwaka wa hijria. Wakati wa kutoa zaka ni tofauti kwa mtu na mtu. Ikiwa wakati huu utakuwa kabla ya wakati wa hija basi kwanza atatoa zaka na kilichobakia ataendea hija. Ikiwa wakati wa zaka utakutana na wakati wa hija, kwanza atakwenda hija kisha atatoa zaka ya kilichobakia.

## FARDHI HAMSINI NA NNE

Mtoto anapokuwa balegh na kafiri anapotamka **(neno la tawhidi)** yaani **(Lailaaha illallahu Muhammadun rasulullah)** hali ya kufahamu

maana na kuamini basi anakuwa ni **(Muislam)**. Kafiri husamehewa madhambi yake yote. Hawa waliosilimu kama ilivyo kwa waislam wengine wanatakiwa wajifunze sharti za imani, wazihifadhi, wajifunze maana yake na kusema kwamba wanayaamini yale yote yaliyomo katika Uislamu, yani yale yote yaliyofunzwa na Muhammad katika maamrisho na makatazo na kwamba yametokana na Allah. Baada ya hapo katika tabia na mambo yote atakayokutana nayo anawajibu wa kujifunza ni yapi yaliyo ya halali na yapi ni haram. Kulikataa lolote kati ya yale ya halali na yale ya haram , yani akikanusha kwa kutokulipa umuhimu, basi imani inaondoka na anakuwa Murtad. Yani katika haya aliyojifunza mfano mwanamke kujistiri stara ya kisheria kama hatopendezwa nalo basi atakuwa ni murtad. **(Murtad)** ikiwa hakutubia kuhusu jambo alilolikosea hawezi kuwa muislam, hata kama atasema **(La ilaaha illallah)**, na akatekeleza baadhi ya amri za Uislam kama kusali, kufunga, kwenda hija na kufanya hasanat na khayrat. Haya mazuri atakayoyafanya hayatampa faida yoyote huko akhera. Inabidi lazima alete toba na ajute kwa lile alilolipinga na kuto kuliamini.

Wanazuoni wa kiisalm wamechagua mambo hamsini na nne ambayo analazimika kila muislam kujifunza, kuyaamini na kuyatekeleza.

Hizi ndizo fardhi hamsini na nne:

1- Kujua kuwa Allahu taala ni mmoja na kutokumsahau yeye.

2- Kula na kunywa vilivyo halali.

3- Kutia udhu.

4- Kusali sala tano kila siku kwa wakati wake.

5- Kukoga ili kutakasika na hedhi na janaba kwa ajili ya sala.

6- Kujua kwa haki na kuamini kwamba riziki ya mtu Allah ameichukulia dhamana.

7- Kuvaa nguo safi zilizochumwa kwa halali.

8- Kufanya kazi hali ya kuwa umetegemea kwa Allah.

9- Kuwa na kinaa (kukinai)

10- Kumshukuru Allah kwa neema zake. Yaani kuzitumia katika sehemu zilizoamrishwa.

11- Kuridhia kadhaa (maamuzi) zinazotokana na Allah.

12- Kufanya subira kwenye misiba. Yaani kutokumsusia Allah.

13- Kutubia madhambi (kusoma istighfari kila siku.)

14- Kufanya ibada kwa ikhlasi.

15- Kujua kwamba mashetani wa kijini na wa kibinaadamu ni maadui.

16- Kuiweka Quran kuwa ndio hoja na dalili. Kuridhia hukumu zake.

17- Kuelewa kuwa mauti ni haki na kujitayarisha nayo.

18- Kuyapenda yale anayoyapenda Allah na kuyakwepa yale anayoyachukia. (hubbi fillah wa bughdhi fillah).

19- Kuwatendea wema baba na mama.

20- Kuamrisha mema na kukataza maovu.

21- Kuwatembelea jamaa walio mahram.

22- Kutokuifanyia khiyana amana.

23- Kumuogopa Allah daima na kukwepa kufanya yale ya haramu.

24- Kumtii Allah mwenye shani tukufu na mtume “sallallahu alayhi wasallam” wake. Yaani kuyafanya ya fardhi na kuyaacha ya haram.

25- Kuacha madhambi na kujishughulisha na ibada.

26- Kutokwenda kinyume na amri za Ulul amri.

27- Kuutizama ulimwengu kwa jicho la mazingatio.

28- Kuzingatia uwepo wa Allahu taala . Yaani sifa zake na vile alivyoviumba.

29- Kuulinda ulimi na maneno ya haramu na machafu.

30- Kuusafisha moyo kutokana na mapenzi ya dunia.

31- Kutokumdhihaki mtu yeyote.

32- Kutokuangalia ya haramu.

33- Kusema kweli katika hali zozote.

34- Kuyalinda masikio na kusikiliza ya haramu na maovu kama ala za muziki.

35- Kujifunza ya halali na haramu.

36- Kufanya uadilifu katika vipimo na mizani.

37- Kutokuwa na hakika ya kuokoka na adhabu ya Allah na kumuogopa daima.

38- Kuwapa zaka na kuwasaidia waislam mafakiri.

39- Kutokukata tamaa na rehema za Allahu adhimu shaan.

40- Kutokufuata matamanio ya nafsi.

41- Kuwalisha wenye njaa kwa kutaka radhi za Allah.

42- Kufanya kazi kwa kutafuta kadri ya riziki ya kutosha (yani kula, kunywa na makazi).

43- Kutoa zaka ya mali na ushur ya mazao.

44- Kutokumkaribia mke alie katika hedhi na nifasi.

45- Kuutakasa moyo kutokana na madhambi.

46- Kujiepusha na kiburi.

47- Kuihifadhi mali ya yatima ambae hajafikia baleghe.

48- Kutokuwa karibu na vijana wa kiume.

49- Kusali sala kwa wakati wake na kutokukiacha kipindi kikapita.

50- Kutokuchukua mali ya mtu kwa dhulma.

[Mwanamke uliyemuacha kumlipa mahari yake nayo ni katika haki ya mja. Kutokumlipa kunasababisha jazaa duniani na adhabu kubwa huko akhera. Miongoni mwa haki za mja zenye adhabu kali ni kutokuwaamrisha mema jamaa na wale walio chini ya amri yako. Kuacha kuwasomesha dini. Kuwazuia wao na waislam wengine wasijifunze au wasitekeleze dini yao kwa kuwatesa au kwa kuwafanyia hadaa, inafahamika hapa kwamba huo ni ukafiri na ni uadui kwa Uislam. Watu wa Bid'a na wale wasio na madhehebu ambao wanaibadilisha itikadi ya ahli-sunna, imani na dini kwa maneno yao na maandishi yao nao pia wanaingia kundi hili.]

1- Kutomshirikisha Allahu adhimu shaan.

2- Kuikimbia zinaa.

3- Kutokunywa pombe.

4- Kutokuapa kiapo cha uongo.

[Pombe, spiriti na vinywaji vyengine vyenje alkoholi vyote ni najsi nzito. Imeandikwa katika **(Bahrur raiq)** na **(Ibn abidin)** kwamba dongo linapochanganyika na maji na likafanya tope, basi mchanganyiko huo utakuwa safi ikiwa kimoja wapo ni kisafi, na kwamba kauli hii ndio iliyo sahihi na ndiyo iliyowafikiana na fat`wa. Pamoja na kwamba kuna wanazuoni wanaosema kwamba hii ni hoja dhaif, lakini imeandikwa katika **(Ibn Abidin)** na **(Hadiqa)** hata kama hoja ni dhaif, inaweza kutumika pahali penye uzito. Kwa hivyo ikiwa kitu kitachanganywa na alkoholi kwa kupatikana kitu chenye mahitaji mengine kama uturi, rangi, vanish na dawa basi mchanganyiko huo utakuwa safi. Imeandikwa na Suleyman Abdalla Shiridy "rahmatullahi alaih" katika sherehe yake ya kitabu kiitwacho **(Al Maafuwat)** kilichoandkwa na Molla Halil Shiridy "rahmatullahi alaih" kwamba kanuni hii pia inafuatwa katika madhehebu ya Shafii. Haitoifanya sala isiwe sahihi kama kuna uzito katika kuvisafisha. Vitu hivi ambavyo vinakubalika ni safi kwa sababu ya uzito tu, haijuzu kuvinywa pasipo na dharura. Pombe haiwezi kuwa safi katika hali yoyote. Kwa sababu alkoholi iliyotiwa kwenye pombe haikutiwa kwa sababu ya faida inayohitajika katika vitu vyengine vilivyomo, bali imetiwa kwa ajili ya kustarehesha. Kila inachochanganyika nacho ni najsi na ni haramu kunywewa bila ya dharura.]

## KUHUSU MADHAMBI MAKUBWA

Madhambi makubwa ni ya aina nyingi. Hapa tutayabainisha sabini na mbili.

1- Kumuua binadamu bila haki.

2- Kuzini.

3- Kufanya liwat. Ni haram kwa dini zote.

4- Kunywa pombe.

5- Kuiba.

6- Kutumia madawa ya kulevya.

7- Kuchukua mali ya mtu mwengine kwa nguvu.

8- Kutoa ushahidi wa uongo.

9- Kula mbele ya waislam katika mfungo wa Ramadhan bila ya udhuru.

10- Kutoa au kuchukua riba.

11- Kuapa sana.

12- Kuwaasi wazazi wawili na kuwapinga.

13- Kuacha kuunga udugu na mahram na jamaa wema.

14- Kukimbia katika vita.

15- Kula mali ya yatima bila ya ridhaa yake. Katika Saadat abadiyya ukarasa wa 1029 anasema (Mlezi wa yatima anaweza kutumia mali ya yatima katika mahitaji ya lazima ila hawezi kutoa sadaka akampa mwengine. Hawezi kuitolea fitra wala kuchinjia.)

16- Kupunguza katika mizani na vipimo.

17- Kuisali sala kabla au baada ya wakati wake.

18- Kumuudhi nduguyo muumini.

19- Kumsingizia mtume “sallallahu alayhi wasallam” kwa neno ambalo hakulisema, na kulitolea sanad.

20- Kuepuka kutoa ushahidi wa haki.

21- Kuchukua rushwa.

22- Kutoilipia mali zaka yake na ushur wake.

23- Kutokumzuia anaefanya munkar hali ya kuwa uwezo wa kumzuia unao.

24- Kumchoma motoni mnyama akiwa bado yuhai.

25- Kusahau kuisoma Quran baada ya kujifunza.

26- Kukata tamaa na rehema za Allahu adhimu shaan.

27- Kumfanyia khiana mtu, akiwa muislam au kafiri.

28- Kula nyama ya nguruwe ni haram.

29- Kumkashifu au kutokumpenda yeyote miongoni mwa masahaba wa mtume “sallallahu alayhi wasallam”.

30- Kuendelea kula hali ya kwamba umeshiba ni haram.

31- Mke kumkatalia mumewe tendo la ndoa.

32- Mke kutoka matembezi bila ruhusa ya mumewe.

33- Kumwita malaya mwanamke mwenye kujiheshimu.

34- Kupitisha maneno ya uchonganishi baina ya watu.

35- Kuonekana sehemu za utupu. (Kwa mwanamme ni baina ya magoti na kitovu. Nywele, mikono na miguu ya mwanamke ni katika utupu.) Kuangalia sehemu za utupu za mtu mwengine.

36- Kula aua kumlisha mwengine nyama ya mnyama aliekufa bila kuchinjwa. Mnyama mwenye kuchinjwa bila kufata maelekezo ya dini pia huwa ni kibudu na hafai kuliwa.

37- Kuifanya khiana amana.

38- Kusengenya.

39- Kufanya husda.

40- Kumshirikisha Allahu adhimu shaan.

41- Kusema uongo.

42- Kufanya kiburi.

43- Kumkwepesha mrithi urithi wakati uko katika maradhi ya kifo.

44- Kuwa bakhili.

45- Kuyapenda mambo ya kidunia ya haram.

46- Kutokuogopa adhabu za Allah.

47- Kutokuitakidi jambo la haramu kuwa ni haramu.

48- Kutokuitakidi jambo la halali kuwa ni halalali.

49- Kuamini unayoambiwa na wapiga ramli.

50- Kutoka katika dini na kuwa murtad.

51- Kumuangalia mke au binti wa watu bila ya udhuru.

52- Mwanamme kuvaa nguo za kike.

53- Mwanamke kuvaa nguo za kiume.

54- Kufanya dhambi katika Kaaba

55- Kuadhini na kusali kabla wakati haujafika.

56- Kwenda kinyume na kutotii amri za viongozi wa dola.

57- Kumfananisha mkeo na mama yako katika jambo la sehemu zao za maharam.

58- Kumtukana mama wa mke.

59- Kuelekezeana silaha.

60- Kula chakula kilicholiwa na mbwa.

61- Kusimulia kwa wema ulioutenda.

62- Wanaume kuvaa hariri.

63- Kudumu juu ya ujahili (kutokujifunza itikadi ya ahli sunna, fardhi zake, haram zake na mengine yaliyo ya lazima.)

64- Kuapa kwa jina lisilokuwa la Allah au lile lililokubalika na sharia ya kiisalm.

65- Kuikimbia elimu.

66- Kutokujua kuwa ujahili ni msiba mkubwa.

67- Kudumu katika kukariri kufanya dhambi ndogo.

68- Kucheka kwa mayowe bila ya dharura.

69- Kutembea na janaba mpaka ukapitwa na wakati wa sala.

70- Kumuingilia mke alie katika hedhi au nifasi.

71- Kuimba nyimbo zisizo na maadili. Kupiga ala za muziki.

Mwanazuoni mkubwa Mirza Mazhari Jani Janan "rahmatullahi alaih" katika kitabu kiitwacho **(Kalimati tayyiba)** kilichoandikwa kwa kiajemi anasema (kupiga na kusikiliza ala yoyote ya muziki ni haram kwa maafikiano ya kauli. Isipokuwa kupiga Nay(firimbi ya muanzi) ni makruh na kupiga dufu kwenye harusi ni mubah. Ikiwa Quran karim na adhana itasomwa kwa kughani na ikasababisha kubadilika maana au kukariri herufi basi itakuwa ni haram. Anasema katika **(Alfikh ala l madhahib)** (Kusoma adhana kwa kughani ni haram. pia haijuzu kusikiliza). Kusoma kwa sauti yenye uzani na maneno yenye uzani huitwa kughani na kusikiliza huitwa **(Simaa).**

Kughani ni kusoma kwa sauti yenye kuvutia. Kuna aina mbili za kughani katika Quran, maulidi adhana na kasida.

1- Kughani ambako ni sunna na kwenye kupelekea thawabu. Ni kusoma kwa kufuata elimu ya tajwid. Kughani huku kunaupa moyo na roho nguvu.

2- Kughani kulikokatazwa na kulokuwa ni haram ni kufuata kwa miangusho ya kimuziki. Kughani huku kunaweza kuharibu herufi, maneno na kubadilisha maana . Miangusho ya wasomaji hawa inapendwa na nafsi inayoamrisha maovu. Wako ambao nafsi zao huwazidi wakaanza kulia au kurukaruka. Hawana habari na maana ya yale yanayosomwa. Mioyo yao na roho zao zimeghafilika na hawawezi kuokoka na haya maradhi.

Katika **(Targhibul salaat)** ukarasa wa 162 na **(Barika)** ukarasa wa 1342 juzuu ya pili na **(Hadika)** juzuu ya pili ukarasa wa 589 (kupanda mnyama aliefungwa kengele kwa ajili ya kuburudika na mchezo tu ni makruh. Kwa sababu kengele ndio ala ya mziki ya shetani. Malaika

wema hawashuki kwenye msafara ambao kuna wanyama waliofungwa kengele. Na kama itakuwa kuna maslaha au manufaa maalum basi itafaa kupanda mnyama aliefungwa kengele.

Kusoma mashairi yasiyoendana na mafunzo ya dini na maadili mema, au kuyasoma katika sehemu zenye ala za muziki, pombe au mchanganyiko wa jinsia mbili, au mashairi yaliyosomwa katika mazingira haya kuyasikiliza kwenye redio au santuri, kusomwa mashairi na wanawake au vijana wa kiume imetajwa kuwa ni haram kwa kauli moja. Mashairi yanayofaa yanajuzu kusomwa sehemu inayofaa. Kama yatasababisha moyo kulainika basi pia husababisha rehema za Allah. Baadhi ya wanazuoni hawakuraghibisha sana kusikiliza hata haya yaliyo halali. Pamoja na kwamba wao hawakuvutiwa na usikilizaji wa mashairi haya , lakini hawakukataa rai za wenzao ambao wameona inafaa kusikiliza. Kusoma Quran, maulidi, kuleta sala za mtume “sallallahu alayhi wasallam” au ilahi (kasida) katika vikao viovu ni haram. Kusoma kwa ajili ya starehe itakuwa ni kufur. Anasema katika **(Durrul maarif)** ukarasa wa sita (ala za mziki, sauti za wanawake na sauti za vijana wadogo wa kiume ni haram. Kwa sauti nyengine zisizokuwa hizi, kusoma na kusikiliza mashairi ni mubah.

72- Kujiua. Hii ni dhambi kubwa kuliko kumuua mtu mwengine. Adhabu ya Jahannam itamjia kaburini. Ikiwa mtu ataleta toba kabla ya kufa basi dhambi zake atasamehewa. Hatopata adhabu ya kaburi. (Toba ya sala zilizoachwa ili ikubaliwe, inalazimu kuzisali hizo sala. Anapoanza kuzilipa inakuwa sawa na kwamba amenuia kuendelea kuzilipa kwa uhai wake wote. Kwa nia hiyo basi deni lake la sala lote atakuwa amesamehewa. Na kwa namna hiyo hiyo kafiri atakaye amini, au mtu wa bid’a alie katika itikadi potofu, ikiwa atatubia kwa kufru yake na itikadi zake potofu, basi anakuwa ametia nia ya kutorejea katika kufur na itikadi potofu hizo na kutoingia katika matendo maovu yaliyopo hivi sasa. Kwa nia hiyo basi husamehewa hayo yote.)

## SEHEMU ZA UTUPU NA STARA YA MWANAMKE

Katika kitabu kiitwacho **(Ashiiatulamaat)** mwanzoni mwa mlango wa ndoa anasema:

1- Imehadithiwa na Abu Hurayra „radiyallahu anh” kwamba alikuja mtu kwa mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allah akasema (Ninataka kuoa binti wa kiansari) Mtume “sallallahu alayhi wasallam” akamwambia **(Kamuone huyo binti kwa sababu, katika macho ya kabila la kiansari kuna kitu.)** Imepokelewa na Muslim. Kumuona mara moja mwanamke unaetaka kumuoa ni suna.

2- Kutoka kwa Abdulla ibn Masud “radiyallahu anh” amesema; amesema mtume “sallallahu alayhi wasallam**” (Wanawake wasiwahadithie waume zao uzuri na wema wa wanawake wenzao wanaokutana nao kwani hilo linakuwa ni sawa na huyo mwanamme kumuona huyo mwanamke.) (Bukhari)** na **(Muslim)**.

3- Kutoka kwa Abusaid Khudhry “radiyallahu anhu”, amesema mtume “sallallahu alayhi wasallam” **(Mwanamme asiangalie utupu wa mwanamme mwenziwe na mwanamke asiangalie utupu wa mwanamke mwenziwe)**. Hapa inaonekana kwamba kama ambavyo ni haramu kwa mwanamke na mwanamme kuangaliana tupu zao basi ni hivyo hivyo kwa mwanamme na mwanamme mwenziwe na mwanamke kwa mwanamke mwenziwe. Utupu wa mwanamme mbele ya mwanamme mwenziwe na mbele ya mwanamke ni baina ya kitovu na magoti. Sehemu hiyo pia ndio utupu wa mwanamke mbele ya mwanamke mwenziwe. Utupu wa mwanamke mbele ya mwanamme wa mbali ni mwili mzima ila uso na viganja. Ndio maana mwanamke huambiwa ni Awrat(utupu) Iwe ni mwanamke wa kikafiri au wa kiislam; ni haram kuuangalia uso wake kwa matamanio, na ni haramu kuziangalia sehemu zake za utupu hata kama si kwa matamanio.

4- Kutoka kwa Jabir bin Abdalla “radiyallahu anhu”; amesema mtume “sallallahu alayhi wasallam” **(Msipitishe usiku kwenye nyumba ya mwanamke wa mbali)**.

5- Kutoka kwa Akaba bin Amir “radiyallahu anhu”, amesema mtume “sallallahu alayhi wasallam” **(Msikae na wanawake wa mbali ndani ya chumba kimoja. Mwanamke kukaa na shemegi yake au mtoto wa shemegi yake ni sawa na kuelekea mauti)** yaani huwa ni sababu ya fitna.

6- Kutoka kwa Abdulla bin Masud “radiyallahu anhu”; amesema mtume “sallallahu alayhi wasallam” **(Mwili wa mwanamke ni utupu.) yani** ni lazima ajifunike. **(Mwanamke anapotoka nje, shetani huwa haachi kumuangalia)** yaani anamtumia yeye kama mtego wa kuwategea wanaume na kuwaingiza kwenye dhambi.

7- Kutoka kwa Burayda “radiyallahu anhu”, mtume “sallallahu alayhi wasallam” alimwambia hadhrat Ali **(Ewe Ali, umwonapo mwanamke basi kwepesha macho yako. Kumuona kwa bahati mbaya si dhambi ila kumrejeshea tena jicho ni dhambi.)** Abu Daud na Darimy.

8- Kutoka kwa Ali „radiyallahu anhu”, amesema mjumbe wa Allah sallallahu alayhi wasallam **(Ewe Ali, usifungue paja lako wala usangalie paja la mwengine awe hai au amekufa.)** Imepokelewa na Abu Daud na Ibn maja. Hapa inafahamika kwamba kama ilivyo kwa alie

hai, haifai pia kuangalia utupu wa maiti. Inatakiwa kujikinga na kuangalia utupu wa wanamichezo na wale wanaoogelea baharini.

9- Kutoka kwa Abdalla bin Omar „radiyallahu anhu", amesema mtume "sallallahu alayhi wasallam" **(Msifunue tupu zenu** [yani msifunue hata mkiwa peke yenu] **kwa sababu kuna ambao kila wakati wako na nyinyi hawaondoki. Waoneeni haya na muwape heshima hao.)** Hao ni wale malaika wanaoitwa Hafaza. Hawa huwalinda binaadam kutokana na majini. Hawaondoki ila binaadamu anapoingia chooni na wakati wa kufanya tendo la ndoa.

10- Anasema Ummu salama „radiyallahu anha" tulikuwa mbele ya mtume "sallallahu alayhi wasallam" mimi na Maymuna „radiyallahu anha". Akaomba ruhusa Ibn Ummi maktum „radiyallahu anhuma" na akaingia ndani. Mtume "sallallahu alayhi wasallam" alipomuona akatwambia **(kaeni nyuma ya pazia)** Nikasema **(huyo si kipofu? Hatuoni sisi)** Mtume "sallallahu alayhi wasallam" akasema (Na nyie ni vipofu? Yeye hamumuoni?) yani anakusudia kusema hata kama yeye ni kipofu nyinyi si vipofu. Hadithi hii imepokewa na Imam Ahmad, Tirmidhy na Abu "rahmatullahi alaih" daud. Kufuatana na hadithi hii, kama ambavyo ni haramu kwa mwanamme kumuangalia mwanamke wa mbali, basi pia haijuzu kwa mwanamke kumuangalia mwanamme wa mbali. Maimamu wa madhehebu yetu "rahmatullahi alaih" kwa kuangalia na hadithi nyengine, ni shida kwa wanawake kutowaangalia wanaume vichwa na nywele zao. Amri ambazo utekelezaji wake ni mzito huitwa **(Azma)**. Utupu wa mwanamme mbele ya mwanamke ni baina ya kitovu na magoti. Amri ambazo ni nyepesi wameziita **(Rukhsa)**.

Inaonekana hapa kwamba wake watahirifu na masahaba wakitekeleza Azima na wakiepuka Rukhsa. Wale wanaojaribu kuuvunja Uislam kwa ndani miongoni mwa waingereza na ma **(Zindik)** wanasema kuwa (Wakati wa mtume "sallallahu alayhi wasallam" wanawake walikuwa hawajitandi. Hii namna wanayojifunika wanawake leo kama mazimwi haikuwepo wakati huo. Kujitanda huku kumeletwa na wajinga na wakandamizaji wa kidini miongoni mwa maalim wa fikhi.) Haya ni maneno ya kizushi. Ni kweli kwamba mwanzo wa Uislam amri hii haikuwepo. Ila katika mwaka wa tatu na wa tano hijria wanawake waliamrishwa kujitanda. Ameandika Baban-zade Ahmed Naim Bey katika **(Tajrid sarih tarjumasi)** kwamba aya za hijab zilishuka mara tatu.

11- Kutoka kwa tabii mkubwa bwana Bahz bin Hakim, kutoka kwa baba yake na babu yake, amesema mtume "sallallahu alayhi wasallam" **(Zifunike sehemu zako za utupu. Usimuoneshe yeyote zaidi ya mkeo**

**na mjakazi wako. Na uwapo peke yako basi muonee haya Allahu taala.)** hadithi hii imepokewa na Tirmidhy, Abu daud na Ibn maja „radiyallahu anhum". Kijakazi ni **(Mulki yamin)** uliyemmiliki kwa mkono wa kulia. Kwa sababu unapomnunua unatumia mkono wako wa kulia katika manunuzi na kulipia pesa.

12- Kutoka kwa Umar ul faruk „radiyallahu anhu", amesema mtume "sallallahu alayhi wasallam" **(Mwanamme anapokaa pekee faragha na mwanamke, watatu yao anakuwa ni shetani.)** Imepokewa na Tirmidhy. [Kukaa faradha na mwanamke wa mbali mmoja au zaidi ni haram. Anasema Ibn abidin katika kuelezea uimamu anaandika (ikiwa kutakuwa na mwanamme mwengine au mwanamke ambae ni maharimu wako basi haitokuwa kukaa pekee.)]

13- Kutoka kwa Jabir bin Abdulla „radiyallahu anhu", amesema mtume "sallallahu alayhi wasallam" **(msiende karibu na wanawake ambao waume zao wako mbali kwa sababu shetani anatembea ndani ya mishipa yetu kama damu.)** Wakamuuliza **(Je, na katika mishipa yako pia anatembea.)** Akajibu mtume "sallallahu alayhi wasallam" **(Kwangu pia anatembea, ila Allahu taala amenisaidia dhidi yake. Amemfanya muislam na amejisalimisha kwangu.)** Imepokewa na Tirmidhy "rahmatullahi alaih" .

14- Anasema Ummu Salama „radiyallahu anha" kwamba mtume "sallallahu alayhi wasallam" alikuwa nami. Mtumwa wa ndugu yangu Abdalla bin Abi Umayya pia alikuwa chumbani. Mtumwa huyu alikuwa baradhuli. Mtume "sallallahu alayhi wasallam" alipomuona alisema **(Watu kama hawa msiwaingize majumbani mwenu.)** Imepokewa na **(Buhari)** na **(Muslim)**. Baradhuli ni yule mwanamme ambae hulka, mwenendo, harakati na maneno yake anafanana na mwanamke. Watu hao wamelaaniwa na Allah. Kuna hadithi inayowahusu hawa isemayo **(Wanaume wanaojifananisha na wanawake, na wanawake wanaojifananisha na wanaume, Allah awalani.)** Hadithi hii inawahusu wale wanawake wanaovaa, wanaokata nywele na kufanya kazi mahsusi za wanaume na wale wanaume wenye kurefusha nywele na kujipamba kama wanawake bila ya dharura.

15- Miswar bin Mahram „radiyallahu anhuma" (amezaliwa mwaka wa pili wa hijra. Alikuwa ni mtoto wa dada yake Abdulrahman bin Auf „radiyallahu anhuma") anasema. Nilikuwa nimebeba jiwe kubwa na nguo yangu ikadondoka na sikuweza kuinyanyua. Mtume "sallallahu alayhi wasallam" akaniona katika hali hii. Akasema **(Nyanyua nguo yako. Msitoke nje uchi.)** Imepokewa na **(Muslim)**. Hadithi hii inakataza

wanaume na wanawake kuto kutoka bila ya kusitiri utupu majiani, fukweni na kwenye viwanja vya michezo.

16- Kutoka kwa Abu umama „radiyallahu anhu”, amesema mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa allah **(Mwenye kuuona uzuri wa binti akalikwepesha jicho lake, Allahu taala atampa thawabu za ibada mpya ambayo ataihisi ladha yake hapo hapo.)** Imepokewa na Ahmad “rahmatullahi alaih”.

17- Anasema Hasan Basri “rahmatullahi alaih” katika habar mursal, amesema mtume “sallallahu alayhi wasallam” **(Allah amlaani mwenye kuacha wazi sehemu zake za utupu na mwenye kuangalia.)** Imepokewa na imam Bayhaki katika **(Shuabul iman).**

18- Kutoka kwa Abdalla bin Umar „radiyallahu anhuma”, amesema mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allah **(Mwenye kujifananisha na kaumu basi naye huwa mmoja wao.)** Imepokewa na Ahmad na Abu Daud “rahmatullahi alaih”. Hii ina maana atakaejifananisha na makafiri katika mwenendo, kivazi na mambo yake basi atakuwa ni mmoja wao (wale wenye kufuata ada mbovu za makafiri katika mambo ya muda, mambo ya haramu wakayapa jina kuwa ni sanaa ya urembo, na wale wenye kufanya ya haramu wakawaita kuwa ni wasanii, wanatakiwa wachukue mazingatio kutoka hadithi hii.

19- Anahadithia Amr Shuayb kutoka kwa baba yake na babu yake, amesema mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allah **(Allahu taala anapenda kuziona neema alizompa mja wake.)** Imepokelewa na Tirmidhy “rahmatullahi alaih”. Hapa inafahamika kwamba Allahu taala anapenda nguo ya mja kuwa mpya, nzuri na safi. Anawapenda wale wenye kufanya hivi kwa kuonesha neema. Na wala hawapendi wenye kufanya kwa kiburi. Kuficha neema ulizopewa na Allah sio jaiz. Elimu pia ni miongoni mwa neema.

20- Anasema Jabir bin Abdalla „radiyallahu anh” mtume “sallallahu alayhi wasallam” alikuja kwetu na akamkuta mtu na nywele zilizokuwa hazikuchanwa. Akasema mtume “sallallahu alayhi wasallam” **(Huyu hakupata kitu cha kuchania nywele zake?)** Na alipomuona mtu na nguo chafu alisema **(Huyu hakupata cha kusafishia nguo zake?)**

21- Tabii Abu Lahwas anahadithia kutoka kwa baba yake ambae anasema. Nilikwenda kwa mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allah. Nguo niliovaa ilikuwa kongwe. Akaniuliza **(Huna mali?)** Nikajibu ninayo. Akasema **(Mali aina gani unayo?)** Nikajibu nina kila aina ya mali. Akanambia (**Wakati Allah anapokupa mali, athari yake anataka kuiona juu yako.)** Imepokewa na ahmad na Nisai. Tarjama ya juzuu ya tatu ya kitabu kiitwacho **(Ashiatul lamaat)** imeishia hapa.

Anasema Yussuf Kardhawi katika kitabu chake **(Alhalaal wal haram fil islam)**, katika Uislam mwanamke kuvaa nguo nyembamba itakayomuonesha maumbile ya ndani ni haram. Katika vitabu vya **(Muslim)** na **(Muwatta)** kuna hadithi sharif isemayo **(wanawake watakaokuwa uchi hali ya kuwa wamejitanda na wale wenye nywele kama nundu za ngamia, hawatoingia peponi. Hawatonusa hata harufu yake pamoja na kwamba harufu hiyo hufika mbali sana.)** Hadithi hii inakataza wanawake kuvaa nguo nyepesi zenye kuonesha na zile zilizobana, pia kusuka misuko yenye kuonesha mituniko ya nywele. Kutembea hivyo ni sawa na kuwa uchi. Wanawake na mabinti wa kiisalm hawatakiwi kuvaa nguo laini zenye kuonesha au zile zilizobana zikakamatana na mwili, au kusuka nywele au kuvaa wigi halafu zikafanya muinuko juu ya kichwa. Haya ni madhambi yenye kupelekea motoni.

[Imekwisha elezwa huko nyuma kwamba Kardavi ni kiongozi wa dini. asie na madhehebu. Uislam umeelezea kuwa ni fardhi kwa mwanamke kujisitiri na umeelezea stara inayotakikana. Hata hivyo haukueleza nguo gani zinatakiwa kuvaliwa ikiwa ni baibui, au skati au gauni. Imeelezwa katika vitabu vya fikh kwamba wanawake wajisitiri kisheria ila nguo za kuvaa ni jambo la **(Sunnatu zawaid)** ambazo huwa zinaendana na mila na wala sio ibada. Kwa hivyo watajisitiri kufuatana na ada ya sehemu wanazoishi. Kuacha ada katika jambo ambalo si ibada ni makruh. Na kama kuacha ada italeta fitna basi hiyo huwa haram. Katika kitabu cha **(Hindiye)** anasema (Kumuangalia mwanamke aliejisitiri vizuri kwa nguo pana na nzito inajuzu. Haijuzu kumuangalia mwanamke alievaa nguo nyembamba yenye kubana. Kuuangalia kwa matamanio uso wa mwanamke aliejisitiri ni haramu. Hata kwa mwanamke asie muislam ni hivyo hivyo. Hawa imesemwa kuwa inajuzu kuziangalia nywele zao.)

Kuvaa nguo moja nzito, pana iliyofika mpaka kwenye visigino na kwenye viganja, yenye rangi ya kiza ni bora kuliko kujisitiri kwa mashuka mawili. Anasema katika **(Halebi kabir)** (Nywele za mwanamke alie huru zenye kuning'inia hadi kufikia masikioni ni sehemu ya utupu kwa mawafikiano ya wanazuoni. Na zile zilizoshuka zikapita masikio nazo pia wengi wa wanazuoni wameziona kuwa ni utupu. Baadhi yao hizi wameziona kuwa sio utupu wakati wa kusali. Lakini mwanamme wa mbali kuziona sio jaiz.) Nywele zote zifunikwe kwa mtandio mzito. Sehemu ya mbele ya mtandio ije kwenye kikomo chake na kushuka kwenye nyusi. Sehemu ya pembeni ipite kwenye ncha za nyusi na ielekee kidevuni kisha ifungwe kwa pini hapo kidevuni na ncha zake zininginie kifuani n apande la nyuma lifunike mgongo.

Ikiwa inakhofiwa kusababisha fitna, basi na mashavu yake pia yafunikwe. Pia atavaa soksi nzito zenye rangi ya kiza. Mwanamke nywele zake zinazoning'inia kama robo yake zitakuwa wazi kwa kiasi ya nguzo moja ya sala basi sala yake haitokuwa sahihi. Na kama nywele chache zitakuwa wazi kwa kipindi hicho basi itakuwa makruh. Hapa hakuna kitabu kilichotafautisha juu ya mwanamke kuwa mzee au kijana. Pamoja na kwamba wako walojuzisha kuitikia salamu ya mwanamke mzee, kumpa mkono na kubaki nae pekee, ila hakuna aliejuzisha kuwa anaweza kuacha nywele wazi na kwamba inajuzu kuziangalia. Wako waliosema kuwa inajuzu kuangalia nywele za mwanamke asie muislam. Lakini hakuna aliejuzisha kuangalia nywele za mwanamke mzee muislam. Wale waliojuzisha kwa mwanamke mzee kwenda msikitini na kuzuru makaburi pia wameweka sharti ya kuwa ajitande.

Katika suratul Ahzab aya ya 59 imewataka wanawake wa kiislam kujistiri kwa **(Jilbab)**. Sio sahihi kusema kwamba aya hii inaamrisha kujisitiri kwa mapande mawili ya mashuka. Lau kama ingekua imeamrisha hivyo basi wake za mtume "sallallahu alayhi wasallam" na masahaba ridhwanullahi alayhim wangevaa hivyo, lakini hakuna kitabu kilichoeleza hayo. Katika tafsiri ya **(Tibyan)** imesema wafunike vichwa vyao. Katika tafsiri ya **(Jalalain)** (Wanawake wafunike vichwa kwa mtandio ambao utashuka usoni) Wakati Sawi alipoielezea hii alisema (ni mtandio na Dir, yani nguo itakayofunika juu ya shati). katika tafsiri ya **(Ruhul bayan)** na **(Abusuud wanasema)** (Jilbab ni ule mtandio unaowekwa juu ya kilemba kinachozuia nywele zisitawanyike. Jilbab ni pana na hushuka hadi kifuani na kufunika ukosi na shingo ya shati.) Aya hii inaamrisha wanawake kufunika kichwa na kiwiliwili chote.] Katika **(Zawajir)** na **(Alfikh alal madhahibil arbaa)** imeelezwa hadithi sharif inayoonesha kwamba wanaume pia wakivaa jilbab. Kwa wanaume jilbab ni kanzu yani shati lililo refu. Kuvaa baibui refu na mtandio au mapande mawili ya mashuka vyote ni sawa katika stara ya mwanamke. Inatakiwa mwanamke ajisitiri kufuatana na ada ya sehemu anayoishi na asilete fitna. Imeandikwa katika **(Buhari)** juzuu ya 6 ukarasa wa 26 kwamba sehemu ya aya ya hijab ilishuka katika harusi ya Zainab „radiyallahu anha". Harusi hii ilifanyika mwaka wa tatu wa hijra.]

Mtu ambae anajisema kuwa muislam basi mambo yake yote inabidi ayafanye kwa kufuata misingi ya kiislam. Ikiwa haifahamu basi inabidi awaulize maalim wa ahli suna au asome katika vitabu vyao. Iwapo jambo halitakuwa linaenda sawa na Uislam basi huwezi kuokoka na dhambi au hata ukafiri. Kila siku ni lazima kuleta toba ya uhakika.

Toba ya uhakika hupelekea dhambi na ukafiri kusamehewa . Iwapo hatoleta toba basi atapata adhabu ya duniani na ya Jahannam. Malipo haya yameandikwa sehemu mbali mbali katika kitabu chetu.

Sehemu ambazo wanaume na wanawake wanatakiwa wazisitiri ndani ya sala au nje ya sala huitwa **(Sehemu za Awra)**. (Utupu). **(Kutokusitiri sehemu za awra au kuangalia sehemu za awra za mtu mwengine ni haram.)** Kwa wanaume pia ni suna kufunika miguu yao. Mwenye kukana kwamba hakuna sehemu ya awra katika Uislam huyo huwa kafiri. Sehemu ambayo yupo mwanamme na mwanamke wasiojisitiri, ala za muziki zikawa zinapigwa, pombe na kamari vikawepo na sauti za waimbaji wa kike zikasikika sehemu hiyo huitwa **(Majlis fasik)**. Kwenda katika majlis fasik ni haramu. Moyo pia lazima uwe safi. Ili moyo uwe safi lazima na tabia ziwe safi. Moyo husafika kwa kufuata maamrisho ya Uislam. Moyo usiofuata maamrisho ya Uislam hauwezi kuwa safi. Kufuatana na ijmaa ya madhehebu manne, yule ambae anasema ni halali kufunua sehemu za awra na kuangalia sehemu za awra za watu wengine, na akawa asilipe umuhimu jambo hilo wala kuogopa adhabu yake huyo huwa kafiri. Hukmu ni hiyo hiyo kwa wanawake wasiojisitiri na wakawa wanaimba nyimbo au maulidi mbele ya wanaume. Katika madhehebu ya Hanbali sehemu iliyo baina ya magoti na hasua(sehemu ya paja) sio sehemu ya awra.

Mtu ambae anasema mimi ni muislam ni lazima kujifunza na kuyapa umuhimu masharti ya imani na Uislam na fardhi na haram ambazo wanazuoni wa ahli suna wamekubaliana kwa ijmaa. Kutokujua sio udhuru. Hii ni sawa na kujua ikawa usifuate. **(Kufuatana na madhehebu manne, wanawake sehemu zao zote ni awra ila uso na viganja.)** Zile sehemu ambazo hazina makubaliano ya ijmaa, yani moja ya madhehebu manne ikaona sio utupu, basi kuiwacha wazi sehemu hiyo na kutoipa umuhimu haiwi ukafiri, ila kufuatana na madhehebu yake atakuwa kafanya dhambi kubwa. Na hii ndio hukmu kwa wanaume kuacha wazi sehemu iliyo baina ya magoti na hasua, yani sehemu ya paja. Ni fardhi mtu kujifunza asiyoyajua na kuleta toba baada ya kuyajua.

## SIFA ZA MUUMINI

Muumini ana haki saba kwa muumini mwenziwe:

Kuitikia mwaliko wake (kwenda).

Kumtembelea anapoumwa.

Kuhudhuria maziko yake.

Kumpa nasiha.

Kumpa salam.

Kumuokoa katika mikono ya dhalim.

Anapokwenda chafya na akasema **(Alhamdulillah)** kumuitikia kwa kusema **(Yarhamukallah)**.

Ubora wa muumini unapatikana katika mambo sita.

Hutekeleza ibada. Hafanyi maovu. Anajiepusha na mambo ya haramu. Haiangalii mali ya mtu kwa jicho la ubaya. Hayasahau mauti.

Hadithi sharif inasema **(Kila mtu humpenda yule anaemtendea wema. Wema huu binaadamu anao ndani ya maumbile yake.)** Yule mwenye kuipenda nafsi yake, huwapenda wale wenye kutoa misaada kwa ajili ya kupata matashi ya nafsi zao. Mwenye akili na elimu, huwapenda wanaotoa misaada kama sehemu ya ustaarabu wao. Kwa ufupi wema huwapenda wema wenzao na waovu huwapenda waovu wenzao. Unaweza kumjua mtu alivyo kwa kuwaangalia wale anaowapenda na marafiki zake. Anatakiwa mtu awe na uso wa bashasha na azungumze kwa maneno mazuri na watu wote(rafiki, adui, muislam, kafiri) isipokuwa kwa watu wa bid'a. Jambo jema la kuwafanyia watu na zawadi njema ya kuwapa ni maneno mazuri na uso wa bashasha. Ukutanapo na muabudia ng'ombe basi mpe ng'ombe majani ili kuepusha uadui baina yenu. Usifanye malumbano yasio na faida na mtu yeyote. Malumbano yanapunguza urafiki na kuzidisha uadui. Ghadhabu husababisha maradhi ya mishipa ya fahamu na moyo. Hadithi sharifu inasema **(Usighadhibike)**.

Mwenye kuficha mambo manne ndiye mbora wa watu:

1- Ufakiri wake,

2- Sadaka yake,

3- Msiba wake,

4- Balaa zake.

Pepo inawasubiri kwa hamu watu wanne:

1- Mwenye ulimi wenye kumdhukuru Allahu taala.

2- Mwenye kuhifadhi maneno ya Allah.

3- Mwenye kulisha chakula.

4- Mwenye kufunga mwezi wa Ramadhani.

Kila mtu anatakiwa asiadimikiwe na mambo saba katika ulimi ake:

Kuanza na **(Bismillahi sharif)** katika kila jambo.

Kusema **(Alhamdulillah)** baada ya kumaliza kila jambo.

Kusema **(Inshaallah)** wakati wa kusema nitakwenda kwa fulani.

Kusema **(Innaa lillahi wa innaa ilayhi rajiun)**.

Anapofanya kosa kuleta toba

Kudumu katika kusema **(Laa ilaha illallahu wahdahu la sharikalah, lahul mulku walahul hamdu wa huwa ala kulli shayin kadir.)**

Kusema sana **(Ashhadu an lailaaha illallah, wa ashadu anna Muhammadan Rasulullah.)**

Inatakiwa kusoma sana maneno yafuatayo usiku na mchana:

**1- (Astaghfirullah.)**

**2- (Subhanallah, walhmdulillah, wala ilaaha illallahu, wallahu akbar wala hawla wala kuwwata illa billahil aliy-yil adhim.)**

## KUZITAMBULISHA TABIA NJEMA

Mtu ana tabia nzuri sabini na mbili:

Imani, Itikadi ya Ahli Sunna, Ikhlas, Ihsan, Tawadhuu, Zikri Minnat, Nasiha, Kuitakasa nafsi, Ghera, Ghibta, Saha, Ithar, Muruwa, Futuwa, Hikma , Shukur, Ridha, Subira, Khofu, Rajaa, Kuchukia kwa ajili ya Allah, Kupenda kwa ajili ya Allah, Hamuul, Istiwai dham na madh, Mujahada, Say, Kasd, Amal, Kukumbuka mauti, Tafwidh, Taslim, Talabul ilm, Salamat, Sadr, Ushujaa, Upole, Rifk, Inaba, Kutimiza ahadi, kutekeleza miadi, Tabia njema, Zuhd, Kinaa, Rushd, Kuyaendea ya kheri, Rikka , Shawk, Haya, Thibat fi amrillah, Unsu billah, Shawk ila likaillah, Wakar, Zakawat, Istikama, Adab, Firasat, Tawakkul, Sidk, Murabat, Musharat, Murakaba, Muhasaba, Muataba, Kasmil ghayth, Kupenda Maisha kwa ajili ya ibada, Toba, Khushuu, Yakin, Ubudiyya, Mukafaa, Riayatul hukukil ibaad.

Tawadhuu ni kuwa na moyo wenye kunyenyekea. Dhikri minnat ni kujua kwamba utiifu wote unatokana na kuwezeshwa na Allahu taala hivyo unashukuru kwa hilo. Nasiha ni kuwanasihi ndugu zako waislam. Tasfiya maana yake ni kuutakasa moyo na tabia mbaya na kuuvisha tabia njema. Ghayr ni kufanya jitihada katika dini. Ghibta ni kutaka upate neema walizonazo wengine. Saha na futuwat ni ukarimu. Ithar ni kumkamilishia mahitaji yake muumini mwenzio. Muruwa ni kuwa mtendaji katika wadhifa wako wa kibinaadam. Hikma ni kufanya amali kwa elimu. Kushukuru ni kutumia neema katika sehemu zinazotakiwa. Ridhaa ni kuridhia kudra zinazotoka kwa Allah. Subira ni kufanya Subira katika balaa.

[Hakuki ibad ni kulinda haki za waja. Miongoni mwa haki muhimu za waja ni haki za baba na mama. Kuwatimizia mahitaji yao kwa uso wa

bashasha na maneno mazuri ili kupata radhi zao. Kisha haki za jirani, haki za mwalim, haki za mke na mume, haki za rafiki na haki za serikali. Asimwambie mtu uongo, asimfanyie hila mtu yeyote, kupima kwa uadilifu, kumlipa mfanya kazi ujira wake kabla jasho kukauka. Kutokulipa deni au kutokulipa nauli ya kwenye basi au vyombo vyengine vya usafiri ni kufanya khiyana. Kutokulipa kodi na ushuru wa serikali ni kula haki ya melfu ya watu. Ikiwa serikali itafanya dhulma na wale waliodhulumiwa wakaamua kufanya uasi basi haitojuzu kuwasaidia wale watakaofanya uasi. Hili limeandikwa katika **(Berika)** kwenye maelezo ya fitna na katika **(Hindiyya)** na **(Durrul muhtar)**. Katika hadithi sharif **(Mwenye kuifanyia khiana serikali basi amemfanyia khiana Allah.)** Yani mwenye kufanya uasi atakuwa fakir na dhalil. Kwa hivyo asidanganyike mtu na yenye kuchochea uasi, ya kibaguzi na ya kivunjaji ya wale wasio na madhehebu kama Sayyid Kutub na Maududy. Serikali iliyo dhalimu haifanyiwi uasi na wale wenye kufanya uasi hawasaidiwi. Wakati Ibn Abidin alipokuwa akielezea uharamu wa wanaume kuvaa hariri anasema(Inajuzu kutumia vitambaa vya hariri na vitu vya dhahabu na fedha kwa kuvitundika au kuvionesha pasi na kuvitumia katika matukio mbali mbali kama sherehe za Idi na harusi, ikawa sio kwa kutaka kujionesha lakini kwa kutii amri ya serikali )Kuwasha mataa mchana, kuweka matangazo yenye mataa haijuzu kwa sababu hii ni kupoteza mali bila ya ulazima. Lakini haya yakiamrishwa na serikali, pia kupeleka watoto katika shule za mchanganyiko wa watoto wa kike na wa kiume inajuzu. Mikutano ambayo wanawake na wanaume wamechanganyika na ikawa watu wanaonekana sehemu zao za awrat basi haijuzu kushiriki. Pia haijuzu kuzipinga kanuni za makafiri katika nchi zao na hili amelitaja **(Ibn abidin)** katika sehemu ya sala ya Ijumaa na sehemu ya ukadhi. Yule mwenye haki ya mja mwengine ibada zake hazitokubaliwa na hatoingia peponi. Kujiokoa na haki ya kafiri ni uzito zaidi kuliko haki ya muislam. Kila mtu amfanyie wema na kutokulipa uovu dhidi ya uovu. Muislam wa kweli anafuata sharia za Allah na kanuni za serikali.

## FADHILA ZA MASAHABA

Miongoni mwa masahaba wote, masahaba wanne wa mtume “sallallahu alayhi wasallam” ndio wenye fadhila zaidi. Ukhalifa wao kwa ujumla ulikuwa ni miaka thelathini. (makhalifa hawa wote ni wenye kubashiriwa pepo na haifai kumzungumza kwa ubaya hata mmoja wao.)

Makarama ya mawalii ni haki na ya ukweli.

Miongoni mwa mawalii wote alie bora na wa juu zaidi ni Abubakar „radiyallahu anhu”. Ukhalifa wake ni wa haki. Kwa ijmaa ya umma yeye ndiye khalifa wa mwanzo. Ni baba mkwe wa mtume “sallallahu alayhi wasallam”. Binti yake Aisha „radiyallahu anha” aliolewa na mtume “sallallahu alayhi wasallam”, nae ni mama yetu. Alikuwa ni mweledi wa elimu ya uhakika. Mali yake yote aliitumia katika njia ya haki mpaka akaishiwa na kila kitu. Akawa anavaa shuka iliyotengenezwa kwa majani ya mtende. Hata Jibril „alaihis-salaam” nae akavaa kama alivyovaa yeye. Jibril alipotokeza mbele ya mtume “sallallahu alayhi wasallam” na vazi hilo mtume “sallallahu alayhi wasallam” akamwambia **(ewe ndugu yangu Jibril, mimi sijawahi kukuona na hali kama hii. Hii hali yako ni ya ajabu)** Jibril „alaihis-salaam” akamwambia (Wewe umeniona mimi na hali hii, lakini malaika wote wako hali kama hii hivi sasa. Hii ni kwa sababu Allahu adhimu shaan amesema **(Mja wangu Abubakar ametumia mali yake yote kwa kutafuta radhi zangu, na ametumia kwenye njia yangu. Sasa anavaa shuka ya majani ya mtende. Enyi malaika wangu. Nanyi vaeni kama yeye.)** Malaika wote hivi sasa wako kwenye vazi hili) Kutokana na imani hiyo ndio maana akaitwa Siddik.

Anayemfuata kwa ubora ni hadhrati Umar „radiyallahu anhum”. Ukhalifa wake umethibiti kwa ijmai ya umma mzima. Alikuwa ni mahiri wa elimu za kiislam. Siku moja mtume “sallallahu alayhi wasallam” alijiwa na myahudi na mnafiki wakiwa na kesi. Baada ya kuiamua haki ikaangukia kwa myahudi. Yule mnafiki hakuridhika na hilo. Mtume “sallallahu alayhi wasallam” akawaambia waende kwa Umar ili akaiangalie kesi yao. Wakaenda kwa Hadhrat Umar na walipofika akawauliza sababu ya ujio wao. Yule mnafiki akamwambia kuwa wana kesi yeye na yule myahudi. Hadhrat Umar akawambia kwa nini wamekwenda kwake hali ya kuwa sahib wa Uislam yupo. Yule mnafiki akawambia kuwa wamesharudi kwa mtume “sallallahu alayhi wasallam” nae amempa haki huyo myahudi hivyo yeye hakuridhia hilo. Sayyidna Umar akawaambia wasubiri, atawatatulia kesi yao mara moja na akaingia ndani. Akatoka na upanga kiunoni alipoutoa tu akamkata kichwa yule mnafiki na kumwambia “haya ndio malipo ya asieridhia hukmu ya mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allah”Kutokana na hili ndio akaitwa Umar al faruk „radiyallahu anhu” anhu.

Mtume “sallallahu alayhi wasallam” amesema **(Mpambanuaji haki na batili ni Umar.)**

Anaemfuta kwa ubora ni Uthman dhi nurain „radiyallahu anhu”. Ukhalifa wake ni wa haki na wa ukweli. Umethibiti kwa ijmaa ya umma.

Rasulullahi sallalalhu alayhi wasallam alimuozesha binti zake wawili kwa mfatano. Alipokufa binti wake wa pili alisema **(Lau kama ningekuwa na binti mwengine basi ningemuozesha)**.

Wakati anamuozesha binti yake wa pili, mtume "sallallahu alayhi wasallam" alimsifu sana sayyidna Uthman „radiyallahu anhum". Baada ya ndoa, siku moja binti alimwambia baba yake (Ewe baba yangu, nuru ya macho yangu. Umemsifu sana hadhrat Uthman ila hana sifa zote hizo.) Mtume "sallallahu alayhi wasallam" sallallahu alayhi wasallam akamwambia: **(Ewe binti yangu! Malaika walio mbinguni wanamuonea haya hadhrat uthman.)**

Kutokana na kuozeshwa binti wawili wa mtume "sallallahu alayhi wasallam" ndio akaitwa dhi nurain, yenye maana mwenye nuru mbili. Alikuwa ni mweledi wa elimu ya maarifa.

Anaemfuata ni Ali karramallahu wajhahu wa „radiyallahu anhu". Ukhalifa wake umethibiti kwa ijmaa ya umma. Ni mkwe wa mtume "sallallahu alayhi wasallam" aliemuozesha binti yake, mama yetu Fatima „radiyallahu anhum". Alikuwa ni mahiri wa elimu ya Tarika. Alikuwepo kijana mmoja, huyo kijana siku moja akataka kumjaribu bwana wake. Wakati hazrat Ali akiwa nje alimwendea yule kijana na kumtuma jambo lakini yule kijana akanyamaza kimya. Kisha Hazarat Ali „radiyallahu anhuma" akamrudia na kumwambia (Ewe kijana, kuna lolote nililokukosea. Ni lipi nililokufanya likakuchukiza na kukuumiza). Hapo kijana akajibu (Hujanikosea lolote. Mimi ni mtumwa wako. Nilikusudia kukujaribu tu. Hakika wewe ni walii mwenye kutenda haki).

[Wale wote wenye kuwapenda masahaba na kufuata njia yao huitwa **(Ahli sunna)**. Wale wenye kuwapenda baadhi yao na kuwachukia wengi wao huitwa **(Shia)**. Wale wenye kuwachukia masahaba wote huitwa **(Rafidhy)**. Wale wenye kusema tunawapenda masahaba wote lakini baadhi ya mambo yao hatuyafuati huitwa **(Wahabi)**. Mchanganyiko wa fikra za kiongozi wa dini mpotofu Ibn Taymiya zikichanganywa na uwongo wa jasusi wa kiingereza Hempher ndio unapatikana **(Uwahabi)**. Wao huwaita ahli suna makafiri kutokana na kutokukubali imani yao. Tamko hilo linawafanya wao wawe makafiri.]

Fikra za kiwahabi ziliasisiwa na waingereza huko ghuba ya Uarabuni katika mwaka 1150 hijria (1737 miladia). Ili kueneza fikra hii waliwauwa waislam wengi. Hivi sasa chini ya taasisi waiitayo **(Rabita al aalamul islam)**. wanatumia pesa nyingi ili kuwawinda viongozi wa dini katika nchi zote. Kwa kuwatumia wao wanawababaisha waislam. Wanawataja vibaya wanazuoni wa ahli suna na kinara wao dola ya

Uthman ambayo imeupigania uislam kwa miaka elfu na mia nne. Wanadai kwamba maelezo ya Nass yaliyotolewa na wanazuoni hawa wa ahli sunna si sahihi.

Baadhi ya mawahabi wanasema (Sisi pia ni miongoni mwa madhehebu ya ahli sunna. Sisi ni wa madhehebu ya Hanbal). Maneno yao haya yanafanana na yale ya Muutazila pale waliposema (Sisi pia ni miongoni mwa madhehebu ya ahli sunna. Sisi ni wa madhehebu ya Hanafi.) Wanasema hivyo kwa sababu wanafahamu kwamba wale ambao si ahli sunna wataingia katika Jahannam. Lakini kuyafuata madhehebu fulani katika amali tu haitoshi. Ili uwe mfuasi wa madhehebu lazima itikadi na amali zako ziwiane na madhehebu hayo. Itikadi za madhehebu nne zinafanana. Wote ni itikadi ya ahli sunna. Ili mtu awe ni mfuasi wa Hanafi au Hanbali lazima itikadi yake iwe ni ya ahli sunna. Itikadi ya Wahabi sio ya ahli sunna.

## MAELEZO JUU YA VYAKULA

Kukosha mikono kabla ya kula ni sunna na ina faida kumi.

Mtu ambae amekosha mikono yake kwa ajili ya kula, akaweka kidole chake kwenye michirizi ya machozi ya macho yake na akapangusa, basi mtu huyo hatapata maumivu ya macho kwa idhini ya Allah. Faida kumi za kukosha mikono kabla ya kula:

1- Ataita malaika kutoka chini ya arshi ya Allah na kumwambia kuwa kama ambavyo aliisafisha mikono yake basi na leo dhambi zake ndogo zimesafishwa.

2- Anapata thawabu sawa na aliesali sala ya nafila.

3- Ataokoka na ufakiri.

4- Atapata thawabu za siddikina (walio wakweli).

5- Malaika watamtakia istighfari.

6- Kwa kila tonge atakayokula, atapata thawabu sawa na kuwa ameitoa sadaka.

7- Kama ataanza kula kwa kupiga bismillahi basi husamehewa dhambi zake.

8- Dua atakayoomba baada ya chakula itakubaliwa.

9- Ikiwa atakufa usiku huo basi atapandishwa daraja ya mashahidi.

10- Na ikiwa atakufa mchana basi atasajiliwa katika kundi la mashahidi.

Kukosha mikono baada ya kula kwa nia ya kutekeleza sunna kuna faida sita:

1- Ataita malaika kutoka chini ya arshi ya Allah na kusema “Ewe muumin, mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allah sallallahu alayhi wasallama yuko radhi nawe”

2- Atapata thawabu mahsusi kwa neema hiyo.

3- Atapata thawabu sawa na wingi wa nywele za mwilini mwake.

4- Atapata sehemu kutoka kwenye mto wa rehema.

5- Atapata thawabu sawa na matone yanayodondoka kutoka mikononi mwake.

6- Atakufa hali ya kuwa ni shahidi.

Amri za Allah ni aina mbili. Amri takwin na Amri taklif.

**(Amri takwin)** ni kusema kwake **(kuwa)** (fanyika, tokea) kwa kile anchotaka kukiumba. Mara tu baada ya kutamka neno hilo basi kitu hicho huwa(hufanyika, hutokea). Hakuna yeyote anaeweza kuzuia kufanyika kwa kitu hicho. Kama ambavyo Allah amejaalia baadhi ya vitu viwe ndio sababu ya kuumbwa kwa vitu vyengine, basi na kwa binaadamu vile vile nguvu zake za kimada na kimaanawy pamoja na aina nyengine za nguvu amejaalia ziwe ni sababu ya kuumbwa vitu tafauti. Wakati anapotaka kumpa mja jema lolote basi humjaalia akaipata ile sababu ya kufikiwa na jema lile. Ile sababu inapoleta athari husika , naye Allah akasema kuwa hilo jambo hapo hutokea. Na asipotaka Allahu taala basi hakuna lolote linaloweza kutokea. Hekima za kuumba kwake amezificha kwa kuziwekea sababu. Watu wengi kwa kuona sababu tu (ambazo ndizo zinazojitokeza juu) wanashindwa kujua hekima ya Allah katika kuumba.

**(Amri taklify)** hizi ni amri wanazotakiwa binaadamu kutekeleza au kuacha. Utekelezaji wa haya unategemea utashi wa binaadamu mwenyewe. Hili Allah ameliwachia huru kuwa chini ya matakwa ya binaadamu, ila hata kama yeye binaadamu atalitaka lazima nalo pia liumbwe na Allah. Allah akipenda huliumba na likatokea na asipotaka haliumbi. Mwenye kuumba kila kitu akakipa sifa na athari zake ni yeye pekee. Kuamini kwamba kuna mwengine mwenye sifa za uluhiyya ni kumshirikisha Allah na kitu chengine. Allah amekemea jambo hili na kusema kwamba siku ya kiama hatomsamehe aliyemshirikisha na atamuadhibu adhabu iliyo kali. Wale wenye kutii amri za Allah, wanapoamua kufanya mema basi Allah nae hulikubali na kuliumba. Na wale waovu wasio watiifu wanapoamua kufanya ovu, Allah nae hulikubali na kuliumba. Wale wenye kumuamini na wakamuomba wakitokea kutaka kufanya maovu, basi yeye Allah kwa rehema zake hukataa na kutokuliumba hilo ovu. Kwa vile maadui wa Allah mambo

yao mengi huwa ni yenye kutokea, huwa na limbikizo kubwa la mambo maovu.

Kufuatana na umuhimu wake, Amri taklify zina daraja tafauti:

1- Ameamrisha watu wote kuamini na kuwa waislam.

2- Wale walioamini amewakataza kutenda ya haramu na yaliyo maovu.

3- Wale walioamini amewaamrisha kutekeleza fardhi.

4- Wale waislam wenye kuacha ya haramu na kutekeleza fardhi, amewaamrisha kuacha yaliyo makruh na kutekeleza ibada za nafila.

Kufuatana na mtiririrko huu haitojuzu kurukia kutekeleza la chini kabla ya lile la juu. Haitokubaliwa, haipendezi wala haina faida. Mfano kutenda mambo mema lakini ikawa hukumuamini Allah au kutekeleza fardhi lakini ikawa hukuacha ya haramu au kutekeleza nafila lakini ukaacha fardhi Allah hatopendezewa wala hatokubali. Kwa hivyo inafahamika hapa kwamba kila mtu anatakiwa atekeleze amri taklify kufuatana na mtiririko ulioainishwa hapo juu. Na iwapo mtu atakuwa anatekeleza jambo la chini na kuliacha lile la juu, na ikiwa kutekeleza huko hakumsababishii kuacha fardhi au kutenda la haramu, basi nalo asiache kulitenda. Kuendelea kwake kutenda , huenda Allah kwa baraka zake akamjaalia siku moja kutekeleza lile aliloliacha katika yaliyo juu. Haya yameandikwa katika **(Ruhul bayan)** juzuu ya sita.

**Fardhi za kula chakula ni nne:**

1. Wakati unakula na kunywa kujua kwamba kushiba kunatokana na Allah.

2. Kula kilicho cha halali.

3. Kutekeleza wajibu wako kwa Allah kutokana na nguvu uzipatazo katika hicho chakula.

4. Kukinai na kile unachokipata.

Wakati mtu anaanza kula atie nia kuwa ninakula kwa ajili ya kupata nguvu za kumtii Allah, kuwafanyia waja wa Allah yale yenye faida na kwa ajili ya kueneza dini ya Allah ili watu wapate furaha ya kudumu. Inajuzu kula kichwa kikiwa wazi.

**Yaliyo mustahab katika kula:** Kula chini, kuvaa nguo safi, kukaa kwa kupiga goti, kuosha mikono na kinywa kabla ya kula, kupiga bismillahi kabla ya kula, kuanza kwa kudota chumvi ulimini, kula mkate wa arpa, kukata mkate kwa mkono, kutokutupa vipande vidogo vya mkate, kula kilicho mbele yako, kutumia siki, kula tonge ndogo ndogo, kuchakua vizuri, kula kwa vidole vitatu, kupangusa sahani kwa kidole,

kuramba vidole mara tatu, kushukuru baada ya kula na kutumia vijiti vya kuchokolea meno.

**Makruh katika kula chakula:** Kula kwa mkono wa kushoto, kukinusa chakula, kuacha kupiga Bismillahi [kama atakumbuka kati kati ya chakula basi alete Bismillahi wakati huo.]

**Yaliyo haramu katika kula chakula:** Kuendelea kupapia chakula hali ya kuwa ameshashiba (ikiwa patakuwa na mgeni nae anaendelea bado kula, basi na yeye awepo na afanye kama bado anaendelea), kufanya israf katika chakula, kupiga Bismillahi hali ya kuwa unachokula ni haki ya mtu mwengine, kwenda kwenye karamu usioalikwa, kula mali ya mtu mwengine bila ya ruhusa yake, kula kitu kitakachodhuru kiwiliwili, kula chakula kilichoandaliwa kwa nia ya kufanya ria na kula kitu ulichokitoa kutokana na nadhiri.

**Kula chakula kimoto kuna madhara yafuatayo:** Inasababisha uziwi, inasababisha uso kupayuka, inafanya macho yasiwe makali, inasababisha meno kuwa manjano, hupati ladha halisi mdomoni, hakishibishi, hupunguza fahamu, hupunguza akili na huufanya mwili kupata maradhi kwa wepesi.

**Kula chakula kichache kuna faida zifuatazo:** Mwili unakuwa na nguvu, moyo unapata nuru, unapata nguvu ya hifdhi, Maisha yake yatamwendea kwa wepesi, kazi zake zitamuongokea, atakuwa amemdhukuru Allah, atakuwa ni mwenye kukumbuka akhera, atazidi kupata ladha ya ibada, atakuwa na uongofu na usahihi katika mambo yake na atapata wepesi wa hesabu siku ya kiama.

Mwenye kujiita muislam

Analazimika sala tano

Kesho, siku ya kiama.

Itakuwa ni vito, taji na burak

## YANAYOHUSU NDOA

Kuoa kuna faida nyingi.

Kunahifadhi dini ya mtu, tabia huwa nzuri, chumo huwa na baraka pia inakuwa umetekeleza sunna. Mtume “sallallahu alayhi wasallam” amesema **(owaneni mzae watoto wengi. Kwani mimi nitajifakharisha mbele ya umati mwengine siku ya kiama).**

Ni lazima kwa mke na mume kuchunga haki zilizo baina yao.

Mtu anapotaka kuowa inabidi atafiti ili kupata mwanamke mwenye dini na ambae si maharimu wake. Mwanamke aliepata uja uzito

kutokana na zina, inajuzu kumuoa. Ikiwa uja uzito ni wa mwanamme mwengine basi haitojuzu kumuingilia hadi azae. (Feyziyye).

Ikiwa ataoa kwa ajili ya mali au uzuri wa mwanamke ajue baadae atadhalilika. Mtume "sallallahu alayhi wasallam anasema **(Mwenye kuoa mwanamke kwa ajili ya mali au uzuri, ajue atavikosa hivyo vitu.)**

Na yule mwenye kuoa mwanamke kwa ajili ya dini na mwenendo wake mwema, basi Allah atamuongezea mali na uzuri. Mwanamke anatakiwa awe chini ya mwanamme katika mambo manne. Umri, urefu, hism na jamaa.

Mwanamke anatakiwa awe juu ya mumewe kwa mambo manne. Awe mzuri zaidi, mwenye adabu zaidi, mwenye tabia njema zaidi na mwenye kuchunga ya haram na yenye shubha zaidi. Asiwe mwenye kutembea kichwa, miguu na mikono wazi mbele ya wanaume wa mbali (ajnabi).

Mtoto mdogo wa kike asiozeshwe mwananme mzee, hili linaweza likaleta ufisadi. Kabla nikah haijafanyika, lazima familia zichunguzane na wachumba wachunguzwe. Hili pamoja na kuwa ni sunna , vile vile litasaidia kupunguza migogoro baada ya ndoa. Katika hili kuna faida tatu. Kuendelea mapenzi baina yao hadi wanakufa. Kuongezeka riziki yao. Kutekeleza jambo la sunna.

Kisha watakwenda kwenye idara husika ili kukamillisha taratibu za ndoa. Kutokufanya nikah ya kisunna ni dhambi. Na kutokuteleza taratibu za kanuni za ndoa ni kosa.

Baada ya nikah ya kisunna kufanyika, upande wa mwanamme utawapelekea upande wa mwanamke vitu vizuri vya thamani. Hili litaongeza mapenzi baina yao. Mwanamke kutumia aina zote za mapambo mbele ya mumewe ni jaiz na la zaidi ni thawabu. Kulisha chakula usiku wa harusi ni suna. Chakula kitaliwa baada ya magharibi na baada ya isha mwanamme atapelekwa nyumbani kwa mwanamke na baada ya dua watu watatawanyika.

Katika sunna zitazofanyika usiku huo ni kwa bwana harusi kumkosha miguu bibi harusi na maji yaliyokoshewa kuyamwaga pembe zote za nyumba. Pia ni sunna kusali rakaa mbili na kuomba dua kwa sababu dua inayoombwa usiku huo hukubaliwa. Inafaa kuwakumbusha maharusi jambo hilo. Na kuwaombea dua kwa kusema **(Barakallahu laka wa barakallahu alayha wajamaa baynakumaa bilkhayri)** maana yake ni kwamba. Allah akubariki wewe, na ambariki yeye na akuwekeni pamoja kwa wema. Kuna baadhi wanaosema(ishini

kwa wema, mpate watoto wanaume.) Hayo ni maneno ya kijinga. Kinachofaa ni kuwaombea dua iliyo sunna kwa wakati huo.

Ni lazima kujifunza mambo ya dini na kumfunza mkewe kwani hilo atakwenda kuulizwa siku ya kiama. Kutokujua sio udhuru. (Kujifunza mambo ya fardhi na ya haramu , na kujifunza itikadi ya ahli sunna na kumfunza mke na watoto ni fardhi. Kujifunza na kuwafunza yaliyo ya sunna ni sunna.

Inatakiwa kutokumruhusu mke kwenda mahala msimoruhusika kisheria. Asitoke nje bila ya stara ya kisheria. Mtume “sallallahu alayhi wasallam” anasema **(Mwanamke mwenye kwenda msikitini hali ya kuwa ananukia manukato basi sala yake haitosihi. Hadi arudi kwake na akoge kama anavyokoga kwa ajili ya janaba.)** Ikiwa haijuzu kwenda hivyo msikitini basi itakuwaje kwa kutembea mabarabarani na kwenye mikusanyiko ya watu; dhambi zake zitakuwa ni za daraja gani? Inafaa kuzingatia ukubwa wa adhabu inayostahili.

Mtume “sallallahu alayhi wasallam” amesema katika hadithi **(Wengi wa watu wa peponi ni mafakiri na wengi wa watu wa motoni ni wanawake)** Akauliza bibi Aisha “Kwa nini watu wa motoni wengi ni wanawake” Akajibu mtume “sallallahu alayhi wasallam” **(Wao hawafanyi subira kwenye matatizo, na hata wakifanyiwa wema kwa miaka kumi, likitokea pungufu moja tu ule wema wa miaka kumi huusahau na wakawa wanazungumzia hayo mapungufu. Wao pia hupenda sana dunia na mapambo yake na hawafanyi jitihada kwa ajili ya akhera. Pia wao ni watu wenye kusengenya sana.)**

Yeyote atakae kuwa na sifa kama hizi, akiwa mwanamme au mwanamke basi ataingia motoni.

Imepokewa kutoka kwa Hadhrat Ali karramallahu wajhahu kwamba alikuja mwanamke mbele ya mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allah akasema (Ewe mjumbe wa Allah, mimi ninataka kuolewa. Je unaniambia nini kuhusu hili?) Akasema mjumbe wa Allah **(Haki za mume kwa mkewe ni nyingi, Wewe utaweza kuzitekeleza?)**. Akasema huyo mwanamke (Ni zipi haki za mume ewe mjumbe wa Allah.) Akasema **(Ukimuudhi basi unakuwa umemuasi Allah na hakutakabalii sala zako.)** Akauliza huyo mwanamke kama kuna haki nyengine. Akasema mjumbe wa Allah **(Mwanamke yeyote atakaetoka nyumbani kwa mumewe bila ya ruhusa, basi atapata dhambi kwa kila hatua anayokanyaga.)** Akauliza huyo mwanamke kama kuna haki nyengine. Akasema mjumbe wa Allah **(Mwanamke mwenye kumwambia maneno mabaya mumewe, basi siku ya kiama ulimi wake utavutwa hadi kisogoni.)** Akauliza huyo mwanamke kama kuna

haki nyengine. Akasema mjumbe wa Allah **(Mwananmke yeyote ambae atakuwa na mali, akawa asisaidie mahitaji ya mumewe, basi atafufuliwa siku ya kiama na uso uliopiga kiza.)** Akauliza huyo mwanamke kama kuna haki nyengine. Akasema mjumbe wa Allah **(Mwanamke yeyote atakaechukua mali ya mumewe na akampa mtu mwengine, kisha asitake uhalali kwa mumewe, basi Allah hatozikubali zaka na sadaka za mwanamke huyo.)** Akauliza huyo mwanamke kama kuna haki nyengine. Akasema mjumbe wa Allah **(Mwanamke yeyote atakaemtukana mumewe au kumpinga ataninginizwa kwa ulimi ndani ya shimo la moto, na mwanamke yeyote atakaetoka nje kuangalia dansi za wanawake na muziki na akatumia pesa kwa hilo basi atafutiwa thawabu zake zote za tangu utotoni. Nguo alizozivaa pia zitamshtaki kwa kusema, sisi badala ya kutuvaa kwa kwenda kwenye mambo ya kheri ametuvaa kwa kujia kwenye mambo ya haramu, na Allah atasema kwa wanawake kama hawa kwamba inafaa awachome miaka elfu.)** [Uovu wa sinema, redio na televisheni unafahamika hapa]. Yule mwanamke akasema (Sikuwa nimeolewa hadi leo. Na baada ya hapa sitaolewa tena.)

Hapo mtume "sallallahu alayhi wasallam" akaamua kumpa nasaha zake akasema **(Ewe mwanamke! Wacha nikuelezee na baraka za kuolewa. Ikiwa mume atamwambia mkewe Allah akubariki kwa neema zake basi hilo ni bora kwake kuliko kuabudu miaka sitini. Mke kumpa maji ya kunywa mumewe kuna thawabu zaidi kuliko kufunga mwaka mzima. Wakati anakoga baada ya kufanya tendo la ndoa na mumewe basi anapata thawabu sawa na ibada ya kuchinja. Ikiwa hatomfanyia hila mumewe basi malaika mbinguni wataleta tasbih kwa ajili yake. Na anapocheza na mumewe basi fadhila zake ni zaidi ya kuachia huru watumwa sitini. Ikiwa atahifadhi riziki inayoletwa na mumewe, akawarehemu jamaa wa mumewe, akasali sala tano ni bora kuliko kwenda alkaaba mara elfu.)** Fatima Zahraa radhiayallahu anha aliuliza **(Ni ipi hali ya mwanamke anapomuudhi mumewe?)** Ndipo baba yake mtukufu akamjibu **(Iwapo mwanamke ataacha kumtii mumewe ghadhabu za Allah zinakuwa juu yake hadi atakapomuomba mumewe msamaha. Ikiwa hatompa unyumba (tendo la ndoa) basi atapoteza thawabu zake zote. Na akijitukuza juu ya mumewe basi atapata ghadhabu za Allah, na kama atamwambia (wewe ni msumbufu unaeingilia mambo yangu), au (sijawahi kupata lolote la kheri kutoka kwako) basi Allah atamharamishia neema zake. Hata kama ataramba damu ya mumewe kwa ulimi basi bado atakuwa hajamlipa haki zake. Na iwapo mume atampa ruhusa kutoka bila ya stara basi mume huyo ataandikiwa uovu ndani ya**

**daftari lake.)** Je itakuwa hali gani kwa wanawake ambao wanatoka majumbani mwao bila ya ruhusa!

Anasema rasulilkiram **(Ewe Fatima, lau kama ingetolewa ruhusa kwa mtu kumsujudia mtu mwengine, basi ningewaamrisha wake wawasujudie waume zao).**

Mama Aisha „radiyallahu anhuma" alisema (Ewe mjumbe wa Allah, niusie) Mtume "sallallahu alayhi wasallam" akamwambia **(Mimi nitakuusia wewe, nawe utawausia wanawake wa umati wangu. Kesho siku ya kiama kwanza wataulizwa juu ya iman, kisha udhu na sala kisha haki za waume. Mwanamme yeyote atakaesubiri kwa maudhi ya mkewe basi ataandikiwa subira ya Nabii Daudi. Na mwanamke yeyote atakaesubiri maudhi ya mumewe basi atapandishwa daraja ya Aisha Siddika.)**

Akasema tena mtume "sallallahu alayhi wasallam" wa Allah **(Mwanamme yeyote atakaempiga mkewe basi nitakwenda kumshitaki siku ya kiama.)**

Inajuzu kwa mwanamme kumpiga mkewe kwa mkono au nguo isiyosokotwa kwa moja kati ya sababu tatu. Kuacha sala au josho la lazima, kukataa kutoa haki ya kitandani na kutoka nyumbani bila ya ruhusa ya mume. Kumpiga mwanamke bakora, ngumi, mateke, nguo iliyosokotwa au kumpiga usoni au sehemu ya mgongo na tumbo haikujuzishwa. Pia haijuzu kumpiga mwanamke kwa makosa mengine. Kinachotakiwa anasihiwe mara kadhaa na kama ataendelea basi bora kumwacha ili mwanamme asije akaingia yeye kwenye adhabu. Anasema katika.

**(Siratul Islam)** (Iwapo mke atakuwa na mwendo usio mzuri, inabidi mtu ajichunguze yeye na aseme lau kama ningekuwa mwema basi naye asingefanya hivi. Ikiwa mke ni mwema basi mume asimuolee mke wa pili. Haijuzu kuoa mke mwengine, kwa mwanamme ambae hawezi kuchunga uadilifu katika mahitaji ya nyumba. Pamoja na kwamba inajuzu kwa yule ambae anaweza kufanya uadilifu, lakini ni bora kutokuongeza mke. Wakati mwanamke anapokwenda sehemu zinazojuzu kwenda ni lazima achunge stara ya kisheria. Ni haramu kwa mwanamke kunukia manukato au kuonesha mapambo wakati anatoka majiani. Mwanamke mwema ndio neema kubwa duniani. Kumfanyia huruma na upole muislam ni bora kuliko kutekeleza ibada za nafila.) Na katika **(Riyadhu nasihina)** anasema [Katika maana ya aya 18 ya Suratu nisaa **(Watendeeni wake zenu wema na upole.)** Na katika hadithi sharif **(Ya Aba bakr, yule mwenye kuzungumza na mkewe kwa uso wa bashasha na upole, anapewa thawabu sawa na za kumuachia**

**huru mtumwa)** na **(mwanamke atakaeolewa na mwanamme fasik, Allah hatompa rehema zake.)** na **(Mwenye kutaka kupata shafaa yangu basi asimuozeshe binti yake kwa mtu fasik)** na **(Aliye mbora katika watu ni yule mwenye kuwafanyia wema wengine na alie muovu miongoni mwa watu ni yule anaewadhuru wengine)** na **(Kumuudhi muislam mara moja bila ya haki ni dhambi zaidi kuliko kuivunja Alkaaba mara sabini.)**

Na anasema katika **(Durul mukhtar)** (Ni fardhi kwa mwanamme muislam kumpa nafaka (mahitaji ya lazima) mkewe. **(Nafaka)** ni chakula, mavazi na sehemu ya kuishi. Amuweke mke ndani ya nyumba yake au aliyokodi. Mke anaweza akataka kuwa kusiwe na jamaa wa mume ndani ya nyumba. Na mume vile vile anaweza akataka kusiwe na jamaa wa mke ndani ya nyumba. Wote wawili wanayo haki hiyo. Nyumba iwe baina ya majirani wazuri. Sauti ya muadhini iweze kufika. Mke kwa kila wiki mara moja asizuwiwe kwenda kuwaona wazee wake. Wazee nao wasizuwiwe kuja kumuona binti yao. Ikiwa mmoja kati ya wazee wawili ataumwa na akahitaji mtu wa kumualisa na ikawa hayupo, basi mke atakwenda kumualisa mzazi wake hata kama mume hatoridhia. Mume hatakiwi kumzuia mkewe kwenda kuwaona jamaa zake wengine wa karibu mara moja kwa mwaka au wao kuja mara moja kwa mwaka. Ikiwa mume atamruhusu mkewe kwenda kwa wengine au kwenda sehemu zisizo halali basi wote wawili watapata dhambi. Mume amzuwie mke kwenda kufanya kazi nje ikiwa ni kwa ujira au kwa shughuli za kheri za kujitolea au kwenda maofisini na kwenye waadhi. Mwanamke akae ndani na kujishughulisha na kazi za ndani, asikae bure. Pia asimruhusu kwenda sehemu ambazo watu wanakuwa wameacha wazi sehemu zao za utupu [kama hamam (bafu za umma) na kwenye fukwe, sehemu za michezo]. Pia asiruhusu televisheni yenye kuonesha mambo haya. Hatakiwi kujipamba akavaa nguo mpya na kutoka majiani. Mbali na wale jamaa ambao ni maharim wa mke wake, anaweza mume akapeleka wageni wengine kwa sharti ya kwamba wanawake na wanaume watakaa sehemu tafauti. Jamaa ambao ni **maharim** kwa mwanamke ni kumi na nane, nao ni.Baba yake na babu zake, watoto na wajukuu zake, ndugu hata ikiwa ni wa baba mmoja au mama mmoja tu, watoto wa ndugu wa kiume au ndugu wa kike, baba wadogo na wajomba. Wanaume hawa saba, pia huwa maharim kwa kupitia njia ya kunyonya ziwa moja au hata kama mtoto amepatikana kwa zina.Kuna wanaume wanne ambao ujamaa wa maharim unapatikana kwa kupitia ndoa nao ni baba mkwe na baba zake, mume wa mwanawe, baba wa kambo na watoto wa kambo (watoto wa mume). Wake wa wajukuu kwa mtu mwanamme na

waume wa wajukuu kwa mtu mwanamke pia ni maharim wao. Maana ya maharim ni kwamba hawezi kuoana nae. Mfano ndugu wa kike ni maharim. Watoto wa ndugu wote ni maharim. Wake wa ndugu zake (shemegi) na watoto wa mjomba, shangazi, ami na mama mdogo na wake zao hao wote si maharim kwa mume. Watoto wa mama mdogo na waume zao sio maharim kwa mke. Ndugu wa kike wa mke si maharim kwa mumewe. Mume wa dada, shangazi au mama mdogo, ndugu wanaume wa mume (mashemegi) hawa wote si maharim kwa mke. Haya yameandikwa katika **(Nimeti islam)** katika mlango wa hija. Ni haram kwa mwanamke kutoka mbele yao bila ya stara ya kisheria, kukaa nao faragha au kusafiri nao. Mama mkwe, mama wadogo wa baba mmoja au mama mmoja nao pia ni maharim. Haijuzu kwa mwanamke kuolewa na watu walio maharim zake na inajuzu kukaa mbele yao bila ya kujitanda. Anaweza kukaa nao faragha na anaweza kusafiri nao. Wanapokuja wageni wanaume wasio maharim zake, katika uwepo wa mumewe au jamaa wa kike, hali ya kuwa amejisitiri stara ya kisheria anaweza kuwakaribisha na kuwakirimu ila hatokaa nao pamoja. Waislam wanatakiwa ada zao zifate Uislam na wala zisifate mila zao. Inalazimu kumfundisha mke elimu ya dini na ikiwa mwenyewe hajui basi amtafutie mwalimu wa kike alie mwema ampeleke. Iwapo mwalimu anaefaa hatompata basi watafute vitabu sahihi vilivyoandikwa na maulamaa wa ahli  sunna na wasome pamoja ili wajifunze itikadi sahihi na yale ya halali na haramu. Vitabu vilivyoandikwa na watu wasio na madhehebu na wale walio waovu wasisome wala wasiviingize nyumbani mwao. Pia asiruhusu redio na televisheni zenye kutangaza maovu kwani hizi ni mbaya zaidi ya rafiki muovu. Zitaathiri na kuharibu dini na tabia za mke na watoto.Mke na watoto wa kike wajishughulishe na kazi za nyumbani na wala wasijishughulishe shambani, sehemu za biashara, viwandani, kwenye mabenki au ajira za serikalini. Si lazima kwa mwanamke na watoto wa kike kumsaidia mume au baba katika shughuli zake za viwandani au kwenye biashara kwa ajili ya kutafuta pesa. Hizi , pamoja na shughuli za kwenda dukani na sokoni kununua mahitaji ni wadhifa wa mwanamme. Ikiwa mwanamke atalazimishwa kufanya haya basi dini yake , mwenendo wake na afya yake vitaharibika. Wote wawili watakuwa wameharibu dunia yao na akhera yao. Hawatoweza kujiokoa na madhambi. Wale wenye kufuata mafunzo ya dini ndio wenye kupata raha ya dunia na akhera. Muislam anatakiwa afuate mafunzo yaliyomo katika vitabu vya sharia ya dini na aachane na tabasamu na maneno ya kilaghai ya marafiki waovu na wanafiki. Inalazimu kuwalinda watoto na mambo ya haramu. Watoto wa kiume

wapelekwe shule zenye walimu waislam. Hakuna haja kuwafanyisha kazi wanawake wakachanganyika na wanaume katika viwanda, masoko na maidarani. Ikiwa mwanamke hana mume au mume ni mgonjwa basi inatakiwa jamaa wa karibu wampatie mahitaji yake ya lazima. Ikiwa jamaa wa karibu ni masikini basi dola inatakiwa impatie mshahara wa kumtosha. Katika uislam Allah amempelekea mwanamke mahitaji yake yote chini ya miguu yake. Kufanya kazi na kutafuta mahitaji ya lazima ni wadhifa wa mwanamme. Hata kama si kwa kufanya kazi, mwanamme anapata ziada ya nusu katika mirathi kwa ajili ya kuhudumia wanawake. Mwanamke kazi yake ni shughuli za nyumbani. Miongoni mwa shughuli hizi ya mwanzo ni malezi ya watoto. Murshid wa mwanzo wa mtoto ni mama yake. Mtoto mwenye kujifunza dini na maadili kutoka kwa mama yake, hatodanganywa na kuhadaiwa na walimu wasio na dini, marafiki waovu na maadui wa Uislam na wazandik. Naye huwa muislam mzuri kama wazee wake. (Angalia **(Tam ilmihal saadet abadiyya)** toleo la 84 na yanayofuata, ukarasa wa 579. Wanafiki wenye kuupiga vita Uislam huitwa **wazandik**).

## KUMTAYARISHA MAITI, KUMKAFINI NA KUMZIKA

Kumsalia maiti , kumkafini, kumuosha na kumzika haya yote ni fardhi kifaya.

Katika kuosha, maiti anaekwa sehemu iliyo juu iliyojengwa kwa marmar au ubao na analazwa juu ya mgongo. Atavuliwa shati lake na kutiwa udhu. Atakoshwa kwa maji yenye vugu vugu kutoka kichwani hadi kitovuni. Kisha atazibwa baina ya kitovu na magoti na kukoshwa. Muoshaji atavaa glovu na kupitisha mkono chini ya shuka aliyofunikiwa maiti na atamnyunyizia maji na kumuosha. Hatochungulia chini ya shuka. Kisha atamgeuza kushoto ili akoshe ubavu wa kulia na kisha atamgeuza kulia ili akoshe ubavu wa kushoto kwa mkono wake wenye glovu. Moja kati ya shuka tatu itatandikwa juu ya sehemu alooshewa maiti na hii atazongwa nayo na kuingizwa nayo kwenye jeneza.

Sanda ziko za aina tatu

Sanda ya fardhi, (hii pia huitwa sanda ya dharura), sanda ya sunna na sanda ya kifaya.

Sanda ya sunna kwa mwanamme ni vipande vitatu na kwa mwanamke ni vipande vitano.

Sanda ya kifaya ni pande mbili kwa mwanamme na pande tatu kwa mwanamke.

Anasema katika kitabu kiitwacho **(Bahar):** Sanda kifaya kwa wanawake itakuwa na izar, lifaf na khimar(mtandio) kwa sababu wanawake katika uhai wao hujisitiri kwa nguo hizo tatu. Izar kwa wakati huo ni ile nguo inayofunika kutoka mabegani hadi miguuni. Lifafe ni kanzu kwa alivyoandika Ibn Abidin. Hapa inafahamika kwamba zama hizo kinamama wakitoka nje na mabaibui mapana na mitandio. Wanasema katika **(Bahar)** na **(Durul muntaka)** (Wajibu wa nafaka wa mume kwa mke ni chakula, mavazi na mahala pa kukaa. Mavazi ni shungi (mtandio) na Milhafa. Milhafa ni nguo inayomfunika juu (baibui). Hapa inaonekana kwamba nguo ya mwanamke ina pande tatu. Yale mashuka meusi (carsaf) hayakutajwa hapa. Ada ya kuvaa mashuka meusi ilikuja baadae. Inajuzu kwa wale wenye ada ya kutumia mashuka meusi basi wavae hivyo na wale wenye ada ya kuvaa baibui wavae baibui pana na mtandio. Kwenda kinyume na ada na tamaduni maana yake ni kujitenga na jamii jambo ambalo linaweza likaleta fitna. Na ni haramu kuleta fitna katika jamii.

Sanda ya fardhi kwa wanaume na kwa wanawake ni kipande kimoja.

Iwapo kitambaa cha kawaida cha sanda hakikupatikana na badala yake kikapatikana kitambaa cha hariri basi kwa wanaume shuka moja na kwa wanawake shuka mbili zitatosha.

Katika sala ya jeneza mwenye kustahiki zaidi uimamu kwanza ni raisi wa nchi kama ni muislam, kisha kiongozi wa mji, kisha imam mteuliwa wa Ijumaa kisha imam hay. Imam hay ni yule kiongozi wa dini muislam ambaye maiti huyu alipokuwa hai alikuwa akimdhania mema mtu huyo. Baada ya hapo anafuata walii wa maiti. Iwapo walii hatakuwepo na maiti akasaliwa na mtu asie kuwa miongoni mwa hao tuliowataja, basi walii atakuwa na hiari ya kusalia tena maiti au kutokusalia. Maelezo zaidi yamo ndani ya kitabu cha **(Saadati abadiyya)**.

Iwapo mwili wa maiti umekatwa (kwa marefu) na ikapatikana nusu moja tu, basi hiyo hailazimiki kusaliwa.

Na iwapo umekatwa vipande vipande vikatawanyika sehemu tafauti basi pia havitosaliwa. Ila hivyo vipande kama vitaletwa pamoja basi hapo atasaliwa.

Ikiwa maiti atakoshwa na wakagundua kuwa kuna sehemu haikupata maji, ikiwa itakuwa kabla ya kukafiniwa basi wataikosha hiyo sehemu. Iwapo wakati ameshafikishwa kaburini wakagundua kuwa kiungo kimoja cha udhu hakikupata maji, basi watakiosha na kumsalia. Ikiwa watapata habari baada ya kuwa keshatiwa kaburini na kufukiwa

basi huyo hatofukuliwa. Ikiwa itakuja habari kwamba maiti amezikwa bila ya kuoshwa basi atafukuliwa ili aoshwe.

Iwapo maiti amefanyiwa tayammam kisha wakati anapelekwa kaburini maji yakapatikana basi kutakuwa na khiyari.

Ikiwa katika mji watakufa watu wengi kwa wakati mmoja wanaweza wakasaliwa wote pamoja kwa sala moja. Hii ni pamoja na kufuata maelekezo ya dini. Ila lililo bora zaidi ni kwa kila mmoja kusaliwa sala yake.

Nia ya sala ya maiti ni **(Ninamsalia maiti huyu wa kike au wakiume hali ya kua ni dua kwake kwa kutaka radhi za Allah, hali ya kumfuata imam aliopo.)**

Iwapo jambazi mwenye kukaba watu majiani na kuwanyanganya mali zao akakamatwa na kuhukumiwa kifo na wahusika wa dola, au yule mwenye kuiasi dola na akauliwa katika mapambano au aliyehukumiwa kifo kutokana na kumuuwa baba yake au mama yake basi watu hawa hawasaliwi. Yule mwenye kujiua mwenyewe atasaliwa. (**Durrul muhtar**)

Watu wa ahlisunna wana dalili kumi:

1- Anadumu katika kusali sala za jamaa.

2- Husali nyuma ya imam ambaye itikadi yake au ufasik wake haufikii daraja ya ukafiri.

3- Mwenye kukubali kujuzu kwa kupangusa khofu (soksi za Ngozi) sehemu ya juu.

4- Hasemi maneno maovu dhidi ya masahaba wote kwa umoja wao.

5- Hafanyi uasi dhidi ya dola.

6- Haingii katika mijadala na malumbano ya dini bila ya haki.

7- Hafanyi shaka katika dini.

8- Anakubali kuwa kheri na shari zote zinatokana na Allah.

9- Hawakufurishi waislam bila ilhad.

10- Anawatanguliza makhalifa wanne mbele ya masahaba wengine.

## HALI ZA KIFO

Ewe usie na pa kukimbilia, wewe unakimbia mauti. Ukisikia fulani amekufa unasema nikikaribia na mimi mauti yatanirukia. Ukisikia maradhi ya tauni yameingia katika mji unakimbia ili wewe usiumwe. Itikadi hiyo ni haramu kwa sababu ni Allah atakapo ndiyo unapata maradhi.

Ewe usie na pa kukimbilia, unakimbilia wapi! Ahadi yako ya mauti imeshaandikwa. Ahadi haisogei mbele. Allahu Khallaq allam itakapofika ahadi yako hatoichelewesha hata kwa mpepeso wa jicho. Wakati uliokwisha kadiriwa hautozidi wala kupungua.

Kwa namna hukmu ya Allah ilivyokwisha pitishwa, binadamu ataacha mali yake, familia yake na watoto wake aelekee anakohitajika. Na hatokufa hadi afike katika ardhi ambayo mwili wake unahusika.

Kila mtu anakufa wakati ahadi yake inapofika. Katika Suratul Aaraf aya ya 33, tunasoma katika maana ya aya **(Itakapofika ajali yao, basi haitoakhirishwa wala kupelekwa mbele.)**

Urefu wa maisha ya binaadamu ulikwisha amuliwa kabla ya yeye kuzaliwa. Na binaadamu wapi atakufa, atakufa ametubia au la, maradhi gani yatamuua, atakufa na imani au la, haya yote yameandikwa katika Lawhil mahfoudh. Aya ya mwisho ya Suratu lukman inaashiria haya.

Allahu khallaqun alim ameumba mauti, kisha akaumba na uhai, kisha akaumba riziki zenu kisha akayaandika haya kwenye Lawh.

Pumzi ngapi utavuta katika uhai wako Hakku taala anazijua na zimeandikwa katika Lawh. Malaika wanazifatilia na wakati ukifika wanampa taarifa malaika wa mauti.

Na ikiwa umeishi kufuatana na mafunzo ya Quran basi utakwenda na furaha. Fahamu kwamba mambo yote yanatokana na Allahu taala. Usipige mayowe kwa kufiwa. Mambo kama haya yanampotezea mtu imani. Naudhubillah. Ufanyapo kosa na dhambi, basi lete tawbatan nasuha.

Hak subhanahu wataala anamwambia Izrail **(Roho za wapenzi wangu zichukuwe kwa upole na Roho za maadui wangu zichukuwe kwa ghadhabu.)** Al-iyadhu billahi ikiwa atakuwa ni asi!

Siku moja ya kiama ni sawa na miaka elfu moja au elfu hamsini. Kuna tafsiri nyingi juu ya jambo hili. Haya yanafahamika kutoka suratul Sajda aya ya 5 na suratul Maarij aya ya 4.

Baada ya hapo malaika wataichukua roho ya mtu asi kwa adhabu ambayo haielezeki kwa maneno. Tunajilinda kwa Allah aliyetuumba hali ya kuwa hatukuwepo. Baadhi ya watu wakati wa kutolewa roho watakuwa wanageuka huku na huko kama spiringi. Allah anayaeleza haya katika sura ya (Wannaziat.) Malaika wataitoa roho yake kwa nguvu na machungu hali ya kuwa wanazungumza baina yao. Jibril „alaihis-salaam"u atakuwa anawapa maelekezo (Msioneshe huruma yoyote kwake.) Roho ya mnafik itafika hadi kwenye pua, kisha

wataiachia kwanza. Wataanza kumbana na kumkamua viungo vyake vyote hadi macho yatamtoka. (Wewe si mja wa peponi. Muumba wa viumbe vyote amekughabikia. Huna msaada wowote hapa leo. Je umesahau uliyoyafanya wakati ulipokuwa hai? Ewe mja muovu wewe!) Tumekuandalia adhabu kali, adhabu ya wanafiki na makafiri. Wewe vile vile hukuwa ukisali, hukutoa zaka, hukutoa sadaka wala hukuwa na huruma kwa mafakiri. Hukuwa ukikaa mbali na maovu na mambo yako yote ni ufisadi. Ukisengenya kisha ukisema Allah karimu. Hii leo adhabu kali kwako. Kisha hapo Allah atatangazia. **(Hawa wanafiki hawakufikiria mauti hata mara moja. Walifanya kiburi. Hawakutekeleza ya fardhi, wajib na sunna. Wacha waione adhabu yangu sasa.)** Kisha mazabania kwa kutumia makucha yao watainganganua roho kutoka kifuani na kuileta kwenye mshipa wa kooni. Hapo wataambiwa tena **(Hivyo nyinyi wanazuoni hawakukuelezeni haya? Hamkua mkisoma vitabu? Hawa-kukwambieni msighafilike na msimfuate shetani? Hawa-kukwambieni mfahamu kuwa kila kitu kinatokana na Allah?)** Msikimbilie mapato ya kidunia. Kinaini kwa kile Allah anachokupeni. Waoneeni huruma mafakiri na walisheni maskini. Allahu taala ndie mfalme ambae wewe amekuumba na akachukua jukumu kwako la kukulisha na kila unapopata shida yoyote basi unamuomba yeye na utatuzi wa matatizo yako yote uko kwakwe. Usiseme kwamba nimewalipa matabibu na wakanitibu. Elewa kwamba hayo yote yametokea kwa kuwezeshwa na Allah. Hiyo unayoisema kwamba ni mali yako, kiuhakika ni amana tu umepewa. Hakuna suluhisho la matatizo yako katika mali hiyo. Hata ikiwa ni halali basi pia una wajibu wa kuitolea maelezo. Kile ambacho Allahu subhanahu wataala amekuandikia ndicho unachokipata. Mali, watoto na marafiki hawatakuokoa. Popote utakapokimbilia katika jangwa lolote lile huwezi kuokoka. Lazima utazikwa kwenye lile lile dongo ulilokwisha andikiwa. Kabla ya kufika ahadi yako hakuna aneweza kukuondoa duniani. Wewe una wajibu wa kujiepusha na mambo ya hatari na kuleta sababu ambazo zitaondosha matatizo yako.

Wakati wowote Allah akikupa neema ya mali, watoto, afya basi unafurahi na kusema Allah amenikirimu. Na ikitokea wakati Allah akikupa msiba au balaa basi unahuzunika, hufanyi subira na unasahau kushukuru.

Kisha itakuja amri ya Allah iseme **(Enyi malaika wa mauti! Mshikeni.)** Malaika watainganganua roho yake kutoka katika kila oteo

la nywele na kisha watamwachia tena. Hakuna anayeweza kuiondosha adhabu alioitoa Allahu taala.

Wakati akiwa katika hali hiyo ya kukata roho huku akipata adhabu hiyo atasema (Ee ole wangu leo, laiti ningelitekeleza yale niliyoamrishwa, leo yasingelinifika haya.) Kisha watanenezwa wale waliomzunguka maiti **(Enyi waja wangu mliotakabari!Huyo hapo sasa rafiki yenu;toweni mali basi mumuokoe. Ninapokuleteeni msiba duniani hamfanyi subira na huwa mnalalamika. Huyu hapa sasa mja, yuko kwenye adhabu na roho yake imefika kwenye mshipa wa shingo(hulkuum). Na hayo yote ni kwa uwezo wangu.)** Malaika watakaposikia maneno hayo watapukutika kusujudu huku wakisema (Ewe Mola wetu, hakika adhabu yako ni haki.) Allahu taala anayaeleza haya yote katika Quran kareem. Kisha malaika wataambiwa tena wamkamate. Kila sehemu ya mwili wake na kila oteo la nywele yake litahisi machungu ya adhabu. Malaika watamkemea kwa ghadhabu (Ewe roho ya mja alie muasi Allah, toka katika kiwiliwili. Leo ni siku ya adhabu. Wewe uliwapenda wengine kinyume na Allah. Na ulikuwa na majivuno kwa masikini, ukifanya mambo ya haramu, yaliyo ya haki ukiyaona ndio batil na yale ya batil ukiyaona ndiyo haki.) Haya pia yameelezwa kwenye Quran kareem.

Kisha mja atawambia malaika wamfanyie wepesi kidogo ili alau arudishe akili, lakini atakuta tayari malaika wa mauti amemsimamia kichwani kwake. Baada ya kumuona malaika wa mauti adhabu zote hizi atazisahau na ataanza kutetemeka huku akisema (malaika wote hawa waliopo hapa wanaonitesa mimi hawatoshi? Wewe nani tena? Umekuja kufanya nini?) Kisha mauti yatamwambia(Mimi ndie mauti. Nimekuja kukuondoa duniani ili watoto wako wabakie mayatima na mali zako zirithiwe na wengine.)

Baada ya kuyasikia maneno haya kutoka kwa mauti atatetemeka na kugeuza uso wake upande wa pili. Hii ndio alama ambayo imetajwa katika hadithi sharif iliyo katika Bukhari. Mtume “sallallahu alayhi wasallam” amesema (**Atakapowasikia malaika atageuza uso wake ukutani na mbele yake atayaona mauti yamemsimamia.)**

Upande wowote atakaogeuka basi mauti anayaona yako upande huo, nae ataendelea kugeuza uso.

Hapo malaika wa mauti atasema (Mimi ndie malaika w a mauti. Mimi ndie niliyemuuwa baba yako na mama yako na wewe ulikuwepo, je kuna lolote uliweza kufanya! Leo, hawa hapa marafiki zote kuna lolote watakaloweza kukusaidia!Mimi ndie huyo malaika wa mauti na wale niliowauwa kabla yako walikuwa na nguvu zaidi kuliko wewe).

Wakati anajibizana na hawa malaika, wale malaika wa adhabu wataondoka na kwenda zao.

Kisha atamuona malaika wa mauti kwa haiba yake ya kimalaika na hapo atazirai.

Kisha Izrail alaihis-salaam atamuuliza ni kipi ulichokipata duniani? Atasema mja (maovu ya dunia yalinihadaa ndiyo nikafikia hali hii).

Kisha Allah atamletea dunia katika umbile la mwanamke mwenye macho mabaya yenye kiza kama mawingu, mwenye meno kama pembe za ng'ombe na mwenye kunuka harufu mbaya.

Huyu atakuja amkalie kifuani pake. Kisha zitaletwa mali zake alizozichuma kwa shida kwa kutumia njia za halali na haramu na mbele ya macho yake ataoneshwa wakirithishwa jamaa zake.

Kisha hiyo mali itamgeukia huyo mmiliki wake na kumwambia **(Ewe asi!Ulinichuma mimi ukanitumia katika mambo yaliyokatazwa. Hukutoa zaka wala sadaka. Je unaona sasa! Nimetoka mikononi mwako na nimeingia mikononi mwa usiowapenda. Wamenichukua bila ya hata shuQuran.)**

Hapo atageuka huku na huko hali ya kuwa na kiu kubwa na unguliko na moyo.

Wakati akiwa katika hali kama hii shetani atapata fursa na kutaka kujaribu kuchukua imani yake. Atakuja hali ya kuwa mkononi mwake ana bilauri ya maji ya baridi na kumsimamia kichwani mwake huku akiyatikisa. Atamwona huyo shetani na kumsikia. Huo ndio wakati na mahali ambapo hali ya masikini na tajiri itakuwa wazi. Ikiwa ni mtu muovu basi atasema kumwambia shetani ampe hayo maji ili anywe.

Shetani nae atamtaka kwanza akanushe kuwepo kwa Allah muumba wa ulimwengu wote.

Ikiwa ni mtu muovu hapo atamkanusha Allah na imani yake itapotea wal-iyadhubillahi mindhalika. Lakini mambo yote yako kwenye hikma ya Allah na mgonjwa alie katika hali hiyo ni vyema awepo mtu mwenye bilauri ya maji na awe kila wakati anamfungua mdomo na kumnywesha maji.

Ikiwa ni mtu mwema basi atamkatalia shetani na kuokoka.

Ukifika wakati wake na ikiwa ni muumim amri hutolewa. Izrail "alaihis-salaam" atachukua roho yake, malaika mia tatu na sitini wataipokea hiyo roho kutoka kwa Izrail "alaihis-salaam" na watatoweka bila ya kuonekana na jamaa na marafiki, wataivisha roho hiyo vazi la peponi, kisha watakwenda kuitembeza kwenye makasri ya peponi na kuirejesha tena na ikiwa ni mja muovu basi watakuja na

majani ya mzakum ambayo ni meusi kuliko makaa, waizonge roho yake. Kisha watashuka nayo chini kwenye mashimo ya moto ili wakaioneshe sehemu yake, kisha watarudi nayo tena.

Ikiwa mtu baada ya kubalegh, aliishi duniani kwa alivyoishi, akafanya madhambi kisha asilete toba. -naudhu billah-huu ndio mwisho atakaoupata. Siku ya kiama atakuwa ni mwenye kuhasarika na ataingia motoni, ila kama atapata uongofu kutoka kwa Allah au shifaa ya mtume “sallallahu alayhi wasallam”.

## KIFO CHA WALIO MAASUM (WATOTO)

Mtoto wa kiislam akiumwa akifa malazi yake yanakuwa ni Makami illiyina yaani pepo. Wakati akiwa anataka kukata roho hujiwa na malaika mia tatu na sitini na humwambia (Ewe maasum! Hongera ziwe kwako. Leo ndio ile siku ambayo mama zako, na mababu zako waliopita pamoja na majirani zako unaweza ukawaombea kwa haki taala utakacho)Malaika mia watamvisha taji la shafaat, malaika mia watamvisha taji la mapenzi, malaika mia watamvisha shati la nguvu na jitihada na malaika sitini watamuondoshea pazia lililo katika macho yake. Baada ya kuondoshwa hilo pazia atawaona mababu zake wote waumini hadi kufikia kwa Adam. Miongoni mwa hawa atawaona wale ambao wameshatayarishwa kwa ajili ya adhabu. Hapo atatetemeka na kuanza kulia. Baadhi ya watu wanadhania kuwa kilio hichi ni cha machungu ya kutoka roho.

Hapo watafika malaika watoa roho. Ila kwa vile watamkuta amevaa taji la shafaat na shati na kwamba pazia la macho limeondoshwa, watashindwa kuchukua roho yake na watamwambia (Ee masum! Muumba wa viumbe vyote anakusalimu na anasema yeye ndie aliyekuumba kwa hivyo urudi kwake. Hiyo roho yeye ndie aliyekupa amana kwa hivyo umrejeshee. Badala yake atakupa pepo na majumba yake. Kama huamini nyanyua macho juu utaona.) Hapo huyo mtoto ataangalia na kuona malaika na Jamalullah(uzuri wa Allah). Atatetemeka kwa furaha midomo ikimcheza na uso utapiga rangi nyekundu. Hapo atataka kuruka ili akabidhi roho yake lakini ataziona tena zile hali za mababu zake walio katika adhabu hivyo atasita kuikabidhisha roho yake. Malaika watamuuliza tena (Ewe Masum, kwa nini huikabidhishi roho yako?) Atasema yule mtoto (Enyi malaika, niombeeni kwa Allah taala, awasamehe jamaa zangu na mababu zangu kwa ajili yangu.) Malaika watasema kumwambia Allahu taala (Ya Rabbi! Yaliyopo baina yetu na huyu mtoto unayaelewa vizuri) Hapo Allah atasema (Kwa hakki ya Izza yangu nimewasamehe) Kisha malaika

watamwambia(ewe maasum, habari njema kwako. Wale walio waumini wamesamehewa madhambi yao na yale yote uliyotaka Allah amekupa) Hapo atakuwa katika hali ya furaha na Allah atampelekea mahuri wawili wakiwa na sura za baba na mama yake, watamnyooshea mikono na watamwambia (Njoo na sisi. Hatuwezi kukaa peponi peke yetu). Hapo watachukua tofaa la peponi lenye harufu ya kuvutia watampa. Huyo mtoto atalichukua hilo tofaa na wakati akilinusa Izrail aleyhi salamu atakuja kwa hali kama yake yeye na ataichukua roho yake.

Katika riwaya nyengine, wakati akilinusa hilo tofaa, roho yake itaganda hapo kwenye tofaa na malaika wa mauti wataichukua roho yake kutoka kwenye tofaa.

Kisha malaika wa mauti wataichukua hiyo roho, watazunguka nayo mbinguni na kwenda nayo peponi. Huko kutakuwa na mji wenye zabardan za kijani. Mtoto atawauliza kwa nini wamempeleka pale nao watamjibu “siku ya kufufuliwa itakuwa na joto sana. Katika eneo hili kuna chemchem za rehema sabini elfu. Mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allah atakaa pembeni ya bwawa na utaona bilauri za nuru. Wakati wazazi wako na mababu zako watakapofika uwanja wa hesabu, basi utajaza bilauri hizi na kuwapelekea, kisha utawashikilia kwa makini ili wasije wakaenda njia ya motoni na wakapata adhabu. Hii ni kwa sababu dua zako wewe zinakubalika mbele ya haki taala. Na siku za Ijumaa utakuwa unashuka chini na kuzifikisha salamu za Allah kwa umati wa Muhammad “sallallahu alayhi wasallam” na utawafikishia nuru juu yao na baraa ya shukrani zao utamfkishia Allahu taala.

Baada ya kumaliza safari hii, roho hurejeshwa pale ulipo mwili. Wakati wa shughuli zote za kutayarisha maiti, kuikafini, kusalia na kuzika, na kuulizwa ndani ya kaburi, roho huwa juu ya kaburi. Iwapo wazazi watakufa bila ya imani basi huwekwa pazia baina ya mtoto na wazee na mtoto hatowatafuta wala hataonana nao wazee wake. Haya ndiyo matokeo ya mtoto wa kiisalm anaekufa kabla ya baleghe.

## KIFO CHA MWANAMKE MUISLAM

Iwapo mwanamke muislam atakufa kwa uja uzito au kwa uzazi, au akafa kwa maradhi ya tauni au bila ya lolote kati ya haya, ikiwa tu alikuwa akijisitiri stara ya kisheria na alikuwa mwema kwa mumewe basi wakati wa mauti yake malaika wa peponi watakuja na kujipanga mbele yake kwa heshima na ukarimu na watasema (Ewe mjakazi shahidi mpenzi wa Allah, toka uje, unataka nini katika kasri za

dunia?Allah yuko radhi nawe. Kutokana na maradhi aliokupa, amekusamehe madhambi yako na amekutunukia pepo. Njoo uisalimishe hiyo amana. Baada ya kuona daraja hili alilofikia huyu mwanamke atakuwa tayari kusalimisha roho yake ila atatizama ubavuni kwake kisha atasema (marafiki zangu wahukumiwe na wasamehewe. Kisha ndio nitasalimisha roho yangu) Malaika watayafikisha maombi yake kwa Allahu taala na hapo Allah atatangazia (Kwa haki ya utukufu wangu, dua zote za mja wangu nimezitakabalia). Malaika watampa habari njema . Kisha atakuja malaika wa mauti na malaika wengine mia na ishirini. Nuru iliyo katika uso wao imepaa hadi kwenye arshi, wamevaa mataji juu ya vichwa vyao na nyuma yao kuna hulla za nuru na miguuni mwao wana vikuku vya dhahabu. Watashuka na matunda ya peponi hali ya kuwa wananukia kuliko miski watamsalimia kwa heshima na upole na watamwambia (muumba wa ulimwengu anakusalimia na amekupa pepo ambayo utakuwa jirani na Muhammad sallallahu alayhi wasallam na utasuhubiana na Aisha).

Huyu mwanamke muumini litaondoka pazia kwenye macho yake na atawaona wanawake wengine waumini waliokuwa na makosa wakiwa adhabuni. Hapo ataomba (Mola wangu wasamehe madhambi yao). Hapo atasema Allah (Ewe kijakazi, matakwa yako yote nimekutakabalia. Salimisha amana. Mke na mtoto wa kipenzi changu wanakusubiri. Mara tu asikiapo wito huu roho itamtetemeka na miguu itakazana huku akitokwa na jasho tayari kukabidhi roho yake. Hapo watakuja malaika wawili wamebeba vijinga vya moto, mmoja atamsimamia kulia na mwengine atamsimamia kushotoni kwake. Shetani alilaaniwa nae atafika huku akijisemea (sitegemei mafanikio kwa huyu lakini wacha nijaribu). Hapo atamuonesha jagi lililotengenezwa kwa vito vya thamani na bilauri yenye maji baridi. Wakati malaika watakapomuona huyu kiumbe muovu watavunja lile jagi na watamfukuza. Huyu mwanamke muumin atacheka kwa kuwaona Kisha malaika watumishi wa peponi watawaita mahuri ambao watakuja na kinywaji cha peponi ndani ya bilauri iliyotengenezwa kwa vito vya thamani. Atapewa maji na wakati anakunywa kwa ladha roho itatoka na kuganda kwenye bilauri, kisha malaika wa mauti ataichukua kutoka kwenye bilauri. Malaika watasema **(Innaa lillahi wa innaa ilayhi rajiun)** Malaika atapaa nayo roho yake hadi peponi, atamuonesha sehemu yake kisha roho atairejesha kilipo kiwiliwili.

Wakati wakimvua nguo na kumfumua nywele zake roho itahudhuria hapo alipo na itasema (ewe mkoshaji !mshike pole pole

kwani makucha ya Izrail tayari yamemtia machungu. Mwili ulipata shida na kutetereka.) Na inapofika wakati wa kumiminiwa maji na kusuguliwa roho itakuja tena na kusema (Maji usiyafanye ya moto sana kwa sababu mwili wangu ni dhaifu. Nisugue kwa wepesi ili nipate raha). Wakati wa kukafiniwa roho pia itasita hapo kidogo na kusema (Hii ndio mara ya mwisho ya kuonekana hapa duniani. Nataka niwaone ndugu na jamaa zangu na wao wanione ili wapate mazingatio. Wao pia karibuni watakufa kama mimi hivyo wasipige mayowe nitakapoondoka. Mimi wasinisahau, wanikumbuke siku zote kwa kusoma Quran. Wasigombane kwa urithi wangu ili nisije nikapata adhabu huko kaburini. Wanikumbuke siku za Ijumaa na siku za sikukuu).

Kisha atakapowekwa kwenye msala roho itasema tena(Kuweni na amani enyi wanangu, baba na mama. Hakuna siku ya kufarikiana inayozidi hii. Hatutaonana tena hadi siku ya kiama. Kwaherini enyi wenye kutoa machozi kwa ajili yangu.)

Na wakati jeneza limebebwa roho itasema (Nipelekeni pole pole, ikiwa lengo lenu ni kupata thawabu basi msinipe shida mimi. Nipelekeni mbele ya Allah kwa utulivu.)

Wakati akifikishwa kaburini roho itasema (Oneni na mpate mazingatio. Mtaniacha katika kiza hichi na mtakwenda zenu. Mimi nitabaki na amali zangu tu. Baada ya kuiona hali hii basi msidanganyike na dunia isiyo na ihsani yenye kudaganya.)

Wakati mwili umeshazikwa, roho itakaa upande wa kichwani. Maiti asiachwe bila ya kusomewa **(Talkin)**. [Kumsomea Talkin maiti mwema ni sunna. Wahabi hawaamini kuwa talkin ni sunna. Wanasema kuwa ni bid’a na kwamba maiti hasemeshwi wala hasikii. Maulamaa wa ahli sunna wameandika vitabu mbali mbali kuthibitisha kusihi kwa Talkin. Miongoni mwa vitabu hivyo ni kitabu kiitwacho **(Nurul yaqin fiy mabhathi talkin)** kilichoandikwa na Mustafa bin Ibrahim Siyami “rahmatullahi alaih”. Hapa imeandikwa hadithi sharif iliyopokewa na Tabarany na Ibn Manda “rahmatullahi alaih”. Katika hadithi hii, imeamrishwa kumsomea maiti talkini. kitabu hiki kiliandikwa mwaka 1396 hijria huko Siyam, Bangkok. Chapa yake ya pili ilitolewa mwaka 1396 hijria (1976 miladia) huko Istanbul.] Kwa amri ya Allah maiti huamka kama mtu aliye usingizini na huona yuko sehemu ya kiza. Atapiga kelele kumwita mtumishi wake, kijakazi chake au msaidizi wake na kumwambia (Niletee mshumaa) Hakuna sauti itakayomjibu kumpa faraja. Kaburi litagawika pande mbili na hapo watatoka malaika wawili waulizaji, Munkar na Nakir. Cheche za moto zinatoka midomoni mwao na moshi unatoka masikioni mwao. Watamkaribia na

kumwambia. **(Man rabbuka, wamaa dinuka, wa man nabiyyuka)**. Maneno haya maana yake (Mola wako ni nani? dini yako ni ipi? na mtume “sallallahu alayhi wasallam” wako ni nani?) Ikiwa atayajibu maswala haya kwa usahihi, watampa bishara njema kutoka kwa Haki taala kisha watakwenda zao. Kisha kaburi litapasuka upande mmoja na atatoka mtu mwenye uso unaong’ara kama mwezi na atamkaribia. Huyu mwanamke muumini atamuuliza (wewe ni nani?) Atajibu (Mimi nimeumbwa kutokana na Subira na shukran ulizozifanya ulipokuwa duniani. Nitakuwa nawe hadi kitakapofika kiama.)

**Nafsi isipoacha kutaka ya haramu**
**Moyo hauwezi kuakisi nuru itokayo kwa mola**

## KIFO CHA WATU WALIODHULUMIWA, WANYONGE WENYE SUBIRA

Hawa wote mauti yao ni sawa. Tutaelezea mauti ya mmoja wao ambayo ndiyo yatawakilisha ya wengine.

Wanyonge ni wa aina mbili. Kuna yule mtu anayeishi mbali na mji wake na jamaa zake na kuna yule anaeishi katika mji wake na jamaa zake lakini yeye ni fakiri. Hakuna mtu anaemthamini. Waumini kama hawa ni wanyonge na wakifa wanakufa shahidi. Ikiwa mtu atafikisha umri wa miaka sitini na akawa hakuacha kusali sala tano basi pia anakuwa shahidi[Yule ambae mauti yake yatatokana na kutenda tendo la haramu, mfano akadhurika kwa pombe aliyokunywa akafa, huyu hawi shahidi. Lakini kama atakufa kwa sababu nyengine wakati anafanya haramu , mfano kuangukiwa na jengo, huyu atakuwa shahidi. Wanawake na watoto wa kike , sehemu yao yote ya mwili ni utupu isipokuwa uso na viganja. Kujifunika ni fardhi. Na kudharau amri ya kujifunika ni ukafiri. Wale watakaoshikama na amri ya stara ya kiislam wakaacha kutembea nywele , vichwa . miguu na mikono wazi, basi nao ni mashahidi. Amri na makatazo ya Allahu kwa ujumla huitwa **(Ahkam za kiislam)**. Baba au mama mwenye kujifunza ahkam za kiislam akawafunza na watoto wake basi huyo nae ni shahidi.] wasio na imani na wale wasio Sali hawawezi kuwa shahidi. Kafiri ambae atauliwa kwa dhulma na mateso hawezi kuwa shahidi. Atakufa kafiri na hatoingia peponi aslani.

Watu hawa wakiweka vichwa vyao kwenye mto wakati wa mauti yao, basi mbingu hufunguka na hushuka malaika ambao idadi yao ni Allah pekee anaeijua. Watakuwa wamebeba taji na nguo inayotokana

na nuru. Wataiita roho ya huyo mtu kwa heshima. Haya anayatambulisha Allah mwishoni mwa suratul Fajr.

Shahidi mwengine ni yule muumini aliyeelekeza uso wake kwa Dargah Iza na kusema (Ewe muabudiwa wangu, mimi sijawahi kuegemeza mategemeo yangu kwa yeyote zaidi ya utukufu wako, wala sikuwahi kuinamisha shingo yangu. Sikuhadaiwa na maovu ya dunia wala na maadui wa dini. Ewe mola wangu, mategemeo yangu hivi sasa kwako ni kwamba uusamehe umati wote wa Muhammad) Huyu pia ni shahidi.

Wale malaika maalum watamvisha hio nguo kisha yatatoka maelekezo kutoka kwa Allah wa Haki (Mpelekeni peponi. Huyu alikuwa akisali duniani kwa ziada na akipenda wageni. Akisamehe wanaomkosa na akileta istighfar anapokosea. Na alikuwa akinitaja sana mimi. Alikuwa hatoki nje bila ya stara ya kisheria. Alikuwa akijitakasa na mambo ya haram na akimtii mtume "sallallahu alayhi wasallam" na Uislam.)

Kisha wale malaika wawili wa kushoto na kulia wenye kuandika ya kheri na shari ya binaadamu watasema(Ewe Mola wetu! Sisi ulituwakilisha kwa mja huyu huko duniani. Na leo tupe fursa ya kuichukua roho yake twende nayo mbinguni.) Amri ya Allah itasema(Nyinyi bakieni pembeni ya kaburi lake. Mtaleta takbir na tasbih na mtanisujudia kisha thawabu za hayo mtazitoa kwa ajili ya mja wangu) Malaika hao watendelea kufanya hivyo hadi siku ya kiama na thawabu hizo zitaandikwa kwa huyo mja.

[**UZINDUZI:** Wanafiki wa huko misri walifanya uasi na kuja Madina kwa ajili ya kumuua Khalifa Uthman. Na wale wanafiki walio Madina waliwaunga mkono kwa maneno ya uongo na uzushi. Nao waliwasema vibaya masahaba kwa kudai kuwa hawakumsaidia khalifa. Uhalisia ni kwamba Khalifa alikuwa akitaka kukutana na mashahidi walio daraja la juu na akiomba dua kwa hilo. Hivyo wale waliokuja kumsaidia aliwazuia. Kutokana na hivyo wale waasi waliweza kumfikia khalifa kirahisi na kumuua. Hivyo khalifa akawa amefikia matakwa yake na dua yake ikawa imekubaliwa. Mashahidi huwa hawapati uchungu wakati wa kukata roho. Huwa wanaoneshwa ladha ya neema watakazozipata peponi, hivyo huzisalimisha roho zao kwa malaika kwa mapenzi kabisa].

## KIFO CHA MAKAFIRI

Mtu kafiri au murtadi ambae haupendi Uislam, ambae anasema Quran kuwa ni kanuni za jangwani, ambae mja bora kuliko wote

Muhammad anamwita kuwa mchunga ngamia, ambae hana akili wala tabia, ambae ni mwenye kichwa kigumu na asiyewafikiana na uislam dini ambayo imeleta utulivu na furaha kwa watu na ikawapa elimu, tabia, usafi, afya na uadilifu, ambae ni dhalili mwenye kusema kuwa dini haina uhitaji, aliejiachia kwa matamanio ya nafsi yake, mjinga huyu wakati anapokufa huondolewa pazia katika macho yake na akaoneshwa pepo. Malaika aliye mzuri atamwambia(Ewe kafir! ambaye uliwaita waislam kuwa ni walio nyuma na wale wenye kukimbizia shahawa za nafsi, wavunjaji wa sharia za maadili mema kuwa ndio walio kwenye muangaza. Ulikuwa kwenye njia isiyo sahihi. Hukuipenda dini ya haki ya Uislam. Wale waliomuamini Muhammad „alaihis-salaam" wakaamini yale yalieshushwa na Allah na wakayaheshimu basi ndio wataingia katika pepo hiyo.) Ataziona neema za peponi. Mahuri walio katika pepo watamwambia (Wale wenye kuamini wataokoka na adhabu ya Allah). Kisha atatokea shetani katika sura ya muhubiri na atamwambia(Ewe fulani bin fulani, wamekwambia uongo hao waliopita. Neema hizo zote ulizoziona zitakuwa zako. Kisha ataoneshwa Jahannam. Ataona milima ya moto, nnge na matandu wakubwa kama nyumbu. Hapo atazishuhudia adhabu zilizotajwa katika hadithi sharif. Malaika wa motoni waitwao mazabbania watawapiga kwa vinga vya moto. Wanatoka chechea za moto midomoni mwao. Urefu wao ni kama mnara na meno yao ni kama pembe za ngombe dume. Sauti zao kama ngurumo za mvua. Wakati kafiri atakaposikia sauti yake atatetemeka kwa woga na kisha atageukia upande wa shetani, lakini shetani nae ataogopa na kukimbia. Malaika watamnyaka shetani na kumpiga na chini kisha watamgeukia kafiri na kumwambia (Ewe adui wa Uislam! Duniani mtume "sallallahu alayhi wasallam" wa allah sallallahu alayhi wasallam hukumuamini. Sasa pia malaika huwaamini!bado unadanganywa na shetani?. )Kisha watamfunga mnyororo wa moto shingoni mwake na watamvuta miguu yake hadi ifike kichwani katika hali ya kwamba miguu itakuwa nyuma ya kichwa. Kisha watauvuta mkono wa kulia upande wa kushoto na mkono wa kushoto upande wa kulia katika hali ya kwamba mikono yote itakuwa imetokeza mgongoni. Kuna aya tukufu inayotuelezea tukio hili. Atalia na kuwaita washiriki wake wa duniani. (Ewe kafiri! Ewe uliekuwa ukiwadhihaki waislam. Wakati wa kuomba umepita. Wakati wa kuamini umepita. Huu ni wakati wa kuadhibiwa kwa ukafiri wako. ) Watauvuta ulimi hadi ufike kisogoni na watayachokoa macho yake. Watamfikishia aina kadhaa za adhabu, kisha wataichukua roho yake khabith na watairembea motoni. Allahu taala atujaalie tusalimishe roho zetu hali ya kuwa tumeamini na

kuyafuata aliyokuja nayo mtume “sallallahu alayhi wasallam” Muhammad sallallahu alayhi wasallam kama yalivyoelezwa na maulamaa wa ahli sunna katika vitabu vyao.

Ishi muda utakaoishi, lakini jua kua mwisho utakufa. Anasema mtume “sallallahu alayhi wasallam **(Wakati binaadamu anapokufa ataita muitaji aseme, ewe binaadamu, je ni wewe ulieiacha dunia au dunia imekuacha wewe? Wewe ndie ulieikusanya dunia au dunia ndio iliyokukusanya wewe? Wewe ndiyo umeiua dunia au dunia imekuua wewe? Wakati maiti anapoanza kuoshwa mambo matatu ataulizwa.**

**1. Uko wapi mwili wako wenye nguvu? Kipi kimekudhoofisha.**

**2. Uko wapi leo ufasaha wako wa maneno? Nani amekunyamazisha?**

**3. Wako wapi rafiki na wapenzi wako? Mbona wamekuacha?**

**Wakati maiti akivishwa sanda itasemwa tena: Usisafiri bila mahitaji. Hii ni safari isiyo na marejeo. Sehemu utakayofikia itakuwa imejaa malaika wa adhabu.**

**Wakati maiti akitiwa kwenye jeneza itasemwa tena: Hongera ikiwa umepata radhi za Allah, furaha na utukufu utakuwa kwako. Lakini ikiwa umepata ghadhabu za Allah basi ole wako. Wakati jeneza limewekwa pembeni ya kaburi basi atasema msemaji: Ewe binaadam! Umetayarisha nini huko duniani kwa ajili ya kaburi? Umeleta nuru gani kwenye kaburi hili lenye kiza? Umeleta nini kutoka kwenye utajiri wako na umaarufu wako? Umeleta nini kwa ajili ya kutandika na kulipamba hili kaburi lililo tupu? Wakati maiti imewekwa ndani ya kaburi litasema kaburi (Ulikuwa ukizungumza nyuma yangu lakini leo umelala ndani yangu kimya.) Shughuli za mazishi zikimaliza na watu wakitawanyika hapo utatoka wito kutoka kwa Allahu taala (Ewe mja wangu! Umebaki pekee. Wamekuacha katika kaburi lenye kiza na wamekwenda zao. Hao walikuwa marafiki zako, wanao, ndugu zako na wapenzi wako. Lakini hakuna hata mmoja mwenye faida na wewe hivi sasa. Ewe mja wangu! Wewe uliniasi, amri zangu hukuzitekeleza na hali hii hukuikumbuka. Na ikiwa maiti ni muumini basi inategemewa kwamba Allahu taala atamdhihirishia msamaha wake na kumwambia:ewe mja wangu muumin, haipendezi kwa shani yangu kukwachia pekee ndani ya kaburi. Kwa haki ya izza na utukufu wangu nitakupa rehema za kuwashangaza marafiki wako. Nitakupa huruma zaidi ya mapenzi ya baba na mama kwa mwanawe. Kwa huruma zake na upendeleo, atamsamehe mja huyo dhambi zake zote, na atalifanya kaburi lake kuwa bustani ya peponi ilojaa mahuri na**

**neema za peponi. Allahu taala ni mwenye rehema nyingi na humsamehe mja wake mwenye dhambi. Ana rehema nyingi kwamba hata anapoyaona madhambi ya waja wake mara kadhaa kila siku basi anawafichia na hawaaibishi. Kwa hivyo inafaa kwa mola kama huyu kuzitii amri zake na kuyaacha makatazo yake. Kila siku inafaa kutenda mambo mema ili kujikinga na adhabu za kesho.)**

[Waumini wote wenye madhambi na wasio na madhambi, wataulizwa kaburini. Makafiri wote na wale waislam ambao madhambi yao hayakusamehewa hao watapata adhabu ya kaburi. Wale wanaotia chokochoko baina ya waislam na wale wenye kurukiwa na cheche za mikojo wakienda haja hao pia watapata adhabu ya kaburi. Adhabu ya kaburi haitokuwa kwa roho pekee bali itakuwa kwa roho na mwili. [Tusijaribu kufumbua kwa akili zetu vitendawili ambavyo akili haiwezi kuvifumbua]

Ikiwa mtu amekufa kafiri basi atapata adhabu hadi siku ya malipo na kisha atarembewa kwenye Jahannam. apate adhabu ya milele.

Ewe mgeni unaeishi, usimpe moyo wako yoyote zaidi ya Allah.

Hatobakia mtu duniani. Zaidi ya Allah hakuna anayeweza kitu. Hakuna atakaebakia zaidi yake.

Kila mtu anapata matatizo. Siku za raha na za shida. Hii dunia dhalili hakuna haja kushughulika nayo.

Mimi pia nilikuwepo wakati fulani. Nilikuwa kama pete ya almasi kwa raisi wa nchi. Nilikuwa kama ndio saini ya maamuzi ya sultani. Lakini kadar hatimae nami imenigeuka**.**

Ulifika wakati moyo wangu uliumwa, nguvu zikapotea naroho nayo ikatoka. Kwa sababu mwili ulikwishamalizika.

Afya yangu ikazimika kama mshumaa. Kila sehemu yangu ikaingia kiza. Jua la akhera likachomoza. Imeangaza kwa nuru ya Allah.

Hapo nikarudi kwa mola wangu. Madhambi yangu yakadhihiri nilipoomba msamaha, akanipa rehema zake zisizo kifani.

Ewe mola, hata kama nitakuwa na dhambi kwa mamia ya maelfu, ninakuja na uso wangu mweusi kwenye mlango wako mtukufu. Naomba msamaha wako.

Jina lako la ghafur nimeliandika tarehe hii (1286). Maana yake bila ya shaka itakuwa madhambi yangu nitasamehewa. Hakuna mwengine zaidi ya Allah anayeweza kufanya lolote. Hakuna mwengine atakaebaki zaidi ya Allah.]

**Abdulrahman Sami pasha alieandika shairi hili alikuwa ni mmoja wa majenerali wa dola ya Uthman. alikufa akiwa ni mjumbe wa seneti mwaka 1295 hijria (1878 miladia).**

**Maisha ni kama ndoto iliyojaa matatizo**
**Tunazaliwa na mara tunakufa**
**Hata ukipata raha, ni za muda gani?**
**Matatizo yanazikimbiza raha zote.**

**Mara tutaondoka, tukiwa majahil tulioghafilika**
**Tutakwenda pweke kwenye kina cha mauti**
**Kwenye dimbwi la mazito na matatizo**
**Dunia inatusukumiza kusiko na suluhisho.**

**Nasi tupo tunaiangalia hii dunia**
**Tunaulizana wapi wametokea wakazi wake**
**Muumbaji wake, viumbe na siri zake**
**Hikma ya kuwepo kwake tungependa kuijua.**

**Lakini siri yake imefichwa na Allah mwenyewe**
**Haiwezi kufahamika kwa akili ya mja**
**Binaadamu ni mwenye kushindwa, alieghafilika na mjinga**
**Ataendelea kukosea kwa sahau juu ya sahau**

## KUZURU MAKABURI NA KUSOMA QURAN

Kuzuru makaburi ni sunna. Wiki mara moja, na kama haiwezekani basi alau siku za sikukuu yafanyiwe ziara. Kutembelea makaburi siku ya Alkhamisi, Ijumaa au Jumamosi kuna thawabu zaidi. Katika **(Shiratul Islam)** sehemu ya mwisho anasema:kuzuru makaburi ni sunna. Mwenye kuzuru makaburi anatakiwa afanye mazingatio kwa hali ya maiti ambaye mwili wake tayari umeoza. Uthman alikuwa akilia sana anapopita karibu na kaburi, hata ndevu zake huroa kwa machozi. Maiti nae hufaidika na dua anazoombewa. Mtume “sallallahu alayhi wasallam” sallallahu alayhi wasallam alikuwa akitembelea makaburi ya jamaa zake na masahaba zake ridhwanullahi alayhim. Baada ya kuwaombea dua akikipa mgongo kibla na akikaa hali ya kuwa amelielekea kaburi. Kupangusa mikono na uso kwenye kaburi na kulibusu dongo lake ni katika ada za wakristo. Katika hadithi sharif tunasoma **(Mtu yeyote atakaekwenda kwenye kaburi la mtu anaemjua na akatoa salamu, basi maiti humfahamu mtu huyo naye humjibu salamu yake.)** Anasema Ahmad ibn Hanbal “rahmatullahi alaih” (Wakati mtu anapopita karibu na kaburi asome ikhlas, kulaudhu mbili na fatiha kisha amzawadie thawabu hizo huyo maiti. Thawabu

hizo zitamfikia)Katika hadithi sharif iliyopokelewa na Anas bin Malik **(Ikiwa itasomwa Ayatul kursiyyu na thawabu zake wakapelekewa maiti, Allahu taala thawabu hizo huwafikishia maiti wote.)**

Anasema katika **(Hazaanatu riwayat)** (Wanazuoni ambao walikuwa wakitembelewa wakati wakiwa hai, basi inajuzu kuwatembelea baada ya kufa hata kama watakuwa masafa ya mbali. Hakuna tafauti katika faida inayopatikana baina ya kuzuru kaburi la mtume “sallallahu alayhi wasallam” sallallahu alayhi wasallam, mawalii na wanazuoni. Tafauti iliyopo ni baina yao wenyewe kwenye daraja zao.

[Iwapo mtu atatundika chumbani bango lenye jina la maiti anaempenda au akaandika jina kwenye jiwe na akalichomeka kaburini kwa huyo mtu, watu watakapoliona jina hilo hapo chumbani au kaburini wakampigia fatha na kumuombea dua maiti huyo, basi Allah humrehemu mtu huyo na kumsamehe madhambi yake. Kutokana na hili, ndio imekuwa ada kwa nchi za kiislam kuandika majina katika kuta za vyumba na makaburini. Ikiwa litaandikwa jina la walii, na likatajwa jina la walii huyo kisha mtu akamtaka amuombee dua na shufaa kwa Allah, basi walii huyo husikia na akamuombea hiyo dua, nae Allah huitakabalia dua hiyo.]

Pamoja na kwamba inajuzu kwa wanawake kuzuru makaburi, lakini lililo bora zaidi kwao ni kutotembelea makaburi zaidi ya lile la mtume “sallallahu alayhi wasallam”. Pamoja na kwamba inajuzu kwenda makaburini hali ya kuwa na janaba na hedhi, lakini lililo sunna ni kuwa na udhu. Katika hadithi sharif tunasoma kwamba (Mtu atakaezuru kaburi la muumin na kasema **(Allahumma inny as-aluka bihakki Muhammadin wa ali Muhammadin anla tuadhiba hadhal mayyit) (basi huondolewa adhabu kwa maiti huyo.)** Ni kaburi la baba na mama tu ndio inajuzu kubusu dongo lake. Katika kitabu kiitwacho **Kifaya** anasema. Kuna mtu alimwambia mtume “sallallahu alayhi wasallam” kwamba ameapa kubusu mkabala (kilicho sawa) wa mlango wa peponi, je afanye nini? Akasema mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allah **(Ibusu miguu ya mama yako).** Akasema huyu mtu kuwa baba na mama yake wameshakufa. Akasema mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa Allah **(Busu makaburi yao. Ikiwa huyajui chora mistari miwili hali ya kunuwia kuwa hayo ni makaburi yao na kisha uibusu. Hapo kiapo chako kitakuwa kimeondoka).**

Inapendeza kwa makaburi ya watu watukufu yaliyo mbali kuyazuru endapo itakuwa tayari mtu anashughuli nyengine inayomfanya asafiri kuelekea huko. Ni ziara ya kaburi la mtume “sallallahu alayhi wasallam” wetu sallallahu alayhi wasallam pekee ndio yenye kupelekea kupata

thawabu. Yule mwenye kumtembelea mtume “sallallahu alayhi wasallam” sallallahu alayhi wasallam na mawalii ridhwanullahi alayhim basi hufaidika na roho zao tukufu. Moyo wake husafika kwa kiasi ya penzi na fungamano lake alilonalo kwao. Ikiwa kwenye makaburi hayo ya watu watukufu kutakuwa na watu wanaofanya madhambi, mfano kuwepo kwa wanawake wasio na stara ya kisheria, haipelekei kuacha kufanya ziara. Ikiwa atashindwa kuwazuia basi achukie kwa moyo. Kwani hata katika maziko ya muumin, iwapo kuna wanawake , au pakaimbwa na kusomwa kasida na mashairi, bado ulazima wa kwenda unabakia pale pale.

Ni haramu kwa wanawake kuzuru makaburi ikiwa hilo litapelekea wao kuhuzunika, kulia na kupayuka au ikiwa itapelekea mchanganyiko na wanaume na kusababisha fitna. Wanawake hawa huwa wanapata laana. Pamoja na kwamba inajuzu kwa wanawake wazee kuzuru makaburi ya jamaa zao na mawalii bila ya kuchanganyika na wanaume, jambo hili kwa wanawake vijana ni makruh. Na hukmu ni hio hio katika jambo la wanawake kwenda mazikoni.

Anasema katika **(Jilaul kulub)**: Mtu anayefika makaburini aseme **(Asalamu alaykum ya ahla daril kawmil muuminin. Innaa Inshaallahu ankaribin bikum lahikun.)** Kisha atapiga Bismillahi, atasoma Ikhlas kumi na moja na Fatiha moja. Kisha atasoma dua ifuatayo **(Allahumma rabbil ajsadil baliyah. Wal idhamin nahirati llati kharajat mina dunya wa hiya bika muuminatun, adhil alayha rawhan min indika wa salaman minni)**. Akifika karibu na kaburi atakwenda upande wa kulia kwa maiti(kibla ya kaburi), upande wa miguu, atatoa salamu. Kisha atasimama au atapiga magoti au kukaa kisha atasoma mwanzo na mwisho wa suratul Bakara, Yasin sharif, Tabaraka, Takathur, Ikhlas sharif na Fatiha na kumzawadia maiti.

**Tanbih**: Wakati wanazuoni wetu walipokuwa wakielezea juu ya kutekeleza hija kwa ajili ya mtu mwengine walisema kwamba sala, funga, sadaka, kusoma Quran, kuleta dhikri, kutufu, kufanya hija na umra, kutembelea makaburi ya mtume “sallallahu alayhi wasallam” na mawalii, kumkafini maiti, na mfano wa haya miongoni mwa ibada za fardhi na nafila, mambo mengine ya kheri na mazuri, thawabu zake kutoa hadiya kwa roho za watu wengine inajuzu. Thawabu atapewa huyo msomaji na wale aliowapelekea. Kwa hivyo ikiwa ni kaburini au pahali pengine inafaa kusoma Quran na kuwapelekea maiti na hapo hapo kuwaombea dua. Pahali panaposomwa Quran hushuka rehema na baraka hivyo dua inayoombwa pahali hapo hutakabaliwa. Kufuatana na madhehebu ya Hanafi, iwapo mtu atafunga sunna, sala ,

sadaka, kisomo na akatoa hadiya thawabu kwa mtu mwengine alie hai au aliekufa basi thawabu hizo huwaendea watu hao. Kuna pia wanaosema kwamba hata ibada za fardhi kama zitatolewa hadiya thawabu zake basi zinamfika mtu. Thawabu hazikatwi pande akapewa maiti, bali kila mmoja wao(msomaji na maiti) hupewa kikamilifu. Kufuatana na madhehebu ya Shafii na Malik, amali ambazo hufanywa kwa kiwiliwili tu (mfano kisomo) hizo haziwezi kutolewa hadiya thawabu zake. Ila ibada hizo njema zinaweza kutumika kama wasila kwa ajili ya kuombea dua.

Anasema katika kitabu cha **(Alfikhi alal madhahibil arbaa)** (Ni sunna kwa wanaume kuzuru makaburi, ili kupata mazingatio na ukumbusho wa mauti. Kufuatana na madhehebu ya Hanafi na Maliki ni kufanya ziara hiyo siku ya Alkhamisi, Ijumaa au Jumamaosi ni sunnat muakkad. Kufuatana na madhehebu ya Shafii ni sunna muakkada kuzuru kuanzia Alkhamisi baada ya laasiri hadi jua linapochomoza siku ya Jumamosi. Mwenye kuzuru maiti anatakiwa amsomee Quran na kumuombea dua. Hayo yana faida na maiti. Wakati wa kuingia makaburini ni sunna kusema **(Assalamu alaykum ya ahla daril kawmil muuminin. Inna inshaallahu ankaribin bikum lahikun.)** Kaburi lililo mbali na lililo karibu, yote yanaendewa. Kuyazuru makaburi ya watu wema na mawalii yaliyo mbali ni sunna. Kuzuru kaburi la mtume “sallallahu alayhi wasallam” sallallahu alayhi wasallam ni katika ibada kubwa. Wanawake wazee wakiwa wamejisitiri vyema inajuzu kwao kuzuru lakini kama itakuwa ni sababu ya fitna na kuleta uovu basi itakuwa ni haramu kwa wanawake kuzuru makaburi. Wakati wa ziara haijuzu kulizunguka kaburi kama kufanya tawafu, kubusu jiwe au dongo lake, au kumuomba maiti kitu). Anaweza mtu akawaomba mawalii wamtakie shafaa, na wawe ni wasila kwa Allah.

**Kuna vitu viwili ambavyo kuondoka kwake**
**Kwa mtu yeyote kunamchoma moyo**
**Hata yatoke machozi ya damu, haki yake hailipiki**
**La kwanza ni ujana, la pili ni ndugu wa dini**

## JUZUU YA TATU, BARUA YA 9

**Imam Rabbani Mujadid alfi sani Ahmed Faruk “rahmatullahi alaih” katika kitabu chake cha Maktubat juzuu ya tatu barua ya tisa iliyoandikwa kwa ajili ya Mir Muhammed Nuuman. Ni ufafanuzi wa aya isemayo (Basi yale aliyokuleteeni Mtume “sallallahu alayhi wasallam”, yachukueni) Barua hii iliandikwa kwa kiarabu na tarjuma yake ni hii hapa chini:**

Bismillahir rahmanir rahim! Maelezo ya aya ya saba ya suratul Hashr **(Basi yale aliyokuleteeni Mtume "sallallahu alayhi wasallam" yachukueni. Na aliyokukatazeni yaacheni. Na mcheni Allah)** [Kutekeleza yaliyoamrishwa na kuacha yaliyokatazwa ndiyo kwenda sawa na **(Uislam)**.] Kusemwa muogopeni Allah baada ya kutakiwa kuacha yaliyokatazwa, ina leta ujumbe wa umuhimu wa kuacha yale yaliokatazwa. Kumuogopa Allah **(Taqwa)** ni kujizuia na ya haramu. Taqwa ndio msingi wa dini. Kujiepusha na yale yenye shubha huitwa **(Waraa)**. Mtume "sallallahu alayhi wasallam" anasema **(Nguzo ya dini yenu ni waraa)**. Na katika hadithi nyengine **(Hakuna jambo lililo sawa na waraa.)** Sababu ya dini yetu kulipa umuhimu jambo la kujiepusha na haramu ni kutokana na wingi wa mambo yanayotakiwa kujiepusha nayo na ukubwa wa faida inayopatikana kwa kuyaepuka huko. Hata unapotekeleza amri fulani basi unakuwa umejiepusha na kitu fulani. Kutekeleza amri uliyopewa maana yake ni kujiepusha na kukataa. Faida yake inakuwa ni kubwa kutokana na kuwa unakuwa umekataa kuitii nafsi. Wakati unafanya jambo nafsi nayo pia hupata ladha. Kila sehemu ya kuitii nafsi inapokuwa ndogo katika utekelezaji wa amri fulani, basi faida yake huwa kubwa zaidi. Kwa sababu hukmu za kiislam zinalenga kuikandamiza nafsi ni kuipunguza nguvu. Nafsi ni adui wa Allah. Katika hadithi qudsi tunasoma **(Kuwa adui wa nafsi yako, kwani hiyo nafsi ni adui wangu.)** Kwa hivyo miongoni mwa Turuq aliya (njia za twarika), zile zenye mafunzo ya kushikamana zaidi na kuacha makatazo, ndio zenye kuwafanya wafuasi wake wawe karibu zaidi na Allah. Kwa sababu hizi zinasisitiza zaidi kutokuitii nafsi. Na kama ambavyo hili linavyofahamika na wale walio katika njia hii, na sisi pia ndio njia tunayofuata. Kutokana na hilo ndio maana kiongozi wetu mkuu. mwanazuoni nguli Bahauddini Buhari anasema (Nimeifahamu njia iliyo fupi kabisa ya kuweza kunifikisha kwa Allah). Katika njia hii kubwa linalofanyika ni kuikatalia nafsi. Ni wepesi kwa mtu mwenye busara na uwelewa kusoma vitabu vilivyoandikwa na waongozaji wetu na akaweza kufahamu uwezo mkubwa wa njia hii katika kuelekeza kwenye kuyaacha makatazo ya Uislam. Hilo ataliona wazi wazi. Pamoja na kuwa hilo liko wazi, pia katika barua nyingi hilo nimeligusia. Usahihi wa kila jambo Allah ndiye anaeujua. Yeye ndie msaidizi wetu. Yeye ndie wakili wetu mwema. Sala na salamu zimuendee mtume "sallallahu alayhi wasallam" wetu Muhammad "sallallahu alayhi wasallam" na wale wale walio katika njia sahihi.

# JUZUU YA TATU BARUA YA 84

Shukrani zote zinamstahikia Allah, na amani iwe juu ya wale waja wake wateule, vipenzi. Wale wanaotaka kuwemo katika njia hii, la kwanza ni kuiambatanisha itikadi yao na kufuatana na mafunzo ya wanazuoni wa ahli sunna. Wanazuoni hawa nguli wamechukua mafunzo hayo yote kutoka kwa masahaba. Hawakuchanganya mafunzo hayo na fikra zao binafsi au dhana za wanafalsafa. Allah awape ujira mkubwa kutokana na kazi yao hiyo. Kisha anatakiwa ajifunze elimu ya fikh inayohitajika na kila mtu na kisha aifanyie kazi. Kisha awe ni mtu mwenye kumdhukuru sana Allah. (Yani moyo wake uwe unazingatia majina na sifa zake. Ila namna hii ya kumdhukuru Allah ni sharti ajifunze kutoka kwa mja ambae ni kamili, mukammil. Kujifunza kutoka kwa mashekhe wapungufu na wale wajinga, waovu hakutomuwezesha kufikia ukamilifu. Katika hatua ya awali anatakiwa awe ni mwenye kumdhukuru sana Allah, kiasi ya kwamba zaidi ya sala za fardhi na sunna zake, basi asishughulikie ibada nyengine. Hata kusoma Quran na ibada za nafila anatakiwa aziakhirishe wakati mwengine. Amdhukuru Allah akiwa na udhu au akiwa hana udhu. Akiwa amesimama, amekaa, anatembea au amelala, kila wakati anatakiwa awe katika jambo hilo. Wakati anapotembea njiani, anapokula au anapolala asiwe bila dhikri. Katika ubeti wa shairi la kiajemi inasemwa:

**Mdhukuru Allah kila ulipo na kila wakati kwa uhai wote**
**Kwa kumdhukuru mpendwa ndio moyo hutakata**

Anatakiwa amdhukuru sana Allah kiasi ya kwamba moyo wake hautafikiri wala kutamani kitu zaidi ya kumdhukuru Allah. Moyoni mwake asijiwe na jambo jengine zaidi ya Allah. Hata kama fikra nyengine zitamjia basi ajitahidi zisifike moyoni mwake. Moyo utakapoanza kusahau vitu vyengine na ukawa unamkumbuka Allah pekee, basi huwo ndio mwanzo wa kumfikia. Kusahau huku ni dalili njema ya kuanza kufikia radhi na mapenzi ya yule anaetafutwa (Allah). Ubeti wa shairi la kiarabu unasema:

**Nashangaa vipi Suad itafikiwa**
**Kuna mabonde na milima baina yake**

[Suad ni jina la kipenzi cha moyo]. Allah ndiye anayewawezesha watu kufikia kila kitu. Salam ziwe juu ya wale walio katika njia sahihi. Imesemwa katika juzuu ya tatu barua ya 17, Kumdhukuru Allah kwa moyo, kunauokoa moyo kutokana na kufungamana na vitu vyengine mbali na Allah. Fungamano hilo ni maradhi ya moyo na mja

asipotokana nalo basi huwa ni uzito kufikia imani ya kweli na wala hawezi kushikamana kikweli na maamrisho ya Uislam na makatazo yake. Pia inakuwa ni dhikri kutia niya wakati wa kuyatekeleza haya, na pale anapofanya yale ya mubaha kutokufikiria ladha inayopata nafsi. Sababu ya maradhi ya moyo ni kuitii nafsi. Nafsi ni adui wa Allah. Haitaki kumtii Allah. Nafsi pia ni adui kwake mwenyewe binaadamu. Moyo unapenda kuvifanyisha viungo vyengine haramu, uovu na yale yenye dhara. Ili kuweza kufaidi matashi mbali mbali, moyo hupendelea kubaki bila imani wala dini. Kufanya urafiki na makafiri na wale wapinzani wa madhehebu, kusoma vitabu vyao na magazeti yao, matangazo yao ya redio na televisheni yenye dhara huusababishia moyo maradhi. Kufuata mafunzo ya Uislam humuokoa mtu na maradhi ya moyo na kuifanya nafsi iathirike, na kuzifanya nguvu za athari yake ya matashi na matamanio kwa moyo zipungue

**Ni nani katika dunia anaefikia matakwa yake kwa nguvu zake**
**Bila ya shaka kitatokea, kile ambacho ni kadar yake.**

## BARUA YA 114

**Katika Makatib sharif, kitabu cha mwanazuoni mkubwa wa India, Abdullah Dehlevi "rahmatullahi alaih" kuna barua mia na ishirini na tano. Barua ya 114 aliandikiwa Haji Abdullah Buhariyina tarjuma yake hii hapa.**

Allahu taala hana pungufu hata moja. Anayoyasema yote ni kweli na huwaonesha waja wake njia sahihi. Sala na salamu zimfikie kiongozi wetu mtukufu, mpenzi wetu Muhammad "sallallahu alayhi wasallam" na jamaa zake na masahaba zake. Ahli tarika wa hapa(katika mji wa Delhi) wanasoma majina ili kupata wanayoyataka. Wanaandika na herizi. Kwa namna hiyo wanawavuta watu upande wao. Wanamtukuza Amirul muuminina Ali karamallahu wajhahu kuliko makhalifa wengine watatu „radiyallahu anhum". Hawa huitwa **(Mashia)**. Wale wenye kuwafanyia uadui makhalifa watatu pamoja na masahaba wengine, hao huitwa **(Rafidhy)**.

Hadhrat Abubakar, Hadhrat Omar na Hadhrat Uthman dhinurain ni wabora kuliko Hadhrat Ali "radiyallahu taala anhum ajmain", na hili limeandikwa na wanazuoni wengi wa **(ahlusunat wal jamaa)** "rahimahumullahu taala". Na hili limethibitishwa kupitia Quran, hadithi sharif na ijmaa ya masahaba „radiyallahu anhum" ajmain. Miongoni mwa vitabu hivyo ni vitabu viwili thamini viitwavyo **(Izalatul hafaa)** na **(Kurratul aynayn)**, vilivyoandikwa na mwanazuoni mkubwa

wa India Shah Waliyullah Muhadith Dehlewy. Hiki cha pili kilifanyiwa tarjama kwa kituruki na kuingizwa ndani ya kitabu kiitwacho **(As-habul kiram)**. Pia kinapatika ndani ya kitabu kiitwacho **(Hak sozun vesikalar)**. Kitabu cha kiarabu kiitwacho **(Asawaikul muhrika)** kilichoandikwa na mwanazuoni mkubwa Ibrahim Hajar Makky kilichapishwa kwa ofset na Hakikat kitabevi huko Istanbul. Yeyote atakaekisoma kitabu hiki kwa insafu atafahamu kwamba wasio na madhehebu hawako njia sahihi. Baadhi yao wanajiita **(Jafary**), na kuwadanganya vijana kwa kusema kuwa wao ni wafuasi wa maimamu kumi na mbili. Uhakika ni kwamba wenye kuwafuata maimamu kumi na mbili ni **(ahli sunna)**. Wanazuoni wa ahlisunna wanasema kwamba (Kuwapenda maimamu kumi na mbili kunapelekea kukata roho hali ya kuwa ni muumin.

Wakati wa jeneza, wanatayarisha mikusanyiko nadhifa kwa lengo la kufanya (Dawr) (Hawasali jamaa misikitini). Wanafanya mikusanyiko ya maulidi na kusoma kasida. Katika zawiya zao wanapiga ala za muziki. Pamoja na haya, kuna aina nyingi za bid'a wanazozifanya chini ya mwamvuli wa (Tarika). Hata wale makafiri wa Jukiyya na Barahman wa India nao ibada zao pia huzipandikiza Utarika. Wako pamoja na wale mafasiki na wale walioipa uso dunia. Katika sala hawayapi umuhimu matendo ya kiyam na julus, bali hata sala ya jamaa na Ijumaa hawazipi umuhimu. Haya hayakuonekana zama za salafi swalih na hayamo ndani ya Uislam. Wanazuoni wa **(Ahli sunna)** rahimahumullahu walikua wakijiweka mbali na mambo hayo maovu ya bid'a. Yule anaetaka kuwa muislam alie katika njia ya salafi swalih, anawajibika kuwa mbali na aina hii ya watu wa tarika. Hawa ni matapeli wa dini tu. Kazi yao ni kuvunja imani na dini iliyo kwa waja wa Allah. Dhikri na mambo mengine wanayoyafanya yanawaletea harakati za nafsi na moyo. Haya yalitakiwa yawasafishe na yale mambo yaliyo mbali na Allah, na sio kuwapelekea katika hayo yanayoshuhudiwa kwao wakiyatenda. Kashf (Karama, kuzungumza na majini na kutoa habari juu ya mambo yasio wazi) si katika jambo linalopewa thamani katika Uislam. Makafiri wa Jukkiya pia huonesha kashf na karama. Wale wenye akili wanatakiwa wafungue macho na kuweza kuyaona yaliyo sahihi na yale maovu. Haiwezekani kwa mtu kuwa ni mwenye kuipenda dunia kisha akawa pia ni mshika dini kwa wakati mmoja. Si jambo la kiakili kuitoa dini yako kwa sababu ya maslahi ya kidunia. Wanazuoni wa mji wa Buhar walikuwa ni wenye tawakkul. Hawakuwa wenye kuipenda dunia. Kufanya dhifa na kuwakusanya watu wapenda dunia, kunaufanya moyo upate kiza. Mabwana hao wakubwa walikuwa wakijiweka mbali na mambo hayo. Hao walishikamana na

sunna za bwana mtume “sallallahu alayhi wasallam” na itikadi ya salafi swalih. Katika mambo yao yote walichukuwa njia ya **(Azma)**. Wakijiweka mbali na bid’a na wakikimbia yale yenye kupelekea kwenye haramu na makruh. Mambo halali ambayo yatapelekea kwenye haramu nayo pia huwa ni haramu. **(Dhikri ya kimya)** kimya ni bora kuliko **(dhikri ya sauti)**. Namna hiyo ndiyo walivyokuwa wakileta dhikri. Walikuwa katika daraja ya Ihsan iliotajwa ndani ya hadithi sharif. Mioyo yao kila wakati ilikuwa mbele ya Allahu taala. Iwapo mtu muumin, alie mkweli atapata tawajjuh kutoka kwa mabwana wakubwa wa tasawwuf wa aina hii tulioitaja, basi moyo wake na Latifa zake zote zitaanza kuleta dhikr. Atapata utulivu wa moyo (yani ndani ya moyo wake kutakuwa na Allah pekee), na hili huitwa **(Mushahada)** pia atapata neema ya nuru za ndani na nje ambazo huitwa **(Waridat)**. Yule ambae atapata nuru kutoka kwa Murshid, basi moyo wake hautofikiria chochote zaidi ya Allah. Viungo vyake vyote hufanya mambo kwa azma na kwa mujibu wa sunna za mtume “sallallahu alayhi wasallam” sallallahu alayhi wasallam. Neema hii ni furaha kubwa ya kiasi gani! Ya Rabbi! tunakuomba uturuzuku neema hii kwa baraka za mtume “sallallahu alayhi wasallam” sallallahu alayhi wasallam na mashekhe watukufu “rahmatullahi alaih” . Mujaddid wa karne Imam Rabbani “rahmatullahi alaih” , nuru yake ilizifanya Latifa za watu kuweza kufikia neema hiyo.

**Maisha yangu yawe fidia kwako**
**Muhammad alie mzuri na mwenye jina zuri.**
**Njoo umuombee mja mnyenyekevu**
**Ewe Muhammad ulie mzuri na mwenye jina zuri.**

**Waumini wanapata mazito hapa duniani**
**Wapate ujira huko akhera**
**Chaguo la ulimwengu elfu kumi na nane**
**Muhammad alie mzuri na mwenye jina zuri.**

**Aliye safiri kwenye mbingu saba**
**Aliyepita kwenye mbingu na kursy**
**Miraj, aliyemuomba Allah kwa umma wake**
**Muhammad alie mzuri na mwenye jina zuri.**

**Dunia hizi mbili zina faida gani kwa Yunus**
**Wewe ni mtume wa kweli bila shaka wala shubha**
**Asie kufuata wewe ataondoka bila imani**
**Muhammad alie mzuri na mwenye jina zuri.**

## NENO LA MWISHO LA KITABU CHA NJIA YA PEPONI

Viumbe vyote vilivyo hai na visivyo hai viko chini ya nidhamu maalum. Katika muundo wa kila kitu, kila tokeo na kila reaction, kuna nidhamu isiyobadilika, ambayo tunafahamu kwamba yana mfungamano wa kihesabati. Mfungamano huu na nidhamu hii huitwa kanuni za fizikia, kemia, biolojia na astronomi. Kwa kufaidika na nidhamu hii isiyobadilika, watu wameweza kuanzisha viwanda, kutengeneza madawa, kwenda kwenye mwezi kufahamu mahusiano ya sayari na ya atom. Imewezekana kutengenezwa redio, televisheni, akili za kielektronia na intaneti. Ingekuwa hakuna nidhamu maalum kwa viumbe, kila kitu kinatokea tu kwa namna yake, basi haya yote yasingeweza kufanyika. Vitu vingekua vinagongana, kuharibika na ingekuwa ni balaa kubwa. Kila kitu kingetoweka.

Viumbe kuwa chini ya kanuni, mfungamano na nidhamu maalum, na kutokuwa vinatokea tu, ni udhihirisho wa wazi kwamba yuko alieviumba ambae ana elimu ya hali ya juu, mwenye uwezo, mwenye kuona, mwenye kusikia na afanyae akitakacho. Yeye huyo ndie anaevifanya viwepo anavyovitaka na kuviondoa asivyovitaka. Ameweka sababu mbali mbali za kuweza kuwepo na kutoweka kwa vitu. Lau kama asingeweka sababu hizo basi kusingekuwepo hii nidhamu iliyo baina ya viumbe. Vitu vyote vingekuwa mchanganyiko. Hivyo kuwepo kwake kusingedhihiri. Sayansi na ustaarabu pia visingepatikana.

Yeye, pamoja na kwamba amedhihirisha kuwepo kwake kwa kupitia hii nidhamu iliyopo, pia kwa huruma zake kwa viumbe amewaeleza wazi wazi kuwa yeye yupo. Tangu uwepo wa Adam „alaihis-salaam”. Na kupitia karne zote, kwa kila kaumu alichagua yule alie mbora wao katika aliowaumba na akamtumia malaika, akamtambulisha uwepo wake na majina yake, na kuwafahamisha wanadamu ni yepi wayafanye na yepi wajiepushe nayo ili waweze kuishi duniani kwa raha na utulivu. Wateule hao miongoni mwa binaadamu ndio huitwa **(Mitume)**. Na yale wanayoyafunza ndio huitwa **(Dini)** na **(Hukmu za dini)**. Kwa vile binadamu anatabia ya kuyasahau ya zamani, na kutokana na kuwa kila wakati walipatikana waovu waliyoyabadilisha maneno na maandishi ya mitume aleyhimu swalaat wasalam, hivyo dini za mwanzo zimesahaulika na kubadilishwa. Waovu hao pia wameleta dini za kubuni.

Allah aliye muumba wa kila kitu kwa huruma yake kwa viumbe ndio amewaletea mtume “sallallahu alayhi wasallam” wa mwisho na dini

mpya. Na ametoa habari njema kwamba dini hii atailinda hadi siku ya kiama na kwamba hata kama watu waovu watajaribu kuihujumu, kuibadilisha na kuiharibu, yeye ataieneza kila pahala hali ya kuwa haijaharibika.

Tunamshukuru Allah kwamba tumeamini kuwepo kwa muumbaji tangu tungali wadogo. Tumepata neema ya kumjua yeye muumbaji kuwa ni **(Allah)**, mtume “sallallahu alayhi wasallam” wake kuwa ni **(Muhammad)** “sallallahu alayhi wasallam” na dini yake kuwa ni **(Uislam)**. Tulitaka tuifahamu hii dini kwa usahihi wake. Wakati tuko sekondari na chuo kikuu tulitafuta vyanzo sahihi vya kuweza kujifunzia. Ila wamasoni, wakoministi, wafuasi wa sayansi walionunuliwa na mawahabi na wapinga madhehebu walikuwa wamewazunguka na kuwazonga vijana. Murtadi hawa ambao wameiuza dini yao kwa ajili ya maslahi ya kidunia walifanya kazi kubwa ya kuchanganya mambo kiasi ya kwamba hali imefikia kuwa ni uzito kuweza kupambanua haki kutokana na batil. Hapakuwa na msaada mwengine zaidi ya kumuomba Allah mtukufu. Allah akatupa bahati ya kuweza kusoma vitabu vya wanazuoni wa Ahli Sunna “rahimahumullahu taala”. Ila fikra za wale walioiweka mbele sayansi **(Matapeli wa sayansi)** na wale wanaoeneza fikra mbovu na kusema ni tarjama ya Quran **(Matapeli wa dini)** zilikuwa tayari zimegusa roho zetu. Shukrani zote zinamstahikia Allah, kwani kutokana na nasaha za viongozi wa dini wa kweli, tumeweza kupambanua yalio sahihi na maovu. Tumefahamu kwamba yale ambayo yalikuwa kichwani mwetu hayakuwa ni elimu bali ni sumu na kutokana na athari yake mioyo yetu pia iliingia kiza. Lau kama tusingepata fursa ya kusoma vitabu vya ahlisunna basi tusingeweza kumpambanua nani rafiki na nani adui, na tungedanganyika na kunaswa kwenye mitego, hila na uwongo wa nafsi zetu na wa maadui wa dini. Mitego ya maadui wa siri, wasio dini na wenye kuona utovu wa maadili kuwa ni maendeleo, tusingeweza kuitambua. Tungeufanyia dhihaki Uislam halisi tuliojifunza kutoka kwa baba zetu na mama zetu. Mtume “sallallahu alayhi wasallam” wetu mpenzi Muhammad sallallahu alayhi wasallam anatuonya tusije kuanguka kwenye mitego ya maadui wa Uislam kwa kusema: **(Jifunzeni dini yenu kutoka kwenye vinywa vya rijal!)** Rijal maana yake ni viongozi wa kweli wa dini, na tusipowapata basi tujifunze kupitia vitabu vyao. Vitabu vya watu wa bid’a, wapinga madhehebu na viongozi wa dini majahil vina madhara sawa na vitabu vya makafiri.

Ni haram kwa wanawake na wanaume kutoka mbele ya wengine bila ya stara ya kisharia. Hii ina maana Allah amekataza. Katika

madhehebu manne yenye kuelezea amri na makatazo ya Allah, wametafautiana katika kuzieleza sehemu za awrat za mwanamme, kwa maana sehemu anazolazimika kuzisitiri na kutozionesha na pia ambazo hazifai kuzitizama. Kila muislam anatakiwa azistiri sehemu za awra kufuatana na madhehebu yake.

Ni haramu kuangalia sehemu iliyo wazi ya awrat ya mtu mwengine. Katika **(Kimyai saadet)** anasema (Kama ambavyo ni haramu kwa wasichana na wanawake kutoka nje kichwa, nywele mikono na miguu wazi, basi pia ni haramu kuvaa nguo zinazobana, nyepesi, zenye mapambo na zenye kunukia. Na wale wanaomridhia yeye kutoka hivyo katika wazee, mume au kaka nao pia wanapata dhambi na watashirikiana nae katika adhabu.) Kwa maana ya kwamba watachomwa pamoja kwenye moto wa Jahannam. Ikiwa watatubia basi watasamehewa na hawatochomwa. Allah anawapenda wenye kutubia. Imeamrishwa katika mwaka wa tatu wa hijra kwamba wasichana wenye akili na waliokwishavunja ungo (baaligha) na wanawake hawatakiwi kuonekana na wanaume wa mbali (ajnabi). Wasidanganyike watu na maneno ya majasusi wa kiingereza na majahili wengine walionaswa na mitego yao wanaodai kuwa stara ya sharia imebuniwa baadae na wanazuoni wa fikhi na kwamba si jambo la kisheria.

Tunaeleza tena hapa kwamba mtoto anapofikia umri wa baleghe na akili kwa maana ya kwamba anaweza kupambanua jema na baya na amefikia umri wa kuingia kwenye ndoa, basi anatakiwa haraka ajifunze sharti sita za imani, kisha ajifunze **(Hukumu za kiislamu)**, yaani yaliyo ya halali na haram, na inakuwa fardhi kwake kuyafuata. Mtoto wa kike afikiapo umri wa miaka tisa na mwanamme miaka kumi na mbili huwa ni baleghe na mwenye akili. Inakuwa ni fardhi kwake kujifunza mambo haya kutoka kwa wazee wake, jamaa zake au marafiki. Pia kwa kafiri alieingia katika Uislam anatakiwa kumfata kiongozi wa dini au mufti ili kujifunza mambo haya, pia inakuwa ni fardhi kumsomesha mambo haya au kumpatia kitabu ili ajifunze na kumtanabahisha juu ya umuhimu wake. Kumpongeza tu bila ya kumfunza au kumpa kitabu cha kujifunzia inakuwa bado jambo la fardhi halijatekelezwa. Asietekeleza fardhi ataunguzwa motoni. Iwapo hatopata mwalimu wala kitabu basi atakuwa na udhuru kwa kutokujifunza.

Tutaendelea kutoa huduma ya kuchagua na kueneza maandishi ya wanazuoni wa ahali sunna ili kuwafikishia vijana elimu sahihi ya dini na kuwawezesha watu kuishi duniani kwa raha na utulivu na kuweza kupata neema za milele huko akhera.

Ili kufikia muradi wake mtu basi na asome **(Salatun tunjina)**: (Allahumma swalli ala sayyidna Muhammadin wa ala aali sayyidna Muhammad. Salatan tunjinaa biha min jamiil ahwaal walaafat, wa takdhi lana biha jamiul hajat, wa tutahhiruna biha min jamii sayyiati, wa tarfauna biha aala darajat, wa tuballighuna biha aksal ghayat, min jamiil khayrat fil hayat wa baadal mamat).

Hadithi sharif zimetueleza kwamba ni vyema kukithirisha **(Istighfari)** ili kujikinga na matatizo na mazito ya aina yote, na dhara na hujuma za shetani na maadui wengine.

**Umri umekuja na kuondoka, kama upepo uliovuma,**
**Kwangu imekuwa ni kama kufumba na kufumbua jicho langu.**
**Maneno haya ya haki ni shahidi kwamba roho ni mgeni wa kiwiliwili,**
**Siku itafika itatoka na kwenda, kama ndege atokavyo tunduni.**